

# Al - Kabair

**Mtungaji:**

**Al-Hafidh Abi 'Abdullah Muhammad bin  
Ahmad bin 'Uthman Adh-Dhahaby**

**Mfasiri:**

**Abdullah Muhammad Said ('Arafat)**

**Al - Kabair**

---

**Tafsiri ya Al - Kabair**

**Kimepitiwa na:**

**Said Bawazir, Yassir Salim na Khalfan Njama.**

**Typesetting:**

**Ally Said Abdallah**

**Chapa ya Kwanza 2017**

**Nakala 3000**

**Printed in:**

**India**

**Msambazaji:**

**Ibn Hazm Media Centre**

**©Haki zote zimehifadhiwa**

**Si ruhusa kukopi au kunakili Kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila ya idhini ya Ibn Hazm Media Centre.**

YALIYOMO:

Utangulizi.....	9
Madhambi Makubwa.....	9
Dhambi Kubwa ya 1: Kumshirikisha Allah.....	13
Dhambi Kubwa ya 2: Kuaa Nafsi.....	19
Dhambi Kubwa ya 3: Uchawi.....	25
Dhambi Kubwa ya 4: Kuacha Swala.....	29
Dhambi Kubwa ya 5: Kuzuia Zaka.....	54
Dhambi Kubwa ya 6: Kutokufunga Ramadhani Bila ya Sababu.....	64
Dhambi Kubwa ya 7: Kutokutekeleza Hija kwa Mwenye Uwezo.....	66
Dhambi Kubwa ya 8: Kuasi Wazazi.....	68
Dhambi Kubwa ya 9: Kuwakimbia Ndugu wa Karibu.....	82
Dhambi Kubwa ya 10: Zinaa.....	87

**Al - Kabair**

---

<b>Dhambi Kubwa ya 11:</b>	
<b>Liwati.....</b>	<b>96</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 12:</b>	
<b>Riba.....</b>	<b>108</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 13:</b>	
<b>Ulaji Mali ya Mayatima.....</b>	<b>113</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 14:</b>	
<b>Kusema Uongo.....</b>	<b>121</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 15:</b>	
<b>Kukimbia katika Medani.....</b>	<b>123</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 16:</b>	
<b>Kiongozi Anayeghushi.....</b>	<b>125</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 17:</b>	
<b>Kiburi, Majivuno na Jeuri.....</b>	<b>135</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 18:</b>	
<b>Kushuhudia Uongo.....</b>	<b>140</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 19:</b>	
<b>Kunywa Pombe.....</b>	<b>142</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 20:</b>	
<b>Kamari.....</b>	<b>159</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 21:</b>	
<b>Kuwasingizia Wanawake.....</b>	<b>166</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 22:</b>	
<b>Kuiba Ngawira.....</b>	<b>170</b>

**Al - Kabair**

---

<b>Dhambi Kubwa ya 23:</b>	
<b>Wizi.....</b>	<b>176</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 24:</b>	
<b>Wizi wa Uharamia.....</b>	<b>179</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 25:</b>	
<b>Kiapo cha Uwongo.....</b>	<b>182</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 26:</b>	
<b>Dhuluma.....</b>	<b>189</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 27:</b>	
<b>Watoza Kodi.....</b>	<b>209</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 28:</b>	
<b>Kula Haramu.....</b>	<b>212</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 29:</b>	
<b>Mtu Kujiua Mwenyewe.....</b>	<b>219</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 30:</b>	
<b>Uongo katika Kauli zetu nyingi.....</b>	<b>223</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 31:</b>	
<b>Hakimu Muovu.....</b>	<b>229</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 32:</b>	
<b>Rushwa.....</b>	<b>233</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 33:</b>	
<b>Wanawake Kujifananisha na Wanaume.....</b>	<b>236</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 34:</b>	
<b>Mwenye Kufurahia Matendo ya Mkewe.....</b>	<b>240</b>

**Al - Kabair**

---

<b>Dhambi Kubwa ya 35:</b>	
<b>Mwenye Kumuoza Mwanamke Aliyeachwa.....</b>	<b>242</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 36:</b>	
<b>Kutojilinda na Mikojo.....</b>	<b>246</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 37:</b>	
<b>Kujionyesha – Riya.....</b>	<b>248</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 38:</b>	
<b>Kujifunza Dini kwa Ajili ya Dunia.....</b>	<b>253</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 39:</b>	
<b>Khiana.....</b>	<b>259</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 40:</b>	
<b>Kusimanga.....</b>	<b>263</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 41:</b>	
<b>Kukanusha Kudura.....</b>	<b>266</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 42:</b>	
<b>Kujisikizisha kwa Watu Wanayoyaficha.....</b>	<b>276</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 43:</b>	
<b>Mwenye Kufitini.....</b>	<b>277</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 44:</b>	
<b>Kulaani.....</b>	<b>283</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 45:</b>	
<b>Uhaini wa Kutotekeleza Ahadi.....</b>	<b>292</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 46:</b>	
<b>Kuamini Makuhani na Wanajimu.....</b>	<b>295</b>

**Al - Kabair**

---

<b>Dhambi Kubwa ya 47:</b> <b>Mwanamke Kutomtii Mumewe.....</b>	<b>299</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 48:</b> <b>Masanamu.....</b>	<b>316</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 49:</b> <b>Kujipiga Makofi, Kuomboleza n.k.....</b>	<b>320</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 50:</b> <b>Uasi.....</b>	<b>350</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 51:</b> <b>Ustahamilivu Juu ya Mnyonge.....</b>	<b>354</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 52:</b> <b>Kumuudhi Jirani.....</b>	<b>368</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 53:</b> <b>Kuwardhi Waislamu na Kuwatukana.....</b>	<b>372</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 54:</b> <b>Kuwardhi Waja wa Allah.....</b>	<b>381</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 55:</b> <b>Kuburuza Mavazi.....</b>	<b>386</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 56:</b> <b>Kuvaa Dhahabu Si kwa Wanaume.....</b>	<b>389</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 57:</b> <b>Utoro wa Mtumwa.....</b>	<b>391</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 58:</b> <b>Kuchinja kwa Ajili ya Asiyekuwa Allah.....</b>	<b>393</b>

**Al - Kabair**

---

<b>Dhambi Kubwa ya 59:</b> <b>Mwenye Kujiita Jina Lisilo la Baba yake.....</b>	<b>397</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 60:</b> <b>Kubishana na kwa Hasira.....</b>	<b>399</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 61:</b> <b>Kuzuia Maji ya Ziada.....</b>	<b>404</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 62:</b> <b>Kupunguza Kilo, Mazao.....</b>	<b>406</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 63:</b> <b>Kujiaminisha na Vitimbi vya Allah.....</b>	<b>410</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 64:</b> <b>Kukatia Tamaa Rehema ya Allah.....</b>	<b>416</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 65:</b> <b>Mwenye Kuacha Swala ya Jamaa.....</b>	<b>417</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 66:</b> <b>Kudumu Kuacha Swala ya Ijumaa.....</b>	<b>419</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 67:</b> <b>Kudhuru katika Wasia.....</b>	<b>425</b>
<b>Dhambi Kubwa 68:</b> <b>Vitimbi na Hadaa.....</b>	<b>428</b>
<b>Dhambi Kubwa 69:</b> <b>Mwenye Kupeleleza Waislamu.....</b>	<b>430</b>
<b>Dhambi Kubwa ya 70:</b> <b>Kumtukana Sahaba Yoyote.....</b>	<b>431</b>



## UTANGULIZI

Alhamdulillah Mola wa walimwengu, wala hapana uadui ila kwa madhalimu, Swala na Salamu zimwendee Mtume Muhammad ﷺ, Bwana wa waliotumwa na Imamu wa wachamungu, ali zake na sahaba zake.

Ama baada ya hayo..kitabu hiki kimekusanywa juu ya kutaja madhambi makubwa, yaliyoharamishwa na kukatazwa.

## MADHAMBII MAKUBWA

Ni kile alichokataza Mwenyezi Mungu na Mtume Wake katika *Qur'an* na *Sunna* na yaliyomo katika athari za *salafu swalih*. Allah ameweka katika kitabu chake kitukufu kwa ambaye ataacha madhambi makubwa na yaliyokatazwa kuwa atamsamehe madhambi yake madogo kwa Kauli Yake Ta'ala:

إِن تَجْتَبُوا كِبَائِرَ مَا تُهَوَّنَ عَنْهُ نُكْفِرَ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَنُدْخِلَكُم مَّدْخَلَ كَرِيمًا ﴿٤٣١﴾

**"Mkiepuka makubwa mnayo katazwa, Tutakufutieni makosa yenu madogo, na Tutakuingizeni mahali patukufu." (4:31).**

Kwa hivyo Allah Mtukuka amehakikisha kwa andiko hili kuwa aliye epuka madhambi makubwa kumtia peponi, Allah Mtukuka pia amesema:

وَالَّذِينَ سَجْتَبُونَ كَبِيرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ وَإِذَا مَا غَضِبُوا هُمْ يَغْفِرُونَ ﴿٤٢:٣٧﴾

**"Na wanao yaepuka madhambi makubwa na mambo machafu, na wanapo kasirika wao husamehe." (42:37)**

Katika aya nyingine:

الَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبِيرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ إِلَّا اللَّمَمَ إِنَّ رَبَّكَ وَاسِعُ الْمَغْفِرَةِ

**"Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vichafu, isipo kuwa makosa khafifu. Hakika Mola wako Mlezi ni Mkunjufu wa maghira..." (53:32)**

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« الصلوات الخمس والجمعة إلى الجمعة ، ورمضان إلى رمضان مكفرات لما بينهن إذا اجتنبت الكبائر »

*"Swala tano, Ijuma hadi Ijuma, na Ramadhani hadi Ramadhani hufuta yaliyo kati yake pindi yaatakapoepukwa madhambi makubwa."*<sup>1</sup>

Hivyo, ametubainishia wazi kuhusu madhambi makubwa ni yapi ili Waislamu wayaepuke. Juu ya hili wanazuoni wametafautiana, wengine wamesema ni saba, na wakatolea hoja kauli yake Mtume ﷺ isemayo:

« اجتنبوا السبع الموبقات »

*"Epukeni matendo maovu saba yenye kuangamiza."*

Akayataja kuwa ni:

« الشرك بالله ، والسحر ، وقتل النفس التي حرم الله إلا بالحق ، وأكل مال اليتيم ، وأكل الربا ، والتولي يوم الزحف ، وقذف المحصنات الغافلات المؤمنات » .

---

<sup>1</sup> Hadithi sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/309-400 na Imam Muslim 233.

<sup>2</sup> Hadithi sahihi imepokewa na Al-Bukhari 2766, 5764 na Muslim 89 kutoka kwa Abu Hurayrah.17902 na Ibn Jariir 9209 yenye sanadi sahihi.

## Al- Kabair

---

" 1. Kumshirikisha Allah. 2. Uchawi. 3. Kuuwa Nafsi ambayo Allah ameharamisha ila kwa haki. 4. Kutumia mali ya mayatima. 5. Kula riba. 6. Kukimbia jihadi au vita. 7. Kuwasingizia wanawake ambao ni waumini."<sup>2</sup>

Abdullah Ibn 'Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا alisema, Madhambi makubwa ni karibu zaidi idadi ya sabini, kuliko kuishia saba tu.<sup>3</sup> Wallahi Ibn Abbaas amesema kweli<sup>4</sup>.

Hadithi haijawekea mipaka maalum madhambi makubwa, badala yake katika hadithi hii ni kuwa yanaainishwa aina ya madhambi, ambayo mtu akiingia katika vifungu hivyo huwa amefanya uhalifu ambao unahitaji kutolewa adhabu za duniani kama vile zina na wizi. Madhambi haya Mtukufu Mtume ﷺ amemlaani mwenye kuyafanya na kwa ameyaeleza kuwa ni madhambi makubwa yenye kuangamiza.

Hapana shaka madhambi mengine ni makubwa zaidi ya mengine. Utaona kuwa Mtume ﷺ anahesabu kumshirikisha ni moja wapo ya dhambi kubwa zaidi na ya kuwa mtu aliye mshirikisha Allah atabaki jahannam daima wala haghuriwi. Allah تعالی Mtukuka zaidi Anasema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

**"Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye...." (4:46)**

\*\*\*

---

<sup>3</sup> Hadithi sahihi imepokewa na Abdur Razzaak 17902, Ibn Jarir 9209 Isinadi Sahihi.

<sup>4</sup> Hilo amelisema Dhahabi, na yeye ni katika watu wa miaka ya mia saba hijiria, Unaona nini alichokuwa anasema Allah Amrehemu.

## DHAMBIBUBWA YAKWANZA

### KUMSHIRIKISHA ALLAH

Dhambi ovu na kubwa sana ni kumshirikisha Allah. Na dhambi hii ipo ya aina mbili: Ya kwanza ni kuamini kuwa Allah تعالی ana mshirika wa kuabudiwa ghairi Yake kama jiwe, mti, nyota, mwezi au Mtume, Shekhe, malaika au ghairi ya hao. Na hii ndio shirki kubwa zaidi ambayo Allah Mtukuka Amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

***“Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye....” (4:48)***

إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ

***“...Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhulma iliyo kubwa.” (31:13)***

Na amesema tena Ta’ala:

إِنَّهُ مَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَهُ النَّارُ

***“...Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni...” (5:72)***

Na aya katika hilo ni nyingi.

Yeyote anayejaribu kumfanya Allah تعالی kuwa na mshirika wake na akafa hali ya kuwa ni Mshirikina ajue kabisa kuwa yeye atakuwa miongoni mwa watu wa motoni. Ni sawa na kuwa mwenye kumwamini Allah na

## Al- Kabair

---

akafa muumini atakuwa mtu wa peponi hata kama ataadhibiwa kwa moto (kwa madhambi mengine)

Tunasoma katika sahihi Al-Bukhari na Muslim kuwa Mtume wa Allah ﷺ aliuliza:

« أَلَا أَنْبِئُكُمْ بِأَكْبَرِ الْكِبَائِرِ » ثَلَاثًا

*"Je nikufahamisheni kuhusu madhambi makubwa?"*. Amesema alisema maneno hayo mara tatu Masahaba wakamjibu: "Ndio ewe mjumbe wa Allah تعالى" Mtume ﷺ akawaambia:

«الإشراك بالله وعقوق الوالدين ، وكان مستكثنا فجلس فقال : ألا وقول الزور،  
ألا وشهادة الزور»

*"Kumshirikisha Allah, kuasi wazazi wawili, na wakati huo alikuwa akiegemea aliposema hivyo, akakaa na kuendelea kusema: Ehe pamoja na kusema uongo (kwa makusudio) na kushuhudia uongo." akawa anakariri hayo hadi tukaambizana: 'Laiti angenyamaza.'" (Al-Bukhari 2654 na Muslim 87)*

Vile vile Mtume ﷺ alisema:

«اجتنبوا السبع الموبقات»

*"Epukeni mambo saba yenye kuangamiza."* (Al-Bukhari na Muslim)

Akataja ndani yake kumshirikisha Allah تعالى na chochote, na akasema:

« من بدل دينه فاقتلوه »

*"Mwenye kubadilisha dini yake muueni."* (Ahmad 1/282, Al-Bukhari 3017 kutoka kwa Ibn 'Abbas)

## Al - Kabair

---

Aina ya pili ya kumshirikisha Allah تعالی: ni ria katika matendo, kama Allah Alivyosema:

فَمَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا ﴿١١٠﴾

**"...Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi." (18:110)**

Yaani asijioneshe katika matendo yake kwa mtu yeyote. Mtume ﷺ amesema:

« إياكم والشرك الأصغر »،

*"Ole wenu na shirki ndogo."*

Wakauliza: "Ewe Mtume wa Allah shirki ndogo ni nini?" Mtume ﷺ akawaambia:

« الرياء . يقول الله تعالى يوم يجازي العباد بأعمالهم اذهبوا إلى الذين كنتم تراءونهم بأعمالكم في الدنيا فانظروا هل تجدون عندهم جزاء » .

*"Ni ria. Allah atasema siku ile atakayowalipa waja wake kwa matendo yao, nendeni kwa wale mliokuwa mkiwaonesha matendo yenu duniani kisha angalieni kama (siku hii leo) wataweza kukulipeni kitu." (Ahmad 5/428-429 na Al-Baihaqi 6831 na ikasahihishwa na Al-Albani katika silsila As-Swahiha namba 951)*

Vile vile amesema Mtume ﷺ:

« يقول الله: من عمل عملاً أشرك معي فيه غير فهو للذي أشرك وأنا منه بريء »

*"Allah anasema: Yeyote atakayefanya jambo lolote ambalo ananishirikisha na mwengine kitendo hicho ni cha aliyeshirikishwa na miye niko mbali nacho." (Ahmad 5/301 na Muslim 2985 kutoka kwa Abu Hurayrah)*

## Al- Kabair

---

Aliendelea kusema ﷺ :

« من سمع سمع الله به ومن رأى رأى الله به »

*“Mwenye kusikia, Allah atamsikia kwa kusikia kwake na atakayefanya ria, Allah atamwadhibu kwa ria hiyo.” (Ahmad 5/301, Al-Bukhari 6499 na Muslim 2987 kutoka kwa Jundub).*

Abu Hurairah رضي الله عنه anaeleza kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema: “Ni

« رب صائم ليس له من صومه إلا الجوع والعطش ، ورب قائم ليس له من قيامه إلا السهر »

*wangapi wanaofunga ni kwa ajili ya kujionyesha na kujipatia umaarufu hao hawana kitu bali ni njaa na kiu, na wangapi wanaosimama kwa Swala za usiku isipokuwa Swala zao hizo ni mkeshu tu.” (Ahmad 2/373 na Al-Hakim na Al-Baihaqi sahihi Al-Jami’ 3490)*

Kwa maana kuwa Swala na fungu za mtu hazipo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu basi mtu hapati thawabu, kama ilivyopokewa kutoka kwa Mjumbe wa Allah ﷺ kuwa alisema:

« مثل الذي يعمل للرياء والسمعة كمثل الذي يملأ كيسه حصى ثم يدخل السوق ليشتري به، فإذا فتحه قدام البائع فإذا هو حصى وضرب به وجهه ، و لا منفعة له في كيسه سوى مقالة الناس له ما أملاً كيسه ولا يعطى به شيئاً فكذلك الذي يعمل للرياء والسمعة فليس له من عمله سوى مقالة الناس ولا ثواب له في الآخرة »

*“ Mfano wa anayejionesha na kujifakhri ni sawa na mtu anayejaza mfuko wake changarawe na kisha akaingia sokoni kununua vitu, na wakati anatoa hivyo vijiwe kumpatia muuzaji, muuzaji akampiga navyo usoni mwake. Na kwa hivyo mfuko wake huwa hauna faida ila mazungumzo ya watu juu yake kuwa mfuko wake umejaa sana*

## Al - Kabair

---

*lakini hawezi kununua kitu. Vivyo hivyo kwa anayefanya ria na kutafuta umaarufu hana katika amali yake isipokuwa kuzungumzwa na watu wala hana thawabu akhera." (Hii sio hadithi lakini ni maneno ya wenye hekima).*

Allah تعالیٰ Aliyetukuka zaidi Anasema:

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِن عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَنْثُورًا ﴿٢٣﴾

***"Na Tutayaendea yale waliyo yatenda katika vitendo vyao, Tuvifanye kama mavumbi yaliyo tawanyika." (25:23)***

Yaani matendo waliyoyafanya kwa ajili ya asiye Allah Mtukuka thawabu zake zitabatilika na zitakuwa kama vile chembe chembe za vumbi zilizotawanyika kama zinavyoonekana katika miale ya jua. 'Adi bin Hatim Twai رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« يؤمر بفتام - أي جماعات - من الناس يوم القيامة إلى الجنة حتى إذا دنوا منها واستنشقوا رائحتها ، ونظروا إلى قصورها وإلى ما أعد الله لأهلها فيها ، نودوا أن اصرفوهم عنها فإنهم لا نصيب لهم فيها فيرجعون بحسرة وندامة ما رجع الأولون والآخرين بمثلها ، فيقولون: ربنا لو أدخلتنا النار قبل أن ترينا ما أُرِيتنا من ثواب ما أعددت لأولائك كان أهون علينا . فيقول الله تعالى: ذلك ما أردت بكم كتمتم إذا خلوتم بارزتموني بالعظائم، وإذا لقيتم الناس لقيتموهم مخبتين تراءون الناس باعمالكم حلاف ما تعطوني من فلو بكم هبتم الناس ولم تهابوني وأجللتم الناس ولم تجلونني ، وتركتم للناس ولم تتركوا لي - يعني لأجل الناس - فالיום أذيقكم أليم عقابي مع ما حرمتكم من جزيل ثوابي »

*"Siku ya kufufuliwa vikundi vya watu vitaongozwa katika bustani, ambayo watakapoikaribia na kunusa harufu yake, na kuona kasri zake na yote aliyowatayarishia Allah wakazi wake, hapo tena amri*



itatolewa kuwatoa pale kwani hawana nafasi humo tena na wao watarejea wakiwa katika hali ya huzuni kubwa na majuto ambayo hawajawahi kuwa nayo waliotangulia au wajao mfano wake, na wao watasema: “Bwana wetu ingekuwa nafuu kwetu ungetutia motoni kabla hujatuonesha zawadi uliyowatayarishia marafiki zako. Hapo tena Allah Mtukuka atasema: “Yale niliyakusudia juu yenu nyiye, lakini kisiri mlikuwa jeuri kwangu, pindi mnapokuwa kati ya marafiki zenu mlividhalilisha na kuwanyenyeka wao tofauti na mlivyonifanyia Mimi na kunipa kutoka katika nyoyo zenu, mkawapa watu na kutonipa na mkawanyenyeka na hamkuninyenyeka Mimi, na mkawaachia watu na hamkuniwachia Mimi (yaani kwa ajili yao hao watu) leo hii Nitawaonjesheni adhabu kubwa pamoja na yale Niliyowanyima miongoni na thawabu nyingi.” (Hadithi dhaifu: Ameipokea Tabarani katika Al-Awsat 5478, Al-Kabiir 17/85 na 86, Al-Mundhiri ameitaja katika At-Targhiibwa Tarhiibkwa lafdhi Aliiopokea, Hadithi ni dhaifu uk 1).

Mtu mmoja alimuuliza Mtume ﷺ juu ya kuokoka. Mtume ﷺ alijibu:

« أن لا تخادع الله »

“Usimhadae Allah”

Mtu huyo akauliza tena. “Vipi itakuwa mtu atajaribu kumdanganya Allah?” Mtukufu Mtume ﷺ alijibu:

« أن تعمل عملاً أمرك الله ورسوله به وتريد به غير وجه الله . واتق الرياء فإنه الشرك الأصغر ، وإن المرائي ينادى عليه يوم القيامة على رؤوس الخلائق بأربعة أسماء : يا مرائي ، يا غادر ، يا فاجر ، يا خاسر ضل عملك وبطل أجرك ، فلا أجر لك عندنا ، اذهب فخذ أجرك ممن كنت تعمل له يا مسخادع »

## Al - Kabair

---

*“Ni kufanya amali aliyokuamrisha Allah na Mjumbe wake ﷺ ukataka njia isio ya Allah, epukana Ria kwani hiyo ni shirki ndogo, na mwenye kujionesha ataitwa siku ya kiama mbele za watu kwa majina manne: Ewe mwenye kujionesha. Ewe mdanganyifu. Ewe muovu: Ewe mwenye hasara, matendo yako yamepotea na ujira wako umebatilika, huna ujira kwetu, ondoka, nenda ukachukue ujira wako kwa uliyekuwa ukimfanyia kazi ewe mdanganyifu.”<sup>5</sup>*

Baadhi ya watu wenye hekima (Allah awarehemu) waliulizwa:

“Ni nani hakika ni mkweli (Kwa Allah)?” Akajibu: “Ni yule asiyependa kusifiwa na watu.”

Na Fudhail bin ‘Iyyadh alisema:

“Kujizuia kufanya amali kwa ajili ya watu, na kufanya amali kwa ajili ya watu ni ushirikina, na Ikhlaas ni kupata himaya ya Allah dhidi ya hayo mawili”. Ewe Allah tulinde na utusamehe.

\*\*\*

---

<sup>5</sup> Dhaifu: Haafidh Iraaqi amesema katika Takhriijil-Ai-Ihyaa: Ameipokea Ibn Abi Dunya kwa riwaya ya Jabalah Yahswabi kutoka kwa swahaba ambae hakumtaja, na isinadi yake ni dhaifu).

DHAMBI KUBWA YA PILI

KUUA NAFSI

Allah Mtukuka Amesema:

وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُتَعَمِدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَلَعَنَهُ وَأَعَدَّ لَهُ عَذَابًا عَظِيمًا ﴿٩٣﴾

*"Na mwenye kumuwa Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu humo atadumu, na Mwenyezi Mungu amemkasirikia, na amemlaani, na amemuandalia adhabu kubwa." (4:93) Na,*

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُونَ<sup>٤</sup> وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَامًا ﴿٩٤﴾ يُضَاعَفْ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَيَخْلُدْ فِيهِ مُهَانًا ﴿٩٥﴾ إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا فَأُولَئِكَ يُبَدِّلُ اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ<sup>٥</sup> وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٩٦﴾

*"Na ambao hawaombi mungu mwengine pamoja na Allah, wala hawau nafsi aliyo iharimisha Allah isipo kuwa kwa haki, wala hawazini-na atakaye fanya hayo atapata madhara. Atazidishiwa adhabu Siku ya Kiyama, na atadumu humo kwa kufedheheka. Ila kuwa atakaye tubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu." (25:68-69) Na,*

مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُمْ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا

**“Kwa sababu ya hayo Tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote”. (5:32). Na,**

وَإِذَا أَلْمَوْهُ دُدَّةٌ سِيلَتْ ﴿٥٣﴾ بِأَيِّ ذَنْبٍ قُتِلَتْ ﴿٥٢﴾

**“ Na msichana aliye zikwa hai atapo ulizwa. Kwa kosa gani aliuliwa? ” (81:8-9)**

Mtume ﷺ amesema: “ Epukeni mambo saba yenye kuangamiza.”

Akataja kati ya hayo saba ni kuuwa kiumbe ambacho Allah ﷻ amekataza kukiua bila sababu ya haki maalum.”

Mtu mmoja alimuuliza Mjumbe wa Allah ﷻ: “ Ni dhambi gani kubwa mbele ya Allah Mtukuka?”

Na Mtume ﷺ akajibu: “ Ni kumjaalia Allah mshirika hali ya kuwa amekuumba.”

Akauliza: ‘Kisha lipi?’ Akasema: “ Ni kumuua mwanao kwa kuogopa kuwa atakula pamoja nawe.”

Kisha jingine lipi? Akasema: “ Ni kuzini na mke wa jirani yako.”

Allah Mtukuka akateremsha aya kuthibitisha hayo kwa kusema:

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ  
وَلَا يَزْنُونَ<sup>٤</sup>

**“ Na wale wasio mwomba mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawau nafsi aliyo iharimisha Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa haki, wala hawazini...” (25:68)**

## Al-Kabair

---

Mtume ﷺ alisema:

وقال ﷺ: «إذا التقى المسلمان بسيفيهما فالقاتل والمقتول في النار، قيل: يا رسول الله! هذا القاتل! فما بال المقتول؟! قال: إنه كان حريصاً على قتل صاحبه»<sup>(٦)</sup>.

*“Wakati waislamu wawili watakapopambana kwa panga, yule anayeua na yule anayeuawa wote watakwenda Jahannam.”*  
“Alipoulizwa: ‘Ewe Mjumbe wa Allah yule ni muuaji lakini kosa gani la aliyeuliwa?’ Alijibu: *“Ni kwa sababu alikuwa na pupa ya kumuua mwenzake.”* (Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/43, 51 na Al-Bukhari 31, 6875 na Muslim 2888 kutoka kwa Abi Bakrah).

Imam Abu Sulayman رحمه الله تعالى amesema: Jambo hili linakuwa hivyo ikiwa hawatauana kwa sababu ya kutofahamiana, lakini wanapigana na kuuwana kwa uadui wao, kugombana kwa ajili ya koo zao, au kwa malengo ya kutafuta dunia, au uongozi au ukuu. Ama akiwa mtu anapigana na watu wanaofanya uasi katika hali ambayo inafaa kupigana nao, au kujilinda yeye binafsi au kumlinda mke wake au dada yake, hayo hayaingii katika hukumu hii. Kwa sababu katika hali hiyo ameamrisha kupigana ili ajilinde nafsi yake hokusudii kumuua yule sahiibu yake hadi itakapopambanuka kuwa sahiibu yake anataka kumuua. Na atakayepigana na muasi katika Waislamu au mkata njia (wanyang’anyi njiani) mtu huyu sio makusudio yake kujali kuuwa, bali anajilinda mwenyewe, na mtu yule akiachana naye anatakiwa amuache wala asimfuatilie. Kwani Hadithi haijaja kwa wenye sifa hii. Ama ambaye anakwenda kinyume na sifa hii anaingia katika Hadithi hii tuliyoitaja, na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

وقال ﷺ<sup>(٦)</sup>: «لا ترجعوا بعدي كفاراً يضرب بعضكم رقاب بعض»

*“Msirejee katika ukafiri mkaanza kukatana vichwa (kuuwana).”<sup>6</sup>*

---

<sup>6</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/85, 87, Al-Bukhari 6166-6868-7077, Muslim 66 kutoka kwa Ibn ‘Umar.

## Al - Kabair

---

Pia Mtume ﷺ amesema:

« لا يزال العبد في فسحة من دينه ما لم يصب دما حراما »

*" Muumini ataendelea kuwa na nafasi katika dini, muda wa kuwa hajamwaga damu ambayo ni haramu kuimwaga."*<sup>7</sup>

Na: *"Umwagaji wa damu ndio litakuwa suala la kwanza ambalo hukumu itatolewa siku ya kufufuliwa."*<sup>8</sup>

Katika Hadithi nyingine Mtume ﷺ amesema:

« لقتل مؤمن أعظم عند الله من زوال الدنيا »

*" Kumuuu muumini ni jambo kubwa kwa Allah kuliko kumalizika kwa dunia."*<sup>9</sup> Na:

« الكبائر الإشراف بالله وقتل النفس واليمين الغموس »

*" Madhambi makubwa ni kumshirikisha Allah na kuuu nafsi na kiapo cha uwongo."*<sup>10</sup> Na,

« لا تقتل نفس ظلما إلا كان على ابن آدم الأول كفل من دمها لأنه أول من سن القتل »

*" Hauwawi nafsi kwa dhuluma isipokuwa itakuwa damu yake hiyo juu ya dhamana ya mtoto wa Adamu wa kwanza kwa sababu yeye ndiye aliyeanzisha jambo hilo."*<sup>11</sup> Na,

---

<sup>7</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6862, 6863, Abu Dawud 4686 na At-Tirmidhi 2193 kutoka kwa Ibn 'Umar.

<sup>8</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/442, Al-Bukhari 6864-6533, Muslim 1678 kutoka kwa Ibn 'Umar.

<sup>9</sup> Sahihi: Imepokewa na At-Tirmidhi 1395, An-Nasai 7/82 Ghayatu Al-Maraam 439 kutoka kwa Ibn 'Umar.

<sup>10</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6870 na At-Tirmidhi 3024 kutoka kwa Ibn 'Amr.

<sup>11</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 3335 na Muslim 1677 kutoka kwa Ibn Mas-'uud.

« من قتل معاهدا لم يرح رائحة الجنة ، وإن رائحتها لتوجد من مسيرة أربعين عاماً »

*“Mwenye kumuua Mu’ahid hatopata harufu ya peponi, na kwa hakika harufu ya pepo hupatikana mwendo wa miaka arobaini.”<sup>12</sup>*

Ikiwa kuuu mu’ahid (Myahudi na mnasara aliye na mkataba) hairuhusiwi katika Darul Islaam – iweje sasa mtu kumuua Muislamu mwenzake?, Na amesema:

« ألا من قتل نفسا معاهدة لها ذمة الله وذمة رسوله فقد أخفر ذمة الله ولا يرح رائحة الجنة وإن ريحها ليوجد من مسيرة خمسين خريقاً »،

*“Tahadharini! Mwenye kumuua mu’ahid mwenye dhima ya Allah na dhima ya Mjumbe wake, hakika amefukia dhima ya Allah, wala hatopata harufu ya pepo na hakika harufu yake hupatikana mwendo wa miaka hamsini.”<sup>13</sup>*

Kwa mujibu wa At-Tirmidhi ni sahihi, na sehemu nyingine Mtume ﷺ amesema:

« من أعان على قتل مسلم بشطر كلمة لقي الله مكتوباً بين عينيه آيس من رحمة الله تعالى »

*“Atakayemsaidia mtu kumuua muislamu hata kwa mchango wa kauli tu, basi mtu huyo atakabiliana na Allahakiwa ameandikwa baina ya macho yake (usoni) maneno ya kukatisha tamaa kupata rehema za Allah.”<sup>14</sup>*

---

<sup>12</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/186 na Al-Bukhari 3166 kutoka kwa Ibn ‘Amr.

<sup>13</sup> Sahihi: Imepokewa na At-Tirmidhi 1403, Ibn Majah 2687 na kusahihishwa na Al-Albani katika sahihi At-Tirmidhi na Ibn Majah 2175 sahihi Al-Jami’.

<sup>14</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na Ibn Majah 2620, Al-Baihaqi 8/22 na Al-Albani ameidhoofisha katika kitabu chake, “Adh-Dwaifah 553

Kutoka kwa Mu'awiyah رضي الله عنه amesema: Amesema Mtume wa Allah:

وعن معاوية [قال] <sup>(٢)</sup>: سمعت رسول الله ﷺ يقول: «كلُّ ذنب عسى الله أن يغفره، إلا الرجلُ يموتُ كافراً، أو الرجلُ يقتلُ مؤمناً متعمداً» أخرجه النسائي <sup>(٣)</sup>.

*“Allah Husamehe madhambi yote ya mtu, isipokuwa mtu anayekufa hali ya kuwa kafiri au mtu aliyemuua muumini kwa makusudi.”<sup>15</sup>*  
Tunamuomba Allah msamaha.

\*\*\*

---

<sup>15</sup> Sahihi: Abu Dawud 4270, Ibn Hibaan 5980, Al-Hakim 4/ 351 na sahihi Al-Jami' 2524 na imesahihishwa na Shaikh katika Ghayatul Maraam 441 kutoka kwa Ibn 'Umar.



## DHAMBI KUBWA YA TATU

### KUHUSU UCHAWI

Kwa sababu mchawi ni lazima akufuru. Allah Ta'ala amesema:

وَلَيْكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ

**“...bali mashet’ani ndio walio kufuru, wakiwafundisha watu uchawi....” (2:102)**

Na shetani mlaaniwa hana lengo lolote la kumfundisha mwanadamu uchawi ila tu apate kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Allah Amesema kuhusu Haruti na Maruti:

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ ۗ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ ۗ وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ ۗ وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلْقٍ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْا بِهِ أَنْفُسَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٢﴾

**“...Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru. Wakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe. Wala hawawezi kumdhuru mtu ila kwa kutaka Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza yatayo wadhuru wala hayawanufaishi. Na hakika wanajua kwamba aliye khiari haya hatakuwa na fungu lolote katika Akhera. Na hakika ni kiovu mno walicho jiuzia nafsi zao laiti wangelijua.” (2:102)**

Tunawaona watu wengi waliopotea wakiingia katika kujifunza uchawi na hali wakijua kuwa hilo ni jambo la haramu, lakini hawajui kuwa ni jambo la ukafiri. Hujifunza namna ya kufanya mazingaombwe (kiini

## Al - Kabair

---

macho) nayo ni uchawi wenyewe, kumfunga mtu na mkewe ni aina ya uchawi, mtu kumpenda mwanamke au kumchukia ni uchawi. Vile vile na mfano wa hayo kwa kutumia maneno yasiyofahamika na mengi ya hayo ni ushirikina na upotofu.

Adhabu ya mchawi ni kuuwawa, kwani huko ni kumkufuru Allah ﷻ na kusambaza ukafiri. Mtume ﷺ amesema:

« اجتنبوا السبع الموبقات »

*“Epukeni mambo saba yenye kuangamiza.”*

Na kati ya hayo kulitajwa uchawi kulitajwa kuwa ni katika madhambi.<sup>16</sup> Yenye kuangamiza. Hivyo inampasa mtu amuogope bwana wake na asijiingize katika mambo ambayo yatamtia hasara duniani na akhera. Imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

« حد الساحر ضربة بالسيف »

*“Adhabu ya mchawi ni kukatwa na upanga.”<sup>17</sup>*

Na kilicho sahihi ni kauli ya Jundub.

Kutoka kwa Bajalah ibn ‘Ubdah kuwa amesema: tumepokea amri ya kimaandishi kutoka kwa ‘Umar ibn al Khatwab رضي الله عنه kabla ya kifo chake kwa mwaka mmoja kuwa,

*“Waueni wachawi wa kike na wa kiume.”<sup>18</sup>*

---

<sup>16</sup> Hadithi dhaifu marfuu’, maelezo yake yametangulia

<sup>17</sup> Sahihi ikiwa ni Mawquuf’: Imepokewa na At-Tirmidhi, Ad-Daraqutni 3/114, na imedhoofishwa na Al-Albani katika Adh-Dwa’ifa 1446 na imesahihishwa na Shaikh katika Waqfu wake na ana maelezo mazuri yarejee hayo kwani ni muhimu.

<sup>18</sup> Sahihi: Imesahihishwa na Al-Albani katika sahihi Abu Dawud 2624 na Ahmad 1/190.

## Al- Kabair

---

Kutoka kwa Wahb bin Munabih amesema: Nimesoma baadhi ya vitabu: Allah anasema:

« لا إله إلا أنا ليس مني من سحر ولا من سحر له ، ولا من تكهن  
ولا من تكهن له ، ولا من تطير ولا من تطير له »

*"Hakuna Mungu asiyekuwa Mimi, sina uchawi wala aliyefanyiwa uchawi, wala kilichofanya au kilichofanyiwa ukuhani, wala kilichofanyiwa mkosi au kuwa na mkosi."*<sup>19</sup>

'Ali ibn Abi Talib رضي الله عنه amesema: Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« ثلاثة لا يدخلون الجنة : مدمن خمر ، وقاطع رحم ، ومصديق بالسحر »

*"Watu wa aina tatu hawatoingia peponi: wanywa pombe, wanaovunja uhusiano wa familia na jamaa zao, na wanaosadiki uchawi."* (Ahmad katika Musnad yake)<sup>20</sup>

'Abdullah ibn Masuud رضي الله عنهما katika Hadithi iliyokuwa marfuu' amesema:

« الرقى والتمايم والتولة شرك »

*" Zinguo (Ruqya) na Tiwala ni shirki."*<sup>21</sup>

*Tamatim* ni wingi wa *Tamima* na hiyo ni hirizi wanazojivalisha wajinga pamoja na watoto wao na vipando vyao wakidai kuwa vinarudisha kijicho. Na haya ni katika matendo ya kijahilia, na anayeamini hayo atakuwa amemshirikisha Allah. *Tiwala* ni aina ya uchawi nayo ni

---

<sup>19</sup> Sahihi: Imepokewa na At-Tabarani 4262 kwa tamko 'Si katika sisi anayeangalia mkosi' sahihi Al-Jami' 5435 kutoka kwa 'Imraan.

<sup>20</sup> Dhaifu: Imepokewa na Ahmad 4/399, Ibn Hibaan 5346 dhaifu Al-Jami' 2597 kutoka kwa Abu Musa Al-Ash'ari.

<sup>21</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/381, Abu Dawud 3883, Ibn Majah 3530 na sahihi Al-Jami' 1632.

## Al - Kabair

---

kumfanya mwanamke ampende mume wake, na kuyafanya haya ni miongoni mwa shirki. Na wajinga huamini kuwa hilo huathiri tofauti na alivyokadiria Allah.

Al-Khatwabi Allah amrehemu amesema: “*Ruqya* ikiwa kwa Qur’an au majina matukufu ya Allah inakubalika, kwa sababu Mtume ﷺ alikuwa akimfanyia *Ruqya* Al-Hasan na Al-Husain na akisema:

*“Kwa maneno yaliyokamilika ya Allah nakutieni katika Himaya Yake dhidi ya kila shetani mdanganyifu na kwa kila jicho lenye husuda.”<sup>22a</sup>*

Kwa Allah tunataka Kwake msaada na Kwake tunamtegemea.

\*\*\*

---

<sup>22a</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 3371, Abu Dawud 4737, At-Tirmidhi 2060 kutoka kwa Ibn ‘Abass

## DHAMBI KUBWA YA NNE

### KUACHA SWALA

Allah تعالی Mtukuka Amesema:

﴿ خَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ أَضَاعُوا الصَّلَاةَ وَاتَّبَعُوا الشَّهْوَاتِ فَسُوفَ يَلْقَوْنَ غِيًّا ﴾

﴿ إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ﴾

***"Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Swala, na wakafuata matamania. Basi watakuja kuta malipo ya ubaya. Isipo kuwa walio tubu, wakaamini, na wakatenda mema..." (19:59-60)***

Ibn 'Abbas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ amesema: "Maana ya kuacha Swala hapa sio kuwa wameacha moja kwa moja, lakini wamechelewesha nyakati zake."<sup>22b</sup> Said bin Musayyab, Imamu wa Tabiina Allah amrehemu amesema: "Ni anayecheleweshwa Swala ya aduhuri hadi ikaingia wakati wa Swala ya Alasiri na haswali Alasiri hadi wakati wa Swala ya Magharibi na haswali Swala ya Isha ila wakati wa Swala ya Alfajiri na haiswali Alfajiri isipokuwa baada ya kuchomoza jua. Yeyote afanyaye hivyo bila ya kutubu na akaendelea kufanya hivyo, Allah تعالی amemuahidi *Baghyun* nalo ni bonde la Jahannam ambalo ni refu sana na ladha yake ni mbaya."

Allah تعالی Mtukuka Anasema:

﴿ فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴾

***"Basi, ole wao wanao swali, ambao wanapuuzwa Swala zao." (107:4-5)***

---

<sup>22b</sup> Imepokewa na Ibn Jariir 16/75.

## Al - Kabair

---

Yaani wenye kughafilika, wenye kudharau na kupuuzia. Sa'ad bin Abi Waqqaas amesema: Nilimuuliza Mjumbe wa Allah تعالی maana ya **“wale wenye kusahau Swala zao”** akanijibu:

« هو تأخير الوقت »

*“ Ni kuchelewesha wakati ”.*<sup>23</sup>

Yaani kuchelewesha Swala katika wakati wake uliopangwa, aliwaita kwa jina la wenye kuswali lakini wamepuuzia na wakachelewesha hadi mwisho wa wakati wake, Allah تعالی amewaahidi adhabu kubwa. Baadhi yao wanasema kuwa *Baghyun* ni bonde lipo huko Jahannam, lau milima yote ya ulimwengu yakiwekwa basi zitayeyuka kwa joto lake kubwa lilivyo, nayo ni makazi kwa anayepuuzia Swala na kuchelewesha ila yule aliyetubia na kujutia.

Allah تعالی Mtukuka Anasema katika aya nyingine:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُمْ ءَمْوَالُكُمْ وَلَا ءَوْلَادُكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ ؕ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ  
فَأُولَئِكَ هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٦٣﴾

**“Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio walio khasiri.” (63:9)**

Wafasiri wamesema: muradi wa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ‘*DhikruLlilah*’ hapa ni kutekeleza Swala tano (za kila siku). Yeyote mwenye kushughulikia mali yake kwa kuuza na kununua tu au kujishughulisha kupata rizki ya kila siku au na watoto wake tu, hata hapati wakati wa kutekeleza wajibu wake wa Swala tano kwa wakati, basi ajue yu miongoni mwa waliopata hasara. Mtukufu Mtume ﷺ amesema hivi:

---

<sup>23</sup> Sahihi: Mawquuf Al-Baihaqi 2/214.

وروى همام، نبأنا قتادة، عن الحسن، عن حُرَيْثِ بْنِ قَبِيصَةَ، قال: حدثني أبو هريرة، قال: قال رسول الله ﷺ: «أول ما يُحاسبُ به العبدُ يومَ القيامةِ من عمله صلواتُهُ؛ فإنْ صلحتْ فقد أفلحَ وأنجحَ، وإنْ فسدتْ فقد خابَ وخسِرَ»<sup>(3)</sup> حسنه الترمذي.

*"La mwanzo kuhesabiwa juu ya mja siku ya kiyama ni Swala. Zikiwa sawa sawa, basi atafuzu mtihani huo, na kufanikiwa na pindi zikiwa pungufu ataanguka mtihani huo na atakuwa mtupu na katika hasara."*<sup>24</sup>

Allah Mtukuka anaelezea kuhusu wakazi wa Jahannam:

مَا سَلَكَكُمْ فِي سَقَرٍ ﴿٤٢﴾ قَالُوا لَمْ نَكُ مِنَ الْمُصَلِّينَ ﴿٤٣﴾ وَلَمْ نَكُ نَطْعِمُ  
الْمَسْكِينِ ﴿٤٤﴾ وَكُنَّا نَخُوضُ مَعَ الْخَائِضِينَ ﴿٤٥﴾ وَكُنَّا نَكْذِبُ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٤٦﴾  
حَتَّىٰ أَتَيْنَا الْيَقِينَ ﴿٤٧﴾

***"Ni nini kilicho kupelekeni Motoni? Waseme: Hatukuwa miongoni walio kuwa wakiswali. Wala hatukuwa tukiwalisha masikini. Na tulikuwa tukizama pamoja na walio zama katika maovu. Na tulikuwa tukiikanusha siku ya malipo. Mpaka yakini ilipo tufikia. Basi hautawafaa kitu uombezi wa waombezi."*** (74:42-47).

Mtukufu Mtume ﷺ amesema:

وقال ﷺ: «العهدُ الذي بيننا وبينهم الصلاة فمن تركها فقد كفر»

*"Tofauti baina yetu na wao wasioamini ni Swala, kwa hivyo atakayeiwacha Swala atahisabiwa ni kafiri."*<sup>25</sup>

<sup>24</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Shi'b 3016 na imesahihishwa na Al-Albani katika As-Silsila As-Swahiha 1358 kutoka kwa Abu Hurayra.

<sup>25</sup> Hadithi Hassan: Imepokewa na Ahmad 5/346, Ibn Majah, At-Tirmidh 2621 na Al-Albani anasema kuwa ni Hassan katika sahihi Al-Jami' 4022.

## Al - Kabair

---

Na akasema: وقال: «بين العبد وبين الشرك تركُ الصلاة»

*“Kati ya Muislamu na Mshirikina ni kuacha Swala.”<sup>26</sup>*

Amesema ﷺ katika Hadithi iliyopokewa na Al-Bukhari:

وقال ﷺ: «مَنْ فَاتَهُ صَلَاةُ الْعَصْرِ حَبِطَ عَمَلُهُ»

*“Atakayepitwa na Swala ya Alasiri basi matendo yake yote yameharibika.”<sup>27</sup>*

Katika sunan tunaona kuwa Mtume ﷺ amesema:

وعنه - صلى الله تعالى عليه وسلم - قال: «من ترك الصلاة متعمداً فقد برئت منه ذمة الله»<sup>(٤)</sup> قاله مكحول عن أبي ذر، ولم يدركه.

*“Atakayeacha Swala kwa kukusudia basi dhima ya Allah kwake imeondoka.”<sup>28</sup>*

Na akasema:

وقال ﷺ: «أُمِرْتُ أَنْ أَقَاتِلَ النَّاسَ حَتَّى يَشْهَرُوا»<sup>(١)</sup> أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ، وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ، فَإِذَا فَعَلُوا ذَلِكَ عَصَمُوا مِنِّي دِمَائِهِمْ وَأَمْوَالَهُمْ إِلَّا بِحَقِّ الْإِسْلَامِ، وَحَسَابُهُمْ عَلَى اللَّهِ»<sup>(٢)</sup> متفق عليه.

*“Nimeamrisha kuwapiga vita watu hadi wakubali na kukiri kuwa hakuna mungu isipokuwa Allah na wadumisha Swala na walipe Zaka. Na endapo wakifanya hayo, basi watakuwa wameweka maisha*

---

<sup>26</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 3/370 na Muslim 82 kutoka kwa Jaabir.

<sup>27</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/349 na Al-Bukhari 553 kutoka kwa Buraidah.

<sup>28</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/238 na At-Tabarani katika Al-Kabiir 20/117-233-234 sahihi At-Targhiib 568.



## Al - Kabair

---

*yao na mali yao katika amani kutoka kwangu, isipokuwa kwa haki ya Uislamu, na matokeo yao yapo kwa Allah."*<sup>29</sup>.

Na akasema:

الله تعالى عنهما-، عن النبي ﷺ أنه قال: «مَنْ لَمْ يَحْفَظْ عَلَى الصَّلَاةِ لَمْ يَكُنْ لَهُ نَوْرٌ وَلَا بَرَهَانٌ وَلَا نَجَاةٌ»<sup>(1)</sup>، وَكَانَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مَعَ قَارُونَ وَفِرْعَوْنَ وَهَامَانَ [وَأَبِي جَهْلٍ]<sup>(2)</sup> وَأَبِي بِنِ خَلْفٍ<sup>(3)</sup> لَيْسَ إِسْنَادُهُ بِذَلِكَ.

*"Atakayezihifadhi atakuwa na nuru na hoja na uokovu siku ya kiama, na yule asiyehifadhi hatokuwa na nuru wala hoja wala uokovu siku ya kiama, na mtu huyo siku ya kiama atakuwa pamoja na Firauni, Qarun, Hamana na Ubayy bin Khalaf."*<sup>30</sup>

'Umar رضي الله عنه amesema: 'Kwa hakika mtu hana nafasi katika Uislamu muda wa kuwa atapoteza Swala'.<sup>31</sup> Baadhi ya wanazuoni (Allah awarehemu) wamesema: 'Muacha Swala atafufuliwa pamoja na watu hao wanne, kwa sababu hushughulishwa dhidi ya Swala kwa mali yake au kwa ufalme au kwa wizara yake (utawala) au kwa biashara yake. Ikiwa atashughulishwa kwa mali yake basi atafufuliwa na Qarun, ikiwa ameshughulishwa na ufalme wake basi atafufuliwa na Firauni, endapo atashughulishwa na wizara yake basi yupo pamoja na Hamana. Na akiwa amewacha Swala kushughulikia biashara basi yupo na Ubayy bin Khalaf, mfanya biashara maarufu Makka ambaye alikuwa kafiri.' Imam Ahmad amepokea kutoka kwa Mu'adh bin Jabal رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

« من ترك صلاة مكتوبة متعمداً فقد برئت منه ذمة الله عز وجل »

*"Atakayeacha Swala ya Faradhi kwa kukusudia basi dhima ya Allah imemwepuka."*

---

<sup>29</sup> Sahihi: Al-Bukhari 25 na Muslim 22 kutoka kwa Ibn 'Umar.

<sup>30</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/169 na Ibn Hibaan katika 1467 na isnadi yake ni nzuri.

<sup>31</sup> Sahihi: Imepokewa na Malik katika Muwatwa 1/51 kutoka katika kitabu cha Twahara ikiwa ni *mawquuf*, na amesema Shaikh Al-Albani: isnadi yake ni sahihi ka sharti zao.

## Al - Kabair

---

Imepokewa na Al-Baihaqi kwa sanadi yake kuwa 'Umar bin Al-Khatwab رضي الله عنه alisema: 'Ewe Mtume wa Allah! matendo gani yenye kupendwa na Allah katika Uislamu?'

Mtume ﷺ alijibu:

« الصلاة لوقتها ، ومن ترك الصلاة فلا دين له ، والصلاة عماد الدين »

*"Swala kwa nyakati zake. Yeyote asiyeswali hana Dini, Swala ndio nguzo ya Dini."*<sup>32</sup>

Baada ya 'Umar رضي الله عنه kuchomwa kisu aliambiwa *As-Swalat*, ewe Amiri wa waumini, 'Umar رضي الله عنه akasema: Ndio, kwa hakika anayekosa Swala hana fungu lolote ndani ya Uislamu, na hapo tena aliendelea kuswali na huku jeraha lake likivuja damu.

'Abdullah bin Shaqiq Ta'bi رضي الله عنه alisema: "Masahaba hawakuona kitu katika amali katika Uislamu ambayo mtu akiiacha atakuwa kafiri zaidi ya Swala."<sup>33</sup>

Wakati 'Ali رضي الله عنه alipoulizwa kuhusu mwanamke asiyeswali alijibu: 'Asiyeswali ni Kafiri.'<sup>34</sup> Na Ibn Masuud alisema: 'Kuwa asiyeswali hana dini.'<sup>35</sup> na ibn 'Abbas alisema: 'Yeyote anayeacha Swala japo moja kwa makusudi, basi atakutana na Allah akiwa amemkasirikia.' Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

---

<sup>32</sup> Dhwaifu: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 2550 na kudhoofishwa na Al-Albani katika dhaiful Al-Jami' 170.

<sup>33</sup> Imepokewa na At-Tirmidhi 2622, Al-Hakim katika Al-Mustadrak 1/7 na kusahihishwa na Al-Albani katika sahihi At-Targhiib 564.

<sup>34</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Abi Shayba marfu' kwa tamshi 'Amekufuru' angalia Sahihi At-Targhiib uk 230.

<sup>35</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Abi Shayba katika Al-Iman 2/184 na akasema Al-Albani katika sanad yake: nzuri.

## Al- Kabair

---

*" Atakayekutana na Allah hali ya kuwa kapuuza Swala basi Allah hatoangalia mema yake mengine madamu amepuuza Swala."*

Ibn Hazm alisema hakuna dhambi kubwa baada ya shirki kama kuchelewesha Swala kwa wakati wake, na kumuua muumini bila ya haki.

Ibrahim Nakhi' alisema: "Anayeacha Swala amekufuru." Na Ayuub As-Sakhastani amenena mfano wa hayo. Ama 'Awn bin 'Abdullah amesema: "Mtu anapoinzwa katika kaburi lake jambo la kwanza ambalo ataulizwa ni kuhusu Swala yake, ikifaulu basi yataaangaliwa matendo yake mengine na isipofaulu hatoulizwa kuhusu matendo yake mengine". Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

*" Mtu yeyote akitekeleza Swala yake katika muda wake wa mwanzo Swala yake hiyo hupanda mbinguni kama mwanga wa nuru hadi kufikia 'arshi ya Allah na hapo tena Swala hiyo humuombea msamaha yule mtu aliyeiswali Swala hiyo hadi siku ya kufufuliwa na husema: Allah akuhifadhi kama ulivyonihifadhi. Lakini mtu akiswali Swala siyo katika wakati usio wake, yaani akiichelewesha, Swala hiyo hupanda mbinguni na huku imefunikwa na kiza, ikifika huko mbinguni hukunjwa kama inavyokunjwa nguo na hutupiwa nayo usoni mwenye Swala hiyo na husema: "Inshallah Allah akupoteze wewe kama ulivyonipoteza mimi." <sup>36</sup>*

Imepokewa kutoka kwa Abu Dawud katika Sunna yake kuwa 'Abdallah bin 'Amru bin Al-'As رضى الله عنه amesema: Mtume wa Allah ﷺ alisema: " Watatu Allah hakubali Swala zao. Mwenye kuongoza watu huku wanamchukia, Mwenye kumfanya mtu huru kuwa mtumwa, na mwenye kujia Swala mwishoni" <sup>37</sup>

---

<sup>36</sup> Hadithi Dhaifu: Al-Baihaqi katika Ash-Shi'ib 2871 kisha angalia Dhwaifu Al-Jami' 400.

<sup>37</sup> Hadithi Dhaifu: Abu Dawud 593, Ibn Majah 970 na imedhoofishwa na Shaikh katika Dhwaif Al-Jami' 119.

## Al - Kabair

---

Imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ tena amesema:

*"Mwenye kukusanya Swala mbili pamoja bila ya sababu huingia mlango wa wale waliotenda matendo maovu makubwa."*<sup>38</sup>

Tunamuomba Allah ﷻ muongozo na msaada kwani hakika Yeye ﷻ ni Mkarimu na Mwenye Rehema, Mkubwa kushinda wote.

\*\*\*

---

<sup>38</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na At-Tirmidhi 188, Al-Hakam 1/275 na kudhoofishwa na Ash-Shaikh katika dhaifu Al-Jami' 2556 kutoka kwa Ibn 'Abbas.

## MUDA UPASAO KUMUAMURU MTOTO KUSWALI

Imepokewa na Abu Dawud رَضِيَ اللهُ عَنْهُ katika Sunan kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

«مروا أولادكم بالصلاة وهم أبناء سبع واضربوهم عليها وهم أبناء عشر وفرقوا بينهم في المضاجع»

*“ Waamrisheni watoto wenu kuanza kuswali wanapofikia umri wa miaka saba na wachapeni endapo hawaswali wanapofikia umri wa miaka kumi na muwatenganishe katika kulala.”<sup>39</sup>*

Na katika riwaya:

« مروا الصبي بالصلاة إذا بلغ سبع سنين ، فإذا بلغ عشر سنين فاضربوه عليها »

*“ Waamrisheni watoto wenu kuswali wakiwa na umri wa miaka saba na wachapeni kama hawakuswali wakiwa na umri wa miaka kumi.”<sup>40</sup>*

Imam Abu Sulayman Al-Khattabi رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى amesema: “Hadithi hii inamaanisha kuwa adhabu itolewe kwa yule asiyeswali ikiwa ameshabaleghe.

Ilikuwa baadhi ya wafuasi wa Imam Shafi رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى wanatolea hoja katika kupasa kuuawa akiwa mtu huyo ataiacha Swala kwa makusudi baada ya kubaleghe, na anasema: ikiwa mtoto anastahiki kupigwa kabla ya kubaleghe basi ni dalili ya kuwa anastahiki kwa mtu yule baada ya kubaleghe apate adhabu kali, na hakuna adhabu kali baada ya kupigwa bali ni kifo.

---

<sup>39</sup> Sahihi: Abu Dawud 494, At-Tirmidhi 407, sahihi Abu Dawud 508 na sahihi Al-Jami' 5867.

<sup>40</sup> Sahihi: Abu Dawud 495-496, Ahmad 2/187, Sahihi Abu Dawud 509, Sahihi Al-Jami' 5868.

### HUKUMU YA MWENYE KUACHA SWALA:

Zipo Khitilafu nyingi baina ya wanazuoni kuhusu hukumu ya mwenye kuacha Swala. Maimamu Shafi, Malik na Ahmad wamesema: 'Mwenye kuacha kuswali hukatwa kichwa chake kwa upanga. Kisha wakatofautiana kuhusu ukafiri wa mtu kama atakuwa ameacha bila udhuru hadi ukaondoka wakati wake, Ibrahim An-Nakhi' na Ayyub Sakhstiyani, 'Abdullah ibn Mubarak, Ahmad bin Hanbal na Ishaq bin Rahwaih wamesema: Huyo ni Kafiri. Na wakatolea dalili kauli yake Mtume ﷺ:

«العهد الذي بيننا وبينهم الصلاة ، فمن تركها فقد كفر»

*"Ahadi iliyo kati yetu na wao ni Swala, atakayeacha amekufuru."*

Na kauli yake:

« بين الرجل وبين الكفر ترك الصلاة »

*"Baina ya mtu na ukafiri ni kuacha Swala."*

### HALI NYINGINEZO

Imekuja katika Hadithi ya Mtume ﷺ kuwa:

"Allah تعالى Mtukuka atawabarikia vyeo vitano watu waliohifadhi Swala zao za faradhi, atamuondoshea ufukara na adhabu ya kaburi, atampa kitabu chake cha hesabu siku ya kiyama kwa mkono wa kulia, atamvusha daraja (*Sirat*) kama umeme, na ataingia peponi bila ya hesabu. Atakayepuuzwa basi Allah atamuadhibu adhabu kumi na nne, tano duniani na tatu anapokufa, na tatu kaburini na tatu zingine anapotoka kaburini. Adhabu za duniani: Kwanza: Huondolewa Baraka katika umri wake, Pili: Alama ya waja wema huondoshwa katika uso wake, Tatu: Kila amali anayofanya Allah hatampa ujira, Nne: Dua yake haitonyanyuliwa mbinguni, Tano: Hatopata fungu katika dua za waja

## Al- Kabair

---

wema. Ama adhabu zitakazomfika anapokufa, ni kuwa: Atakufa akiwa dhalili, Pili: Atakufa akiwa mwenye njaa, Tatu: Atakufa mwenye kiu hata akinyweshwa bahari ya dunia hatoishibisha kiu chake. Ama adhabu atakazopata kaburini, ya Kwanza: Kaburi lake litambana hadi mbavu zake ziachane, Pili: Kaburi litamuwashia moto akijigeuza katika vijiwe vya moto usiku na mchana, Tatu: Nyoka aina ya *Shuja' Al-Aqra'* atamtesa, macho yake ya moto na kucha zake za chuma, urefu wa kila ukucha ni mwendo wa siku nzima, atamwambia maiti: " *Mimi ni Shuja' Al-Aqra'* na sauti yake ni kama radi huku akisema: Mola wangu ameniamrisha nikupige kwa kuipoteza kwako Swala ya asubuhi, kuanzia asubuhi hadi jioni, na nikupige kwa kuipuuzia Swala yako ya aduhuri hadi Alasiri, na nikupige kwa Swala yako ya Alasiri hadi Magharibi na kwa Magharibi hadi Isha, na kuipuuzia Isha nitakupiga hadi Asubuhi, kila akimpiga kipigo hudidimia ndani ya ardhi kwa dhiraa sabini, ataendelea kuadhibiwa hivyo ardhini hadi ifike kiama. Ama ambaye ataadhibiwa atakapotoka kaburini katika kisimamo cha kiama ni ugumu wa hesabu, hasira za Mola wake na kuingizwa motoni."

Na katika riwaya nyingine:

« فإنه يأتي يوم القيامة وعلى وجهه ثلاثة أسطر مكتوبات . السطر الأول :  
يا مضيع حق الله ، السطر الثاني : يا مخصوصا بغضب الله ، السطر الثالث :  
كما ضيعت في الدنيا حق الله فأيس اليوم من رحمة الله »

*"Ataletwa siku ya kiama katika uso wake kuna mistari mitatu imeandikwa: Mstari wa Kwanza: Ewe uliyepoteza haki ya Allah, Mstari wa pili umeandikwa: Ewe mwenye uadui na ghadhabu ya Allah, na wa tatu umeandikwa: Kama ulivyopoteza haki ya Allah basi kata tamaa na rehema za Allah."*<sup>41</sup>

---

<sup>41</sup> Hadithi Maudhui: Imetajwa na Ibn Hajar Al-Haithami katika Az-Zawaid 1/136 kwa tamshi 'Wamesema baadhi yao.' Na akasema Adh-Dhahabi katika Al-Mizan 3/653 katika historia ya Muhammad bin 'Ali Al-'Abas Al-Baghdadi Al-'Atwar-amemsingizia 'Ali Abu Bakr bin Ziyaad An-Niisaburi hadithi batili kuhusu mwenye kuacha Swala.

## Al - Kabair

---

Kutoka kwa Ibn 'Abas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمamesema: "Siku ya kiama mtu ataletwa na kuwekwa mbele ya Allah kisha itaamrisha apelekwe motoni, atasema: 'Ewe Mola wangu, kwanini?' Allah Atasema: "Kwa kuchelewesha Swala katika wakati wake na kuniapia kwa uongo."<sup>42</sup>

Siku moja Mtume ﷺ aliwaambia sahaba zake:

« اللهم لا تدع فينا شقيا ولا محروما » .

*"Ewe Mola wetu usimuache katika sisi muovu wala aliyenyimwa."*

Kisha Mtume ﷺ akasema tena:

« أتدرون من الشقي المحروم ؟ »

*"Mnajua ni nani muovu aliyenyimwa?"*

Wakajibu: Ni nani huyo ewe Mtume wa Allah ﷺ akasema:

« تارك الصلاة »

*"Ni mwenye kuacha Swala."<sup>43</sup>*

Na imepokewa kuwa watu wengi siku ya kiama ambao nyuso zao zitakuwa nyeusi ni waacha Swala, na katika jahannamu kuna bonde liitwalo 'Al-Malham' ambamo kuna nyoka wengi, kila nyoka mmoja ana shingo kama ya ngamia, urefu wake ni mwendo wa mwezi mzima humdonoa mwenye kuacha kuswali na sumu ya nyoka yule itamchemsha mwili wake miaka sabini kisha mwili wake utaiva na ngozi kutoka.

---

<sup>42</sup> Az-Zawaajir 1/292.

<sup>43</sup> Sikuiona Hadithi hii, ingawaje mfano wa Hadithi hii ipo kwa Ahmad 4/191 kwa sanad dhaifu.



## KISA

Imesimuliwa kuwa mwanamke wa Bani Israil alikwenda kwa Mtume Mussa عليه السلام akasema: “Ewe Mjumbe wa Allah miye nimetenda dhambi kubwa sana, lakini baadaye nikatubia kwa Allah تعالى, hivyo niombe msamaha kwa Allah تعالى anisamehe madhambi yangu. Mtume Mussa عليه السلام akamuuliza: “Dhambi yako ni nini? Akamjibu: ‘Ewe Mtume wa Allah mie nilizini halafu nikazaa na nikamuua.’ Mtume Mussa عليه السلام akamwambia: “Ondoka hapa ewe mwanamke muovu, usije moto ukatushukia kutoka mbinguni ukatuunguza kwa maovu yako. Hapo mwanamke huyo alivunjika moyo kwa huzuni. Akateremka Jibril kwa Mussa na akamwambia: “Ewe Musa Allah anakuambia: ‘Kwa nini umemfukuza mwanamke aliyetubia? Kwani hujapata kumuona mtu mbaya zaidi kumshinda huyu? Musa akamuuliza Jibril: Je, kuna aliye mbaya kumshinda huyo mwanamke? Jibril akamjibu: ‘Yule anayewacha Swala kwa makusudi.’

## KISA KINGINE

Kutoka kwa baadhi ya *Salaf* ni kuwa mtu alifiwa na dada yake, akadondosha mfuko wenye mali katika kaburi lake lakini hakuhihi hilo. Kisha akaondoka na alipokumbuka baadae alikuja kaburini na kuchimba ili kuuangalia mfuko wake wakati huo watu walikwishaondoka. Alipochimba akaona kaburi likiwaka moto na akarudishia udongo haraka haraka na kurudi kwa mama yake huku akilia na akiwa mwenye huzuni na kusema: ‘Ewe mama yangu nijulishe alichokuwa akifanya dada yangu?’ Mama yake akauliza: ‘Swali lako lina maana gani?’ Akasema: ‘Nimeona kaburi lake likiwaka moto.’ Mama yake akalia na kusema: ‘Ewe mwanangu dada yako alikuwa akizembea Swala na kuchelewesha kuswali kwa wakati wake.’<sup>44</sup> Hii ndio hali ya mwenye kuchelewesha Swala kwa wakati wake, sasa itakuwaje hali ya yule ambaye haswali kabisa? Tunamuomba Allah atusaidie katika kuhifadhi Swala zetu kwa wakati wake kwa hakika Yeye ni Mkarimu Mkwasi.

---

<sup>44</sup> Kisa hiki kimetajwa na Ibn Al-Jawziy katika kitabu Al-Muqliq namba 39.

### MLANGO: ADHABU YA MWENYE KUDONOA SWALA

Miongoni mwa adhabu za mwenye kudonoa Swala na hakamilishi rukuu wala sujudi yake. Imepokewa katika tafsiri ya maneno ya Allah:

﴿فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ﴾ ﴿الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ﴾

**“Basi, ole wao wanao swali, Ambao wanapuuza Swala zao.”**  
**(107:4-5)**

Imethibiti katika sahihi mbili kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه: Kuwa mtu mmoja aliingia msikitini wakati Mjumbe wa Allah ﷺ akiwa amekaa humo ndani, (huyo mtu) akaswali kisha akaenda kumsalimia Mtume ﷺ,

Mjumbe wa Allah ﷺ akamjibu salamu yake na akamwambia:

«ارجع فصل فإنك لم تصل»

*“Karudie Swala yako, kwani hujaswali.”*

Akarudi na kuswali kwa mfumo ule ule. Akarejea kumuamkia Mtukufu Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akamjibu na kumuambia tena:

«ارجع فصل فإنك لم تصل»

*“Nenda ukarudie ile Swala yako tena kwani wewe hukuswali.”*

Kwa hiyo akarudi akaswali kama alivyoswali, kisha akaja akamsalimia Mtume ﷺ, Mtume ﷺ akamjibu, akasema:

«ارجع فصل فإنك لم تصل ثلاث مرات».

*“Nenda ukarudie ile Swala yako tena kwani wewe hukuswali.” Mara tatu*

## Al- Kabair

---

Akasema katika mara ya tatu: 'Naapa kwa ambaye amekutuma wewe kwa haki, siwezi kufanya vizuri zaidi ya hivyo, basi nifundishe'. Mtume ﷺ akasema:

« إذا قمت إلى الصلاة فكبر ، ثم اقرأ ما تيسر معك من القرآن ، ثم اركع حتى تطمئن راكعاً ، ثم ارفع حتى تطمئن قائماً ، ثم اسجد حتى تطمئن ساجداً ، ثم اجلس حتى تطمئن جالساً ، ثم اسجد حتى تطمئن ساجداً ، وافعل ذلك في صلاتك كلها »

*"Unaposimama kwa ajili ya Swala, sema Allahu Akbar, kisha soma unachoweza katika Qur'an, kisha rukuu utulie kwa rukuu, kisha inuka na usimame umenyooka, kisha usujudu na utulie umesujudu, kisha kaa utulie umekaa, kisha sujudu na utulie umesujudu" kwa muda kidogo na ufanye hivyo hivyo katika Swala yako yote.*"<sup>45</sup>

Imepokewa kutoka kwa Imam Ahmad kutoka kwa Al-Badriy رضي الله عنه amesema: Amesema Mtukufu Mtume ﷺ:

« لا تجزئ صلاة لا يقسم الرجل فيهما صلبه في الركوع والسجود »

*"Hakika hakuna Swala kwa yule asiyenyoosha uti wake wa mgongo katika Rukuu' na Sujud."* Imepokewa na Abu Dawud vile vile na At-Tirmidhi, na akasema: 'Hadithi Hassan Sahihi'.

Na katika riwaya nyingine:

*"Hadi anyooshe mgongo wake katika Rukuu' na Sujud."*<sup>46</sup>

Maelezo haya kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa mwenye kuswali na wala asinyooshe mgongo wake baada ya Rukuu na Sujud kama alivyokuwa

---

<sup>45</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 757, 6252 na Muslim 397.

<sup>46</sup> Imepokewa na Ahmad 4/119, Abu Dawud 855, Ibn Majah 870 na Sahihil Jami' 7224 na 7225.

## Al - Kabair

---

yeye Mtume ﷺ akifanya, basi Swala ya mtu huyo itakuwa ni batili, na hii ni katika Swala za faradhi na utulivu uoneshwe na viungo vyote vya mwili.

Imethibiti kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alisema:

*"Mwizi mkubwa zaidi ni ambaye anaiba Swala yake".*

Kukasemwa: 'Ni vipi mtu anaiba Swala yake?' Akajibu:

*"Hatimizi rukuu zake wala sijida zake, wala kisomo ndani yake".<sup>47</sup>*

Imepokewa na Imam Ahmad Hadithi kutoka kwa Abu Hurayra رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

*"Allah hamuangalii mtu ambaye hanyooshi mgongo wake katika Rukuu na Sujuud yake."<sup>48</sup>*

Na akasema:

*"Hiyo ni Swala ya mnafiki anangoja hadi pembe mbili za jua zinapotokeza ndio huamka na hudonoa mara nne hamtaji Allah ila kidogo tu"<sup>49</sup>.*

Kutoka kwa Abu Mussa رضي الله عنه amesema: 'Kuwa siku moja Mtukufu Mtume ﷺ aliswali pamoja na wafuasi wake na akakaa, mtu mmoja aliingia msikitini akaanza kuswali, na akawa anarukuu na kusujudu kwa haraka haraka, Mtume ﷺ akasema:

---

<sup>47</sup> Imepokewa na Ibn Hibbaan 1888, Al-Hakam 1/229, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 2847, Sahihi Al-Jami' 966, 987.

<sup>48</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/25 na sahihi At-Targhiib 532.

<sup>49</sup> Sahihi: Imepokewa na Malik 1/220 na Muslim 622.

## Al-Kabair

---

*"Mnaona lau atakufa, atakufa huyu katika hali yake hii, basi atakuwa amekufa katika mila isiyokuwa ya Muhammad. Anadonoa donoa ndani ya Swala yake kama kunguru anayedonoa damu."*

Ameipokea Abu Bakr bin Khuzaymah katika sahihi yake.<sup>50</sup> 'Umar bin Al-Khatwab رَضِيَ اللهُ عَنْهُ amesema; 'Mtume ﷺ amesema:

*" Hakuna mwenye kuswali ila amemiliki kuume kwake na kushoto kwake, akikamilisha itakwenda kwa Allah ikiwa hajakamilisha atapigwa nayo usoni mwake."<sup>51</sup> Imepokewa na Al-Baihaqi kwa sanad yake kutoka kwa 'Ubadah bin Samit رَضِيَ اللهُ عَنْهُ: kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema: " Mtu akitawadha sawa sawa na akasimama katika Swala na kusoma ndani ya Swala na kurukuu na kusujudu kwa unyenyekevu basi Swala inamwambia: Inshaa Allah, Allah akuhifadhi na kukutunza kama ulivyonitunza na kunihifadhi mimi, tena hupanda mbinguni kwa kutoa nuru na mwangaza na hufunguliwa milango ya mbinguni hadi inafika kwake mbele ya Allah Mtukuka na kumtetea na kumuomba kwa Allah, lakini akiripua tu kwa kurukuu na kusujudu kwa haraka wala kutosoma vizuri Qur'an tukufu basi Swala yake humuambia: "Allah Mtukuka akupoteze kama ulivyonipoteza mimi kisha hupanda mbinguni huku imezongwa na kiza na milango ya mbingu ikiwa imefungwa kisha hukunjwa na kufungwa kama inavyokunjwa kanzu na hufurumishwa usoni mwake."<sup>52</sup>*

Salman Al-Farsi amesema kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

*" Swala ina vipimo, yeyote akikamilisha hicho kipimo, basi atapewa zawadi yake ya kipimo hicho kamili, atakayepunja kipimo".*

---

<sup>50</sup> Sahihi: Ibn Khuzaimah 665, Al-Baihaqi 2/89 na Sahihi

<sup>51</sup> Hadithi Dhaifu: Ad-Daraqutni katika Al-Afraad na imedhoofishwa na Shaikh katika Dwaifu Al-Jami' 5226.

<sup>52</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na Al-Bazzar 1/177 namba 350, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 2871 na kudhoofishwa na Shaikh katika Dhaif Al-Jami' 400.

Allah Mtukuka Amesema:

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿٨٣﴾

**"Ole wao hao wapunjao!" (83:1)**

Na Mpunjaji ni mpunguzaji wa kipimo na mizani au dhira au Swala, Allah تعالى amewaahidi *Waylun* nayo ni bonde lililopo Jahannam, Jahannam inachukua maji yake kupunguza joto lake, tunaomba himaya ya Allah kwa hilo. Kutoka kwa Ibn 'Abbas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا kuwa Mtume ﷺ amesema:

*"Atakaposujudu mmoja wenu, basi aweke uso wake, pua yake mikono yake ardhini. Hakika Allah amenielekeza mie kuwa nisujudu kwa viungo saba; uso, viganja viwili, magoti mawili, na ncha za vidole vya miguu miwili (nyayo) na nisifunge nywele au nguo. Mtu akiswali na akawa hazipi sehemu zote hizo zilizotajwa haki zake basi kiungo katika viungo hivi vitamlaani hadi anapomaliza Swala yake."*<sup>53</sup>

Imepokewa na Al-Bukhari kutoka kwa Hudhaifa bin Al-Yamaan kuwa alimuona mtu akiswali bila kukamilisha Rukuu wala Sujuud zake, Hudhaifa akamwambia: 'Hukuswali na hata ukifa na wewe una swali namna hii, utakuwa umekufa katika isiyokuwa fitra ya Muhammad ﷺ.'<sup>54</sup>

Katika riwaya ya Abu Dawud amesema: Tokea muda gani unaswali swala hii? Akasema: 'Tokea miaka arubaini.' Akasema: 'Miaka arubaini yote hukuswali kitu, na kama utakufa katika hali hii utakuwa umekufa bila fitra ya Muhammad ﷺ.'<sup>55</sup>

Hassan Al-Basry alikuwa akisema: "Ewe mwanadamu utajifakharisha na kitu gani katika dini yako ikiwa unaipuuza Swala yako, na hicho ndicho

---

<sup>53</sup> Angalia Nailul Awtwaar 2/259.

<sup>54</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 791, 808, An-Nasai 3/58, Ibn Hibaan 1894 na Al-Baihaqi 2/118.

<sup>55</sup> Sahihi: Ibn Hibaan 1894, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 2860 na sio ambayo ipo kwa Abu Dawud.

## Al- Kabair

---

cha mwanzo utakachoulizwa siku ya kiyama kama Hadithi ya Mtume ilivyozungumza: “Jambo la mwanzo na kupimwa siku ya kiyama ni Swala yake, ikiwa iko sawa sawa, basi atafuzu, na ikiharibika basi atakuwa amefeli na kupata hasara, ikipungua katika Swala ya faradhi chochote Allah atasema: “Angalieni mja wangu je, ana Swala za sunna akamilishe kilichopungua katika faradhi, kisha hali hiyo itaendelea katika hali za amali zake zote.”<sup>56</sup> Kwa hali hii inabidi mtu aongeze Swala zake za sunna kwa wingi ili akamilishe kilichopungua katika faradhi.

\*\*\*

---

<sup>56</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/290, Abu Dawud 865, At-Tirmidhi 413, Sahihi Al-Jami’ 2568 kutoka kwa Abu Hurayrah.

**MLANGO: ADHABU YA KUACHA SWALA YA  
JAMA'A HALI INAWEZEKANA**

Allah Mtukuka amesema:

يَوْمَ يُكْشَفُ عَن سَائِرٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٤٢﴾ خَشِيعَةً أَبْصَرُهُمْ  
تَزَهَّقُهُمْ ذِلَّةً ۖ وَقَدْ كَانُوا يُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ وَهُمْ سَلِيمُونَ ﴿٤٣﴾

***“Siku utakapo wekwa wazi mudi, na wataitwa kusujudu, lakini hawataweza, Macho yao yatainama chini, fedheha itawafunika. Na hakika walikuwa wakiitwa wasujudu walipo kuwa wazima.” (Al - Qalam 68:42:43)***

Ibrahim At-Tamimi amesema: Yaani katika Swala ya faradhi kwa adhana na ikama.

Amesema Said bin Musayyab: “Walikuwa wakisikia: (Njooi katika Swala, njooi katika mafanikio) hawaitikii na wao ni watu waliojisalimisha.

Amesema Ka'ab Al-Ahbaar: Wallahi aya hizi ziliteremshwa kuhusu wale ambao hawajajiunga na Swala za jamaa. Ni onyo na kitisho kiasi gani kuliko hili kwa mwenye kuacha Swala ya jamaa wakati ana uwezo wa kufanya hivyo. Katika Sunna ambayo imethibiti katika sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

*“Niliingiwa na hima kuamrisha Swala ikimiwe kisha nimuamuru mtu aswalishe, kisha niondoke pamoja na watu wenye kuni kwa wale ambao hawahudhuria Swala katika jamaa, niunguze nyumba zao kwa moto.”<sup>57</sup>*

---

<sup>57</sup> Sahihi: Imepokewa na Malik 1/129-130, Al-Bukhari 644, 2420, Muslim 651 kutoka kwa Abu Hurayrah.



## Al- Kabair

---

Wala hahofishi kuunguza nyumba zao isipokuwa ni kwa kuacha wajibu licha ya vilivyo ndani ya nyumba hizo miongoni mwa mali na watoto.

Katika sahihi Muslim kuwa mtu mmoja kipofu alikwenda kwa Mtume ﷺ akasema: Ewe Mtume wa Allah sina mtu wa kuniongoza msikitini na akamuomba Mtume ampe ruhusa aswali nyumbani kwake, Mtume ﷺ akamruhusu lakini alipoondoka alimuita na kumuuliza:

*"Je, unasikia mwito wa Swala."*

Akasema: 'Ndio', akasema:

*"Basi itikia."*<sup>58</sup>

Na imepokewa na Abu Dawud kutoka kwa 'Amru bin Umri Maktuum kuwa alimuendea Mtume ﷺ akamwambia: 'Ewe Mtume wa Allah kwa hakika mji wa Madina una wanyama wengi wakali na mimi ni kipofu nataka mbali, na nina mtu anayeweza kuniongoza lakini hanifai, je, nitapata ruhusu ya kuswalia nyumbani?' Akasema:

« هل تسمع النداء؟ »

*"Je, unasikia mwito wa Swala?"*

Akasema: 'Ndiyo', Akasema:

« فأجب فإني لا أجد لك رخصة »

*"Basi itikia mwito kwani mimi siwezi kukupa ruhusa."*<sup>59</sup>

---

<sup>58</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 217 na An-Nasai 2/109.

<sup>59</sup> Sahihi: Imepokewa na Abu Dawud 553, An-Nasai 2/10, Ibn Abi Shayba 1/345,346 na sahihi At-Tirmidhi 427.

## Al - Kabair

---

Huyu ni mtu kipofu ambaye amelalamikia hali yake na mashaka ayapatayo anapokwenda msikitini na hana anayeweza kumuongoza kwenda msikitini, pamoja na hayo yote Mtume hakumpa ruhusa kuswali nyumbani kwake, sasa iweje mtu mwenye kuona amesalimika apate udhuru wa kuswali nyumbani kwake? Na ndio maana alipoulizwa Ibn 'Abass رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا kuhusu mtu anayefunga mchana na kusimama usiku na haswali katika jamaa?' Akasema: 'Akifa katika hili mtu huyu atakuwa ni mtu wa motoni.'<sup>60</sup>

Amesema Abu Hurayra رَضِيَ اللهُ عَنْهُ: 'Sikio la binadamu kujaa risasi iliyoyeyushwa ni bora kwake kuliko kusikia adhana kisha asijibu'<sup>61</sup>

Imepokewa na Ibn 'Abass رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا amesema: kuwa Mtume ﷺ amesema:

« من سمع المنادي بالصلاة فلم يمنعه من اتباعه عذر »

*"Mwenye kumsikia muadhini wa Swala na hana udhuru wa kwenda kuswali jamaa."*

Ikasemwa ni udhuru gani ewe Mtume wa Allah? Akasema:

« خوف أو مرض لم تقبل منه الصلاة التي صلى »

*"Ni khofu ya khatari au maradhi haitokubaliwa Swala yake." Yaani nyumbani kwake.<sup>62</sup>*

Imepokewa na Al-Hakam katika Mustadrak yake kutoka kwa Ibn 'Abbas vile vile amesema: kuwa Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>60</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na At-Tirmidhi 218 na dhaifu sunan At-Tirmidhi 36.

<sup>61</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na Ibn Abi Shayba 1/38/4 na sanad yake ni dhaifu.

<sup>62</sup> Sahihi: Imepokewa na Abu Dawud 551, Ibn Majah 793, Ibn Hibaan 2064 na kusahihishwa na Al-Albani katika dhwaifu Al-Jami' 5624 na kusahihishwa na Al-Albani bila ya tamshi 'Udhuru wake ni nini?' katika sahihi At-Targhiib.

## Al- Kabair

---

«ثلاثة لعنهم الله : من تقدم قوما وهم له كارهون ، وامرأة باتت وزوجها  
ساخط عليها، ورجل سمع حي على الصلاة حتى على الفلاح ثم لم يجب »

*“Watatu Allah atawalaani: Atakayewaongoza watu ilhali  
wanamchukia, mwanamke aliyelala na mumewe akiwa amekasirika,  
na mtu amesikia munadi wa Swala kisha asijibu.”<sup>63</sup>*

‘Ali ibn Abi Talib رضي الله عنه’ amesema: “Hakuna Swala ya anayeswali jirani  
na msikiti ila aswalie msikitini. Ikaulizwa ni nani jirani wa msikiti?’  
Akasema: ‘Anayesikia adhana.’

Imepokewa na Al-Bukhari katika Sahihi yake kutoka kwa ‘Abdullah bin  
Mas’uud رضي الله عنهما’ amesema: ‘Atakayependezwa kukutana na Mwenyezi  
Mungu (siku ya kiama) hali ya kuwa Muislamu basi ahifadhi Swala tano  
za faradhi anayoitiwa nayo Muislamu kila siku. Allah ameweka sheria  
kwa nabii wenu sunna ya uongofu, na hizo Swala ni katika sunna za  
uongofu, hata kama nyie mtaswali nyumbani kwenu kama anavyoswali  
huyu aliyekosa Swala ya jamaa mtakuwa mmekwenda kinyume na sunna  
ya Nabii, na kama mkiacha sunna ya Nabii wenu basi mtapotea, na hakika  
mmetuona kuwa hakosi Swala hiyo isipokuwa mnafiki anayefahamika  
unafiki wake au mgonjwa. Ilikuwa mtu analetwa akibebwa baina ya watu  
wawili na husimamishwa katika safu kwa ajili ya kuswali Swala ya  
jamaa.”<sup>64</sup>

Rabi bin Khaytham alianguka na kiwiliwili chake kilipooza, lakini  
alikuwa akienda kuswali jamaa huku akiwaegemea watu wawili,  
akaambiwa: ewe Abu Muhammad, wewe una ruhusa ya kuswali  
nyumbani kwako, kwani wewe unasameheka, akawajibu: “Ni kama hivyo  
mnavyosema, lakini mimi namsikia muadhini akisema: njooni katika

---

<sup>63</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na At-Tirmidhi 357 na akasema Al-Albani katika dhaifu  
sunan At-Tirmidhi ni kuwa isnadi yake ni dhaifu mno.

<sup>64</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 654 na sio kama alivyosema mwandishi kuwa ipo  
katika Al-Bukhari.

## Al - Kabair

---

Swala njooni katika kufaulu” Atakayeweza kujibu na kuitikia kwa kuiendea hata kama atatambaa basi na afanye.”<sup>65</sup>

Hatim Al-Aswam alisema: Siku moja nilikosa Swala ya jamaa, Abu Ishaq Al-Bukhari alinipa pole (kwa msiba huo), na lau ningefiwa na mtoto basi wangenipa pole watu zaidi ya makumi ya maelfu, kwa sababu msiba wa dini kwa watu ni mwepesi kuliko msiba wa dunia!  
Baadhi ya *Salaf* walikuwa wakisema: Haikumpita mtu Swala ya jamaa ila kwa dhambi iliyompata.

Na ilikuwa Ibn ‘Umar رضي الله عنه akisema: “Siku moja ‘Umar alikwenda kwenye bustani yake ya matunda na aliporudi tayari watu walikuwa wamekwisha swali Swala ya Alasiri hapo ‘Umar akasema *Inna lil-lahi wa Ina Ilayhi Rajiuun* hakika nimeikosa Swala ya Alasiri katika jamaa, Shuhudieni kuwa mie ninalitoa shamba langu sadaka kwa wale wanaohitaji ili iwe ni kafara kwa aliyoyafanya ‘Umar.”

## MLANGO

Swala ambayo walikuwa wakijali sana ni Swala ya Isha na ya Alfajiri kwa jamaa, Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«إن هاتين الصلاتين أثقل الصلوات على المنافقين ، يعني العشاء والفجر ،  
ولو يعلمون ما فيهما من الأجر لآتوهما ولو حبوا »

*“Kwa hakika Swala hizi mbili ni nzito zaidi kwa wanafiki, yaani Swala ya Isha na Alfajiri, na kama wangeyajua yaliyomo katika Swala hizi mbili katika ujira basi wangezija hata kwa kutambaa.”<sup>66</sup>*

---

<sup>65</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Sa’ad 6/189-190 na Abu Nua’im 2/113.

<sup>66</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/242, Al-Bukhari 658, Muslim 651 kutoka kwa Abu Hurayrah.

Na Ibn 'Umar amesema: ilikuwa mmoja wetu anapokosa Swala ya Isha au Alfajiri katika jamaa anasikitika akidhania kuwa amefanya unafiki."<sup>67</sup>

### **KISA**

Kutoka kwa 'Ubaidullah bin 'Umar Al-Qawariyriy رَضِيَ اللهُ عَنْهُ amesema: Maisha yangu sijapata kukosa Swala ya jamaa ya Isha, lakini siku moja mgeni alikuja kwangu na nikawa naye hadi kuchelewa kuswali Swala ya Isha kwa sababu yake, nikatoka kwenda kwenye Swala katika misikiti ya Basra, nikakuta watu wote wameshaswali na misikiti imefungwa, nikarejea nyumbani nikajisemeza: Imekuja katika Hadithi: "Hakika Swala ya jamaa huizidi Swala ya mtu binafsi kwa daraja ishirini na saba." Hivyo nikaswali Swala ya Isha mara ishirini na saba kisha nikalala, nikaota ndoto nipo na watu walio na farasi na mimi nipo kwenye farasi tunashindana, nami nikikimbiza farasi wangu lakini siwafikii, nikageuka kwa mmoja wao akaniambia: Usimsumbue farasi wako kwani wewe huwezi kutufikia, nikamuuliza: "Kwa nini?" Akanijibu: "Kwa sababu sisi tumeswali Isha katika jamaa na wewe umeswali peke yako. Nikaamka nikiwa katika hali ya huzuni sana." Tunamuomba Allah تَعَالَى Muongozo wake, hakika Yeye تَعَالَى ni Mkarimu na Mtukufu Mkubwa.

\*\*\*

---

<sup>67</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Abi Shayba 1/332, Ibn Khuzaimah 1485, Al-Baihaqi 3/59 sahihi At-Targhiib 414.

DHAMBI KUBWA YA TANO

KUZUIA ZAKA

Allah تعالیٰ Aliyetukuka Anasema:

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْتَخُلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ حَتِيرًا هُمْ بَلْ هُوَ شَرٌّ هُمْ  
سَيُطَوَّقُونَ مَا يَحْمِلُونَ بِيَوْمِ الْقِيَامَةِ

**"Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake kuwa ni kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao. Watafungwa kongwa za yale waliyo yafanyia ubakhili Siku ya Kiyama...."** (3:180)

وَوَيْلٌ لِّلْمُشْرِكِينَ ﴿٦١﴾ الَّذِينَ لَا يُؤْتُونَ الزَّكَاةَ

**"...na ole wao wanao mshirikisha, Ambao hawatoi Zaka..."**  
(41:6-7)

Allah Amewaita wao kuwa ni washirikina. Na:

وَالَّذِينَ يَكْتُمُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ  
﴿٦٢﴾ يَوْمَ نُحْمِي عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَتُكْوَى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ هَذَا  
مَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٦٣﴾

**"...Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu. Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao, wakaambiwa: Haya ndiyo mlio jilimbikia nafsi zenu, basi onjeni mliyo kuwa mkilimbika."**  
(9:34-35)

Imethibiti kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

« ما من صاحب ذهب ولا فضة لا يؤدي منها حقها إلا إذا كان يوم القيامة صفحت له صفائح من نار ، فأحمي عليها في نار جهنم فيكوى بها جنبه وجنبه وظهره . كلما بردت أعيدت له في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة حتى يقضي الله بين الناس ، فيرى سبيله إما إلى الجنة وإما إلى النار.»

*“Yeyote mwenye kumiliki dhahabu au fedha, na hatekelezi haki zake, siku ya kiama ikiwadia sahani zitafanywa za moto, zitachomwa kidani cha moto wa Jahannam kisha kwa sahani hizo vipaji vyao vya uso, mbavu zao na migongo yao itaunguzwa na moto. Kila mara vikipoa, watarejeshwa tena humo wakati wa mchana urefu wake ni sawa na miaka 50 watachapwa, hadi hukumu ya Allah itakapotolewa kwa binadamu. Halafu ataoneshwa njia yake ni ya peponi au motoni.”*

Aliulizwa Mtume ﷺ : ‘Nini khabari ya ngamia?’ Akajibu:

« ولا صاحب إبل لا يؤدي منها حقها إلا إذا كان يوم القيامة بطح لها بقاع قرقر أو فر ما كانت لا يفقد منها فصيلا واحدا تطؤه بأخفافها وتعضه بأفواهها ، كلما مر عليه أولها رد عليه آخرها في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة حتى يقضي الله بين الناس فيرى سبيله إما إلى الجنة وإما إلى النار.»

*“Ikiwa mtu anamiliki ngamia na hatekelezi haki zao basi siku ya Kiama itapowadia, uwanja laini wa mchanga utatandazwa, na atawaona ngamia wake wote hakosekani hata mmoja watawaponda watu hao kwa kwato zao na kuwatafuna kwa midomo yao na mara tu akipita wa kwanza, basi yule wa mwisho atarejea, mchana wote ambao urefu wake ni sawa na miaka 50 hadi hukumu ya Allah itakapopitisha juu ya umma na atajua kama njia yake ya peponi au motoni.”* Aliulizwa ewe Mjumbe wa Allah vipi suala na ng’ombe na kondoo? Akajibu ﷺ :

« ولا صاحب بقر ولا غنم لا يؤدي منها حقها إلا إذا كان يوم القيامة بطح لها بقاع قرقر ليس فيها عقصاء ولا جلعاء ولا عضباء تنطحه بقرونها وتطؤه بأظلافها كلما مر عليه أولها رد عليه آخرها في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة حتى يقضي الله بين الناس ، فيرى سبيله إما إلى الجنة وإما إلى النار »

*“Wala mmiliki wa ng’ombe na kondoo ikiwa asiyetekeleza haki zao, basi siku ya kiama ikifika basi ardhi iliyonyooka na laini itakuwepo, na hatokosekana wanyama wake hata mmoja, hakuna atakayekosa pembe wala kuvunjika na watamchota kwa pembe zao na kumkanyaga kwa kwato zao. Akimaliza wa mwisho ataanza tena yule wa mwisho kuwa wa kwanza kutwa nzima ambayo urefu wake ni sawa na miaka 50 hadi Allah atakapotoa Hukumu Yake, siku ya umma na yeye atajijua kama mtu wa peponi au motoni.” (Ahmad 2:262-286; Muslim 987)*

Mtukufu Mtume ﷺ akasema tena:

« أول ثلاثة يدخلون النار : أمير مسلط . وذو ثروة من مال لا يؤدي حق الله تعالى من ماله ، وفقير فخور . »

*“Aina tatu (ya watu) ndio watakoingia motoni: wa kwanza ni kiongozi atakayewanyanya watu wake, na mtu tajiri mwenye mali na hatoi haki ya Allah katika Zaka kutokana na mali aliyokuwa nayo, na maskini anayejivuna.”<sup>68</sup>*

Kutoka kwa Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَاليسema: “Mtu yeyote mwenye uwezo na kwenda kuhiji Makkah na asifanye hivyo, au kutoa Zaka,na asitoe, mtu huyo ataomba wakati wa kufa kwake arudishwe duniani. Mtu mmoja akamwambia Ibn ‘Abass mche Allah kwani anayeomba kurudishwa duniani ni kafiri? Ibn ‘Abbaas akasema: ‘Nitakusomea Qur’an kuhusu jambo hilo, Allah تعالى Amesema:

---

<sup>68</sup> Dhaifu: Imepokewa na Ahmad 2/479, At-Tirmidhi 1642 kwa tamshi, ‘Watatu wa mwanzo kuingia motoni.’...na Ibn Khuzaymat katika sahihi yake 3/2249 na dhaifu Al-Jami’ 3703.



وَأَنْفِقُوا مِنْ مَّا رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَا أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُن مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٦٩﴾

***“Na toeni katika Tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?” (63:10)***

Yaani atoe Zaka na وَأَكُن مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٦٩﴾

***“ na niwe katika watu wema ”***

Akaulizwa wajibu wa Zaka na akajibu: ‘Wakati mali ikifikia dirham 200 inapasa Zaka, akaulizwa wajibu wa Hijja, alijibu: “Ni masurufu na kipando.”<sup>69</sup>

Wala haipasi Zaka kwa mapambo ya halali ikiwa yametayarishwa kutumika, hata hivyo kama yatakuwa yamewekwa kama vile kukodishwa basi yanapasa kutolewa Zaka.<sup>70</sup>

Inapasa kutoa Zaka katika thamani ya biashara. Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: Amesema Mtume ﷺ:

«من أتاه الله مالا فلم يؤد زكاته مثل له يوم القيامة شجاعاً أقرع له زبيبتان يطوقه يوم القيامة فيأخذ بلهزمتيه ( أي بشدقيه ) فيقول : أنا مالك، أنا كنزك »

***“ Atakayepewa mali na Allah wala asitoe Zaka yake atawekewa siku ya kiama Shuja’ Al-Aqra’ mwenye pembe mbili atamzingira shingoni siku ya kiama kisha atasema: Mimi ni mali yako, mimi ni hazina yako”.***

---

<sup>69</sup> Imepokewa na At-Tirmidhi 3316 na akasema Al-Albani katika dhaifu Sunan At-Tirmidhi ambayo isnadi yake ni dhaifu.

<sup>70</sup> Kilicho cha sawa ni kuwa mapambo yawe ni ya kutumika au yasiwe ni ya kutumika yapasa kutolewa Zaka. Allah Anajua zaidi.

## Al - Kabair

---

Kisha baada ya hapo atasoma aya:

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخُلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَّهُمْ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَّهُمْ  
سَيُطَوَّقُونَ مَا بَخَلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ<sup>71</sup>

**“Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake kuwa ni kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao. Watafungwa kongwa za yale waliyo yafanyia ubakhili Siku ya Kiyama....” (3:180)**  
imepokewa na Al-Bukhari.<sup>71</sup>

Abu Masuud<sup>رضي الله عنه</sup> katika kuelezea sura At-Tauba kuhusu waliokataa kutoa Zaka:

يَوْمَ نَحْمِي عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَتَكْوَى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وظُهُورُهُمْ هَذَا مَا  
كَرَرْتُمْ لِأَنْفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٥٨﴾

**“... Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao...” (9:35).**

Amesema: ‘Dinari moja haitowekwa juu ya dinari wala dirham, lakini ngozi ya binaadamu itanyooshwa hadi kila dinari na kila dirham (ambayo hakuitolea Zaka) iwekwe juu ya ngozi yake na joto lake litampata’.<sup>72</sup>

Ikiulizwa: “Kwanini kipaji, mbavu, na mgongo vimeainishwa (katika sura) kuwa vitachomwa?’ Ikasemwa: “Wakati huo tajiri bakhili akimuona maskini hukunja uso wake na kiganja chake na hugeuka, yule masikini akimkaribia tajiri hugeuka hivyo basi viungo vyote hivi vyake huadhibiwa ili iwe ni malipo kwa matendo yake yale na jinsi ya amali aliyofanya.’

---

<sup>71</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 1403, 565, 4659 na An-Nasai 5/39 kutoka kwa Abu Hurayra.

<sup>72</sup> Imepokewa na At-Tabari 10/124 na watu wake ni Thiqah (waaminifu).

## Al - Kabair

---

Mtukufu Mtume ﷺ amesema: "Tano kwa tano."

Wakasema: 'Ewe Mtme wa Allah ni nini tano kwa tano?'akajibu:

*"Endapo watu watawunja mkataba Allah huwapa nguvu maadui juu yao, endapo watu wakihukumiana kwa kile ambacho Allah hakukiteremsha basi ufakiri utaenea kwao, na ikidhihiri uchafu basi vifo vitasambaa kati yao, na wakipunja katika kupima mizani na kasoro ya uzito unaostahiki, basi njaa na uhaba wa maji (Malisho) huwepo, na kama hawatoi Zaka mvua itazuiliwa kwao."*<sup>73</sup>

### MAWAIDHA:

Waambie wale walioshughulishwa na kiburi cha dunia, kuwa kesho ndio maangamizi yao hakitowanufaisha walichokikusanya pindi, atakapokuja mwenye kuwahadharisha:

يَوْمَ نَحْمِي عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَيُكْوَى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وظُهُورُهُمْ هَذَا مَا كَنَزْتُمْ لِأَنْفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٥٣﴾

**"...Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao..." (9:35).**

Imekuwaje nyoyo na akili zao zikaghafilika,

يَوْمَ نَحْمِي عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَيُكْوَى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وظُهُورُهُمْ هَذَا مَا كَنَزْتُمْ لِأَنْفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٥٣﴾

---

<sup>73</sup> Hadithi Hassan: Imepokewa na Ibn Majah 4019, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 3042 kutoka kwa Ibn 'Umar na ikafanywa ni Hassan na Al-Albani katika As-Swahiha uk 106.

**“ ...Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao...” (9:35).**

Kachukua mali kwenda hadi nyumba ya adhabu akaweka katika mkoba wake ili ipate moto na adhabu iongezeke. Akavingirwa vingirwa ili viingizwe motoni ili adhabu ienee. Kisha itajiwa kwa neema ya uongofu iliopotea, hutafuta sehemu inayong’aa ambapo nuru yao itatafutwa. Kisha zitakapotiwa katika moto wa jahannam na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao. Mtakapokutana na fakiri anapata na adha, akiwaomba watu kitu wao huruka huku wameghadhika, wakimfanyia wema huuliza: Umemsaidia yule, na maswali kama hayo, na lau mola wako angetaka angemtajirisha muhitaji, na wakasahau hekima ya Muumba kumtajirisha fulani na kumfakirisha fulani na ajabu hukutana nao kwa huzuni mtakapokutana na makaburi yenu:

فَتَكْوَىٰ بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ ﴿٣٥﴾

**“...na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao...” (9:35).**

Mrithi atachukua bila ya tabu yoyote, na atauliza mkusanyaji umepata wapi na wapi, bali mwiba ni wake na wenye kurithi unyevunyevu wake. Yuko wapi mwenye kujali na kupupia kukusanya, zipo wapi akili zenu?

يَوْمَ نَحْمِيٰ عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فُتُكْوَىٰ بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ ۗ هٰذَا مَا

كَتَبْتُمْ لَآنْفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٥﴾

**““ ...Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao...” (9:35)**

## Al- Kabair

---

Lau kama mtaona matabaka ya moto, hujigeuza katika mawe ya moto katika dinari na dirhamu, na atakuwa amejigeuza kulia pamoja na kushoto, walipofanya ubakhili pamoja na kushotoni lau mtakapowaona huko motoni wakinywa katika Al-Hamiym. Subira zao zilileta fujo,

يَوْمَ نَحْمِي عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَيُكْوَى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ هَذَا مَا كُنْتُمْ لَا تَفْسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿١٥﴾

**“...Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao...” (9:35)**

Ni mara ngapi wakitoa mawaidha duniani na wapo pamoja na wanaowasikiliza, waliwakhofisha kiasi gani adhabu za Allah wakiwa pamoja nao wanaoogopa kama walivyowajulisha wanaokataa kutoa Zaka wakiwemo vile vile wanaotoa, kama kwamba kwa mali zao wakati huo Shujaa’ Al-Aqra amempindua, ni ipi fimbo ya Musa na Tuuri yao:

يَوْمَ نَحْمِي عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَيُكْوَى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ هَذَا مَا كُنْتُمْ لَا تَفْسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿١٥﴾

**“...Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao...” (9:35)**

## KISA

Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Yusuf Al-Faryabi alisema: “Wakati fulani, mimi nilikwenda pamoja na kundi la jamaa zangu kumtembelea Abu Sinan رحمته الله تعالى, tulipoingia nyumbani mwake, na tukaketi, alisimama na kusema: “Twendeni kumhani jirani yetu ambaye

ndugu yake amefariki, hapo tukasimana na tukafuatana naye kwenda nyumba ya jirani. Tukamkuta akimlilia sana nduguye aliyefariki. Tukamfariji na kumpa pole lakini akawa hataki kufarijiwa wala kupewa pole: Tukamuuliza: 'Kwani hufahamu kuwa mauti ndio njia yetu hatuna budi nayo?' Akasema: 'Najua, lakini kinachoniliza ni adhabu atakayoipata ndugu yangu asubuhi na jioni.' Tukamuuliza kwani Allah تعالى amekupa taarifa juu ya elimu ya ghaibu (isiyoonekana) akasema: "Hapana lakini wakati tulipomzika nikatulia katika kaburi lake watu walipoondoka, nikasikia sauti ndani ya kaburi lake ikisema: "Ah, mmeniwacha peke yangu ninapata adhabu hii! Nilikuwa nikiswali na nikifunga." Akasema: (kutokana na maneno haya) nilipata mshtuko kwa maneno haya nikalia na nikalifukua kaburi ili nione hali yake, nilichokiona ni kuwa kaburi limejaa moto na shingoni mwa ndugu yangu palikuwepo na ringi ya moto. Nilipata huzuni kubwa wa udugu na kumuonea huruma na nilijaribu kunyoosha mkono wangu nilivue, lakini vidole na mkono wangu uliungua." Hapo akatuonesha mikono yake imekuwa myeusi kwa kuungua, akaendelea kusema: 'Nikarejesha udongo na kuondoka, vipi nisilie kwa hali yake na nisimsikitikie?' Tukamuulizia: "Ni jambo gani nduguyo alikuwa akikosea hapa duniani?" Akajibu, 'Alikuwa hatoi Zaka kutokana na mali yake.

'Tukasema huu ni ukweli wa maneno yake Allah:

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخُلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَّهُمْ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَّهُمْ  
سَيُطَوَّقُونَ مَا بَخُلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

***"Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake kuwa ni kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao. Watafungwa kongwa za yale waliyo yafanyia ubakhili Siku ya Kiyama..." (3:180)***

Na: "Adhabu juu ya nduguyo imetangulizwa kabla ya siku ya kiyama." Tukaondoka na kumuacha huyo kijana na kwenda kwa mmoja wa

## Al - Kabair

---

masahaba wa Mtukufu Mtume ﷺ Abu Dhar رضي الله عنه na tukamuhadithia kisa cha bwana yule, na tukamuambia: "Tunawaona wakristo na wayahudi wakifa lakini hatuoni hilo kwao?" Abu Dhar رضي الله عنه akasema: "Ama wao bila shaka wamo motoni, lakini baadhi ya wakati Allah تعالى hutuonesha adhabu (sisi tuliopata imani) ili tupate mazingatio." Allah تعالى Mtukuka anasema:

فَمَنْ أَبْصَرَ فَلْتَنْفَسْهُ ۗ وَمَنْ عَمِيَ فَعَلَيْهَا ۗ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ ﴿٦٣﴾

**"...Basi anaye ona ni kwa faida yake mwenyewe, na anaye pofuka basi ni khasara yake. Nami si mtunzaji wenu." (6:104)**

Tunamuomba Allah تعالى msamaha na ulinzi hakika Yeye Ndiye Mkaribu Mkubwa.<sup>74</sup>

\*\*\*

---

<sup>74</sup> Kisa hiki bila shaka ni cha uongo kwa sababu mhadithiaji na Abu Dhar hawakukutana, labda iwe Abu Dhar ameishi maisha yanayokaribia miaka mia mbili, na hili jambo halijatokea.

## DHAMBI KUBWA YA SITA

### KUTOKUFUNGA SIKU MOJA YA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI BILA YA SABABU

Allah Mtukuka Amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ  
تَتَّقُونَ ﴿١٨٤﴾ أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ ۚ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ

***“Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama walivyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu. (Mfunge) siku maalumu za kuhisabika. Na atakaye kuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimize hisabu katika siku nyengine.... ” (2:183-184)***

Imethibiti kutoka katika sahihi mbili kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

« بني الإسلام على خمس : شهادة أن لا إله إلا الله وأن محمداً رسول الله ، وإقام الصلاة ، وإيتاء الزكاة ، وحج البيت ، وصوم رمضان »

*“Uislamu umejengwa kwa misingi mitano: Shahada (Hapana Mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah na kuwa Muhammad ni mjumbe wa Allah) na kusimamisha Swala, kutoa Zaka, na Kuhiji, na kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhan.”<sup>75</sup>*

Na akasema tena Mtume ﷺ:

« من أفطر يوماً من رمضان بلا عذر لم يقضه صيام الدهر وإن صامه »

---

<sup>75</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/143, Al-Bukhari 8, 16 na 22 na Muslim 16.



## Al - Kabair

---

*" Mwenye kufungua siku moja ya Ramadhani na hakuwa na udhuru hatoweza kuilipa siku hiyo hata akifunga maisha yake yote."*<sup>76</sup>

Kutoka kwa Ibn 'Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَ alisema: " Uislamu na msingi wa dini ni mambo matatu: Kushuhudia kuwa Hapana Mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah رَضِيَ اللهُ عَنْهُ na Swala na kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhan - yeyote atakayeacha moja katika hayo basi yeye ni kafiri." Tunajilinda kwa Allah dhidi ya hayo.<sup>77</sup>

\*\*\*

---

<sup>76</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na Ahmad 2, 442, 470, Abu Dawud 2396, At-Tirmidhi 726 na Dhaifu Al-Jami' 5471.

<sup>77</sup> Dhaifu: Imepokewa na Abu Ya'ala Al-Mawswali 2345 na Albani akasema: Dhaifu As-Silsila 1/94.

## DHAMBI KUBWA YA SABA

### KUTOKUTEKELEZA HIJA KWA MWENYE UWEZO

Allah Mtukuka Amesema:

وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا

**“...Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea...” (3:97)**

Umar bnul Khattaab amesema: “Nimetamani kutuma watu kuangalia kwenye miji hii kila mwenye uwezo na hakuhiji, basi niwatoze kodi, kwani wao sio waislamu”

Kutoka kwa Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ alisema: “Mwenye uwezo wa kwenda Makkah na asifanye hivyo, au anatakiwa kutoa Zaka na asitoe Zakat, mtu huyo ataomba wakati wa kufa kwake arudishwe duniani.” Mtu mmoja akamwambia Ibn ‘Abbas, “Mche Allah kwani anayeomba kurudishwa duniani ni kafiri” Ibn ‘Abbas akasema: ‘Hilo limo ndani ya kitabu cha Allah Mtukuka’:

وَأَنْفِقُوا مِنْ مَا رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَا أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ ۗ

**“Na toeni katika Tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka....” (63:10)**

Yaani nitoe Zaka

وَأَكُنْ مِنَ الصَّالِحِينَ ۗ

**“na niwe katika watu wema.”**

## Al- Kabair

---

Yaani ni hiji,

وَلَنْ يُؤَخِّرَ اللَّهُ نَفْسًا إِذَا جَاءَ أَجْلُهَا ۗ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٦١﴾

***“Wala Mwenyezi Mungu hataiakhirisha nafsi yoyote inapo fika ajali yake; na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.”(63:11)***

Akaulizwa kuhusu wajibu wa Zaka, akajibu ikiwa mali imefikia kiwango cha Dirham 200, Zaka inakuwa wajibu. Akaulizwa kuhusu Hija na yanayowajibisha Hija, akajibu: ‘Ni masurufu na kipando.’<sup>78</sup> Said bin Jubair anasema: ‘Jirani wangu mwenye uwezo alikufa bila ya kuhiji nami sikumswalia.’

\*\*\*

---

<sup>78</sup> Dhaifu: Imepokewa na At-Tirmidhi 812 na Al-Baihaqi katika Ash-Shi’b na imedhoofishwa na Albani katika dhaifu Al-Jami’ 5872.

## DHAMBI KUBWA YA NANE

### KUASI WAZAZI

Allah Mtukuka anasema:

﴿ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۗ ﴾

**“Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote  
ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema....” (17:23)**

Yaani kuwafanyia wema na kuwahurumia.

﴿ إِنَّمَا يَتَلَفَعْنَ عِنْدَكَ الْكَبِيرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أَفٍّ وَلَا تَتَّبِعُهُمَا ۖ ﴾

**“...Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote  
wawili, basi usimwambie hata: Ah Wala usiwakemee!...”**

Kuwahurumia wale usiwaambie *uff!* maana yake msiwakatae na wala kuwadharau kwa upungufu wao kutokana na uzee na makosa yao kutokana na umri wao. Ni wajibu wako wewe kuwahudumia kama walivyokuhudumia na jambo bora ni kwa aliyeanza kufanya, wala hailingani. Walikuwa wakivumilia udhia wako wakitamani maisha yao yaendeleo, na wewe kwa upande wako ukivumilia maudhi yao basi utatamani vifo vyao, Allah Akasema:

﴿ وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ۖ ﴾

**“...Na sema nao kwa msemu wa hishima.” (17:23)**

Yaani laini kwa wema na upole.

﴿ أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَيَّ الْمَصِيرُ ۖ ﴾

**“...Nishukuru Mimi na wazazi wako. Ni kwangu Mimi ndiyo marudio.” (31:14)**

Tizama namna gani alifungamanisha shukrani juu ya wazazi na shukrani kwa Allah تعالى. Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا amesema: “Aya tatu zimeunganishwa na mambo matatu haikubaliki bila ya viungisho vyake. Allah تعالى anasema Kwanza:

أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ ﴿٣١﴾

**“Mtiini Allah na mtiini Mtume.”**

kwa hivyo mtu akamtii Allah تعالى lakini hamtii mjumbe wake basi Utii wake hatokubalika tena kutoka kwake. Pili: Allah تعالى anasema:

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ ﴿٣٢﴾

**“Tekelezeni Swala na toeni Zaka.”**

Kwa hivyo mtu akaitekeleza Swala lakini hatoi Zaka haitakubalika Swala yake. Tatu: Allah Mtukuka zaidi anasema:

أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلَوْلَدَيْكَ ﴿٣٣﴾

**“...Nishukuru Mimi na wazazi wako.”**

Atakayemshukuru Allah wala hatoshukuru wazazi wake haitokubaliwa shukrani zake. Ndiyo maana mtukufu Mtume ﷺ anasema:

«رضا الله في رضی الوالدين ، وسخط الله في سخط الوالدين»

**“Radhi ya Allah ndio radhi za wazazi wawili, na ghadhabu ya Allah ni ghadhabu za Wazazi wawili.”<sup>79</sup>**

---

<sup>79</sup> Sahihi: Imepokewa na At-Tirmidhi 3424, Al-Bukhari katika Al-Adab Al-Mufrad 22 na imesahihishwa na Al-Albani katika As-Silsila As-Swahihha 515.

## Al - Kabair

---

Kutoka kwa Ibn 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا amesema: "Alikuwa mtu mmoja akaomba ruhusa ya Mtume ﷺ ya kwenda kwenye Jihadi pamoja nae. Mtukufu Mtume ﷺ akamuuliza:

« آحى والدك؟ »

"Je, wazazi wako bado wako hai?". Akamjibu: 'Ndio. 'Mtukufu Mtume akamwambia:

« ففیهما فجاهد »

"Wafanyie Jihadi (wahudumie)."<sup>80</sup>

Angalia namna gani umuhimu wa kutunza wazazi na kuwahudumia kumetangulizwa zaidi kuliko Jihadi

Katika sahihi mbili Mtume wa Allah ﷺ amesema:

« ألا أنبئکم بأکبر الكبائر : الإشرک بالله وعقوق الوالدين »

"Je, nikuambieni juu ya dhambi kubwa zaidi? Ni kumshirikisha Allah na kuwaasi wazazi wako."

Angalia jinsi gani Mwenyezi Mungu alivyounganisha suala la kuwatendea vibaya wazazi na kumshirikisha yeye. Tunasoma katika sahihi mbili vile vile kuwa Mtume ﷺ amesema:

« لا يدخل الجنة عاق ولا منان ولا مدمن خمر »

"Haingii peponi muasi wa wazazi, na mwenye kuwakumbusha mambo anayowafanyia na yule mwenye kuhudumia pombe."<sup>81</sup>

---

<sup>80</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 3004 na Muslim 2549 kutoka kwa Ibn 'Umar.

<sup>81</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/201, Ad-Darimi 2094 na ikasahihishwa na Ash-Shaykh katika As-Swahiha 670.

## Al- Kabair

---

Na kutoka kwake Mtume ﷺ vile vile:

« لو علم الله شيئاً أدنى من الأف لنهى عنه، فليعمل العاق ما شاء أن يعمل فلن يدخل الجنة. وليعمل البار ما شاء أن يعمل فلن يدخل النار »

*“Endapo Allah anajua hata jambo dogo tu ambalo lingewaudhi wazazi kama kutamka Uffu! Basi angelikataza, basi asiyeheshimu wazazi basi na afanye chochote akitakacho basi hatoingia peponi. Na mwema na afanye atakavyofanya basi hatoingia motoni.”<sup>82</sup>*

Mtume ﷺ akasema tena:

« لعن الله العاق لوالديه »

*“Allah amemlaani asiyeheshimu wazazi wake.”<sup>83</sup>*

Akasema: « لعن الله من سب أباه ، لعن الله من سب أمه »

*“Allah amemlaani mwenye kutukana wazazi wake wawili, Allah amemlaani mwenye kumtukana mama yake.”<sup>84</sup>*

Na akasema katika tukio jingine:

« كل الذنوب يؤخر الله منها ما شاء إلى يوم القيامة إلا عقوق الوالدين فإنه يعجل لصاحبه »

---

<sup>82</sup> Amesema As-Suyuuti katika Ad-Dur 4/310, imepokewa na Ad-Dailami kutoka kwa Al-Hassan bin ‘Ali ikiwa ni Marfuu’ ambayo ndani yake yupo Asram bin Hushab naye ni mzushi wa Hadithi.

<sup>83</sup> Dhaifu: Imepokewa na Al-Hakam 4/356, At-Tabarani katika Al-Awsat 897 kwa tamshi, ‘Allah amelaani viumbe saba juu ya mbingu saba... amelaaniwa asiyeheshimu wazazi wake.’ isnadi yake ni dhaifu. Imepokewa na Muslim 1978 na An-Nasai 7/232 kutoka kwa ‘Ali bin Abi Talib kwa tamshi Allah amemlaani anayewalaani wazazi wake wawili.

<sup>84</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/309, At-Twabarani 1546, Ibn Hibaan 4417 na sahihi Al-Jami’ 5112.

## Al - Kabair

---

*" Dhambi zote Allah huziakhirisha hadi siku ya kiyama, isipokuwa kuwaasi wazazi wawili, kwani humharakishia swahibu wake "*

Yaani atapata adhabu Duniani kabla ya siku ya kiyama."<sup>85</sup>

Ka'ab-Al-Ahbaar alisema: " Allah تعالی huharakisha kumuangamiza na kumpa adhabu mtu anayeasi wazazi wake, na Allah huongeza umri wa mtu ambaye anawatendea wema wazazi wake ili amzidishie mema na kheri. Miongoni mwa mema kwao ni kuwapa matumizi wakihitaji. Mtu alikwenda kwa mtukufu Mtume ﷺ na akamwambia: " Ewe Mjumbe wa Allah baba yangu anataka kuchukuwa mali yangu yote. Yeye ﷺ alimjibu:

« أنت ومالك لأبيك »

*"Wewe na mali yako ni vya baba yako"*<sup>86</sup>

Ka'ab-al Ahbaar aliulizwa kuhusu maana ya kuasi wazazi na akajibu:

"Endapo atampa baba yake au mama basi hatofanya wema katika mgao wao, na pindi akiamrisha nao hatii, na wakimuomba kitu hawapi, na wakimuamini kitu au jambo anafanya udanganyifu ndani yake."<sup>87</sup>

Ibn Abbas رضي الله عنهم aliulizwa, 'Ni nani watu As-haabu 'Aaraf na nini maana yake?' Akajibu:

'Aaraf ni mlima kati ya motoni na peponi, na imeitwa kwa jina la Al-'Aaraf kwa sababu inaangalia peponi na motoni - ndani yake kuna miti,

---

<sup>85</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/36, Abu Dawud 4902, At-Tirmidhi 2511, Ibn Majah 4211 kwa tamshi lililokaribiana na Abu Bakra na kusahihishwa na Al-Albani katika As-Swahiha 918 na sahihi Al-Jami' 5704.

<sup>86</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Majah 2291, At-Twahawi katika Mushakal Al-Athar 2/230, Abu Dawud 3530 na kusahihishwa na Ash-Shaykh katika sahih Ibn Majah na Al-Mishkat 3354 na Al-Irwaaa 838.

<sup>87</sup> Sahihi: Imepokewa na ikiwa katika Jami' yake 89, 'Abdrur - Razzaaq 11/137 na Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 7894 na isnadi yake ni sahihi.



## Al- Kabair

---

matunda, mito na chemchem, ama wakazi wake ni watu waliotoka kwenda jihadi bila ya radhi za wazazi wao na mama zao na wakauawa katika jihadi, wamekufa kwa ajili ya njia ya Allah ndio maana hawaingizwi motoni lakini wakati huo hawakuwatendea vizuri wazazi wao nao wakanyimwa kuingia peponi, wao wapo katika 'Aarafhadi pale Allah atakapowahukumu'.<sup>88</sup>

Imepokewa katika sahihi mbili kuwa mtu alikuja kwa Mtume ﷺ akasema: "Ewe mjumbe wa Allah ni nani anayestahiki zaidi usuhuba wangu?" Mtume ﷺ alijibu:

« أمك »

"Mama yako."

Akamuuliza tena: 'Kisha nani?' Akamjibu:

« أمك »

"Mama yako."

Kisha akauliza tena: 'Kisha nani?' Akamjibu tena:

« أمك »

"Mama yako".

Na akauliza tena, "Halafu nani? Akamjibu:

« أبوك ثم الأقرب فالأقرب »

"Baba yako kisha wakaribu zaidi, anayefuatia kwa ukaribu zaidi".<sup>89</sup>

---

<sup>88</sup> Ameitaja As-Suyuti katika Ad-Dur 3/162-163: kila kilichokuja kuhusu hili ni Marfu' na Mawquf lakini hayakosi maneno juu yake.

<sup>89</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 2548 na Ibn Majah 3658 kutoka kwa Abu Hurayra.

## Al - Kabair

---

Kwa hivyo Mtukufu Mtume ﷺ alimpa uzito mara tatu mama kuliko baba, na baba mara moja tu. Na hilo ni kwa sababu uangalizi wa mama kwa mtoto ulikuwa ni mkubwa zaidi kuliko baba, na huruma yake inatakiwa iwe kubwa zaidi, kwa mateso aliyoyapata ya kubeba mimba, kuzaa, kunyonyesha na kukesha.

Ibn 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا alimuona mtu akimbeba mama yake mabegani wakati akiizunguka al-Ka'aba mtu huyo akasema: "Ewe Ibn 'Umar unaona miye namna ninavyomchukua nikizunguka naye je, nitakuwa nimemlipa?" Akasema Ibn 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا: hata kidogo kwa alichokifanya, hata hivyo umefanya uzuri hivyo, Allah atakulipa kwa malipo machache au mengi."<sup>90</sup>

Kutoka kwa Abu Huraira رَضِيَ اللهُ عَنْهُ amesema: Mtume ﷺ alisema:

« أربعة نفر حق على الله أن لا يدخلهم الجنة ولا يذيقهم نعيمها : مدمن خمر ، وآكل الربا ، وآكل مال اليتيم ظلماً ، والعاق لوالديه إلا أن يتوبوا »

*"Watu wanne ni haki kwa Allah kutowaingiza peponi, wala kuwaonjesha neema zake: 'Mdumu kunywa pombe, mla riba, mla mali ya yatima kwa dhuluma na aliyeasi wazazi wake ila watubie.'"*<sup>91</sup>

Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

« الجنة تحت أقدام الأمهات »

*"Pepo ipo chini ya nyayo za mama zenu."*<sup>92</sup>

---

<sup>90</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari katika al-Adab al-Mufrad 11 lakini kwa tamshi 'Amesema Hapana wala kwa Zafra moja na kusahihishwa na Ash-Shaykh katika sahihi Al-Adab Al-Mufrad namba 9.

<sup>91</sup> Dhaifu: Imepokewa na Al-Hakam 2/37 na akasema Al-Albani: Dhaifu mno, katika dhaifu Al-Jami' 848.

<sup>92</sup> Dhaifu: Kwa tamshi hili ni sahihi lighayrihi: Hadithi hii kwa tamshi hili pamoja na umaarufu wake haina asili lakini imesahihishwa kwa tamshi 'Jilazimisheni kwani pepo ipo chini ya miguu yake.' Imepokewa na Ibn Majah 2781, Ahmad 3/429 na kusahihishwa na Ash-Shaykh katika sahihi Al-Jami' 1249 na Al-Mishkaat 4939.

## Al- Kabair

---

Mtu mmoja alikwenda kwa Abu Darda رضي الله عنه na kumwambia: Abu Darda رضي الله عنه, nimemuoa mwanamke, mama yangu ameniamuru nimaliki. Abu Darda رضي الله عنه akamjibu: Nimemsikia Mjumbe wa Allah ﷻ akisema:

« الوالد أوسط أبواب الجنة فإن شئت فأضِعْ ذلك الباب أو احفظه »

*“Mzazi yu katikati ya mlango wa peponi, hivyo chagua unavyopenda, uupoteze au uutunze mlango huo (wa pepo).”<sup>93</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

« ثلاث دعوات مستجابات لا شك فيهن: دعوة المظلوم، ودعوة المسافر،  
ودعوة الوالد على ولده »

*“Dua tatu ni zenye kukubaliwa, hazina shaka ndani yake, dua ya mdhulumiwa, dua ya msafiri, dua ya mzazi kwa mwanae”. Al-Al-Bukhari katika Al-Adabul-Mufrad (32,481), Abu Dawuud (1536), Tirmidhi (1905), Ibn Maajah (3862), Na Shaikh ameisahihisha katika sahihul Jaami’i (3022), na As-Swahihah (1797)*

Na amesema Mtume ﷺ:

« الخالة بمنزلة الأم »

*“Mama mdogo ni katika nafasi ya mama.”<sup>94</sup>*

Yaani katika kumfanyia wema na kumkirimu na kumtembelea. Wahab bin Munabbih amesema:

“Allah Mtukuka alimfunulia Musa عليه السلام rehema za Allah تعالى na amani zimfikie: “Ewe Musa watunze wazazi wako, kwani yeyote

---

<sup>93</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/196, 197, Ibn Majah 2089, At-Tirmidhi 1900 na ikasahihishwa na As-Shaykh katika sahihi Al-Jami’ 7145 na As-Sahih 910.

<sup>94</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 1844, 2699, 4251 na Ahmad 4/298.

## Al - Kabair

---

anayewatukuza wazazi wake Nitamuongezea uhai wake na Nitampa watoto ambao watamtukuza yeye, lakini yeyote atakayewavunjia heshima wazazi wake, nitampunguzia kiwango cha uhai wake, na nitampa mtoto atakayemuasi.”

Abu Bakra bin Abu Maryam, amesema: Nimesoma kutoka Taurat kuwa: “Yeyote atakayempiga baba yake basi anastahili kupigwa mawe hadi kufa.”

Wahb alisema nilisoma kutoka Taurati kuwa: “Yeyote anayempiga mama yake basi anastahili kupigwa mawe hadi kufa.”

Ama ‘Amru bin Murrah al-Juhani رضى الله عنه alisema: ‘Mtu mmoja alikuja kwa Mtume wa Allah ﷺ akauliza: “Je, nikiwa ninatimiza Swala zangu tano za kila siku na ninafunga kikamilifu mwezi mtukufu wa Ramadhani na ninatoa Zaka na ninatimiza Hija nyumba ya Allah jaza ya yangu itakuwa nini?” Mjumbe wa Allah ﷺ akamjibu:

« من فعل ذلك كان مع النبيين والصديقين والشهداء والصالحين إلا أن يعق والديه »

*“Mwenye kutenda hayo atakuwa pamoja na Mitume na wakweli (Al-Siddiqeen) na mashahidi (Ash-Shuhadda) na watenda mema (Assaliheen) isipokuwa kama akiwaasi wazazi wake.”<sup>95</sup>*

Na akasema ﷺ: « لعن الله العاق والديه »

*“Allah amemlaani mwenye kuwaasi wazazi wawili.”<sup>96</sup>*

Pia imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

---

<sup>95</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari katika Tarikh Al-Kabiir 6/308 Hadithi namba 6/308 Hadithi nambari 3487 sahihi At-Targhiib 748.

<sup>96</sup> Ishaelezwa upokezi wake

## Al- Kabair

---

« رأيت ليلة أسري بي أقوامًا في النار معلقين في جذوع من نار فقلت :  
يا جبريل من هؤلاء ؟ قال : الذين يشتمون آباءهم وأمهاتهم في الدنيا »

*“Nimeona usiku nilipopelekwa, watu ndani ya moto wame ning’inizwa katika visiki vya moto, nikasema: ‘Ewe Jibril ni nani hawa? Akasema: “Ni wanaotukana baba na mama zao duniani.”<sup>97</sup>*

Imepokewa kuwa atakayewatukana wazazi wake wawili huteremshiwa katika kaburi lake mawe ya moto kwa idadi ya kila tone linaloshuka kutoka mbinguni, na imepokewa kuwa atakapozikwa mwenye kuwaasi wazazi wawili kaburi litamminya hadi zitofautiane mbavu zake, na watu wenye adhabu kubwa zaidi siku ya kiama ni watatu: Mshirikina, Mzinifu na wale wanaowaasi wazazi wao.”

Amesema Bishr: ‘Anayemkaribia mama yake na akamsikiliza anachomwambia ni bora kushinda anayetumia upanga katika njia ya Allah ﷻ na kumuangalia mama yako ni jambo bora kushinda jambo lingine lolote.’

Mtu na mkewe walikuja kwa mjumbe wa Allah ﷻ wakigombana kuwa nani mwenye haki ya kumtunza mtoto. Mwanamume alisema ewe Mjumbe wa Allah ﷻ mtoto wangu ametokana na mgongo wangu, na mkewe akamwambia: “Ewe mjumbe wa Allah yeye aliyembeba kwa wepesi, katika mwili wake kwa manii tu na akampa yeye yaani manii yake tu kwa starehe, wakati mimi nilitwaa kubeba mzigo huo na kujifungua kwa maumivu na nilimnyonyesha huyo mtoto kwa miaka miwili.” Mjumbe wa Allah ﷻ hapo tena akaamua kumpa mtoto mama.<sup>98</sup>

---

<sup>97</sup> Dhaifu: Imetajwa na Al-Haithami katika Az-Zawaid 2/68.

<sup>98</sup> Hadithi Hassan: Imepokewa na Ahmad 2/182, Abu Dawud 2276, na akaifanya kuwa Hassan Al-Albani katika Irwau 2187 kutoka kwa ‘Umar

## MAWAIDHA

### Mwenye kubadili wema kwa wazazi kwa maasi

Ewe mwenye kupoteza haki za watu, mwenye kupunguza kuwafanyia wema wazazi wako wawili, mwenye kusahau yanayompasa, mwenye kughafilika yaliyo chini yako. Kuwafanyia wema wazazi wako wawili ni dini, na wewe unaacha kwa kufanya mambo mabaya, unajidai unatafuta pepo, nayo ipo chini ya nyayo za mama yako. Amekubeba katika tumbo lake miezi tisa kama kwamba ni Hija tisa. Na ukamsumbua wakati wa kujifungua kiasi cha kuyeyusha moyo, na akakunyonyesha maziwa katika matiti yake, na ikamruka akili kwa ajili yako, Akakuosha uchafu kwa mkono wake wa kuume, akakupendelea wewe chakula na yeye kujinyima, na ukafanya paja lake na chumba chake ni tandiko lako wema na utegemezi.

Yakikupata maradhi au cha kulalamika, unadhihirisha masikitiko hakuna mfano wake, na huzuni ikazidi ukomo na kilio, akatoa mali yake kwa daktari. Na lau atakhiyarishwa kati ya maisha yako na kifo chake basi angechagua maisha yako kwa sauti ya juu. Ni mara ngapi ulimfanyia tabia mbaya ya kumchukiza, na yeye akakuombea tawfiki kwa siri na kwa jahari. Alipofika utu uzima na kukuhitajia, ukamfanya katika vitu visivyo na maana kwako, Unashiba, hali yeye ni mwenye njaa, na unatosheleza kiu chako naye ana kiu, Ukaitanguliza familia yako kuwafanyia wema na yeye umemsahau na jambo lake limekuwa gumu kwako pamoja na wepesi wake, na umri wake kwako umekuwa mkubwa pamoja na kuwa ni mdogo, unamuhama naye hana mwingine wa kuwa naye. Katika hili Mola wako anakukataza na anakulaumu kwa upole, utapata adhabu hapa duniani kwa watoto kukufanyia hivyo hivyo, na huko akhera utakuwa mbali na Mola wa walimwengu, anakuita kwa ulimi wa kukemea na kuonya:

ذَلِكَ بِمَا قَدَّمْتَ يَدَاكَ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَمٍ لِلْعَبِيدِ ﴿٧٨﴾

**"(Ataambiwa): Hayo ni kwa sababu ya iliyo tanguliza mikono yako. Na hakika Mwenyezi Mungu si dhaalimu kwa waja." (22:10)**

Wakati wa Mtukufu Mtume ﷺ palikuwepo na kijana mmoja akiitwa 'Al-Qamah, alikuwa mtiifu sana na kufuata amri za Allah ﷻ kwa kushughulika na Swala, Funga na Zaka, akapata ugonjwa (maradhi) na maradhi yake yalimzidi yakawa ya hatari. Mkewe alikwenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kumuambia: Mume wangu Al-Qamah, yuko katika *Sakaratul Mauti*, miye kwa hivyo nimekuja kukupa taarifa ewe Mjumbe wa Allah ﷻ juu ya hali yake. Mtukufu Mtume ﷺ hapo tena akawaita Ammar, Suhaib na Bilal na akawaambia: "Nendeni kwake (Al-Qamah) na mwambieni arudie shahada."

Hapo tena wakaenda na wakamkuta yumo katika maumivu ya kifo, wakamlakinia shahada na wakamwambia aseme: "*Laillah illa Allah.*" Lakini ulimi wake haukuweza kutoa shahada (kuitamka), kutokana na hali hiyo wakamwendea Mjumbe wa Allah ﷻ na kumueleza kuwa kijana huyo hawezi kutamka shahada.

Mtukufu Mtume ﷺ akauliza: "*Je kuna mzazi wake yoyote yu hai?*".

Wakajibu: "Ewe Mtume wa Allah ﷻ mama yake yu hai, lakini ni mzee sana. Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "*Mwambie akiweza kuja basi na aje kwa Mtume ﷻ vinginevyo basi bakia ndani ya nyumba hadi akujie.*"

Akafika Mjumbe aliyetumwa na Mtukufu Mtume ﷺ akaenda kwa huyo mama na kumtaarifu ujumbe huo, mama huyo akasema: "Acha maisha yangu yawe muhanga, mimi ni bora kwenda kwake. Akasimama huku akichukua na mkongojo wa kuendea na akaenda kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kumuamkia Mtukufu Mtume ﷺ akamjibu salamu yake na Mtume ﷺ akamwambia: "*Umm Al-Qamah niambie ukweli, ukinidanganya Allah aliyetukuka zaidi atanifunulia ukweli kwangu, nini hali ya mwanao 'Al-Qamah?*"

## Al - Kabair

---

Mama akajibu: "Mjumbe wa Allah ﷻ yeye anaswali sana, anafunga sana na anatoa zaka sana." Mtukufu Mtume ﷺ alimuuliza: "Vipi kwako anakutizama?"

Akajibu: "Ewe Mjumbe wa Allah ﷻ mie nimemkasirikia." Mjumbe wa Allah ﷻ akauliza: "Kwa nini?"

Akasema: 'Anamfadhilisha mke wake na mimi ananiasi.' Mtume ﷺ akamwambia: "Hasira za mama Al-Qamah zimezuia ulimi wa 'Al-Qamah kutamka Shahada."

Kisha Mtume ﷺ akasema: "Ewe Bilal nenda kanikusanyie kuni nyingi."

Yule mama akasema: "Ewe Mjumbe wa Allah unapanga kufanya nini?" Mtume ﷺ akajibu: "Nitamchoma kwa moto mbele ya macho yako."

Mama 'Al-Qamah akasema: 'Ewe Mtume wa Allah yeye ni mwanangu! Na moyo wangu hautovumilia kuchomwa mbele yangu!' Mtume ﷺ akamwambia: "Ummu 'Al-Qamah adhabu ya Allah ni kali na ya kudumu! Huyu ukitaka Allah amsamehe, basi msamehe kwa Yule ambaye Nafsi yangu ipo Mikononi Mwake 'Al-Qamah haitomfaa Swala, Funga, na Zaka yake ikiwa wewe utaendelea kumkasirikia."

Mama 'Al-Qamah akasema: "Ewe mjumbe wa Allah mimi ninamshuhudia Allah Mtukuka na malaika Wake na waislamu waliohudhuria kuwa mashahidi kuwa mimi ni radhi kwa mwanangu 'Al-Qamah." Mjumbe wa Allah ﷻ akasema: "Ewe Bilal nenda kwake na uangalie je ataweza kukusema: La illah illa Allah au havezi? pengine Ummu 'Al-Qamah amesema kisicho moyoni mwake kwa kunionea haya mimi tu."

Hapo Bilal akaenda na wakati anaingia mlangoni akamsikia 'Al-Qamah akisema: "La illah illa Allah."

Bilal akaingia na kusema: "Enyi watu kwa hakika mama Al-Qamah alimkasirikia mwanawe na ulimi wake ulifungika kutamka shahada, na



## Al- Kabair

---

sasa mama amekuwa radhi naye hivyo ulimi wake umewachwa huru. Kisha siku ile ile 'Al-Qamah alifariki dunia." Mtukufu Mtume ﷺ alikwenda kwake na akatoa amri aoshwe na kuvishwa sanda, na akamswalia na kumzika, tena Yeye Mtume ﷺ akasimama karibu na kaburi lake na akasema mbele ya Muhajiruun na Answaar: " Yeyote kati yenu atakayemtukuza mke wake na akamuacha mama yake Allah na malaika wake wote na watu wote watamlaani. Allah hakubali zaka yako na uadilifu wako hadi ajute kwa Allah Mtukuka, na amfanyie wema mama yake na atake radhi zake, kwani radhi za Allah zinafuatana na radhi za mama yake na ghadhabu za Allah huingizwa na ghadhabu zake. "99

Tunamuomba Allah تعالی atuwafikishe Radhi Zake, na atuepushe na ghadhabu zake, kwa hakika Yeye تعالی ni Mtukufu, Mkarimu, na Mwenye Kurehemu.

\*\*\*

---

<sup>99</sup> Kisa kilichozushwa amepokea Al-'Uqayli katika Adh-Dhua'afaa 3/461, Al-Baihaqi 7892, Ibn Al-Jawzy katika Al-Mawdhu'at 2/78. Laiti watoa hotuba wataacha kukitoa kisa hiki kilichozushwa, wakitaka kutoa visa zipo visa vilivyo sahihi ambazo zinatoshleza kuliko hiki.

DHAMBI KUBWA YA TISA

KUWAKIMBIA NDUGU WA KARIBU

Allah Mtukuka Anasema:

وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ

**"...Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu..." (4:1).**

Yaani: Ogopeni kukata udugu. Na akasema tena Allah تعالی:

أُولَئِكَ الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فَأَصَمَّهُمْ وَأَعَمَّى أَبْصَرَهُمْ

**"Hao ndio Mwenyezi Mungu alio walaani, na akawatia uziwi, na akawapofoa macho yao." (47:23)**

Na akasema tena katika sura nyingine:

الَّذِينَ يُوفُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَلَا يَنْقُضُونَ الْمِيثَاقَ

وَالَّذِينَ يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِ أَنْ يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ سُوءَ الْحِسَابِ

**"Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu, wala hawavunji maagano. Na wale ambao huyaunga aliyo amrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanaikhofu hisabu mbaya.."(13:20-21). Na:**

يُضِلُّ بِهِ

**"huwapoteza"**

Yaani Kwa Qur'an Tukufu:

كثيراً وما يُضِلُّ بِمَةِ إِلَّا الْفَاسِقِينَ ﴿٢٦﴾ الَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ  
وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِمَةِ أَنْ يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ  
الْخٰسِرُونَ ﴿٢٧﴾

**" (Kwa mfano huu) huwapoteza wengi na huwaongoa wengi; lakini hawapotezi ila wale wapotovu, Wanao vunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kwisha ifunga, na wakayakataa aliyo amrisha Mwenyezi Mungu kuungwa, na wakafanya uharibifu katika nchi; hao ndio wenye khasara." (2:26-27)**

Hivyo basi wenye hasara kubwa ni wale wenye kufanya madhambi dhidi ya Muumba. Na yatamsibu yale Allah تعالٰyomuahidi mja wake. Imepokewa katika sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

وقال النبي ﷺ: «لا يدخل الجنة قاطع»

*" Mwenye kukata udugu haingii peponi." <sup>100</sup>*

Atakayekata udugu na jamaa zake dhaifu na kuwahama na kuwafanyia kiburi wala asiwafikishie wema wake na wakati huo yeye ni tajiri na hao wanaokatwa ni fukara atakuwa anaingia katika onyo na tahadhari hii ya kuharamishiwa pepo, ila baada ya kutubia kwa Allah na awafanyie wema. Imekuja katika Hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

*"Mwenye kuwa na jamaa zake masikini na badala ya kuwatizama na kuwapa sadaka wao akawa anawapa watu wengine, basi sadaka yake huwa haipokelewi na Allah siku ya kiyama na hatomtizama, lakini naye akiwa maskini basi inampasa awatembelee na aweke mawasiliano na muungano na kujua hali zao." <sup>101</sup>*

---

<sup>100</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 5984 na Muslim 2556.

<sup>101</sup> Dhaifu: Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Awsat 8/346 na isnadi yake ni dhaifu.

## Al - Kabair

---

Na kauli yake Mtume ﷺ :

*“Shikamana na jamaa zako, japo kwa njia ya kusalimiana tu.”<sup>102</sup>*

Vile vile amesema tena:

«مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلْيُصِلْ رَجْمَهُ»

*“Yeyote anayemuamini Allah na siku ya mwisho, basi na aunge udugu wake.”<sup>103</sup>*

Na katika Hadithi nyingine kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

*“Sie mwenye kuunga yule mwenye kulipiana, bali mwenye kuunga ni yule unapokatwa udugu kwake yeye huunga.”<sup>104</sup>*

Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

وقال ﷺ: «إن الله خلق الخلق، حتى إذا فرغ منهم قامت الرحمة، فقالت: هذا مقام العائذ بك من القطيعة، قال: نعم، أما ترضين أن أصيل من وصلك، وأقطع من قطعك؟ قالت: بلى»<sup>(5)</sup> متفق عليه.

*“Hakika Allah Ameumba viumbe, hadi alipomaliza kuviumba udugu ukasimama ukasema: Hapa ni mahali pakujikinga nawe kutokana na kukatwa udugu, akasema: Ndio, je, huridhiki nimuunge anayekuunga na nimkate anayekukata? Akasema: Kwanini.” (Bukhari na Muslim).<sup>105</sup>*

---

<sup>102</sup> Hadithi Hassan: At-Tabarani 7973, Al-Baihaqi 7972 na Albani ameifanya kuwa ni Hassan katika sahihi Al-Jami' 2838 kwa tamshi 'Ungeni udugu na jamaa zenu hata kwa salamu.'

<sup>103</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6138 kutoka kwa Abu Hurayrah.

<sup>104</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 5991, Abu Dawud 1697, At-Tirmidhi 1908 kutoka kwa Ibn 'Amr.

<sup>105</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bayhaqqi katika Ash-hi'b 7966 na sahihi Al-Jami' 4314.

## Al- Kabair

---

Kutoka kwa 'Ali ibn Al-Hussain رضي الله عنه kuwa alimwambia mwanawe: 'Mwanangu usisuhubiane na mtu ambaye amevunja uhusiano na familia yake. Kwani nimeona katika kitabu cha Allah تعالى kuwa mtu huyu amelaaniwa katika sehemu tatu.'

Abu Hurairah رضي الله عنه akasema: "Yeye amemkataza yoyote aliyevunja ahadi ya kuvunja uhusiano wake na jamaa zake kukaa kwenye kikao hicho." Imepokewa kutoka kwa Abu Hurayra kuwa wakati fulani alikuwa akihadithia kuhusu Mtume ﷺ kuwa alisema:

'Kama yupo yoyote kati yenu amefanya hivyo basi asimame na aondoke. Hakuna aliyesimama isipokuwa kijana mmoja nje ya duara letu. Aliondoka na akaenda kwa dada wa baba yake (Shangazi) ambaye alikuwa hajamzuru kwa miaka mingi kwa dhambi ya kumtaka radhi (kwa tabia aliyokuwa nayo ya kutomtembelea) shangazi akamuuliza nini kilichokuleta hapa?" Yeye akamjibu: "Mimi nilikuwa katika mkusanyiko msikitini na Abu Hurairah رضي الله عنه mfuasi wa Mjumbe wa Allah ﷻ akatuambia kama kuna yeyote aliyevunja uhusiano na jamaa zake katika kikao hicho na aondoke. Shangazi yake akamwambia rudi kwake Abu Hurairah رضي الله عنه na umuulize kwanini alisema hivyo, akarejea, kijana huyo kwake Abu Huraira na kumuelezea nini kimetokea baina yake na shangazi yake na akamuuliza: "Kwanini humruhusu mtu anayevunja udugu katika **darsa** yako? Abu Hurairah رضي الله عنه akamjibu: Mimi nimemsikia Mjumbe wa Allah ﷻ akisema:

*"Kwa hakika rehema haiteremki kwa watu ndani yao kuna mkata udugu."*<sup>106</sup>

---

<sup>106</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na Al-Bukhari katika Al-Adab Al-Mufrad, Dhaifu Al-Jami' 1463 na Dhaifu al-adabu al-Mufrad 14.

## KISA

Imehadithiwa kuwa tajiri alikwenda kuhiji Makka, alipofika aliacha mali yake kiasi cha dinari elfu moja kwa mtu aliyekuwa akisifika kwa kutunza amana. Baada ya kisimamo cha 'Arafa na kurudi Makka alimkuta mtu yule ameshakufa. Akawauliza familia yake kuhusu mali yake, akajua kuwa hawakuwa na taarifa ya mali ile na hivyo alikwenda kwa wanazuoni wa Makka na kumjulisha hali yake na mali yake wakamwambia: 'Ikifika katikati ya usiku njoo katika maji ya Zamzam uangalie ndani yake, akaita ewe fulani ikiwa ni mtu wa peponi itakuitikia kwa mara ya kwanza tu, mtu yule akaondoka na akaita ndani ya Zamzam na hakuitikiwa na yeyote, wakaenda kwao na akawaambia wakasema: "Inna Lillahi waina Ilayhi Rajiu'un." Tunahofia isije ikawa sahibu yako ni mtu wa motoni, nenda katika ardhi ya Yemen kuna kisima kiitwacho Barhuut inasemekana kuwa ndio mdomo wa Jahannam angalia huko usiku, kisha uite ikiwa ni katika watu wa motoni ataitika, akaelekea hadi Yemen na kuulizia kisima na kuelekezwa, akafika usiku na akaangalia ndani yake akaita ewe fulani, akamjibu akamuuliza, 'Ipo wapi dhahabu yangu?' Akamjibu: 'Nimeifukia sehemu fulani nyumbani kwangu na sikumuamini mtoto wangu, nenda ukachimbe huko utaipata.' Akamuuliza: 'Ni nini kilichokuteremsha hapa wakati ambapo sisi tunakudhania kheri?' Akajibu: 'Nilikuwa na dada yangu fakiri nikamuhama na nilikuwa simuonei huruma, Allah akaniadhibu na kuniteremsha hapa."<sup>107</sup> Na kusadikisha maneno hayo katika Hadithi sahihi kutoka kwa Mtume ﷺ:

« لا يدخل الجنة قاطع »

*"Haingii peponi mkataji udugu."*

Yaani mwenye kukata udugu wa watu kama vile: dada, mjomba, shangazi, mtoto wa dada na wengine katika jamaa wa karibu. Tunamuomba Allah ﷻ atuongoze ili tufuate amri zake. Hakika Yeye ﷻ Mkarimu Mkubwa, na Mwenye ukarimu.

---

<sup>107</sup> Hii hekaya haikuswihi.

## DHAMBI KUBWA YA KUMI

### ZINAA

Baadhi yake ni makubwa kuliko mengine.

Allah Mtukuka amesema:

وَلَا تَقْرَبُوا الزَّيْفَ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

***“Wala msikaribie uzinzi. Hakika huo ni uchafu na njia mbaya.” (17:32)***

Na akasema tena Ta’ala:

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ  
وَلَا يَزْنُونَ<sup>٤</sup> وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَامًا ﴿٣٣﴾ يُضْعَفُ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ  
وَيَخْلُدُ فِيهِ مُهَانًا ﴿٣٤﴾ إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا فَأُولَئِكَ يُبَدِّلُ  
اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ<sup>٥</sup> وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٣٥﴾

***“Na wale wasio mwomba mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawau nafsi aliyo iharimisha Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa haki, wala hawazini - na atakaye fanya hayo atapata madhara, Atazidishiwa adhabu Siku ya Kiyama, na atadumu humo kwa kufedheheka. Isipo kuwa atakaye tubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu”. (25:68-70)***

Na akasema tena katika aya nyingine:

الرَّائِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ وَلَا تَأْخُذْكُم بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ  
إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَيَشْهَدَ عَذَابُهُمَا طَآئِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

***“Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mtandikeni kila mmoja wao bakora mia. Wala isikushikeni huruma kwao katika hukumu ya Allah, ikiwa nyinyi mnamuamini Allah na Siku ya Mwisho. Na lishuhudie adhabu yao kundi la Waumini.” (24:2)***

Wanazuoni wamesema: Hii ni adhabu ya mzinifu mwanamke na mwanamume duniani wakiwa si wanandoa, ikiwa wenye ndoa au walisha oa japo mara moja katika umri, watapigwa mawe hadi wafe. Kadhalika imethibiti katika Sunna kutoka kwa Mtume ﷺ, wakiwa hawajapata kisasi duniani na wakafa bila ya toba basi wataadhibiwa motoni kwa bakora za moto. Kama ilivyokuja katika Zaburi: “Hakika wazinifu wataningi’inizwa motoni kwa tupu zao, kisha watachapwa mijeledi ya moto, akiomba uokozi wa adhabu Zabaniya atamuita: ‘Sauti hii ilikuwa wapi, nawe ukicheka na kufurahi wala humjali Allah Taalaa? wala humsitahi?! Imethibiti kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

وقال -عليه الصلاة والسلام-: «لا يزني الزاني حين يزني وهو مؤمن، ولا يسرق السارق حين يسرق وهو مؤمن، ولا يشرب الخمر حين يشربها وهو مؤمن»<sup>(٧)</sup>.

*“Hazini mzinifu wakati anapozini awe ni muumini, wala haibi mwizi wakati anapoiba awe ni muumini, wala hanywi pombe wakati anapoinywa awe ni muumini, wala hapokonyi kitu chenye heshima, watu wananyanyua macho yao kwake pindi anapokipokonya awe ni muumini.”<sup>108</sup>*

Na akasema Mtume ﷺ:

<sup>108</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/276, Al-Bukhari 2475, 6772, Muslim 57 kutoka kwa Abu Hurayrah.



## Al- Kabair

---

« إذا زنى العبد خرج منه الإيمان فكان كالظلة على رأسه ثم إذا أقلع رجع إليه  
الإيمان »

*"Mja wa Allah anapozini imani yake inatoka, kama kivuli kichwani  
mwake kisha aking'oka inarudi imani."*<sup>109</sup>

Katika Hadithi nyingine amesema ﷺ:

« من زنى أو شرب الخمر نزع الله منه الإيمان كما يخلع الإنسان القميص  
من رأسه »

*"Atakayezini au kunywa pombe Mwenyezi Mungu anaondosha  
imani kama mtu anavyovua kanzu kutoka kichwani mwake."*<sup>110</sup>

Katika Hadithi ya Mtume ﷺ amesema:

« ثلاثة لا يكلمهم الله يوم القيامة ولا ينظر إليهم ولا يزكّيهم ولهم عذاب  
أليم، شيخ زان، وملك كذاب وعائل مستكبر »

*"Watatu Allah hatozungumza nao siku ya kiyama wala  
hatowaangalia wala hatowatakasa na wana adhabu kali, mzee  
mzinifu, mfalme mwongo na maskini mwenye kiburi."*<sup>111</sup>

Na kutoka kwa Ibn Masud amesema: Nilimuuliza Mjumbe wa Allah ﷻ ni  
dhambi gani kubwa mbele ya Allah? Mtume ﷺ akamjibu:

« أن تجعل لله ندا وهو خلقك »

*"Ni kumshirikisha Allah wakati ndiye aliyekuumba."*

---

<sup>109</sup> Sahihi: Imepokewa na Abu Dawud 4690, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 4979 kutoka kwa Abu Hurayra na kusahihishwa na Al-Albani katika As-Swahiha 509, na sahihi Al-Jami'.

<sup>110</sup> Dhaifu: Imepokewa na Al-Hakam 1/22, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 4981 na kudhoofishwa na Al-Albani katika Adh-Dhwaifa 1274 kutoka kwa Abu Hurayrah.

<sup>111</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 107 na An-Nasai 5/86 kutoka kwa Abu Hurayrah.

## Al - Kabair

---

Nikasema: Kwa hakika hilo ni kubwa, kisha lipi? Mtume ﷺ akasema:

« أن تقتل ولدك خشية أن يطعم معك »

*"Ni kumuua mwanao kwa woga wa kula pamoja nawe."*

Nikauliza, 'Kisha ipi?' Mtume ﷺ akasema:

« أن تزني بحليلة جارك »

*"Kuzini na mke wa jirani yako."*

Allah akateremsha aya kusadikisha hayo:

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ  
وَلَا يَزْنُونَ<sup>٤</sup> وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَامًا ﴿٥﴾ يُضْعَفُ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَيَخْلُدُ  
فِيهِ<sup>٦</sup> مُهَانًا ﴿٦﴾ إِلَّا مَنْ تَابَ ﴿٧﴾

***"Na wale wasio mwomba mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawai nafsi aliyo iharimisha Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa haki, wala hawazini - na atakaye fanya hayo atapata madhara, Atazidishiwa adhabu Siku ya Kiyama, na atadumu humo kwa kufedheheka. Isipo kuwa atakaye tubu...." (25:68-70)***

Angalia jinsi Allah anavyofananisha uzinifu kwa mke wa jirani na kumshirikisha Allah na kuua Nafsi ambayo Allah ameharamisha kuiuwa ila kwa haki, na Hadithi hii imo ndani ya sahihi mbili.

Katika sahihi Al-Bukhari kuna Hadithi ya ndoto ya Mtume ﷺ aliyoota iliyopokelewa na Samura bin Jundub, ambayo Jibril na Mikail walikuja na wakasema:

## Al- Kabair

---

“Tulikwenda na kulifikia shimo ambalo lilikuwa kama tanuri, na kusikia sauti za kilio kutoka shimoni, tulichungulia na tukaona wanaume na wanawake wakiwa uchi, waliokuwa wakilia wakati moto ukiwachoma kutoka chini yao. Nikamuuliza Jibril nani hawo? Jibril alijibu: “Wanaume na wanawake ambao moto ulipowajia tulipiga mayowe kwa namna ulivyokuwa mkali walitenda zina na hii ni adhabu yao itaendelea hadi siku ya kiyama.”<sup>112</sup>

Tunamuomba Mwenyezi Mungu msamaha.

Kutoka kwa 'Atwa katika kueleza maana ya kauli ya Allah kuhusu Jahannam:

هَٰذَا سَبْعَةُ أَبْوَابٍ

**“ Ina milango saba...” (15:44)**

Anasema Mlango wenye maumivu zaidi, joto, majonzi na matatizo na harufu kali inayonuka ni mlango wa wale watenda zina ambao walifanya tendo hilo baada ya kuwa na elimu yake.<sup>113</sup>

Kutoka kwa Makhuul Ad-Dimishq amesema: Watu wa motoni watasikia harufu kali yenye kunuka na hivyo kuuliza: ‘Harufu hii inatokea wapi?’ Wataambiwa: ‘Hii ni harufu ya tupu za wazinifu.’<sup>114</sup>

Ibn Zaid mmoja wa wanazuoni wa tafsiri amesema: “Watu wa motoni wataudhika na harufu mbaya ya wazinifu.”<sup>115</sup>

---

<sup>112</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 1386, Ibn Hibaan 655 na At-Tabarani katika Al-Kabiir 6984.

<sup>113</sup> Ibn Al-Jawziy katika ‘Kuelezea ubaya wa maovu.’ 157.

<sup>114</sup> Ibn Al-Jawziy katika ‘Kuelezea ubaya wa maovu.’ Uk 155, 156 insadi yake ni Mu’dhal.

<sup>115</sup> Imepokewa na Al-Kharaitwiyy katika ‘Maadili maovu.’ Kutoka kwa ‘Ali bin Abi Talib katika Hadithi ndefu.

## Al - Kabair

---

Hizo ni katika aya kumi alizoandika Allah kwa Musa ni kuwa: Wala usiibe, wala usizini na ufiche uso wako, ikiwa haya ndio hali ya maneno ya Allah kwa Musa vipi kwa mwingine.?!

Imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ :

*"Iblisi anatuma jeshi na kuyasambaza ardhini na huwaambia: 'mwenye kumpoteza Muislamu nitamvalisha taji kichwani mwake, kikubwa zaidi ni fitna, anakuja mmoja wao na kumwambia: Sikumuacha fulani hadi alipompa talaka mke wake. Shetani anamwambia: Hujafanya kitu kwa mtu huyo kwani atamuoa mke mwingine, kisha atakuja mwingine sikumuacha fulani bin fulani hadi yeye na nduguye wakawa maadui, Shetani atasema hujafanya kitu watapatana hao. Mwingine atakwenda kwake na kumuambia miye sikumuacha fulani bin fulani mpaka akazini, hapo Iblisi atasema: Naam, ulichofanya ni kizuri na hivyo atamuita amsogele na kumvisha taji kichwani mwake."*<sup>116</sup>

Tunaomba himaya yako Allah utulinde dhidi ya uovu wa Shetani na askari wake.

Kutoka kwa Anas رضي الله عنه amesema: Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*" Hakika imani ni juba la Allah humvalisha amtakaye, hivyo mtu akitenda tendo la zina Allah humvua juba hilo la imani lakini akijuta na kutubia basi humrudisha."*<sup>117</sup>

Imepokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ :

---

<sup>116</sup> Imepokewa na Abu Nu'aim katika Al-Hilyat 8/128 na sanad yake ni dhaifu, Muslim 283 kutoka katika Hadithi ya Jaabir.

<sup>117</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na Al-Baihaqi 4981 na kudhoofishwa na Al-Baani katika Adh-Dhwaifa 1274.

## Al- Kabair

---

*“Enyi kundi la waislamu iogopeni zina, kwani ina mambo sita, matatu yatampata mtu hapa duniani na matatu siku ya akhera. Ama ya hapa duniani kwa wale watendao zina ni kuwa nuru yao itapotea usoni, maisha yao yanafupishwa, na hupata ufukara. Ama yale ya siku ya mwisho ni kuwa Allah Mtukuka ataghadhibika juu yake, na hesabu yake itakuwa kali, kaburini atapewa adhabu na atatiwa motoni na kupata adhabu motoni.”<sup>118</sup>*

Kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

*“Atakayekufa akiwa amekazania kunywa pombe Allah atamnyweshwa katika mto wa Al-Ghautwa nao ni mto unaopita motoni katika tupu za malaya (wenye kuzini).”<sup>119</sup>*

Yaani maji hayo ya mto hupita katika tupu zao na katika vyuma vya moto kisha maji hayo hunywa aliyekufa hali anaendelea kunywa pombe. Mtume ﷺ amesema:

*“Hakuna dhambi kubwa baada ya ushirikina kuliko mtu kumwaga mbegu yake katika tupu isiyo halali yake.”<sup>120</sup>*

Na amesema vile vile:

*“Katika Jahannam kuna bonde lenye nyoka wengi na kila nyoka mnene kama shingo ya ngamia humgonga mwenye kuacha Swala na sumu yake kuchemka mwilini mwake mara sabini, kisha ngozi yake inatoka. Katika Jahanamu kuna bonde liitwalo Jib Al-Huzni*

---

<sup>118</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na Ibn 'Addiy 6/317 na Al-Kharaitwi katika maadili mabaya 476 nayo ni Hadithi ya uongo mno. Imefanyiwa Tahqiq na Al-Bani katika As-Silsila 141, 142.

<sup>119</sup> Dhaifu: Imepokewa na Ahmad 4/399, Ibn Hibaan 5346 na kudhoofishwa na Al-Bani katika Adh-Dwaif al-Jami' 2597.

<sup>120</sup> Dhaifu: Imepokewa na Ibn Al-Jawziy katika kushutumumu matamaniao ukurasa 154 na kudhoofishwa na Al-Albani katika Adh-Dhwaifa 1580.

*ambamo mna nyoka na tandu na kila tandu kwa ukubwa wake ni kiasi cha mnyama wa kupandwa (nyumbu) ana kucha sabini na katika kila ukucha ni wenye kutoa sumu, kisha mzinifu hupigwa na kuenezwa sumu yake kutoka katika kiwiliwili chake anapata maumivu uchungu wake ni mara miaka elfu, kisha damu na usaha unatoka kwenye tupu yake...*<sup>121</sup>

Kadhalika imepokewa kutoka kwake kuwa:

*“Endapo mtu akitenda zina na mwanamke, aliyeolewa, basi kaburini mwake kutakuwa na adhabu sawa na nusu ya adhabu ya umma. Siku ya kiyama Allah Mtukuka atahesabu kitendo hicho na kumpa mumewe mema ya huyu ikiwa mumewe hakuwa na habari ya kitendo hicho, ikiwa alijua na akakaa kimya Allah atamuharamishia pepo kwani kwa hakika Allah Mtukuka ameandika mbele ya mlango wa peponi: “Unazuiliwa wewe usie na wivu.”*<sup>122</sup>

Imepokewa vile vile:

*“Mwenye kuweka mkono wake kwa mwanamke asiye halali yake kwa matamano atakuja siku ya kiyama huku mikono yake imefungwa shingoni mwake. Akimbusu midomo yake itakatwa motoni, na atasema: Mimi nimepanda ya haramu, Allah atamuangalia kwa jicho la ghadhabu, nyama ya uso wake itaanguka na kusesitiza, na kusema: Sijafanya kitu na hapo ulimi wake utashuhudia: Mimi kwa yasiyokuwa halali kwangu nimetamka, na mkono wake atasema: Mimi katika ya haramu nimeshika, na macho yake yatasema: Mimi katika ya haramu nimeangalia. Na miguu yake itasema: Mimi katika yasiyo ya halali nimekwenda, na tupu yake kusema: Mimi nimefanya. Na anasema muhifadhi katika Malaika: Na mimi nimesikia, na mwingine atasema: Nami nimeandika, Allah atasema: Nimeona na nimeyaficha.”*

---

<sup>121</sup> Dhwaifu: Imepokewa na Ahmad 4/191 katika isnadi yake kuna udhaifu.

<sup>122</sup> Sikuiona Hadithi hii.

## Al- Kabair

---

Kisha Allah Ta'ala Atasema: "Ewe Malaika wangu mchukueni na muonjesheni Adhabu Yangu, kwani Ghadhabu Yangu imezidi kwa ambaye haya yake imepungua Kwangu."

Na usadikisho wake uko kwenye kitabu cha Allah:

أَتَاتُونَ الذُّكْرَانَ مِنَ الْعَلَمِينَ ﴿٢٤﴾ وَتَذَرُونَ مَا خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ ۗ إِنَّكُمْ  
قَوْمٌ عَادُونَ ﴿٢٥﴾

**"Siku ambayo zitawashuhudia ndimi zao na mikono yao na miguu yao kwa waliyo kuwa wakiyatenda." (24:24)**

Zina ambayo ni chafu zaidi ni zina na mama au dada au mke wa baba na watu wa karibu na jamaa na imethibiti katika Al-Hakam:

«مَنْ وَقَعَ عَلَى ذَاتِ مُحْرَمٍ فَاقْتُلُوهُ»

*"Yeyote atakayezini na maharimu wake (Mahram) basi muueni."*<sup>123</sup>

Kutoka kwa Al-Bara<sup>رضي الله عنه</sup> anatoa taarifa kuwa Mtukufu Mtume<sup>عليه السلام</sup> alimtuma mjomba wake kwa mtu aliyemuoa mke wa baba yake (mtu huyo) na akamuamuru kuwa amuue huyo mtu na achukue khums (moja ya tano).<sup>124</sup>

Tunaomba himaya ya Allah<sup>تعالى</sup> mkuu wa rehema kutusamehe madhambi yetu, kwani hakika Yeye<sup>تعالى</sup> Ndiye Mwenye Rehema na Mkarimu Mkubwa.

\*\*\*

---

<sup>123</sup> Dhaifu: Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Awsat 9350, Al-Kabiir 11565, Al-Hakam 4/356, Al-Baihaqi 8/237 na Hadithi ni dhaifu.

<sup>124</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 4/292, 297, Abu Dawud 4456, An-Nasai 6/109, Ibn Majah 2607 na kusahihishwa na sahihi Ibn Majah 2113.

## DHAMBBI KUBWA YA KUMI NA MOJA

### LIWATI

Allah Mtukuka ametusimulia kisa cha kaumu ya Luti zaidi ya sehemu moja, na katika hayo ni Kauli yake Taala:

فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا جَعَلْنَا عَلَيْهَا سَافِلَهَا وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ ﴿٨٢﴾

**"Basi ilipo fika Amri Yetu Tuliigeuza nchi juu chini, na Tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu ...." (11:82).**

Yaani, kutokana na udongo uliochomwa:

مَنْضُودٍ ﴿٨٣﴾

**'mgumu'**

Yaani: ulioshikamana bara bara:

مُسَوَّمَةٌ ﴿٨٤﴾

**'Zilizo tiwa alama'**

Kuwa mawe haya si mawe yaliyozoeleka ya watu wa duniani:

عِنْدَ رَبِّكَ ﴿٨٥﴾

**'kwa Mola wako Mlezi'**

Yaani kutoka katika hazina Yake ambayo hawezi kuyatumia ila kwa idhini yake tu.



وَمَا هِيَ مِنَ الظَّالِمِينَ بَعِيدٍ ﴿٥٦﴾

**'Na haya hayako mbali na wenye kudhulumu wengineo'.**

haya hayako mbali kwa madhalimu wa Ummah huu wanapotenda kitendo chao kuwajalia adhabu ilo washukia wao. Kwa ajili hii Mtume ﷺ amesema:

*"Ninachokihofia kwenu ni kitendo cha kaumu Luutw. "*<sup>125</sup>

Na akamlaani mara tatu anayefanya kitendo hicho akasema:

وعنه ﷺ قال: «لعن الله من عمل عمل قوم لوط»

*"Allah amlani anayefanya matendo ya kaumu Luutw, Allah amlani anayefanya matendo ya kaumu Luutw, Allah amlani anayefanya matendo ya kaumu Lut. "*<sup>126</sup>

Katika Hadithi nyingine amesema ﷺ:

قال النبي ﷺ: «أقتلوا الفاعل والمنفعل به»

*"Mtakayempata akifanya kitendo cha kaumu Luutw basi muueni mtenda na mtendewa. "*<sup>127</sup>

Ibn 'Abbas رضِيَ اللهُ عَنْهُمَا amesema: 'Linaangaliwa jumba refu zaidi katika mji na anarushwa halafu na kupigwa na mawe (hadi kifo) kama ilivyokuwa kwa kaumu ya Luutw.'

---

<sup>125</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 3/382, At-Tirmidhi 1482, Ibn Majah 2563 na kusahihishwa na Al-Albani katika sahihi Ibn Majah 2077 na sahihi Al-Jami' 1552.

<sup>126</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/317, 309, Al-Kharaitwi katika kitabu chake 'Tabia mbaya.' 437 na sahihi Al-Jami' 5891.

<sup>127</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/300, Abu Dawud 4462, At-Tirmidhi 1481, Ibn Majah 2561 na sahihi Al-Jami'.

## Al - Kabair

---

Wanazuoni wa Kiislamu wamekubaliana kuwa Liwati ni katika madhambi makubwa aliyoharamisha Allah. Allah Amesema:

أَتَأْتُونَ الذُّكْرَانَ مِنَ الْعٰلَمِينَ ﴿١٦٥﴾ وَتَذُرُونَ مَا خَلَقَ لَكُمْ رَبُّكُمْ مِنْ أَزْوَاجِكُمْ ۚ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ عَادُونَ ﴿١٦٦﴾

**" Je! Katika viumbe vyote mnawaingilia wanaume? Na mnaacha alichu kuumbieni Mola wenu Mlezi katika wake zenu? Ama kweli nyinyi ni watu mnao ruka mipaka! " (26:165-166)**

Yaani wanaipita halali na kuiendea haramu, Allah Ta'ala Amesema:

وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْحٰكِمُونَ ﴿٧٤﴾ وَعَلِمًا وَبِحَيْرَتِهِ مِنَ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ تَعْمَلُ الْخَبِيثٰتِ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا سَوِيًّا ﴿٧٥﴾

**" Na Luut'i Tukampa hukumu na ilimu na Tukamwoko na ule mji ulio kuwa ukifanya maovu. Hakika hao walikuwa watu wabaya, wachafu.." (21:74)**

Jina la mji wao lilikuwa linaitwa Sodom,<sup>128</sup> na watu wa mji huo walikuwa wakifanya mambo machafu aliyoyataja Mwenyezi Mungu katika kitabu chake, yaani walikuwa wakiwaingilia wanaume katika duburi zao pamoja kutangaza katika vilabu vyao na maovu mengine.

Imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا kuwa amesema: Tabia kumi ni kaumu ya Luutw: 'Kuchoma nywele, kutofunga vizuri vifungo, kutupa kwa kutumia vijiti, kucheza na njiwa, kupiga mbinje kwa vidole, kufungua shati kwa kuonyesha kifua, unywaji pombe, uvaaji wa suruali refu zinazoburura chini na kulawitiana, na kitakachoongezeka katika Umma huu ni wanawake kusagana.'

---

<sup>128</sup> Hii ni jina la vijiji vitatu kwa pamoja vilivyopo katika ya mji wa Madina na Shaam.

## Al-Kabair

---

Imekuja kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ amesema:

ويروى عن النبي ﷺ أنه قال: «سَحَاقُ النِّسَاءِ زِنَاءٌ بَيْنَهُنَّ»

*"Kusagana wanawake baina yao ni zina." (Dhaifu: Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Kabair 22/63, 153, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 5082 na amesema Al-Bani dhaifu angalia As-Silsila Adh-Dwaifa 1601.*

Kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه amesema: Amesema Mtume ﷺ

*"Wanne wanapambazuka katika ghadhabu ya Allah, na wanakuchwa katika ghadhabu ya Allah."*

Ikaulizwa, 'Ni nani hao ewe Mtume?' Akasema:

*"Wanaume wanaowaiga wanawake, na wanawake wanaoiga wanaume, wale wanaofanya mapenzi na wanyama, na wanaume wanaolawitiana (Mume kwa mume)." (Hadithi hii ina daraja ya Munkar, imepokewa na Bayhaqi katika shiib 5385)*

Inasemekana kuwa wakati mwanaume anampanda mwanamume mwenzake, kiti kitakatifu ('Arshi) hutetemeka kwa kuogopa adhabu ya Allah تعالى na mbingu hutetemeka na malaika husoma: *"Qul Huwa Liwahu Ahad."* Hadi mwisho hadi ghadhabu za Allah zitulie." <sup>129</sup> na <sup>130</sup>

Imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

*"Saba wamelaaniwa na Allah wala hatowaangalia siku ya kiama, na atasema: Ingieni motoni pamoja na watakaoingia: Mfanyaji na*

---

<sup>129</sup> Dhaifu: Amesema Al-Mundhiri: Imepokewa na At-Tabarani na Al-Baihaqi kutoka kwa njia ya Muhammad bin Salaam Al-Khuzai' wala hafahamiki baba yake kutoka kwa Abu Hurayrah, Al-Bukhari amesema Hadithi yake haifuatwi. Hadithi ni dhaifu.

<sup>130</sup> Imepokewa na Ibn Al-Jawziy katika kuchukizwa na matamano uk 160 kutoka kwa 'Umar na Hadithi ni maudhu'.

## Al - Kabair

---

*anayefanyia (wanaolawitiana), anayefanya mapenzi na wanyama, na yule anayemuingilia na kumuoa mama na mwanae wa kike na mwenye kuoa mkono wake (punyeto) isipokuwa wakitubu.”<sup>131</sup>*

Imepokewa kuwa watu watafufuliwa siku ya kiama na mikono yao ikiwa na mimba kutokana na zina ambayo walikuwa wakiichezea duniani. Imepokewa kuwa katika jumla ya michezo ya watu wa kaumu ya Luutw ni: mchezo wa domino, kushindanisha njiwa, kupiganisha mbwa, kondoo kuchomana pembe au majogoo kudonoana, kuingia bafuni uchi, na kupunja vipimo na mezani. Ole wao watakaofanya hivyo.

Kuna mapokezi kuwa mwenye kucheza na njiwa Qallabah hatakufa ila baada ya kuonja uchungu wa ufukara.

Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُم alisema endapo mtu anayetenda liwati na akafa bila ya kutubia, basi hugeuzwa nguruwe kaburini.<sup>132</sup> Na amesema Mtukufu Mtume ﷺ :

*“Allah hatomtimzama mtu aliyemlawiti mwanamume mwenzake au mwanamke katika duburi.”<sup>133</sup>*

Abu Said As-Swa'aluki amesema: Katika Umma huu kutakuwa na kundi liitwalo Al-Luutwiyuun (watu wenye tabia za watu wa Luutw) nao wapo aina tatu: Kundi la wenye kuangalia (matendo yale), kundi lenye kushangilia, na kundi lenye kufanya matendo hayo ya kikhabithi.<sup>134</sup>

---

<sup>131</sup> Dhaifu: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 5087 na kudhoofishwa na Ash-Shaikh katika Adh-Dhwaifah 319.

<sup>132</sup> Dhaifu: Imepokewa na Ibn Al-Jawziy katika Hadithi maudhui 3/113 kutoka kwa Ibn 'Abass na akasema: Haifai na imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 5018 kutoka kwa Ibn Siirin ikiwa ni Mawquuf.

<sup>133</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/297, At-Tirmidhi 1165 kutoka kwa Ibn 'Abass na ni Hassan kulingana na At-Timidhi katika sahihi sunan At-Tirmidhi na Al-Mishkaat 3195 na sahihi Al-Jami 7801.

<sup>134</sup> Dhaifu: Imepokewa na Al-Baihaqi 5019 na sanadi yake ni dhaifu mno.

## Al- Kabair

---

Kumtizama kwa jicho la matamano mwanamke na mwanamume ni katika zina, kama alivyosema Mtukufu Mtume ﷺ:

*“Zina ya macho ni kuangalia, zina ya ulimi ni mazungumzo, zina ya mkono ni kushika, zina ya mguu ni mwendo na zina ya sikio ni kusikiliza. Moyo una matamano na hamu na sehemu za siri ima zinakubali au kunyima.”<sup>135</sup>*

Na kwa ajili ya hiyo waja wema kuwasifia wanaume walichukua hadhari kubwa ya kutokuchanganyika na watoto wa kiume wazuri na kuwaangalia na kuchanganyika nao. Al-Hassan bin Dhukraan amesema: ‘Msikae pamoja na wavulana wa kitajiri sura zao kama wanawali. Wao ni hatari kuliko wanawake.’<sup>136</sup>

Baadhi ya Taabi’ina wamesema: Mimi simuhofii kijana anayefanya ibada kwa wanyama wenye kudhuru kuliko kijana wa kiume (*Amrad*) anayekuwa nae.

‘Ilikuwa ikisemwa: Kijana hakai pamoja na kijana mzuri sehemu moja’<sup>138</sup>.

Baadhi ya wanazuoni wanakataza wanaume wakubwa kukaa peke yao na watoto wa kiume vijana ndani ya nyumba au dukani au bafuni kwa msingi wa kuwa kufananisha kuwa amekaa pamoja na mwanamke mgeni kwa sababu Mtukufu Mtume ﷺ amesema:

*“Mwanamume hakai faragha na mwanamke isipokuwa shetani huwa wa watatu wao.”<sup>139</sup>*

---

<sup>135</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/411, At-Twahawi katika Mushakal Al-Athar 3/298 kutoka kwa Abu Hurayra kwa tamshi ‘Macho mawili yanazini.’ Imesahihishwa na Al-Albani katika sahihi Al-Jami’ 4150, Irwaa 2370, Ahmad 2/239, Al-Bukhari 6243, Muslim 2657 kwa tamshi, ‘Hakika Allah ameandika kwa mwanadamu.’

<sup>136</sup> Dhaifu: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi’b 5014 na isnadi yake ni dhaifu.

<sup>138</sup> Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi’b 5015 na Ibn Al-Jawziy katika mabaya ya matamano uk 92.

<sup>139</sup> Sahihi: Imepokewa na At-Tirmidhi 165, Ibn Majah 2363 na kusahihishwa na Al-Albani katika sahihi At-Tirmidhi 1757.

## Al - Kabair

---

Kuwa wanaume (*Amrad*) wanaowazidi wanawake kwa uzuri wao, mtihani wao ni mkubwa zaidi na inawezekana akafanyiwa jambo la shari zaidi ya mwanamke. Na yanaingia mashaka na uovu upande wake kuliko ya mambo hayo kwa upande wa wanawake. Hivyo ni bora kuharamisha hilo.

Siku moja Sufyan Thawri aliingia bafuni na baadaye akaingia mtoto wa kiume mzuri, Sufyan akapiga kelele na kusema: "Mtoeni huyo kijana mbele yangu kwani mimi ninaona katika kila mwanamke yupo shetani na kwa kijana mwenye sura nzuri wapo mashetani wengi."<sup>140</sup>

Mtu mmoja alimzuru Imam Ahmad bin Hanbal akiwa pamoja na mtoto wa kiume mzuri. Imam Ahmad akamuuliza: 'Huyu ni nani kwako?' Akajibu: 'Mtoto wa dada yangu.' Imam Ahmad akamwambia: 'Usije naye tena mara nyingine, wala usitembee naye njiani kwani watu wasiokujua na wasiomjua yeye watakudhania vibaya.'

Imepokewa kuwa ujumbe wa 'Abd Qais ulipokuja kwa Mtume ﷺ alikuwepo pamoja nao mwanamume mzuri, Mtume ﷺ akamuweka nyuma ya mgongo wake na akasema:

*"Ilikuwa fitna ya Nabii Dawud ni kuangalia."*<sup>141</sup>

Na hivyo wakaimba shairi:

*Matukio yote huanza kwa kuangalia  
Na moto mkubwa hutokana na cheche kidogo  
Na madam mtu anakuwa ni mwenye macho anayoyazungusha  
Katika macho ya kheri amesimamishwa hatarini*

---

<sup>140</sup> Imepokewa na Al-Baihaqi 5021 na Ibn Al-Jawziy katika 'Dhami Al-Hawa' uk 94.

<sup>141</sup> Hadithi Maudhu': Imepokewa na Ad-Dailami na Ibn Abi Shayba katika Al-Musanaf 6/342 na akasema Al-Albani katika Adh-Dhwaifa 313 Maudhu' kwa tamshi, 'Kosa la Dawud (a.s) Ilikuwa ni kuangalia.'

**Al - Kabair**

---

*Ni mara ngapi kutazama kumefanya katika moyo wa swahibu wake,  
kitendo cha Mishale isiyo na upinde  
Imemfurahisha anayeangalia na yenye kudhuru akili yake  
Haikaribishwi furaha anayerejea madhara.*

Na inasemwa: 'Kuangalia ni posta ya zina'. na katika hadithi:

*"Kuangalia ni mshale miongoni mwa mishale ya Ibilisi, basi mwenye  
kuiacha kwa ajili ya Allah. Allah ataurithisha moyo wake utamu wa  
ibada anaoupata hadi siku ya kiyama". (Dhaif; al-Hakim 4:313;  
Tabarani: 10362)*

\*\*\*

## MLANGO WA: ADHABU YA ANAYEKUBALI JAMBO HILI NAFSINI MWAKE

Kutoka kwa Khalid bin Al-Waliid رضي الله عنه alimuandikia Abu Bakr As-Swadiq رضي الله عنه kuwa mahali fulani alikuwemo mlawiti mwanamume na mlawitiwa. Abu Bakr رضي الله عنه akashauriana na masahaba wa Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu jambo hilo, 'Ali bin Talib رضي الله عنه alisema: "Hii ni dhambi ambayo hawakufanya watu wengine isipokuwa kaumu ya Luutw na Allah Mtukuka ametuarifu sisi juu ya namna ya kuwatia adabu watu hao, kwa mawazo yangu auawawe mtu huyo kwa moto." Hivyo Abubakar رضي الله عنه akamuandikia Khalid naye akamchoma.<sup>142</sup>

Ali رضي الله عنه amesema: "Mwenye kujitakisha mwenyewe kulawitiwa Allah atampa matamano ya mwanamke na kumfanya shetani mlaaniwa katika kaburi lake hadi siku ya kiama".

Umma umekubaliana kuwa atakayefanya hivyo kwa mtumwa wake basi yeye ni Luutwi muovu, na kilichopokewa kuwa 'Issa bin Maryam alipita katika matembezi yake pindi alipoona moto uliowashwa kwa mtu, 'Issa akachukua maji ili auzime moto, ule moto ukabadilika na kuwa kijana mdogo na yule mtu akabadilika na kuwa moto, 'Issa akashangazwa na hali ile, na akasema: Ewe mola wangu warejeshe katika hali yao walipokuwa duniani ili niwaulize kuhusu habari yao. Hapo tena Allah تعالى akawarudisha hali yao duniani na wakawa mwanamme na mvulana. Nabii Issa عليه السلام akawauliza: "Nini hali yenu? Mwanamume akajibu: "Ewe Roho kutoka Allah nilipokuwa hai nilikuwa ninampenda sana kijana huyu na nikawa nikimlawiti, nilipokufa na mtoto akafa moto ukawa ukiniunguza mimi na wakati mwingine ni zamu ya kumuunguza kijana, hii ikawa ndio adhabu yetu hadi siku ya kufufuliwa kiyama.

Tunajikinga kwa Allah dhidi ya adhabu ya Allah na tunamwomba msamaha na taufiki kwa anayoyapenda na kuyaridhia.

---

<sup>142</sup> Imepokewa na Ibn Abi Dunya na Al-Baihaqi 8/232 na akasema Al-Mundhiri: Ni nzuri.



## FASILI

Kulawiti mke ni aina ya ulawiti, na imekatazwa na Allah تعالی na Mtume wake, Allah ﷺ amesema:

نَسَاؤُكُمْ حَرْتُ لَكُمْ فَأْتُوا حَزَنَكُمْ أَنِّي سَعَيْتُمْ ﴿٢٢٣﴾

**"Wake zenu ni konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo..." (2:223)**

Yaani kusema, ikiwa kuelekeana (kukabiliana) kupeana mgongo katika kilango kimoja yaani sehemu moja tu.

Sababu ya kuteremshwa kwa aya hii ni kuwa wayahudi wakati wa Mtume ﷺ walikuwa wakisema: Ikiwa mtu atamuingilia mkewe katika utupu wa mbele lakini kwa kupitia nyuma mtoto atazaliwa mwenye makengeza. Wafuasi wa Mtukufu Mtume ﷺ wakamuuliza Yeye Mtume ﷺ jambo hilo, Allah تعالی akaiteremsha aya kuwakanushia:

نَسَاؤُكُمْ حَرْتُ لَكُمْ فَأْتُوا حَزَنَكُمْ أَنِّي سَعَيْتُمْ ﴿٢٢٣﴾

**"Wake zenu ni kama konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo..." (2:223)**

'Iwe kwa mbele au kwa nyuma la msingi ni kuingia katika tupu ya mbele (kilango kimoja cha mbele tu)'. Muslim.<sup>143</sup>

Na katika mapokezi: « اتقوا الدبر والحیضة »

*"Epukeni duburi au wakati wa hedhi."*<sup>144</sup>

---

<sup>143</sup> Sahihi: Al-Bukhari 4528, Muslim 1435, At-Tirmidhi 2977, Abu Dawud 2193 na Ibn Majah 1925.

<sup>144</sup> Hassan: imepokewa na Ahmad 1/298, An-Nasai katika At-Tafsiir 260, At-Twabarani 12317, Ibn Hibaan 4190 kutoka kwa Ibn 'Abass kwa sanad Hasan.

## Al - Kabair

---

Na kauli yake: "Katika kilango kimoja nayo ni utupu wa mbele na kuwa hapo ndipo, yaani mahali pa kupanda mtoto, ama duburi ni njia ya kutoa uchafu napo ni pachafu." Imepokewa kutoka kwa Abu Hurayra رضي الله عنه kutoka kwa Mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

« ملعون من أتى حائضاً أو امرأة في دبرها »

*"Amelaaniwa anayemuingilia mwenye hedhi au duburi ya mwanamke."*<sup>145</sup>

At-Tirmidhi amepokea kutoka kwa Abu Hurara رضي الله عنه vile vile amesema: kuwa Mtume wa Allah ﷺ amesema:

« من أتى حائضاً أو امرأة في دبرها أو كاهناً فقد كفر بما أنزل على محمد »

*"Yeyote akimuingilia mwanamke kwenye hedhi au katika duburi yake, au kwenda kwa mganga (kuhani) na kumsadiki kwa hakika amekufuru aliyoteremshiwa Muhammad."*<sup>146</sup>

Hivyo, mtu akimuingilia mke wake hali akiwa na hedhi au katika duburi yake basi amelaaniwa na anaingia katika onyo hili kali. Kadhalika kama atamuendea kuhani, naye ni mnajimu na anayejifanya hujua kitu kilichoibiwa na huzungumzia mambo ya ghaibu hivyo mtu akamuuliza kuhani na kumsadikia.

Watu wengi wajinga wasiokuwa na elimu hutenda madhambi haya kutokana na uhaba wa elimu. Na kuhusu hili Abu Hurayra amesema:

---

<sup>145</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 4/444, 479, Abu Dawud 2162 Juzuu ya pili, kutoka kwa Abu Hurayra sahihi Al-Jami' 5889.

<sup>146</sup> Sahihi: imepokewa na Ahmad 2/408, 486, Abu Dawud 3904, An-Nasai 1/ 78, At-Tirmidhi 135 kutoka kwa Abu Hurayra sahihi Al-Jami' 5942, Al-Mishkaat 551.

## Al - Kabair

---

*'Uwe ni mwenye elimu au mwenye kujifundisha elimu au mwenye kusikiliza elimu au mpenzi wa elimu wala usiwe katika kundi la tano, utaangamia.'*<sup>147</sup>

Mtu wa aina hii ni mtu asiyejua wala hajifunzi, hasikilizi wala hapendi mwenye kufanya hivyo. Na inapasa kwa mja kutubu kwa Allah kwa madhambi yake yote na makosa yake yote. Amuombe Allah تبارك و تعالیٰ msamaha kwa madhambi na makosa wakati wa kutojua kwake, na aombe msamaha katika umri wake uliobakia.

Ewe Allah tunaomba msamaha na afya hapa duniani na akhera na Wewe Ndiye Mrehemevu zaidi.

\*\*\*

---

<sup>147</sup> Hadithi Maudhui: Imepokewa na Al-Bazaar katika musnadi yake 3626, At-Twabarani katika As-Swaghiir 786 na akasema Al-Albani katika dhaifu al-Jami' 100 maudhu'

## DHAMBI KUBWA YA KUMI NA MBILI

### RIBA

Allah Mtukuka Anasema:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوا الرِّبَا أَضْعَافًا مُضَاعَفَةً وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣١٣﴾

**"Enyi mlio amini! Msile riba mkizidisha juu kwa juu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa." (3:130)**

Na Akasema Taalaa:

الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ الَّذِي يَتَخَبَّطُهُ الشَّيْطَانُ مِنَ الْمَسِّ ۗ

**"Wale walao riba hawasimami ila kama anavyo simama aliye zugwa na Shet'ani kwa kumgusa..." (2:275)**

Yaani, hawaamki kutoka makaburini ila wanakuwa kama wale wa aliopagawa na shetani au na kumwanguka "**Hayo**" yaani ambayo yamewasibu

بِأَنَّهُمْ قَالُوا إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا ﴿٢٧٦﴾

**"...ni kwa kuwa wamesema: Biashara ni kama riba..." (2:276)**

Yaani ni halali na hivyo kuhalalisha yale aliyoyaharamisha Allah, Allah akiwafufua watu siku ya kياما watatoka upesi upesi, isipokuwa wale waliochukuwa riba, watasimama na baadaye wataanguka kama wenye kifafa. Kila wakijaribu kuinuka wataanguka kwa sababu wamechukua na kula hapa duniani na Allah تعالى akawajaza matumbo yao vitu vizito ili kutokana na uzito huo hawatoweza kusimama bila ya kuanguka chini watajaribu kuharakisha ili wawe pamoja na watu wengine lakini hawatoweza kufanya hivyo.

## Al- Kabair

---

Qatadah رضي الله عنه<sup>148</sup> alisema: Siku ya kiyama wala riba watafufuliwa wakiwa na wazimu. Hiyo itakuwa ni alama ya wala riba itakayowatambulisha siku ya kiama.<sup>148</sup> Imetoka Kutoka kwa Abu Said Khudri رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

*“Nilipopelekwa Israi nilipita kwa watu matumbo yao yako baina ya mikono yao, kila mmoja wao tumbo lake ni mfano wa nyumba kubwa, na yalikuwa yamepinda ubavuni mwa njia ya uma wa Firauni wakipita asubuhi na jioni kupelekwa kuteswa motoni. Wanaporudishwa, watu wa Firauni walikuwa kama ngamia waliokuwa hoi, hawasikii wala hawafahamu lolote, wanapowahisia wale watu wa matumbo makubwa husimama na miili yao kuwaegemea wala wasiweze kuondoka hadi watakapofunikwa na watu wa Firauni. Hivyo huwarejesha wanapokwenda na wanaporudi, na hii ni adhabu yao katika Barzakh baina ya dunia na akhera.” Akasema ﷺ:*

*“Nikamuuliza Jibril; ni nani hawa?’ Akasema: Hawa ni watu wanaokula riba, hawasimami ila kama wasimamavyo waliopagawa na shetani.”<sup>149</sup>*

Katika riwaya nyingine amesema:

*Nilipopandishwa Miraji mbingu ya saba juu ya kichwa changu, nilisikia sauti ya radi na umeme, Nikaona watu matumbo yao yako mbele yao kama nyumba ndani yake kuna nyoka na ng'e walioweza kuonekana kutoka nje. Nikamuuliza “Nani hawa Jibril? Akanijibu: “Hao ni wala riba.”<sup>150</sup>*

Imepokewa na ‘Abdur-Rahman bin ‘Abdullah bin Mas`ood رضي الله عنه kutoka kwa baba yake akisema:

---

<sup>148</sup> Imepokewa na At-Twabari katika Tafsiir 2/102 na sanadi ya watu wake ni thiqah.

<sup>149</sup> Dhaifu mno: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ad-Dalail 2/390, 397.

<sup>150</sup> Dhaifu mno: Imepokewa na Ahmad na Ibn Majah 2273 nayo ni dhaifu mno katika Al-MiShkaat 2828.

*"Itakapodhihiri zinaa na riba katika kitongoji Allah ataidhinisha kuangamia kwake".<sup>151</sup>*

Kutoka kwa Ibn 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا hadithi ikiwa ni marfu':

*"Watu watakapofanyiana uchoyo kwa dinari na dirham, na kuuziana kwa riba na wakafuata mikia ya ng'ombe na wakaacha jihadi katika njia ya Allah basi Allah atawashushia balaa ambayo haitoondoka kwao hadi warejee katika dini yao."<sup>152</sup> Akasema ﷺ :*

*Haidhihiri katika watu riba isipokuwa kutadhihirika ndani yao wazimu, na haidhihiriki katika watu zina isipokuwa kutadhihirika ndani yao mauti, na watu hawatapunja vipimo na mizani isipokuwa Allah atawanyima mvua".*

Imekuja katika Hadithi ndefu:

*" Hakika wala riba wataadhibiwa tokea watakapokufa hadi siku ya kiama kwa kuogelea katika mto mwekundu wa damu, na atalishwa mawe, nayo ni mali ya haramu aliyokuwa akiikusanya duniani na akipata tabu juu ya hilo, na kulishwa mawe kutokana na moto kama vile alivyokuwa akimeza haramu aliyokuwa akiikusanya duniani. Adhabu hii atakua nayo huko Barzakh kabla ya siku ya kiama pamoja na laana ya Allah juu yake."<sup>153</sup>*

Kama ilivyothibiti kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

*" Wane wana haki kwa Allah asiwaingize peponi wala asiwaonjeshe neema yake: Mnywa pombe, mla riba, mla mali ya yatima bila ya haki na anayewaasi wazazi wake isipokuwa wakitubu."*

---

<sup>151</sup> Hadithi Hasan: Imepokewa na Ahmad 1/393,394-402. Abu Dawud 3333, At-Tirmidhi 1206, Ibn Majah 2277, na Al-Albani ameifanya kuwa ni Hassan katika Al-Irwaa 5/184.

<sup>152</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/42, 84, At-Twabarani katika Al-Kabir 13583, 13585, Abu Dawud 3462 na Sahihi Al-Jaami' 675.

<sup>153</sup> Sahihi: Riwaya ya Al-Bukhari imetangulia.

## Al- Kabair

---

Imepokewa kuhusu wala riba kuwa watafufuliwa katika sura za mbwa na nguruwe kutokana na hila yao ya kula riba kama walivyobadilishwa watu wa *Sabti* (Jumamosi) walipofanya hila ya kuwatoa samaki ambao Allah aliwakataza wasiwavue siku ya Jumamosi, wakawa wanawachimbia malambo wanaangukia humo siku ya Jumamosi wanawachukua siku ya Jumapili. Kutokana na hayo Allah تعالی aliwabadili na kuwageuza kima na nguruwe. Hivi hivi kwa watu wanaofanya aina za hila katika riba, Kwani Allah تعالی hila za wenye hila hazifichiki mbele yake. Ayyub As-Sakhstani anasema: "Walitaka kumdanganya Allah kama wanavyowadanganya watoto. Afadhali kwao kama wangepanya hivyo kwa dhahiri".

Mtume ﷺ amesema:

*"Riba ina milango sabini, mwepesi zaidi ni mtu kumingilia mama yake, na ya kuwa riba kubwa ni mtu kupitiliza katika heshima ya nduguye Muislamu."*<sup>154</sup>

Kwa hiyo ikaswihi kuwa huo ni mkubwa mno miongoni mwa milango ya riba. Na kutoka kwa Anas رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ alituhutubia akataja riba na akakuza jambo lake akasema:

*"Dirhamu ambayo anayoipata mtu kwa ajili ya riba ni kubwa zaidi kuliko zina mara thelathini na sita katika Uislamu."*<sup>155</sup>

Na kutoka kwake Mtume ﷺ vile vile amesema:

« أهونها كالذي ينكح أمه »

*"Nyepesi yake zaidi ni kama kumingilia mama yake."*<sup>156</sup>

---

<sup>154</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 5135, Ibn 'Adi 4/1548 na kusahihishwa na Ash-Shaikh katika sahihi Al-Jami' 3375 nayo ipo kwa At-Tabarani 2703 katika Al-Awsat.

<sup>155</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Majah 2275, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 5131 na kusahihishwa na Al-Albani katika sahihi Al-Jami'.

<sup>156</sup> Sahihi: imepokewa na Ibn Majah 2274, Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 5134 na kusahihishwa na Al-Albani katika sahihi Al-Jami' 3541.

Kutoka kwa Abu Bakri Siddiq رضي الله عنه alisema:

*"Mwenye kuzidisha na mwenye kuzidishiwa ni katika moto".<sup>157</sup>*

Yaani mwenye kuchukua na mwenye kutoa riba wote wataingia motoni." Tunamuomba Allah msamaha.

### **FASILI: ZAWADI YA MDENI**

Ibn Masood رضي الله عنه amesema: 'Unayem dai Akikupa zawadi, usichukuwe kwani ni riba',<sup>158</sup> Al-Hasan رضي الله عنه alisema: 'Ukila ndani ya nyumba ya mdeni ni haramu.' Hii ni kwa kauli ya Mtume ﷺ:

*"Kila mkopo unaoleta faida na manufaa basi ni riba."<sup>159</sup>*

Ibn Masood akasema vile vile: 'Pindi mtu akimletea mdai zawadi na yule mdai akapokea ile zawadi basi itakuwa ni haramu (Suhti).<sup>160</sup> Na kusadikisha hayo kutokana na kauli ya Mtume ﷺ iliyosema:

*"Pindi mtu mmoja akimletea mdai zawadi na yule mdai akapokea zawadi ile, basi mtu huyo atakuwa ameingia katika mlango mpana kati ya milango ya riba." (Imepokewa na Abu Dawud).<sup>161</sup>*

---

<sup>157</sup> Imepokewa na Ibn Abi Shayba katika Al-Musanaf 4/398, Abdur-Razaq katika Al-Musannaf 8/128 na Al-Bazzar katika musnad yake 45 kutoka kwa Abu Bakr ikiwa ni marfu'.

<sup>158</sup> Dhafu: Imepokewa na Al-Baihaqi 5/35 katika njia ya Khalid bin 'Ubaid imepokewa vile vile kutoka kwa Ibn 'Abass na sanad ya kwanza ni dhafu, ameidhoofisha Al-Albani katika Al-Irwaa 1398 na zimekuja riwaya nyingi kutoka kwa Ubay bin Ka'ab na Ibn Mas'ud na Ibn 'Abas kuwa wao walikataza mkopo unaopelekea manufaa na kusahihishwa na Ash-Shaykh katika Al-Irwaa 1397.

<sup>159</sup> Sahihi: Imepokewa na Abdur-Razzaq katika Al-Muswannaf 14664, kutoka kwa Abdillaahi bin Umar kwa tamshi karibu na hilo na isinadi yake ni sahihi

<sup>160</sup> Hadithi Hasan: Imepokewa na Ahmad 5/261, Abu Dawud 3524, At-Twabarani katika Al-Kabir 7853, 7928 kutoka kwa Abu Umama na Al-Albani kuifanya ni Hassan katika sahihi Al-Jami' 6316.

<sup>161</sup> Hasan: Ahmad 5/261, Abu Dawud 3524, Twabaraani katika Al-Kathir 7928, 7853, kutoka kwa Abu Umaamah na Al-Baani katika Sahihil Jaami' i 6316.

<sup>162</sup> Suratin Nisaai (10)



## DHAMBI KUBWA YA KUMI NA TATU

### ULAJI MALI YA MAYATIMA

Allah Mtukuka Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا ۖ وَسَيَصْلَوْنَ

سَعِيرًا ﴿١٦٢﴾

***“Hakika wanao kula mali ya mayatima kwa dhulma, hapana shaka yoyote wanakula matumboni mwao moto, na wataingia Motoni.”(4:10)***<sup>162</sup> Na,

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۗ

***“Wala msiyakaribie mali ya yatima ila kwa njia ya wema kabisa, mpaka afikilie utu-uzima.”(6:152)***<sup>163</sup>

Abu Saïid Khudri رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ wakati amesema katika Miraji:

*“Nikakuta watu, ndevu zao zilikuwa zikivutwa na wengine walikuwa wa kiwadhhibiti hao, na wengineo wakileta mawe ya moto na wakiyashindilia midomoni mwao, na makalioni mwao, Nikamuuliza Jibril “Nani wale? Jibril akasema: “Wanaokula mali ya mayatima kwa dhuluma, hapana shaka yoyote wanakula matumboni mwao moto”.<sup>164</sup>. (Muslim)*

---

<sup>163</sup>Suratiil Israa (34)

<sup>164</sup> Ni Dhaifu sana, Ibn Kathiir ameitilia nguvu katika tafsiri yake kwenye kauli yake: *“Wala msikaribie mali ya yatima isipokuwa kwa lile zuri”*. Mwanzo wa Surat Israa kwa Ibn Abi Haatam na katika isinadi yake yupo Abu Haaruun Baghdadadi na jina lake ni Ammaar bin Juwein Jarjuuh, kuna waliomkadhibisha kama katika Taqriib, na isinadi yake hii ni dhaifu sana, Na kauli ya Dhahabi: *“Ameipokea Muslim Pengine maelezo yake yametangulia ya kunasikhiwa”*.

Abu Huraira رَضِيَ اللهُ عَنْهُ anasema: Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« يبعث الله عز وجل قوماً من قبورهم تخرج النار من بطونهم تأجج أفواههم نارا »

*“Allah Mtukuka atawafufua watu makaburini mwao matumboni mwao kunatoka moto na midomo yao inawaka moto.”*

Wakasema: ‘Ni nani hao ewe mjumbe wa Allah?’. Akajibu:

« ألم تر أن الله تعالى يقول :

*“Hamuoni kuwa Allah Anasema:*

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا

***“Hakika wale wanaokula mali ya yatima kwa dhuluma, huwa wanakula moto matumboni mwao.”<sup>165</sup>***

As-Sudi alisema: “Mla mali ya yatima kwa dhuluma atafufuliwa siku ya kiyama mdomo wake unatoka moto, masikioni, puani na machoni mwake, Na kila anae muona anajua kuwa yeye ni mla mali ya yatima. Atakayeniona atajua huyo ni mlaji mali ya yatima.”<sup>166</sup>

Wanazuoni wanasema ikiwa walii wa mayatima ni masikini na akatumia humo kwa wema kwa kadiri ya kuitunza kwake, na kuikuza, basi hana kosa lolote, chenye kuzidi katika utumiaji basi kitakuwa haramu kwa mujibu wa maneno ya Allah:

وَمَنْ كَانَ غَنِيًّا فَلْيَسْتَعْفِفْ ۖ وَمَنْ كَانَ فَقِيرًا فَلْيَأْكُلْ بِالْمَعْرُوفِ ﴿١٦٧﴾

---

<sup>165</sup> Ameipokea Ibn Hibbaan (5566), Abu Ya’alaa (3.73) na hadithi hii isinadi yake ni dhaifu sana.

<sup>166</sup> Ameipokea Ibn Jarir (8722)

***“Na aliye kuwa tajiri naajizuilie, na aliye fakiri basi naale kwa kadri ya ada”. (4:6)<sup>167</sup>***

Katika kula kwa wema kuna kauli nne: (Ya kwanza) ni kutumia kwa njia ya karadha. (Pili) Kula kwa kadiri ya haja bila isirafu. (Tatu) Kutumia kwa kadiri ya namna alivyomfanyia kazi yatima. (Nne) Kutumia wakati wa dharura ikirahisika kulipa asipoweza kulipa basi yeye yu katika kutatua. Kauli hizi amezitaja Ibn Al Jawzi katika tafsiri yake<sup>168</sup>. Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

« أنا وكافل اليتيم في الجنة هكذا »

*“Mimi na mlezi wa yatima tutakuwa kama hivi peponi”*

Na akaashiria kwa kidole chake cha shahada na cha kati na akaachanisha baina yake<sup>169</sup>. Na katika riwaya nyingine amesema:

*“Mlezi wa yatima, wake au wa mwingine, mimi na yeye ni kama hivi viwili”.*<sup>170</sup>

Na akaonyesha kidole cha shahada na kidole cha kati, na akatanua baina yake.” (Muslim)

Ulezi wa yatima maana yake, ni kushughulikia masilahi yake, kama vile kumlisha, kumvisha na kuendeleza mali yake endapo anayo mali. Kama hana mali atamlisha na kumvisha, kwa ajili ya kutaka radhi za Allah تعالی, na kauli yake Mtume ﷺ,

*“ Yatima wake au wa mwingine”.*

---

<sup>167</sup> An-Nisaa:6

<sup>168</sup> Zaadul Masiir, (2/16)

<sup>169</sup> Sahihi, Ameipokea Ahmad (5/333) Bukhari (5304) Abu Dawud (5150) Tirmidhi (1918).An-Nisaa (4:6)

<sup>170</sup> Sahihi Ameipokea Muslim (2973) na Ibn Maajah (3679) kutoka kwa Abu Hurairah.

Yaani, ni sawa sawa awe jamaa wa karibu au mtu wa kando. Jamaa kwa mfano ni kulelewa na babu yake, ndugu yake, mama yake, shangazi yake, baba wa kambo, mjomba au jamaa zake wasiokuwa hao, wakando ni asiye na udugu nae. Mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

*“Mwenye kukusanya yatima katika chakula chake na kinywaji chake hadi Allah akamtosha Allah atamuwajibishia pepo, isipokuwa akitenda dhambi ambayo haisamehewi”<sup>171</sup>*

Alisema Mtume ﷺ :

*“Mwenye kupapasa kichwa cha yatima, hampapasi isipokuwa kwa ajili ya Allah, atakuwa kwa kila unywele unapopita mkono wake ana jema, na atakayefanya mema kwa yatima mwanamume au mwanamke aliyekuwa katika dhamana yake, mimi na yeye peponi”<sup>172</sup>*

Mtu mmoja alimwambia Abu Darda رضي الله عنه: “Niusie wasia wowote” Abu Darda akamwambia: “Muonee huruma na fanya urafiki na mayatima, walishe unachokula, nilimsikia Mjumbe wa Allah ﷺ akimwambia mtu aliyemlalamika ugumu ndani ya moyo wake:

*“Ukitaka kulainisha moyo wako, fanya urafiki na yatima na upapase kichwa chake, na mlishe chakula chake, hivyo utaulainisha moyo wako na utatia nguvu nafsi yako na kupata mahitaji yako”<sup>173</sup>.*

Mmoja wapo katika salaf anasimulia: “Hapo awali nilizama katika maasi na unywaji pombe. Siku moja nilikutana na mtoto yatima maskini, na nikamchukua nikamfanyia ukarimu, nikamlisha nikamvisha,

---

<sup>171</sup> Dhaifu Ameipokea Baihaqi katika Shi'ib (11031). Tirmidhi (1918), kutoka kwa Ibn Abbaas na AlBaani ameidhoofisha. Dhaiiful Jaami' (5757). (5671) na mfano wake.

<sup>172</sup> Dhaifu ameipokea Ahmad (5/250, 265) Twabarani katika Al - Kabiir (7821,7929) na isinadi yake ni dhaifu, amelisema hilo Ibn Hajar katika Al Fat'hi (11/155)

<sup>173</sup> Sahihi ameipokea Ahmad na Baihaqi na katika Shi'ib (11034), na Shaikh Al - Baani ameisahihisha katika Sahihi Al Jaami'i (1410) Na Silsilah Sahiihah (804)

## Al- Kabair

---

nikamuingiza bafuni nikamuondoa uchafu wake, nikamkirimu kama mtu anavyo mfanyia ukarimu mwanae.

Baadaye nikalala usiku, nikaota kuwa ni siku ya kiyama na miye niliitwa kuhesabiwa nikahukumwa na kuamrisha kutiwa motoni kwa dhambi zangu. Malaika wa motoni akanivuta kuelekea Motoni. Nikawa mbele yao mnyonge, dhalili wakini buruza motoni. Yule yatima akasimama njiani akamwambia malaika: “Mwache huyo ewe malaika, nimuombe kwa Bwana wangu, kwani yeye alinifanyia mema na ukarimu.” Malaika wakamjibu: “Hatukupewa amri kufanya hivyo”.

Ghaffla sauti ikatoka upande wa Allah تعالی ikasema, “Mwachilieni nimepokea na kukubali maombi ya yatima huyo kutokana na namna alivyomtukuza na kumtendea mema yatima na hisani yake.” Nikaamka na kumuomba Allah تعالی msamaha. Kutoka siku hiyo nilizidisha bidii zangu kuwahurumia yatima ili nipate Radhi Zake.

Kwa ajili ya hayo Anas bin Malik رضي الله عنه, Mtumishi wa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*“Nyumba iliyo bora ni ile ambayo ndani yake yumo yatima ambaye anatendewa mema, na nyumba iliyo mbaya ni ambayo ndani yake yatima anatendewa ubaya, watumishi wa Allah تعالی ambao ni wapenzi wa Allah zaidi ni ambao wamefanya jambo zuri kwa yatima, au wajane”<sup>174</sup>.*

Inatolewa taarifa kuwa Allah Mtukuka alimfunulia Mtume Dawud: “Ewe Dawud kuwa kama baba mpendwa kwa mayatima na kama mume mwenye huruma kwa wajane, na ujue kama upandacho basi ndivyo utakavyo vuna. Maana yake lolote utakalolifanya kwa wengine na wao.

---

<sup>174</sup> Dhaifu Ameipokea Baihaqi katika Shi'ib (11038) na Shaikh Al-Baani ameisahihisha katika Sahih al Jaami'i, (1410) , Abu Nuaim 6/338, Ibn Maajah 3679, na sheikh ameidhoofisha katika as-Silsilah ad-Dhaiifah 1638, na at-Ta' aliiq ar-Raghiib 3/230

uliowatendea watakurudishia na kuwa ipo siku utakufa na kuacha watoto yatima au mjane.” Moja katika dua alizokuwa akiomba Mtume Dawud, “Ewe Allah nini malipo ya mtu ambaye kwa ajili yako aliwatunza na kuwatizama mtoto yatima au mwanamke mjane?”<sup>175</sup>

Allah تَعَالَى akamjibu: “Malipo yake ni kumfunika kivuli changu siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa kivuli changu tu.” Maana yake kivuli cha Arshi siku ya kiyama

### **KISA**

Miongoni mwa yaliyokuja katika fadhila za kuwatendea wema wajane na yatima kwa baadhi ya watu wa ukoo wa Alawi uajemi, Mtu mmoja katika familia ya heshima alifika Balkh kutoka Iran, akifutana na mkewe. Walikuwa katika na mali na neema, mume alifariki na mke na mwanawe wa kike wakafukarika, kutokana na khofu ya kuchekwa na maadui zake. Mke akaondoka na binti zake akaenda mji mwingine. Siku ile aliyowasili mji huo ilikuwa ni siku ya baridi mno. Basi akawaacha wanawe wa kike katika misikiti iliyohamwa na akaenda kutafuta chakula. Akapita kati ya vikundi viwili vya watu. Moja ya kikundi hicho walikusanyika kumzunguka Muislamu mmoja ambaye alikuwa ni Sheikh wa mji huo, na kikundi kingine walimzunguka mmajusi ambaye alikuwa mkuu wa usalama wa mji huo. Mama huyo akaenda kwa Muislamu na akamuelezea shida zake akasema: “Miye ni mwanamke kutoka familia ya heshima na nina watoto wa kike niliowaacha kwenye misikiti iliyohamwa, na nimekuja kutafuta chakula chao cha usiku.” Akamwambia. “Nipatie ushahidi kuwa wewe unatoka katika familia nzuri ya waalawi.” Akamwambia: “Mie ni mgeni hapa mjini na kwa hivyo simjui mtu yoyote anayeweza kunishuhudia.” Akaondoka hali ya kuvunjika moyo.

---

<sup>175</sup> Sahihi: Ameipokea Baihaqi katika Shi'ib (11039) na Al-Bukhari na Adabul- Mufrad 138 na Shaikh Al-Baani ameisahihisha.

Akaenda kwa yule Mmajusi na kumuelezea hali yake na kumueleza juu ya heshima yake na kuhusu watoto wake wa kike. Akamuelezea namna gani Sheikh alivyomtendea. Yule Mmajusi akasimama na kuwapeleka baadhi ya wakeze wakawachukua yeye na bintize ampeleke nyumbani kwake akawalisha chakula kizuri akawapa nguo za kitajiri na akawapa chumba ndani ya nyumba yake akawatendea heshima kubwa. Usiku ule Sheikh akaota kuwa ilikuwa siku ya kiyama na bendera zikimzunguka Mtume ﷺ na mbele kulikuwa na kasiri la kijani lililopambwa na majohari, nguzo zake za lulu na rubi, na makuba yake ya lulu na marijaan.

Sheikh akamuuliza Mtukufu Mtume ﷺ, 'Kasr lile ni la nani?' Mtume ﷺ akamjibu "Ni kwa ajili ya Muislamu mwenye kuleta umoja." Sheikh akasema, "Mie ni Muislamu mwenye kuleta umoja."

Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia: "Thibitisha kuwa wewe ni Muislamu mwenye kuleta umoja." Sheikh akabaki hapo hawezi kusema. Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia: "Wewe ulimuuliza mwanamke kutoa ushahidi kuwa yeye ni wa ukoo wa Alawi na kwa hivyo miye nakuuliza wewe utoe ushahidi kama kweli wewe Muislam." Sheikh akatanabahi na akaanza kuhuzunika kwa kutomkarimu yule mwanamke. Akaanza kumtafuta yule mwanamke na binti zake mpaka akajulishwa kuwa yupo kwa wajane na mayatima wa Mmajusi. Akamtumia salamu Mmajusi aende kwake, alipofika akamwambia Mmajusi ampeleke yule mwanamke na binti zake kwake. Mmajusi akamjibu kwa hali yoyote ile, 'Katu sitawaleta nimepata baraka kubwa kutoka kwake.' Sheikh akamwambia, "Chukua dinari 1000 kutoka kwangu na waleta kwangu." Akamjibu, 'Haiwezekani! Sikiliza ambacho unakitaka ni haki yangu, na Kasr uliloliona ndotoni limeumbwa kwa ajili yangu, utanionyesha Uislamu? Wallaahi! miye sikulala jana kucha, mimi na familia yangu hadi tuliposilimu mkononi mwa mwanamke wa Alawi, na niliota ndoto kama uliyoota wewe, na Mjumbe wa Allah ﷻ aliniuliza: "Mwanamke mtukufu na binti zake wapo kwako?' Nikamjibu: 'Ndiyo' Mjumbe wa Allah ﷻ akaniambia, 'Kasiri hili ni lako na familia yako wewe na familia yako ni wakazi wa peponi. Allah ﷻ alikuumba Muislamu tangu zamani.' Sheikh Muislamu

## Al - Kabair

---

akaondoka kwa hali ya huzuni na kusononeka, haijui yoyote (huzuni hiyo) isipokuwa Allah.

Angalia na Allah akurehemu baraka, ya kuwafanyia hisani wajane na yatima, aliyoipata mwenye kuifanya katika karama na fadhila hapa duniani<sup>176</sup>. Kwa hili imethibitika katika sahihi mbili kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

« الساعي على الأرملة والمسكين كالمجاهد في سبيل الله ».

*“Mwenye kukimbilia kusaidia mjane na masikini ni kama mujahidi katika njia ya Allah.”*

Mpokezi amesema: Nadhani alisema:

« وكالقائم لا يفتر والصائم لا يفطر »

*“Na kama mwenye kusimama usiku (kwa ibada) bila kupumzika, na mwenye kufunga bila kufungua”<sup>177</sup>.*

Allah Atuwezeshe kwa hilo kwa Ukarimu Wake na Karama Yake. Hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu, Mpole Msamehevu, Mwingi wa Rehema.

\*\*\*

---

<sup>176</sup> Kisa hiki kina ishara za uongo na uzushi, pengine ni katika uzushi wa mashia au uzushi wa masufi

<sup>177</sup> Ameipokea Bukhari (26007) na Muslim (2982)



## DHAMBI KUBWA YA KUMI NA NNE

### KUSEMA UONGO JUU YA ALLAH NA MJUMBE WAKE

Allah Mtukuka Anasema:

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ تَرَى الَّذِينَ كَذَبُوا عَلَى اللَّهِ وُجُوهُهُم مُّسْوَدَّةٌ أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى  
لِّلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٣٩﴾

***“Na Siku ya Kiyama utawaona walio msingizia uwongo Mwenyezi Mungu nyuso zao zimesawijika. Je! Si katika Jahannamu makaazi ya wanao takabari?”(39:60)***

Al-Hassan alisema: “Hao ni wale wanaosema: Tukitaka tunafanya tusipotaka tunaacha.” Ibn Al-Jawzi, katika maelezo yake katika Qur - aan anasema: Baadhi ya wanazuoni wanaona kuwa kumsingizia Allah na Mtume wake ni ukafiri na kunahamisha kutoka kwenye mila (ya Uislamu). Na hakuna shaka kumsingizia Allah na Mtume Wake katika kuhalalisha haramu na kuharamisha halali ni ukafiri wa wazi, na si vingine shani katika uongo juu yake ni katika yasiokuwa hayo. Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« من كذب عليَّ بُني له بيت في جهنم »

*“Mwenye kusema uongo juu yangu, atajengewa nyumba Jahannam”<sup>178</sup>*

Vile vile amesema:

« ومن كذب عليَّ متعمداً فليتبوأ مقعده من النار »

---

<sup>178</sup> Dhaifu ameipokea Ahmad 4/201,159, Twabaraani katika Al-Kabiir 17/843, Amezidiha tamshi: “Mwenye kusema uongo juu yangu, basi yeye ni motoni” Baihaqi 7533, Shaikh Al Baani ameidhoofisha katika Dhaiifil Jaami'i 5168.

## Al - Kabair

---

“Mwenye kusema uongo juu yangu basi na ajiandalie makazi yake Motoni”<sup>179</sup>.

Na akasema:

« من روى عني حديثاً وهو يرى أنه كذب فهو أحد الكاذبين »

“Mwenye kusimulia hadithi kutoka kwangu na yeye anaona kuwa hiyo ni uongo, basi atakuwa mmoja wa waongo”<sup>181</sup>.

Na akasema:

« إن كذباً عليّ، ليس ككذب علي غيري . من كذب عليّ متعمداً فليتبوأ مقعده من النار »

“Hakika uongo juu yangu si kama uongo kwa wengine, kwa hiyo mwenye kusema uongo juu yangu makusudi ajiandalie makazi yake Motoni”<sup>182</sup>.

Na akasema: « من يقل عني ما لم أقله فليتبوأ مقعده من النار »

“Mwenye kusema anisilosema na ajiandalie makao yake motoni”<sup>183</sup>

« يطبع المؤمن على كل شيء إلا الخيانة والكذب »

“Kila kitu kinapigwa muhuri juu ya muumini isipokuwa juu ya khiana na uongo”<sup>184</sup>.

Tunamuomba Allah taufiki na hifadhi hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu. Na hakika inahusu uongo mwingine usiokuwa huo.

---

<sup>179</sup> Sahihi: ameipokea Bukhari 1291, Muslim 4, Ahmad 4/252 Tirmidhi 1805.

<sup>181</sup> Sahihi: ameipokea Muslim 1: Muqaddima ukurasa 9, Ibn Maajah 39-41.

<sup>182</sup> Sahihi: ameipokea Bukhari 2448. Muslim 1829, kutoka kwa Mughirah bin Shu`ubah.

<sup>183</sup> Sahihi: ameipokea Bukhari 109 Ummu Salamah

<sup>184</sup> Dhafu: Ameipokea Ibn Adiy 2/44, Al-Bazaar 1/69 katika Kashf, Abu Ya`alaa 117, na Al-Bayhaqi katika Shi`ibi 6944 na Sheikh akaidhoofisha katika Dhafiil-Jaami`i 4846.

## DHAMBI KUBWA YA KUMI NA TANO

### KUKIMBIA KATIKA MEDANI (UWANJA WA VITA)

Ikiwa adui hawatazidi zaidi ya mara mbili ya waumini isipokuwa kwa mbinu za vita au kuungana na kikosi hata wakiwa mbali.

Allah تعالیٰ Aliyetukuka Anasema:

وَمَنْ يُؤْلِهِمْ يَوْمَئِذٍ دُبُرُهُمْ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ أَوْ مُتَحَيِّرًا إِلَىٰ فِئَةٍ فَقَدْ بَاءَ بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ وَنَفْسٌ أَنصِرٌ ﴿١٦﴾

***“Na atakaye wageuzia mgongo wake siku hiyo - isipo kuwa kwa mbinu za vita au kuungana na kikosi - basi atakuwa amestahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na pahala pake ni Jahannamu, na huo ni mwisho muovu.” (8:16)***

Abu Hurairah رضي الله عنه amesema: Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« اجتنبوا السبع الموبقات ».

*“Epukeni mambo saba angamizi”.*

Wasikilizaji masahaba wakamuuliza, “Ni yapi hayo ewe mjumbe wa Allah?’, Akasema:

« الشرك بالله ، وقتل النفس التي حرم الله إلا بالحق ، وأكل الربا ، وأكل مال اليتيم ، والتولي يوم الزحف ، وقذف المحصنات الغافلات المؤمنات »

*“Kumshirikisha Allah, kuua nafsi ambayo Allah ameiharamisha (kuiua) isipokuwa kwa haki, na kula riba, na kula mali ya yatima, na kukimbia vitani, na kuwasingizia wanawake wenye kujichunga (dhidi ya maasi), na ni waumini”.* (Maelezo yake yametangulia)

Ibn 'Abbaas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَ alisema wakati aya ilipoteremshwa:

إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ عَشْرُونَ صَابِرُونَ يَغْلِبُوا مِائَتِينَ ۝

**“...Wakiwapo kati yenu ishirini wanao subiri watawashinda mia mbili...” (8:65)**

Kwa hiyo Allah akaandika kuwa ishirini wasiwakimbie mia mbili. Kisha ikateremka:

الَّذِينَ خَفَّفَ اللَّهُ عَنْكُمْ وَعَلِمَ أَنَّ فِيكُمْ ضَعْفًا فَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ مِائَةٌ صَابِرَةٌ يَغْلِبُوا مِائَتَيْنِ ۝ وَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ أَلْفٌ يَغْلِبُوا أَلْفَيْنِ بِإِذْنِ اللَّهِ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ۝

**“Sasa Mwenyezi Mungu Amekupunguzieni, na anajua kuwa upo udhaifu kwenu. Kwa hivyo wakiwapo mia moja kati yenu wenye kusubiri watawashinda mia mbili. Na wakiwapo elfu moja watawashinda elfu mbili, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wenye kusubiri.” (8:66)**

Kwa hivyo Allah ameamuru kuwa waumini mia moja wasiwakimbie makafiri mia mbili, Imepokewa na Al-Bukhari<sup>185</sup>.

\*\*\*

---

<sup>185</sup> Bukhari 46052 - 4653

DHAMBBI KUBWA YA KUMI NA SITA

KIONGOZI ANAYEGHUSHI RAIA NA KUWADHULUMU

Allah Aliyetukuka Anasema:

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ أُولَئِكَ لَهُمْ  
عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٢﴾

**“Bali lawama ipo kwa wale wanao wadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Hao watapata adhabu iliyo chungu.” (42:42).**

Allah Akasema:

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَفْلًا عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ إِنَّمَا يُؤَخَّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ  
الْأَبْصَارُ ﴿٤٣﴾ مُهْطِعِينَ مُقْنِبِينَ رُءُوسِهِمْ لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ وَأَفْئِدَتُهُمْ هَوَاءٌ ﴿٤٤﴾

**“Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayo yafanya madhaalimu. Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku yatapo kodoka macho yao. Nao wako mbioni, vichwa juu, na macho hayapepesi, na nyoyo zao tupu.” (14:42-43)**

Akasema tena Allah:

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ ﴿٢٢٧﴾

**“... Na wanao dhulumu watakuja jua mgeuko gani watakao geuka” (26:227)**

Na akasema tena Allah:

كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَنْ مُنْكَرٍ فَعَلُوهُ لَبِئْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٢٢٨﴾

**“Walikuwa hawakatazani maovu waliyo yafanya. Hakika ni maovu yalioje mambo waliyo kuwa wakiyafanya!” (5:79)**

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

« من غشنا فليس منا »

“Yoyote anayedaganya sio kati yetu (mwenzetu)”<sup>186</sup>

« الظلم ظلمات يوم القيامة »

“Dhuluma ni kiza katika viza vya siku ya kiama”<sup>187</sup>

Na akasema:

« كلكم راع وكلكم مسئول عن رعيته »

“Kila mmoja wenu ni mchungaji na ni mdhamini kwa anachokichunga.”<sup>188</sup>

Na akasema:

« أيما راع غش رعيته فهو في النار »

“Mtawala yoyote anayewadaganya raia wake makazi yake yatakuwa motoni.”<sup>189</sup>

Na akasema:

« من استرعاه الله رعية ثم لم يحطها بنصحه إلا حرم الله عليه الجنة »

“Ambaye Allah amempa uangalizi juu ya raia kisha hakuwapa nasaha zake, isipokuwa Allah atamharamishia pepo” Ameitoa Bukhari katika Lafudhi:

---

<sup>186</sup> Ameipokea Ahmad 2/242. Muslim 101. Abu Dawud 3455. Tirmidhi 1315. Ibn Maajah 2224. kutoka kwa Abu Hurairah.

<sup>187</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 2448. Muslim 1829, kutoka kwa Ibn Umar

<sup>188</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 4554, 5188. Muslim 1829. Tirmidhi 1805.

<sup>189</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 5/20, Na Albaani ameitia nguvu kwa Ibn Asaakir Swahihil Jaami'i 5168.

« يموت وهو غاش لرعيته إلا حرم الله عليه الجنة »

*"Anakufa akiwa mwenye kughushi raia wake isipokuwa Allah atamharamishia pepo"*<sup>190</sup>.

« ما من حاكم يحكم بين الناس إلا حبس يوم القيامة وملك آخذ بشفاه ، فإن مال ، ألقاه فهوى في جهنم أربعين خريفًا »

*"Hakuna hakimu yoyote anahukumu baina ya watu ila atafungwa siku ya kiama na malaika amemshika kisogo chake, akipondoka, atamtupa katika Jahannam miaka arubaini."* (Ahmad).<sup>191</sup>

Na akasema Mtume ﷺ :

« ويل للأمرء ، ويل للعرفاء ، ويل للأمناء ، ليمنين أقوام يوم القيامة أن ذوائبهم كانت معلقة بالثريا يعدبون ولم يكونوا عملوا من شيء » .

*"Ole wao watawala, Ole wao wajuzi, Ole wao wadhamini, watu watatamani siku ya kiama mikia yao ingekuwa imening` inizwa na nyota (thuraya) nao wanaadhibiwa na hawakuwa wamefanya chochote."*<sup>192</sup> (Ahmad).

« ليأتين على القاضي العدل يوم القيامة ساعة يتمنى أنه لم يقض بين اثنين في ثمرة قط »

*"Itamjia hakimu saa siku ya kiama atatamani kuwa hakuhukumu baina ya watu wawili walioshitakiana hata kipande cha tende"*<sup>193</sup>.

---

<sup>190</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 8150, 8151, Muslim 142.

<sup>191</sup> Dhaifu ameipokea Ahmad 1/430, Baihaqi 7533, Shaikh Al Baani ameidhoofisha katika Dhaiifil Jaami'i 5168.

<sup>192</sup> Dhaifu ameipokea Ahmad 2/352, Hakim 4/91, Na Shaikh Al Baani ameidhoofisha katika Al Mishkaati 3698.

<sup>193</sup> Dhaifu ameipokea Baihaqi katika Shi'ibi 7382, Ahmad 2/431, Twabarani katika Al Irwaa 274, 6265. Ahmad 2/352, Hakim 4/91, Na Shaikh Al Baani ameidhoofisha katika Al Mishkaati 3698. Dhaiiful Jami'i 4863.

## Al - Kabair

---

Na akasema:

« ما من أمير عشرة إلا يؤتى به يوم القيامة مغلولة يده إلى عنقه إما أطلقه عدله أو أوبقته جوره »

*“Hakuna kiongozi wa watu kumi isipokuwa ataletwa siku ya kiama huku mikono yake imefungwa shingoni mwake, ima uadilifu wake utamwacha huru au jeuri yake itambakisha (humu)”*.<sup>194</sup>

Na miongoni mwa dua zake Mtume ﷺ kuwa amesema:

« اللهم من ولي من أمر هذه الأمة شيئاً فرقق بهم فارقق به . ومن شق عليهم فاشقق عليه »

*“Ewe Mola yeyote atayekuwa mdhamini kwa kitu chochote juu ya umma huu akiwa mwenye huruma nao, basi nawe mhurumie. Na yeyote mwenye kuwafanyia ugumu nawe mfanyie ugumu”*<sup>195</sup>.

Na akasema Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

« من ولاه الله شيئاً من أمور المسلمين فاحتجب دون حاجتهم وخلتهم وفقرهم احتجب الله دون حاجته وخلته وفقره »

*“Mwenye kuteuliwa na Allah usimamizi wa mambo ya waislamu na akajificha kwa shida zao, na akawaacha na ufukara wao, Allah atajificha dhidi ya haja zake na atamuacha na ufukara wake.”*<sup>196</sup>

---

<sup>194</sup> Dhaifu ameipokea Ahmad 6/75, Twayaalisi 1546, Ibn Hibbaan 1563, Twabaraani katika Al Awswat 388, na Shaikh Al Baani ameidhoofisha katika Dhaiiful Jaami'i

<sup>195</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 6/93, Muslim 1828.

<sup>196</sup> Ameipokea Abu Dawuud 2948, Tirmidhi 1332, 1333, na Shaikh Al Baani ameisahihisha katika sahihah. 629.



## Al - Kabair

---

Na akasema:

« سيكون أمراء فسقة جوررة ، فمن صدقهم بكذبهم وأعانهم على ظلمهم  
فليس مني ولست منه ولن يرد عليّ الخوض »

*“Kutakuwa na watawala waovu na wajeuri, yoyote atakaye wakubali  
na akasaidia juu ya dhuluma yao, basi huyo sio katika mimi, nami sio  
katika yeye, na hatokunywa katika birika”<sup>197</sup>.*

Na akasema:

«صنفان من أمتي لن تنالهم شفاعتي : سلطان ظلوم غشوم، وغال في الدين  
يشهد عليهم ويتبرأ منهم »

*“Aina mbili za watu katika uma wangu hazitapata uombezi wangu,  
mtawala dhalimu na mwenye kughushi, na mghali katika dini  
anashuhudia dhidi yao, na anajitenga nao”<sup>198</sup>.*

Na akasema: « أشد الناس عذاباً يوم القيامة إمام جائر »

*“Mkali wa kuadhibiwa siku ya kiama ni imamu jeuri”<sup>199</sup>*

Na akasema:

« أيها الناس مروا بالمعروف وانهاوا عن المنكر قبل أن تدعوا الله فلا  
يستجيب لكم ، وقبل أن تستغفروا الله فلا يغفر لكم . إن الأحبار من  
اليهود والرهبان من النصارى لما تركوا الأمر بالمعروف والنهي عن  
المنكر لعنهم الله على لسان أنبيائهم ، ثم عمهم بالبلاء»

---

<sup>197</sup> Dhaifu Ameipokea Ahmad 5/384, na ndani yake kuna Ibrahiim bin Nuaim amedhoofisha Abu Haatim na Ibn Hibbaan akawafikiana nae.

<sup>198</sup> Ameipokea Twabarani katika Al Kabiir 8079. Shaikh Al Baani ameitia nguvu kwa Abu Ishaq (Al Harbi Ghariibul Hadiith).

## Al - Kabair

---

*“Enyi watu, amrisheni mema na katazeni munkari kabla hamjamuomba Allah asiwajibuni, na kabla hamjamuomba msamaha na asikusameheni, hakika watawa wa kiyahudi na mapadre wa kinaswara walipoacha kuamrisha mema na kukataza maovu, Allah aliwalaani kwa ndimi za Mitume yao kisha akawaenezea balaa”.*<sup>200</sup>

Na Mtume ﷺ akasema tena:

« من أحدث في أمرنا هذا ما ليس منه فهو رد »

*“Mwenye kuzua katika jambo letu lisilokuwepo basi ni lenye kurudishwa”*<sup>201</sup>

Na akasema:

« ومن أحدث حدثا أو آوى محدثا فعليه لعنة الله والملائكة والناس أجمعين ، لا يقبل الله منه صرفا ولا عدلا »

*“Mwenye kuzua jambo au akamuhifadhi mwenye kuzua basi ni juu yake laana ya Allah na Malaika Wake na watu wote, Allah hatakubali kwake Swala za Sunna wala za Faradhi.”*<sup>202</sup>

Na katika hadithi zingine:

« من لا يرحم لا يُرحم »

*“Ambaye hahurumii hahurumiwi”*<sup>203</sup>

---

<sup>199</sup> Ameipokea Abu Ya'laa 1073, Twabarani katika Al Awswat 1389, Swahiihul Jaami'i 1001.

<sup>200</sup> Ameipokea Twabarani katika Al Awswat 1379, na Al Mundhinri katika at - Targhriib 3/230. na akasema Ameipokea Al Asfahaani na Al Baani ameifanya hasan katika Sahiihil Jaami'i 1001.

<sup>201</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 6/24,27, Bukhari 2697, Muslim 1718. kutoka kwa Aisha

<sup>202</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 1870. Muslim 1370. Abu Dawud 2391

<sup>203</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 5997. Muslim 2318. kutoka kwa Abu Hurairah

« لا يرحم الله من لا يرحم الناس »

“Allah hamhurumii asiye hurumia watu”<sup>204</sup>

Na akasema:

« الإمام العادل يظله الله في ظله يوم لا ظل إلا ظله »

“Allah atamfunika Kiongozi muadilifu katika kivuli Chake siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa kivuli Chake.”<sup>205</sup>

«المقسطون على متابر من نور ، الذين يعدلون في حكمهم وأهليهم وما ولّوا»

“Waadilifu watakuwa juu ya mimbari za nuru, wanafanya uadilifu katika hukumu zao na watu wao na waliodhaminiwa”<sup>206</sup>

Mtukufu Mtume ﷺ alipomtuma Mu'adh Yemen alimwambia:

« إياك وكرائم أموالهم ، واتق دعوة المظلوم فإنها ليس بينها وبين الله حجاب »

“Tahadhari na mali zao tukufu, na tahadhari dua ya mwenye kudhulumiwa, kwani hakuna kizuizi baina yake na Allah.”  
Imepokewa na Al-Bukhari<sup>207</sup>.

Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

« ثلاثة لا يكلمهم الله يوم القيامة : فذكر منهم الملك الكذاب »

---

<sup>204</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 7376. Muslim 2319. kutoka kwa Jariir

<sup>205</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 660, 680. Muslim 1031. Tirmidhi 2391. kutoka kwa Abu Hurairah.

<sup>206</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/ 160. Muslim 1827. Nasaai 8/9221.

<sup>207</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 1458, 1395. Muslim 19,13. Abu Dawud 1584, Tirmidhi 2391. kutoka kwa Ibn Abbaas.

## Al - Kabair

---

*“Watu watatu Allah hatawasemesha siku ya kiyama, na akamtaja miongoni mwao mfalme muongo.”<sup>208</sup> Na akasema:*

«إنكم ستحرصون على الإمارة وستكون ندامة يوم القيامة»

*“Hakika nyinyi mtapupia juu ya uongozi na itakuwa juu yenu majuto siku ya kiama” Ameipokea Bukhari<sup>209</sup>*

Na ndani yake akasema:

«وإنا والله لا نولي هذا العمل أحداً سألته أو أحداً حرص عليه»

*“Wallahi sisi hatumteuji juu ya jambo hili yoyote ambaye ameiomba au yoyote aliyeifanyia pupa”<sup>210</sup>.*

Na akasema:

وقال -عليه الصلاة والسلام-: «يا كعب بن عجرة! أعاذك الله من إمارة السُّفهاء؛ أمراء يكونون من بعلي، ولا يهتدون بهديي، ولا يستنون بسُنِّي»

*“Ewe Ka’ab bin ‘Ujrah, Allah akulinde kutokana na kutawala wajinga, watawala watakaokuja baada yangu, hawaongoki kwa uongofu wangu, wala hawatashikamana na Suna zangu”<sup>211</sup>*

Kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه amesema:

*“Mwenye kutafuta kuwahukumu waislamu mpaka akaupata, kisha uadilifu wake ukashinda ujeuri wake ataingia peponi na ambaye ujeuri wake utashinda uadilifu wake ataingia motoni”<sup>212</sup>.*

---

<sup>208</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/ 160. 480. Muslim 107. kutoka kwa Abu Hurairah.

<sup>209</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/ 448,476. Bukhari 7148. kutoka kwa Abu Hurairah

<sup>210</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 7189, Muslim 3/1456/14. kutoka kwa Abu Musa Al Ash’ari

<sup>211</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 3/2231, Abdur Razaak 20719. Ibn Hibbaana 4514, Tirmidhi 614, na ameisahihisha Al Baani katika At Taliqir Raghiiib 3/15, 150.

<sup>212</sup> Dhaifu ameipokea Abu Dawuud 3575, Baihaqi 88/10. na Shaikh ameidhoofisha katika dhaiiful Jaami’I 5679.

## Al - Kabair

---

Na akasema:

وقال النبي ﷺ: «إنكم تحرصون على الإمارة، وستكون ندامة يوم القيامة»<sup>(213)</sup> رواه البخاري.

*"Mtapuia utawala na utakuwa majuto siku ya kiyama"*<sup>213</sup>.

'Umar رضي الله عنه alimwambia Abu Dhar رضي الله عنه "Niambie hadithi uliyoisikia kwa Mjumbe wa Allah ﷻ, Abu Dhar رضي الله عنه akasema: "Nimemsikia Mjumbe wa Allah ﷻ akisema:

« يجاء بالوالي يوم القيامة فينبد به على جسر جهنم فيرتج به الجسر ارتجاجة لا يبقى منه مفصل إلا زال عن مكانه فإن كان مطيعاً لله في عمله مضى به ، وإن كان عاصياً لله في عمله انخرق به الجسر فهوى به في جهنم مقدار خمسين عاماً »

*"Siku ya kufufuliwa kiyama mtawala ataletwa na kuwekwa kichwa juu ya daraja la Jahannam, daraja hilo litamtikisa kwa nguvu, hadi hakuna kiungo chochote cha daraja kitakachobaki isipokuwa kitaondoka mahali pake, kwa hiyo ikiwa alikuwa mtiifu kwa Allah katika kazi yake atalivuka, na ikiwa alikuwa muasi kwa Allah katika kazi yake, basi daraja litabomoka na yeye atatumbukia nalo Jahannam, na kwa makadirio (ya kuzama) miaka Hamsini"*.

'Umar رضي الله عنه akasema: "Kwa hivyo nani anataka elimu yake (wadhifa huo) ewe Abu Dharr?". Abu Dhar رضي الله عنه akamjibu: "Yule atayekuwa tayari kuvutwa pua yake kwa ajili ya Allah na akakandamiza shavu lake na udongo"<sup>214</sup>.

---

<sup>213</sup> Maelezo ya mapokezi yake yametangulia.

<sup>214</sup> Al Mundhir amesema: 3/139 ameipokea Twabarani katika Al Kabair 2/39 na amesema Al Haythami katika Al Majma'a 5/205 ndani yake kuna Suwaid bin Abdul Aziiz yeye ni mwenye kuachwa hadithi zake.

## Al - Kabair

---

'Amru bin Al-Muhaajir amesema, 'Umar bin 'Abdul 'Azizi رضي الله عنه aliniambia: "Utakaponiona nimepinda katika haki kamata joho langu kisha niambie: "Ewe 'Umar unafanya nini?"

Ewe mwenye kuridhia jina la dhalimu, una dhuluma ngapi?, Jela ni Jahannam na haki ndio hakimumu, wala huna hoja utakaposhitakiana, kaburi linatisha, basi kumbuka anayekutosha. Na hesabu ni ndefu basi okoa nafsi yako, na umri ni kama siku moja basi iwahi nafsi yako. Unafurahia mali yako na chumo ni chafu, na unazama katika matarajio yako na mwendo ni haraka. Hakika dhuluma haiachi kwake hata kiasi cha ncha ya kidole, basi unapomuona dhalimu ameimarika na kushamiri, pengine akalala na mwili wake ukapatwa na jeraha kutokana na siafu watakaomtafuna mwili wake.

\*\*\*

DHAMBI KUBWA YA KUMI NA SABA

KIBURI, MAJIVUNO NA JEURI

Allah Aliyetukuka Anasema:

وَقَالَ مُوسَىٰ إِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ مِنْ كُلِّ مُتَكَبِّرٍ لَا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٤٧﴾

**"Na Musa akasema: Mimi najikinga kwa Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi anilinde na kila mwenye jeuri asiye iamini Siku ya Hisabu." (40:27)**

Katika sura nyingine Allah Amesema:

إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْتَكْبِرِينَ ﴿٢٣﴾

**"Kwa hakika Yeye hawapendi wanao jivuna." (16:23)**

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

وقال ﷻ: «بينما رجلٌ يتبختر في بُرْدِيهِ، إذ خسف الله به الأرض، فهو يتجلجلُ فيها إلى يوم القيامة»<sup>(١)</sup>.

**"Wakati ambapo mtu (mmoja mwenye majivuno) anajivuna katika mwendo wake, tahamaki Allah akamdidimiza, nae anadidimia ndani yake hadi siku ya kiyama."<sup>215</sup>**

Na akasema:

وقال ﷻ: «يُحْشَرُ الْجَبَّارُونَ وَالْمُتَكَبِّرُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَمْشَالُ النَّارِ»<sup>(٢)</sup>،  
يَطْوَهُمُ النَّاسُ»<sup>(٣)</sup>.

---

<sup>215</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/325, 531. Bukhari 2789, Muslim 2088. kutoka kwa Abu Hurairah

## Al - Kabair

---

*“Majabari na wenye kiburi (kiburi) watafufuliwa siku ya kiyama wakiwa dhalili kama punje (Dharra) watu wanawakanyaga, wakigubikwa na udhalili kila mahali”<sup>216</sup>*

Baadhi ya Salafu Swalih walisema kuwa: “Dhambi ya kwanza alioasiwa Allah ni kiburi”. Allah Aliyetukuka Anasema:

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ وَاسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٤﴾

***“Na wakati Tulipowaambia msujudieni Adam wote walimsujudia isipokuwa Ibilisi alikataa na alijivuna na akawa kati ya waliopinga” (2:34)***

Kwa hiyo atakayefanyia kiburi haki imani yake haitamfaa kama alivyofanya Ibilisi.

Na kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

قال النبي ﷺ: «لا يدخل الجنة أحدٌ في قلبه مثقالُ ذرةٍ من كبر»

*“Haingii peponi ambaye katika moyo wake kuna chembe ya kiburi”  
Ameipokea Muslim<sup>217</sup>*

Allah Aliyetukuka anasema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٣١﴾

***“...Hakika Allah Hampendi kila anaye jivuna na kujifakhirisha.” (31:18)***

---

<sup>216</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/279, Tirmidhi 2623. na Shaikh akaisahihisha katika Swahihil Jaami'i.8040.

<sup>217</sup> Sahihi ameipokea Muslim 91, Abu Dawud 4091, Tirmidhi 2623, Ibn Maajah 4173, kutoka kwa Ibn Masuud.



## Al - Kabair

---

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

وقال ﷻ: يقول الله -تعالى-: «العظمة إزاري، والكبرياء ردائي، فمن نازعني فيهما ألقىته في النار»<sup>(٥)</sup> رواه مسلم.

*“Allah anasema: Utukufu ni nguo yangu na kiburi ni joho langu. Yoyote atakaye nyang`anyana Nami kimoja wapo, Nitamvurumisha motoni.”<sup>218</sup>*

Mtukufu Mtume ﷻ alisema:

وقال ﷻ: «اختصمت الجنة والنارُ إلى ربِّهما، فقالت الجنة: يا رب! ما لي يدخلني ضعفاء الناس وسقَّاطهم<sup>(٢)</sup>؟! وقالت النارُ: أوْثرتُ بالجَّارين والمتكبرين...»<sup>(٣)</sup> الحديث.

*“Pepo na moto walibishana, pepo ikasema: nina nini mimi hawaingii kwangu isipokuwa wadhaifu kati ya watu, na wale wa chini wao? Moto ukasema: “Nimependelewa majabari na wenye kutakabari”<sup>219</sup>.*

Allah Aliyetukuka Anasema:

وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٣١﴾

***“Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna na kujifakhirisha.” (31:18).***

Yaani usigeuze shavu lako kwa kiburi na maringo.

Salama Bin Akwa'ana رضي الله عنها alisema: “Mtu mmoja alikula kwa mkono wa kushoto mbele ya Mjumbe wa Allah ﷻ.

---

<sup>218</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/444, Muslim 262, Abu Dawuud 4090, kutoka kwa Abu Hurairah.

<sup>219</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 4848, 4849, 4840, Muslim 2846. kutoka kwa Abu Hurairah.

Mjumbe wa Allah ﷻ akamwambia:

« كل بيمينك »

*“Kula kwa kulia kwako.”*

Yule bwana akamjibu: “Siwezi.” Mtukufu Mtume ﷺ Akasema:

ما منعه إلا الكبر-، قال: « لا استطعتُ

*“ Hutaweza, hakikumzuia isipokuwa kiburi.*

Baada ya hapo hakuweza tena kunyanyua mkono wake wa kulia na kuuweka mdomoni.”<sup>220</sup> (Muslim).

Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

« ألا أخبركم بأهل النار؟ كل عتل جواز مستكبر »

*“Mnataka miye niwapeni habari ya wakazi wa motoni?” Kila jeuri, na mwenye majivuno mwenye kiburi<sup>221</sup>.*

Ibn 'Umar رضي الله عنهما amesema: nilimsikia Mjumbe wa Allah ﷻ akisema:

« ما من رجل يخال في مشيته ويتعاضم في نفسه إلا لقي الله وهو عليه غضبان »

*“Hakuna mtu yoyote anayejivuna katika kutembea kwake, na anajikweza katika nafsi yake, isipokuwa atakutana na Allah akiwa amemghadhibikia”<sup>222</sup>.*

---

<sup>220</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 4/45, 46, Muslim 2021.

<sup>221</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 4918, 2853, Muslim 2846. kutoka kwenye riwaya ya Haarithah bin Wahb

<sup>222</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/118, Bukhari katika Al Adabul Mufradi 549, Swahiihul Jaami'i 5711.

## Al - Kabair

---

Abu Hurairah رضي الله عنه anatarifu kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

«أول ثلاثة يدخلون النار : أمير مسلط أي ظالم ، وغني لا يؤدي الزكاة ،  
وفقير فخور»

*“Watatu wa mwanzo watakaolingia motoni; mtawala dhalimu, na tajiri ambaye hatekelezi Zaka ya mali yake, na fukara mwenye kujifakhiri”<sup>223</sup>.*

Katika Sahihi Bukhari imepokewa kuwa Mtume ﷺ amesema:

*“Watu watatu Allah hatowatazama Siku ya kiyama wala hatowatakasaa, nao wana adhabu kali: mwenye kuburuza nguo, mwenye kusimbulia, na anayeuzua bidhaa zake kwa yamini ya uongo.”<sup>224</sup>*

Na mwenye kuburuza nguo ni ambaye anaburuza kikoi chake au suruali yake hadi kwenye nyayo zake, kwani Mtume ﷺ amesema:

« ما أسفل من الكعبين من الإزار فهو في النار »

*“Kilichozi chini ya nyayo mbili hicho ni motoni”<sup>225</sup>.*

Kiburi kibaya zaidi ni ambacho ndani yake mtu anajikweza kwa elimu yake, anajitukuza kwa fadhila yake, huyu elimu yake haitamnufaisha. Ama yule anayetafuta elimu na kuitumia kwa ajili ya kesho, na hajioneshi kati ya watu, na moyo wake umejaa khofu na nafsi yake imetulia, kwani akighafilika nayo itamuangamiza. Na mwenye kutafuta elimu kwa ajili ya kujifakhiri na ukubwa, na akafanya kiburi juu ya waislamu, na akawafanyia upumbavu, na akawadharau. Huyu yumo katika kiburi kikubwa. Wala hataingia peponi ambaye moyoni mwake kuna uzito wa punje ya kiburi. Hapana hila wala nguvu, isipokuwa kwa Allah Aliye juu Aliyetukuka.

---

<sup>223</sup> Dhaifu, ameipokea Ahmad 2/425, Tirmidhi 1642, Haakim amesema: Amir bin Shaybi ni mnyoofu wa hadithi na ameitoa Dhahabi, na Ibn Khuzaimah katika sahihi yake 3/246. Al Baani ameidhooifisha katika Dhaiiful Jaami'i 3703.

<sup>224</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 5/148, 126, Muslim 106, Abu Dawud 4087, Tirmidhi 1211.

<sup>225</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 5787. kutoka kwa Abu Hurairah.

## DHAMBI KUBWA YA KUMI NA NANE

### KUSHUHUDIA UONGO

Allah Aliyetukuka Anasema:

وَالَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٧٢﴾

**“Na wale ambao hawatoi ushahidi wa uwongo...” (25:72)**

Na katika masimulizi mengine ushahidi wa uongo umelinganishwa na ushirikina. Allah Amesema:

وَأَجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ ﴿٣٠﴾

**“...na jiepusheni na usemi wa uwongo” (22:30)<sup>226</sup>**

Na katika hadithi:

« لا تزول قدما شاهد الزور يوم القيامة حتى تسجب له النار »

*“Hazitaondoka nyayo za mshuhudia uongo mahali pake hadi moto umzunguke”.*<sup>227</sup>

Mtunzi anasema: Anayeshuhudia uongo amefanya madhambi makubwa mengi. La kwanza; uwongo na kumzulia Allah Aliyetukuka. Allah amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ كَذَّابٌ ﴿٦٨﴾

---

<sup>226</sup> Imepokewa na Ahmad 4/321,322), Abu Dawud (3599), Ibn Majah (2372) na kusahihishwa na Al-Albani katika At-Ta’aliq Ar-Raghiib 3/166.

<sup>227</sup> Ni Maudhuu (ya uongo) Ameipokea Ibn Maajah 2373, Haakim 4/98, Al Baani amesema: ni Maudhuu, Dhaiiful Jaami’i 4871, na Al Baani amesahihisha katika at Taaliqir Raghiib, 4871, na Silsilah Dhaiifah 1259.

**“...Hakika Mwenyezi Mungu hamwongoi apindukiaye mipaka, mwongo mkubwa.” (40:28)**

Na katika hadithi:

« يطبع المؤمن على كل شيء ليس الخيانة والكذب »

“Kinamfuata muumini kila kitu chake kisichokuwa khiana na uongo”.<sup>228</sup>

La pili; ni kuwa amemdhulumu ambaye amemshuhudia na kumpelekea yeye mali ya haramu, kwa hiyo akaichukua kwa ushahidi wake, kwa hiyo ikapasa juu yake moto. Mtume ﷺ amesema:

« من قضيت له من مال أخيه بغير حق فلا يأخذه فإنما أقطع له قطعة من نار »

“ Ambaye nimemhukumia mali ya ndugu yake bila ya haki, basi na asichukue kwa hakika nitakuwa nimemkatia kipande cha moto ”<sup>229</sup>.

Tatu; amemdhulumu aliyemshuhudia dhidi yake hadi akachukuliwa kwa ushahidi wake, mali yake, heshima yake na roho yake. Nne: ni kuwa amehalalisha ambalo Allah ﷻ ameliharamisha, miongoni mwa mali, damu na heshima. Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

« ألا أنبئكم بأكبر الكبائر؟ الإشراف بالله، وعقوق الوالدين، ألا وقول الزور،  
ألا وشهادة الزور »

“Je nikuelezeni juu ya dhambi kubwa? ni kumshirikisha Allah na chochote, kuwaasi wazazi wawili, na kauli ya uongo, sikieni na kushuhudia uongo”.

Hakuacha kuyakariri maneno hayo hadi tukasema laiti angenyamaza. Ameipokea Bukhari<sup>230</sup>. Basi Tunamuomba Allah salama na afya.

---

<sup>228</sup> Maelezo yake yametangulia.

<sup>229</sup> Ameipokea Bukhari 2680, Muslim 1713.

<sup>230</sup> Maelezo yake yametangulia.

DHAMBI KUBWA YA KUMI NA TISA

KUNYWA POMBE

Allah Aliyetukuka Anasema:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ  
فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ  
فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَن ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ ﴿٩١﴾

***“ Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shet’ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa. Hakika Shet’ani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mmeacha?” (5:90-91)***

Allah Mtukufu Amekataza pombe katika aya hii na akaitahadharisha. Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« اجتنبوا الخمر فإنها أم الخبائث »

*“Kaeni mbali na pombe, kwani hiyo ni mama wa maasi.”<sup>231</sup>*

Kwa hiyo basi ambaye hatoiacha atakuwa amemuasi Allah ﷻ na Mtume wake ﷺ na anastahiki adhabu. Allah Aliyetukuka anasema:

وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ عَذَابٌ  
مُّهِينٌ ﴿٩٢﴾

<sup>231</sup> Ameipokea Ibn Hibbaan Baihaqi katika Shi’ibi 5198, Ni sahihi ambayo ni mauquuf kwa Nasaai5666. na Taaliiqi juu ya Al Mukhtaar.320

**"Na anaye muasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akaipindukia mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) atamtia Motoni adumu humo, na atapata adhabu ya kudhalilisha." (4:14)**

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema wakati aya ya kuharamisha pombe ilipoteremshwa maswahaba walizungukiana baadhi yao wakasema: "Pombe imeharamishwa na imelinganishwa na ushirikina"<sup>232</sup>.

Ibn 'Umar رضي الله عنهما ana msimamo wa kuwa pombe ni dhambi kubwa kabisa miongoni mwa madhambi makubwa. Na hiyo bila shaka ni mama wa machafu. Na mnywaji wake amelaaniwa katika hadithi nyingi. Imepokewa na Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema:

« كل مسكر خمر وكل خمر حرام ومن شرب الخمر في الدنيا ومات ولم  
يتب منها وهو مدمنها لم يشربها في الآخرة »

*"Kila kinacholeweshwa ni pombe, na kila pombe ni haramu, na mwenye kunywa pombe duniani na akafa na hakutubu basi hatoinywa akhera". Amejipokea Muslim<sup>233</sup>.*

Jabir رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ anasema:

« إن على الله عهداً لمن شرب المسكر أن يسقيه الله من طينة الخبال »

*"Allah ana ahadi juu ya mnywa pombe, kumnyweshwa-Twiinatul Khibaal"<sup>234</sup>*

Kukasemwa: Ninini Twiinatul-Khibaal Ewe Mtume wa Allah?, Akasema:

---

<sup>232</sup> Sahihi ameipokea Haakim katika Al - Mustadrak 4/144, na akasema: Ni sahihi, na Dhahabi akaafikana nae. Na Haithami akaitaja katika majma'a Zawaaid 5/52 na akasema ameipokea Twabarani. Na watu wake ni watu wa Sahihi. Na Mundhir katika Targhiib 3/260 na akasema mfano wake.

<sup>233</sup> Sahihi ameipokea Muslim 2003, Abu Dawud 3679, Tirmidhi 1861, kutoka kwa Ibn Umar.

<sup>234</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 3/361, Muslim 2003, Nasaai 8/328

« عرق أهل النار أو عصارة أهل النار »

“Jasho la watu wa motoni au usaha wa watu wa motoni”.

Na katika Sahihi mbili kuwa Mtume wa Allah ﷺ amesema:

« من شرب الخمر في الدنيا يحرمها في الآخرة »

“Mwenye kunywa pombe hapa duniani, basi huko Akhera itaharamishwa juu yake”<sup>235</sup>.

Imetajwa kuwa mwenye kudumu na pombe ni kama muabudu masanamu, ameipokea Imamu Ahmad katika Musnadi yake kutokana na Hadithi ya Abu Hurairah kuwa Mtume ﷺ amesema:

« مدمن الخمر كعابد وثن »

“Mwenye kudumu kunywa pombe ni kama mwenye kuabudu masanamu”<sup>236</sup>.

Ametaja kuwa mwenye kudumu kunywa pombe na anapokufa na hakutubia haingii peponi. Ameipokea Nasaai kutokana na hadithi ya Ibn Umar رضي الله عنهم kuwa Mtume ﷺ amesema:

« لا يدخل الجنة عاق ولا مدمن خمر »

“Haingii peponi mwenye kuwaasi wazazi na mwenye kudumu kunywa pombe.”<sup>237</sup>

---

<sup>235</sup> Sahihi ameipokea Al-Bukhari 5575, Muslim 2003, kutoka kwa Ibn ‘Umar.

<sup>236</sup> Dhaifu ameipokea Ahmad 1/272, Twabarani 14328, Al Bazaar 2934, na Al- Baani ameidhoofisha katika Dhaiifil Jaami’i 5737.

<sup>237</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/201, Nasaai 8/218, Twahaawi katika Mushkilul Aathaar 1/395 Al-Baani ameisahihisha katika Sahihil Jaami’i 7553



## Al-Kabair

---

Na katika riwaya nyingine:

«ثلاثة قد حرم الله عليهم الجنة: مدمن الخمر، والعاق لوالديه، والديوث وهو الذي يقر السوء في أهله»

*“Watu watatu Allah amewaharamishia pepo; mwenye kudumu kunywa pombe, asiyewaheshimu wazazi wake, na dayuuthi, ni yule ambaye anakubali uovu kwa mkewe”<sup>238</sup>.*

Imetajwa kuwa Allah hakubali hata jema moja la mlevi. Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

«ثلاثة لا يقبل لهم صلاة ولا ترفع لهم حسنة إلى السماء: العبد الأبق حتى يرجع إلى مواليه فيضع يده في أيديهم، والمرأة الساخط عليها زوجها حتى يرضى عنها، والسكران حتى يصحو»

*“Watu watatu hawakubaliwi Swala zao na matendo yao mema hayapandi mbinguni: “Mtumwa mtoro, hadi arudi kwa bwana wake, na huyo bwana wake ampe mkono (Alama ya kumkubali), mwanamke ambaye mume amemkasirikia, hadi mume huyo amridhie, na mlevi mpaka azinduke.”<sup>239</sup>*

Pombe ni kitu kinachofunika akili ni sawa kiwe cha majimaji, au kikavu, au kinacholiwa, au kinachonywewa.

Kutoka kwa Abu Said Al-Khudri رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« لا يقبل الله لشارب الخمر صلاة ما دام في جسده شيء منها »

---

<sup>238</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 2/69,128, Haakim 4/174, Baihaqi 8/288, Ameisahihisha Shaikh Al Baani katika sahihi Al Jaami'i 4553.

<sup>239</sup> Dhaifu ameipokea Ibn Khuzaimah 940, Ibn Hibbaan 5355, Al-Baihaqi 8/288, Shaikh Al-Baani katika Sahihil Jaami'i 1075.

*" Allah hakubali Swala ya mnywa pombe maadamu mwilini mwake kumbaki chochote kutokana nayo"<sup>240</sup>.*

Katika riwaya nyingine:

*"Mwenye kunywa pombe Allah hakubali kwake chochote, na mwenye kulewa kutoka nayo, basi Swala yake haikubaliwi kwa muda wa siku arubaini. Endapo akitubu na baadaye akarudia tena itakuwa ni haki juu ya Allah kumnyweshwa shaba nyeupe iliyoyeyushwa ya Jahannam"<sup>241</sup>.*

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

« من شرب الخمر لم يقبل الله منه شيئاً ، ومن سكر منها لم تقبل له صلاة أربعين صباحاً ، فإن تاب ثم عاد كان حقاً على الله أن يسقيه من مهل جهنم »

*"Mwenye kunywa pombe na hakulewa Allah atampa nyongo siku arubaini, na ambaye amekunywa pombe na akalewa, basi Allah hatakubali kwake, swala za faradhi wala za sunna kwa siku arubaini, na akifa ndani yake atakufa kama mwenye kuabudu masanamumu. Na itakuwa ni haki juu ya Allah kumnyweshwa usaha na damu inayochururika kutoka wakazi wa motoni."<sup>242</sup>.*

Abdullah bin Abi Awfa alisema: "Anayekufa na amedumu kunywa pombe, anakufa kama mwenye kuabudu Al-Laata na Al-'Uzza (masanamumu makubwa wakati wa Jaahiliya) alipoulizwa maana ya kudumu kunywa pombe, ni hali ya yule ambaye hazinduki kwenye ulevi wake?, Akajibu: Hapana! Huyo ni ambaye anainywa anapoipata hata ikiwa baada ya miaka mingi kupita.

---

<sup>240</sup> Riwaya ya kwanza ameipokea Abdu bin Humaid 983, katika Al Muntakhab na isinadi yake ni dhaifu.

<sup>241</sup> Riwaya ya pili Ahmad 2/178, Haakim 4/146. na isinadi yake ni Hasan.

<sup>242</sup> An-Nasaai 8/317, Ibn Maajah 3377, Ibn Hibbaan 5333, Ahmad 2/189, na Shaikh amesahihisha katika Sahihil Jaami'i 7189, tofauti na tamshi: (Akifa ndani yake anakufa kama mwenye kuabudu masanamumu).

## FASILI

Imetajwa kuwa mwenye kunywa pombe hawi muumini wakati anapokunywa pombe. Abu Huraira رَضِيَ اللهُ عَنْهُ anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*"Haibi mwizi wakati anapoiba akawa muumini, mzinzi hazini wakati anapozini akiwa muumini, wala hanywi pombe wakati anapokunywa akawa muumini, na toba itaonyweshwa baadae"<sup>243</sup>. Ameipokea Bukhari*

Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

*"Mwenye kuzini au kunywa pombe, Allah humvua imani, kama mtu anavyovua kanzu kichwani mwake"<sup>244</sup>.*

Ndani yake kutoka kwa Mtume ﷺ kuna:

*"Mwenye kunywa pombe jioni anaamka asubuhi ni mshirikina, na anayekunywa asubuhi huchwewa akiwa mshirikina."*

Na ndani yake kuna hadithi ya Mtume ﷺ:

*"Hakika harufu ya pepo husambaa masafa ya safari ya miaka mia tano, lakini hayatmfikia mtu ambaye hawaheshimu wazazi wake, yule anayehadithia fadhila alizofanya hadharani kwa wengine. Wala mwenye kudumu kunywa pombe, wala mwenye kuabudu masanamu."<sup>245</sup>.*

---

<sup>243</sup> Maelezo yake yametangulia.

<sup>244</sup> Maelezo yake yametangulia.

<sup>245</sup> Dhaifu: Mundhiri amesema: Ameipokea Twabarani katika As-Saghiir1/250, kutokana na hadithi ya Abu Hurairah na isinadi yake ni dhaifu.

Imamu Ahmad amepokea kutokana na hadithi ya Abu Musa Al 'Ash'ari رضي الله عنه<sup>246</sup> amesema:

Mtume ﷺ amesema:

« لا يدخل الجنة مدمن خمر، ولا مؤمن بسحر ولا قاطع رحم ، ومن مات وهو يشرب الخمر سقاه الله من نهر الغوطة، وهو ماء يجري من فروج المومسات - أهل النار ريح فروجهن »

*"Mlevi wa Pombe, muumini wa uchawi na mwenye kukata udugu, hatoingia peponi, na mwenye kufa huku anakunywa pombe, Allah atamnyweshwa kwenye mto wa ghawtwa. Na hayo ni maji yanayopita kwenye tupu za wazinifu, harufu yake itawaudhi watu wa motoni".<sup>246</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

« إن الله بعثني رحمة وهدى للعالمين ، بعثني لأصحق المعازف والمزامير وأمر الجاهلية . وأقسم ربي تعالى بعزته لا يشرب عبد من عبيدي جرعة من الخمر إلا سقيته مثلها من حميم جهنم ، ولا يدعها من مخافتي إلا سقيته إياها مع خير الندماء »

*"Hakika Allah amenituma kuwa rehema na uongofu kwa walimwengu wote, amenileta kuondosha ala za muziki na desturi za ujahilia, na Mola wangu Ta'ala ameapa kwa Utukufu Wake, mja hanywi pombe miongoni mwa waja Wangu, japo funda la pombe, isipokuwa Nitamnyweshwa kutokana na maji ya moto ya Jahannam wala hataiacha kwa kuniogopa Mimi isipokuwa Nitamnyweshwa hiyo katika hadhira ya Al-Quqsi, pamoja na wabora wa wanywaji"<sup>247</sup>*

---

<sup>246</sup> Hasan: amepokea Ahmad 4/399, Haakim 4/146, Al Baani ameifanya Hasan katika As Swahiihah 678.

<sup>247</sup> Dhaifu: Ameipokea Ahmad 5/287, 268, twabarani katika Al Kabiir 8/232

## FASILI

Waliolaaniwa katika pombe: Abu Dawuud amepokea kuwa Mtume ﷺ amesema:

« لعنت الخمر بعينها وشاربها وساقياها وبائعها ومبتاعها وعاصرها  
ومعتصرها وحاملها والمحمولة إليه وآكل ثمنها »

*“Pombe imeilaaniwa yenyewe, na amelaaniwa mwenye kuitengeneza na yule anayetengenezewa, na anayekunywa, na muuzaji wake, na mnunuzi wake, na anayeikamua, na anayekamuliwa, na mbebaji wake, na mwenye kubebewa, na mwenye kula thamani yake.”<sup>248</sup>*

Na Imamu Ahmad kutokana na hadithi ya Ibn ‘Abbaas amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema:

« أتاني جبريل عليه السلام فقال : يا محمد إن الله لعن الخمر وعاصرها ومبتاعها  
ومعتصرها وبائعها وشاربها وآكل ثمنها وحاملها والمحمولة إليه وساقياها ومستقياها »

*“Alinjia Jibrili akasema: Ewe Muhammad hakika Allah ameilani pombe na mkamuaji wake, na mbebaji wake, na mwenye kukamuliwa, na muuzaji wake na mnunuzi wake, na mwenye kula thamani yake, na mnyweshaji wake na mwenye kunyweshwa.”<sup>249</sup>*

## FASILI

Imetajwa kutomzuru mnywaji pombe anapougua na vile vile kumsalimia.

---

<sup>248</sup> Ameipokea Ahmad 5/25,71, Abu Dawud 3674, Ibn Maajah 3380, Shaikh ameisahihisha katika Al Irwaa 1529, Al Mishkaati 2777, Ar Rawdhul Anfu 846.

<sup>249</sup> Ameipokea Ahmad 1/316, Twabarani 12936, Haakim 4/145, As Swahihah 839, Swahihul Jaami'i, 72.

## Al - Kabair

---

Abdullah ibn 'Amru binil-'Aas Amesema. Msiwazuru wanywa pombe wakati wakiwa wagonjwa<sup>250</sup>, Bukhari amesema: Ibn 'Umar alisema: "Msimsalimie mnywa pombe<sup>251</sup>."

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

« لا تجالسوا شراب الخمر ولا تعودوا مرضاهم ولا تشهدوا جنازتهم وإن شارب الخمر يجيء يوم القيامة مسوداً وجهه ، مدلعا لسانه على صدره ، يسيل لعابه يقذره كل من رآه وعرفه أنه شارب خمر »

*"Msikae pamoja na wanywaji pombe, wala msizuru wagonjwa wao, hakika wanywaji pombe watakuja siku ya Kiyama na nyuso zao ni nyeusi, ulimi wake unaning'inia kifuani mwake, na udenda wake na uchafu wake unachuruzika na kila mtu atakayemuona atajua kuwa huyo ni mnywaji."*<sup>252</sup>

Baadhi ya wanazuoni wanasema kukatazwa kuwazuru wanywaji pombe wakati wao ni wagonjwa, na kuwasalimia, ni kwa sababu mnywaji pombe ni fasiqi amelaaniwa na Allah na Mjumbe wake, kama ilivyonukuliwa katika kauli yake:

« لعن الله الخمر وشاربيها . . . »

*" Hakika Allah ameilaani Pombe na mnywaji wake."*

Yoyote anayeinunua (zabibu) na akaitengeneza basi analaaniwa mara mbili. Na akimnyweshwa mwingine basi hulaaniwa mara tatu, kwa ajili hiyo amekataza kumzuru huyo anapokuwa mgonjwa na kumsalimia, isipokuwa akitubu. Na mwenye kutubu, Allah anaikubali toba yake.

---

<sup>250</sup> Hadithi Maudhuu: Ameipokea Bukhari katika Adabul Mufrad; ameidhoofisha albani kuhusu hadith dhaifu zilizomo katika Adabul Mufrad 160.

<sup>251</sup> Ameitaja Bukhari katika kitabu cha Istiidhan - alFat'h 41/11

<sup>252</sup> Ibn Adiy2/214, na Suyyuti ameitaja katika Al la aalii 2/205

## FASILI

### ULEVI SIO DAWA

Ummu Salamah رضي الله عنها mke wa Mtukufu Mtume ﷺ alisema; Binti yangu alikuwa mgonjwa, basi mie nikaroweka tende ndani ya chungu, Mjumbe wa Allah ﷻ akaja nyumbani kwangu akaona mapovu yanavyowiva (hamira) akaniuliza:

« ما هذا يا أم سلمة ؟ »

*“Nini hiki Ewe Ummu Salamah?”*

Miye nikamwambia kuwa ninawivisha tende kuwa kama dawa ya binti yangu. Mtume ﷺ akaniambia:

« إن الله تعالى لم يجعل شفاء أمتي فيما حرم عليها »

*“Hakika Allah Aliyetukuka hakufanya dawa ya umma wangu itokane na alichokiharamisha”.*<sup>253</sup>

### Kutaja Hadithi mbalimbali zilizopokewa katika pombe

Katika hizo ni zile alizozitaja Abu Nua'ym katika 'Al-Hilyah' kutoka kwa Abu Musa رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa wakati Mtume ﷺ alipoona chungu cha kuchachua juisi alisema:

« اضربوا بهذا الحائط فإن هذا شراب من لا يؤمن بالله واليوم الآخر »

*“Kipigeni na ukuta huu kwani kinywaji hiki ni cha asiyeamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.”*<sup>254</sup>

---

<sup>253</sup> Hadithi Maudhuu: Ameipokea Twabarani 23/749. Baihaqi 10/5. Na ina ushahidi mwingine kutokana na hadithi ya Ibn Masuud, na ina ushahidi kwa Muslim, na hadithi hii Bukhari ameisherehesha iliyoishia kwa Ibn Masu'ud.

<sup>254</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Baihaqi 8/303 na Abu Nu'aym 6/84 na kuna ushuhuda wa Hadithi ya Abu Dawud 3716 na Ibn Majah 3409 katika As-Swahiha 3010.

## Al - Kabair

---

Mtume ﷺ amesema:

« من كان في صدره آية من كتاب الله وصب عليها الخمر يجيء يوم القيامة كل حرف من تلك الآية فيأخذ بناصيته حتى يوقف بين يدي الله تبارك وتعالى فيخاصمه، ومن خاصم القرآن خصمه فالويل لمن كان القرآن خصمه يوم القيامة»

*“Mwenye kuwa katika moyo wake kuna aya hata moja katika kitabu cha Allah, na akaimwagia pombe atakuja siku ya kiama kila herufi moja kwenye aya hizo, zitamchukua kwa utosi wake mpaka asimamishwe baina ya Allah Aliyetukuka, na zitamshitaki na ole wake atakaye shitakiwa na Qur`an, Basi ole wake ambaye Qur`aan itagombana nae siku ya kiama.”<sup>255</sup>*

Kutoka kwa Abu Musa Al Ash`ari kuwa Mtume ﷺ aliletewa kiriba cha pombe, akasema:

« ما من قوم اجتمعوا على مسكر في الدنيا إلا جمعهم الله في النار ، فيقبل بعضهم على بعض يتلاومون ، فيقول أحدهم للآخر : يا فلان لا جزاك الله عني خيراً فأنت الذي أوردتني هذا المورد ، ويقول له الآخر مثل ذلك »

*“Hawatakuwa watu wenye kukusanyika kwa ajili ya ulevi hapa duniani isipokuwa Mwenyezi Mungu atawakusanya motoni, kisha watakabiliana na kulaumiana, mmoja anamwambia mwengine: Ewe fulani Allah asikupe kheri wewe ndie ambaye umenipelekea hapa nilipo, na mwingine anasema mfano wa maneno hayo.”<sup>256</sup>*

Na imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

« من شرب الخمر في الدنيا سقاه الله من سم الأسود شربة يتساقط لحم وجهه في الإناء قبل أن يشربها ، فإذا شربها تساقط لحمه وجلده يتأذى به أهل النار، ألا وشاربها وعاصرها ومعتصرها وحاملها والمحمولة إليه وأكل

---

<sup>255</sup> Hadithi hii sijaiona.

<sup>256</sup> Hadithi hii sijaiona.



ثمنها شركاء في إثمها ، لا يقبل الله منهم صلاة ولا صوم ولا حجاج حتى يتوبوا ،  
فإن ماتوا قبل التوبة كان حقاً على الله أن يسقيهم بكل جرعة شربوها في الدنيا  
من صديد جهنم، ألا وكل مسكر خمر وكل خمر حرام «

*“Mwenye kunywa pombe katika dunia Allah atamnyweshwa sumu  
ya nyoka nyeusi, nyama za uso wake zitadondoka katika chombo  
kabla ya kuinywa, na pindi akiinywa nyama zake na ngozi yake  
zitaanguka, watu wa motoni wataudhika kwazo, na yule  
aliyetengeza, na yule aliyetengenezewa, na yule atakayeibeba, na  
yule anayebebewa, na yule mwenye kula thamani yake ni mshirika  
katika dhambi yake. Allah hatakubali swala zao, funga zao na hija  
zao, hadi watubu. Na wakifa kabla ya kutubia itakuwa haki juu ya  
Allah kumnyweshwa usaha wa Jahannam kwa kila funda (la pombe)  
alilolinywa katika dunia. Jua kuwa kila kinacholeweshwa ni pombe, na  
kila pombe ni haramu”<sup>257</sup>.*

Inaingia katika kauli yake:

«كل مسكر خمر»

*“ Kila kinacholeweshwa ni pombe. ”<sup>258</sup>*

Bangi, kama maelezo yake yatakapokuja baadae, InshaaAllaah. Na imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

« أن شربة الخمر إذا أتوا على الصراط يتخطفهم الزبانية إلى نهر الخبال  
فيسقون بكل كأس شربوها من الخمر شربة من نهر الخبال ، فلو أن  
تلك الشربة تصب من السماء لأحرقت السماوات من حرها «

*“Kuwa wanywaji pombe watapofika juu ya daraja iliyopo juu ya  
Jahannam (Swiraat) malaika wa Jahannam watawakwapua hadi  
kwenye mto Al-Khibaal na watawanyweshwa, kwa kila glasi ya pombe*

---

<sup>257</sup> Hadithi hii sijaiona.

<sup>258</sup> Imepokewa na Muslim 2003 kutoka kwa Ibn 'Umar.

*aliyokunywa (wakati wa maisha yake) kinywaji kutoka katika mto wa Al-Khibaal, lau kinywaji hicho kingemwagwa mbinguni, mbingu ingeungua kutokana na joto lake”<sup>259</sup>.*

Tunamuomba Allah atukinge na hayo. Amin.

## **FASILI**

### **Baadhi ya Simulizi Kutaja Salaf Kuhusu Pombe**

Ibn Masuud amesema: “Anapokufa mnywa pombe mzikeni, kisha msulubuni juu ya mbao, kisha fukueni kaburi lake mkiona uso wake haujageuzwa kibla vinginevyo muacheni akiwa amesulubiwa”.<sup>260</sup>

Fudhail Bin ‘Iyyaadh رضى الله عنه alisema: “Nilikwenda kwenye kitanda cha mmoja wa wanafunzi wangu aliyekuwa katika Sakaratil mauti na kumwambia atoe shahada, lakini hakuweza kuitamka, nikamkariria akasema: Siitamki kwani mimi niko mbali nayo, Fudhail akatoka kwake huku analia, kisha akamuona baada ya muda katika ndoto anakokotwa motoni, Akasema: nikamwambia: “Ewe masikini, kwa nini elimu yako imekutupa?” Yeye akanijibu: “Ewe mwalimu wangu, mie nilikuwa na ugonjwa kwa hiyo nikamuuliza tabibu akaniambia ninywe glasi moja ya mvinjo kila mwaka, usipofanya hivyo basi ugonjwa utabaki. Kwa hiyo mie nikawa nikitumia glasi moja ya mvinyo kila mwaka kwa dawa! Je, ikiwa hii ni hali ya mtu anayekunywa mvinyo kwa ajili ya dawa, itakuwa vipi kwa yule mtu ambaye anayeinywa kwa sababu isiyo kuwa hiyo? Tunamuomba Allah تعالى msamaha, na afya kwa kila balaa.

Mtubiaji mmoja aliulizwa kuhusu toba yake akasema: “Nilikuwa nafukua makaburi nikaona humo maiti wamegeuzwa na kibla, nikawauliza watu wao, wakasema walikuwa wanakunywa pombe, na wakafa bila toba.”

---

<sup>259</sup> Hadithi hii sijaiona. Baihaqi ameitaja katika Az Zawaajir 2/158-159.

<sup>260</sup> Habari hii haijasimama juu ya isinadi yake, na habari ya Ibn Masuud ni ngeni mno haingii akilini.

Mcha Mungu mmoja alisema: “Mtoto wangu mdogo wa kiume alifariki, na miye nilimzika, baada yake nikamuona baada ya muda usingizini amekuwa na mvi, nikamuuliza, mwanangu nimekuzika nawe ulikuwa mdogo, ni jambo gani limekupa mvi?, Yeye akanijibu: Umenizika karibu ya wanywa pombe duniani, kwa hivyo Jahannam ikapumua kwa ujio wake kwa hivyo hakubaki mtoto yoyote isipokuwa kichwa chake kimepata mvi kutokana na ukali wa fukuto lake. Tunajilinda kwa Allah kutokana na moto, na tunamuomba Allah msamaha na afya kutokana na yenye kupasisha adhabu katika Akhera.

Kwa hiyo ni wajibu juu ya kila muumini kutubia kwa Allah ﷻ kabla hajapatwa na mauti akiwa juu ya athari ya hali yake.

### **FASILI**

Hashishi inatokana na jani la mbingi ambalo ni haramu na mtumiaji wake anaadhibiwa kama mnywaji pombe, na hiyo ni chafu zaidi kuliko pombe, kwa upande wa akili, kwani humfanya mtu kuwa khanithi, na kuwa dayuthi, na mengine katika uharibifu. Pombe ni mbaya zaidi kushinda bangi kwa upande mwingine, kwa kuwa inapelekea kugombana na kupigana, na yote hayo yanazuia kumtaja Allah na kuswali.

Baadhi ya wanazuoni wa mwisho walisita (kutafuta hukumu) katika adhabu yake, wakaona kuwa mtumiaji wake anaaziriwa bila kupewa haddi. Kwa vile walidhani kuwa hashishi inabadilisha akili bila kulevya, tofauti na bangi, wala hapajapatikana kauli yoyote kutoka kwa wanazuoni waliotangulia, wala sio hivyo kwani mtumiaji wake anapata kuchangamka zaidi kama vile walevi wa pombe na zaidi, na kuwazuia na dhikrullaahi na Swala, pamoja na udayuthi, ukhanithi na uharibifu wa tabia na akili na mengine.

Lakini ikiwa ni kavu yenye kuliwa sio kinywaji, wanazuoni wanatofautiana juu ya unajisi wake, kwa kauli tatu katika madhehebu ya Imamu Ahmad na wengine, Ikaambiwa: hiyo ni najisi kama pombe

## Al - Kabair

---

inayonyweshwa. Na haya ni mazingatio sahihi, na ikasemwa hapana ni kwa ukavu wake, na ikasemwa inatofautishwa baina ya ukavu wake na umajimaji wake. Kwa hali zote, hiyo inaingia katika aliyoyaharamisha Allah na Mjumbe Wake, katika pombe na ulevi kwa tamshi na maana.

Abu Musa رضي الله عنه alimuulizia Mtukufu Mtume ﷺ: “Ewe Mjumbe wa Allah tupe fatwa kuhusu vinywaji viwili tulivyokuwa tunatengeneza katika Yemen, (Bit`i), kutokana na asali na kinginecho kutokana na ngano. Zinachachuka hadi zinakuwa kali’.

Abu Musa akasema na Mtume ﷺ amepewa ufasaha wa maneno kwa kuhitimisha kwake, hivyo akasema Mtume ﷺ:

« كل مسكر حرام »

“Kila kilevi ni haramu.” Muslim<sup>261</sup>.

Vile vile alisema:

« ما أسكر كثيره فقليله حرام »

“Chenye kuleweshwa kingi chake basi kidogo chake ni haramu.”<sup>262</sup>

Mtume ﷺ hakutofautisha baina ya vilevi vinavyonywewa au vinavyoliwa, na kuwa pombe inaweza kutengenezwa kwa mkate, Na hashishi inayeyushwa kwa maji. Na pombe inanywewa na inaliwa, na hashishi inanywewa na inaliwa.

Wanazuoni wakaitaja kwa kuwa haikuwepo katika zama za Salafi swalih. Hiyo imezuka katika zama za ujio wa mangoli (Watatari) katika miji ya Uislamu, kumeimbwa mashairi kwa ajili ya wasifu wake:

---

<sup>261</sup>Sahihi: Ameipokea Ahmad 3/361, Muslim 2002, kwa njia nyingine, na Bukhari ameipokea 5575, kutoka kwa Ibn Umar

<sup>262</sup>Sahihi: Ameipokea Ahmad 6/190, Bukhari 5585, Muslim 2001 kutoka kwa ‘Aishah

## Al - Kabair

---

فآكلها وزارعها حلال      فتلك على الشقي مصيبتان

*Basi kula kwake na kulima kwake ni halali,  
Na hilo juu ya muovu ni misiba miwili.*

Wallaahi Ibilisi hajafurahi kama furaha yake kwa hashishi. Kwani ameipamba kwa watu duni wakaihalalisha na wakairuhusu.

قل لمن يأكل الحشيشة جهلا      عشت في أكلها بأفبح عيشة  
قيمة المرء جوهر فلماذا      يا أبا الجهل بعته بحشيشة

*Mwambie anayekula hashishi kwa ujinga,  
Unaishi kwa kula kwake maisha mabaya zaidi  
Thamani ya mtu ni johari basi kwa nini  
Ewe ndugu wa ujinga umeiuza kwa hashihi?*

### HEKAYA<sup>263</sup>

Abdul Malik bin Marwaan anatoa taarifa kuwa kijana mmoja alikwenda kwake, huku akilia kwa uchungu, na akasema: “Kiongozi wa waumini, miye nimetenda dhambi kubwa, je, mimi nitapata toba?” Akamuuliza: ‘Ni nini dhambi zako?’ Akasema: ‘Dhambi zangu ni kubwa’, akamwambia: ‘Ni ipi hiyo?, Tubia kwa Allah Aliyetukuka kwani yeye anakubali toba kwa waja wake na husamehe makosa.’ Yule mtu akasema: “Ewe amiri wa waumini Mimi nilikuwa nikifukua makaburi na mimi niliona mambo ya ajabu.” ‘Abdul Malik akamuuliza: “Uliona nini?” Yule mtu akamjibu: “Ewe kiongozi wa waumini, usiku mmoja nilifungua kaburi nikaona uso wa mfu (mtu alikua) umegeuka upande sio wa kibla. Kutokana na hayo miye nilianza kuogopa na kutaka kukimbia, nikasikia sauti ya mtu ndani ya kaburi ikiniambia: “Kwa nini Je, hutuulizi sisi maiti sababu gani tumekipa mgongo Qibla?” Hapo nikamuuliza: “Kwa nini umekipa

---

<sup>263</sup> Hekaya hii nitofauti na ni ya uongo.

Qibla mgongo? Yeye akasema: “Nilikuwa nikipuuza Swala”. Haya ni malipo ya mfano wake.

“Wakati mwengine nilifukua kaburi, nikamuona mkazi wake amegeuka nguruwe, na ana minyororo shingoni mwake. Niliogopa na kutaka kuondoka nikamsikia mtu akiniambia: “Kwa nini humuulizi matendo yake, kwa nini anaadhibiwa?” Basi mie nikamuuliza maiti: “Kwa nini una hali hii?” Yeye akanijibu, ‘miye nilikuwa nikinywa pombe wakati wa uhai wangu na nilikufa bila kutubia.” Kwa mara ya tatu tena ewe kiongozi wa waumini nilifukuwa kaburi na nikamuona mkazi wake amezongwa na nyuzi za moto. Na ulimi wake unanin’ginia niliogopa na nikataka kuondoka, nikaambiwa nimuulize maiti kisa cha kuwa hivyo. Mie nikamuuliza “Kwa nini uko hivyo? Akanijibu: “Mie sikuwa nikijichunga na mkojo, na alikuwa anahamisha maneno baina ya watu, basi haya ni malipo ya mfano wake.”

Na wanne, ewe kiongozi wa waumini, Mie nilipofukua kaburi nilimkuta mkazi wake ameunguzwa na moto, niliogopa na nilitaka kuondoka, niliuliza: “Hutaki kumuuliza kwa nini yu hali hiyo?” Nikamuuliza, ‘kwa nini?’ Na yeye akanijibu: “Mie nilikuwa nimeacha Swala’. Na la tano ewe kiongozi wa waumini, nilipolifukua niliona kaburi hilo kubwa likiwa wazi kiasi cha upeo wa macho yangu na mlikuwa na mwangaza unaong’aa, na maiti ilikuwa imelala juu ya kitanda, amevaa nguo nzuri na mwanga umesambaa juu ya kiwiliwili chake, nikapata woga nikataka kuondoka, pakasemwa: ‘Kwa nini humuulizi sababu ya utukufu huu.’ Nikaulizia: “Kwanini ametukuzwa hivyo?” Niliambiwa kuwa alikuwa kijana mtiifu akitenda wajibu wake kwa Allah تعالی na Alitukuka na alikuwa na bidii katika kumuabudu Yeye تعالی.

‘Abdul Malik akasema: “Hakika katika hili kuna mazingatio kwa waasi na bishara kwa watiifu.” Kwa hivyo, wajibu kwa mwenye kujaribiwa na aibu hizi basi arudi haraka kwenye toba na utii. Allah ajutaalie sisi na nyinyi tuwe miongoni mwa watii na atuepushe na matendo maovu. Hakika Yeye تعالی ni Mpaji Mkarimu.

## DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI

### KAMARI

Allah Aliyetukuka Anasema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْحَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ  
فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ  
فِي الْحَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيُضِدَّكُمْ عَنِ ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ ۗ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ ﴿٩١﴾

***“Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shet’ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa. Hakika Shet’ani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mmeacha?” (5:90-91)***

Maana ya *Maysir* inajumuisha aina zote za kamari kwa mfano chess, karata, vijiwe au mifano yake, na huko ni katika kula mali za watu kwa batili. Allah Ta’laa ameyakataza kwa Kauli Yake:

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُم بَيْنَكُم بِالْبَاطِلِ

***“Wala msiliane mali zenu baina yenu kwa baat’ili..” (2:188)***

Inaingia katika kauli ya Mtukufu Mtume ﷺ :

« إن رجالا يتخوضون في مال الله بغير حق فلهم النار يوم القيامة »

***“Hakika watu wanazama katika mali ya Allah bila haki wana moto siku ya kiyama.”*** <sup>264</sup>

<sup>264</sup> Ameipokea Bukhari 3118

Na katika Sahihi Bukhari Mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

« من قال لصاحبه : تعالى أقامرك، فليصدق »

*"Pindi yoyote akimuambia mwenzake, njoo tucheze, kamari basi na atoe sadaka"*<sup>265</sup>.

Kwa hivyo, ikiwa kutamka tu kucheza kamari, kunawajibisha kutoa kafara, au sadaka, Nini dhana yako katika kutenda?!

### KAMARI

Kushindana na kuwekeana dau ni jambo maarufu ambalo linatokea kati ya watu wawili ambao wanatofautiana katika kitu na hivyo kumfanya mmoja wao aseme: ikiwa mimi niko sawa basi ni juu yako kadha wa kadha, na ikiwa kama unasema ni sawa basi juu yangu hili na lile. Kufanya hivi ni haramu kwani inaingia katika kamari ambayo Allah ameifananisha na pombe.

Allah Amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْحَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ  
فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ  
فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ ﴿٩١﴾

***"Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shet'ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa. Hakika Shet'ani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari..." (5:90-91)***

---

<sup>265</sup> Sahihi ameipokea Bukhari 4860,6301, Muslim 1648 kutoka kwa Abu Hurairah.



## FASILI

Wanazuoni wametofautiana kuhusu chesi wakati wachezaji hawaweki dau wanapocheza kati yao hata hivyo kuna muafaka kuwa kucheza domino inakatazwa kwa kauli ya Mjumbe wa Allah ﷺ:

« من لعب بالتردشير فكأنما صبغ يده في لحم الخنزير ودمه »

*“Yeyote anayecheza domino ni kama aliye pakaza mkono wake nyama ya nguruwe na damu yake.”<sup>266</sup> Muslim*

Na akasema:

« من لعب بالترد فقد عصي الله ورسوله »

*“Mwenye kucheza domino amemuasi Allah na Mjumbe wake”<sup>267</sup>*

Ama kuhusu *domino* wanazuoni wote wanakubaliana uharamu wa kucheza kwake kuwe na kuwekeana dau au kwa vinginevyo. Ama kukiwa na dau hiyo ni kamari bila khilafu ya wanazuoni. Endapo pakiwa hakuna dau baadhi ya wanazuoni wanasema ni haramu. Lakini Shafi'iyā wanaruhusu, kwa masharti ichezwe faragha, na haisababishi kupuuza wajibu wa Swala kwa wakati wake. Imamu An-Nawawi aliulizwa kuhusu kucheza mchezo wa chesi, na alijibu: ‘Hiyo ni haramu kwa wengi wa wanazuoni.’ Akaulizwa tena kuhusu mchezo wa chesi inafaa au la. Akajibu: ‘Ikiwa itasababisha kukosa Swala kwa wakati wake, au kukiwepo dau, basi hiyo ni haramu, vinginevyo ni makuruhu kwa Shafi, na ni haramu kwa wengine.’ Kwa hiyo haya ni maneno ya Nawawi kwenye fatwa zake. Wanazuoni wengi dalili yao ni kauli ya Allah Taala:

---

<sup>266</sup> Sahihi ameipokea Ahmad 5/352, 357, Muslim 2260, kutoka kwa Buraidah.

<sup>267</sup> Ameipokea Ahmad 4/279, Abu Dawud 4938, Ibn Maajah 3762, Swahihul Jami'i 6562, Al Irwaa 2670.

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالْدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنْزِيرِ

**“Mmeharimishiwa nyamafu, na damu, na nyama ya nguruwe”(5:3)**

Hadi kauli yake

وَأَنْ تَسْتَقْسِمُوا بِالْأَزْلَمِ

**“Na ni haramu kupiga ramli”**

Sufyaan na Waqii`u ibnul Jarraah wamesema: “Hiyo ni Chess.” ‘Ali bin Abi Twaalib رَضِيَ اللهُ عَنْهُ amesema: “Chesi ni kamari ya waajemi.” Alipita kwa watu wanaocheza chesi, akasema: “Ni nini haya masanamu ambayo mnayaabudu?, Ni bora mmoja wenu kushika kaa la moto hadi lizimike kuliko kuigusa (chesi)”<sup>268</sup>.

Kisha akasema: “Wallaahi mmeumbwa kwa ajili ya lisilokuwa hili”. Na akasema vile vile: “Mcheza chesi ni mtu mwongo zaidi wa watu, kwani mmoja wao anasema: “Nimeua.” Na kwa hakika yeye hajaua, Na nimekufa na hajakufa”.

Abu Musa Al Ash’ari anasema: “Hachezi chess isipokuwa mkosaji.”<sup>269</sup> Ishaq bin Raahawayhi aliambiwa: “Unaona kosa lolote katika kucheza chesi?”. Akasema: “Makosa yote yamo ndani yake”. Akaambiwa: ‘Hakika watu walinzi wa mipakani wanacheza chesi kwa ajili ya vita’, Akasema; ‘huo ni uovu.’

Muhammad binil Quradhi aliulizwa kuhusu chesi, akasema: ‘Kwa uchache atachokuwa nacho mcheza chesi siku ya kياما ni kufufuliwa na watu wa batili”.

---

<sup>268</sup> Dhaifu: Ameipokea Baihaqi katika Shi’ib 6518, Sunan 10/212, na isinadi yake ni dhaifu.

<sup>269</sup> Hassan: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Shi’ib 10/212 na Ash-Sha’ab 5/241.

## Al- Kabair

---

Ibn 'Umar aliulizwa kuhusu chesi akasema: "Hiyo ni mbaya zaidi kuliko nardi (backmmon)". (Na maelezo yake yametangulia).

Imam Malik aliulizwa kuhusu chesi akasema: 'Chesi ni kutokana na domino.' Ibn 'Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَالi alisimamia mali ya yatima, akaikuta chesi katika mirathi ya mzazi (wake) akaichoma.<sup>270</sup> Ingekuwa mchezo wa chesi ni halali basi Ibn 'Umar isingefaa kwake kuichoma moto kwa vile ni mali ya yatima. Kwa kuwa kuucheza ni haramu ameimwaga, kwa hiyo inakuwa ni jinsi ya pombe inapokutwa katika mali ya yatima inapasa kumwagwa, vile vile.

Haya ni madhehebu ya mwanachuoni wa umma Ibn 'Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَاIbrahim an-Nakhaai aliambiwa: "Unasemaje katika kucheza chesi?" Akasema: "Hiyo imelaaniwa".<sup>271</sup>

Abu Bakri bin al-Athram amepokea katika Jaami'i yake kutoka kwa Waathila bin al-Asqaa kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

« إن الله في كل يوم ثلاثمائة وستين نظرة إلى خلقه ليس لصاحب الشاه فيها نصيب - يعني لاعب الشطرنج - لأنه يقول: شاه مات »<sup>1</sup>

*"Hakika Allah ana mitazamo mia tatu na sitini kwa waja wake; kwa mwenye kucheza chesi hana fungu katika hiyo - kwa sababu anasema kuwa Shah amekufa."*<sup>272</sup>.

Abu Bakri Al Ajri amepokea kwa isinadi yake kutoka kwa Abu Hurairah رَضِيَ اللهُ عَنْهُkuwa Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>270</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Shi'ib 5/241 na Ibn Abi Dunya katika Dhammil-Malaahi, 102.

<sup>271</sup> Kaipokea Bayhaqi katika Sunan 10: 212 na Shiib 6520 kwa sanadi Dhaifu. Angalia Al Irwaa 2671.

<sup>272</sup> Kaipokea Ibn Hibban katika Majrihiin 2: 297 na Ibn Jawzi katika 'Ilal angalia Al-Irwaa 2601

« إذا مررتم بهؤلاء الذين يلعبون الأزلام النرد والشطرنج وما كان من اللهو فلا تسلموا عليهم ، فإنهم إذا اجتمعوا وأكبوا عليها جاءهم الشيطان بجنوده فأحرق بهم ، كلما ذهب واحد منهم يصرفه عنها لكره الشيطان بجنوده ، فلا يزالون يلعبون حتى يتفرقوا كالكلاب اجتمعت على جيفة فأكلت منها حتى ملأت بطونها ثم تفرقت ، ولأنهم يكذبون عليها فيقولون: شاء مات »

*“Mnapopita kwa hao ambao wanacheza azlami ambazo ni backgammon na chesi na laghwi zilizopo msiwasalimie, kwani wao wanapokusanyika na wakamwagia juu yake shetani anawajia na jeshi lake, na anawakodolea macho, kila mmoja wao anapoondoa jicho lake shetani humpiga kofi, kwa hiyo hawaachi kucheza mpaka watawanyike kama mbwa waliokusanyika kwenye mzoga wakaula hadi matumbo yakajaa kisha wakatawanyika, na kuwa wao wanadanganya juu yake wanasema: ‘Shah (mfalme) amekufa”<sup>273</sup>.*

Amepokea tena kutoka kwake kuwa Mtume ﷺ amesema:

أشد الناس عذاباً يوم القيامة صاحب الشاه ، يعني صاحب الشطرنج ،  
ألا تراه يقول : قتلته ، والله ما مات ، والله افتري ، وكذب على الله »

*“Mwenye kupata adhabu kali zaidi siku ya kiama ni mcheza chesi, kwani huoni anasema: Nimemuua, Wallaahi amekufa, Wallaahi amedanganya juu ya Allah”<sup>274</sup>.*

Mujaahid alisema: Hakuna maiti yoyote anakufa analetewa rafiki zake ambao alikuwa anakaa nao, akaja mtu aliyekuwa anacheza chesi akaambiwa: Sema: “Laa ilaaha illa Ilaahu.” Alijibu: “shahaaka (mfalme-vidude katika chess), kisha akafa, kwa hiyo kile kilichozeewa katika uhai wake katika mchezo, Kwa hiyo mbadala wa neno la ikhlasi ni shahaaka.”

<sup>273</sup> Hadithi hii sijaiona, Mundhir amesema: Kumekuja utajo wa chesi katika hadithi nyingi sijui usahihi wake

<sup>274</sup> Hadithi hii sijaiona

## Al - Kabair

---

Na imekuja kwa mtu mwingine, miongoni mwa wanywa pombe aliokuwa anakaa nao, wakati alipojiwa na mauti, mtu akamjia anamlakinia shahada, basi yule mtu akamwambia: “Kunywa na ninyweshe, kisha akafa, *Fa Laa hawla wala quwwata illa billaahil aliyyil adhiim*. (Kwa hiyo hakuna hila wala nguvu isipokuwa kwa Allah Aliye juu Aliyetukuka”. Na hii ni kama ilivyokuja katika Hadithi:

*“Mtu hufa katika hali aliyo ishi nayo, na atafufuliwa katika hali aliyo kufa nayo”<sup>275</sup>.*

Tunamuomba Allah تعالیٰ Mkarimu Mkuu Atujaalie tufe kama waislamu.

\*\*\*

---

<sup>275</sup> Sahihi: Ameipokea Imamu Ahmad 3/331,366. Muslim 2878, kutoka kwa Jaabir kwa tamshi: “Hufufuliwa kila mtu kwa alichofia.”

DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI NA MOJA

KUWASINGIZIA WANAWAKE WENYE KUJIHIFADHI

Allah تعالیٰ Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ الْغَافِلَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ لُعُنُوا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَهُمْ  
عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾ يَوْمَ تَشْهَدُ عَلَيْهِمْ أَلْسِنُهُمْ وَأَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٤﴾

***"Hakika wanao wasingizia wanawake, wanao jihishimu, walio ghafilika, Waumini, wamelaaniwa duniani na Akhera, nao watapata adhabu kubwa. Siku ambayo zitawashuhudia ndimi zao na mikono yao na miguu yao kwa waliyo kuwa wakiyatenda." (24:23-24)***

Akasema:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ ثَمَانِينَ جَلْدَةً وَلَا  
تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٤﴾

***"Na wanao wasingizia wanawake mahashumu, kisha wasilete mashahidi wane, basi watandikeni bakora thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena. Na hao ndio wapotovu." (24:4)***

Allah تعالیٰ amebainisha katika aya hizi kuwa yoyote atakayemsingizia mwanamke aliyejihifadhi, muungwana, na mwenye kujichunga dhidi ya zina na uchafu, huyo hulaaniwa hapa duniani na kesho Akhera, na ana adhabu kubwa, duniani atachapwa viboko themanini, na ushahidi wake utaanguka, hata kama akiwa mwadilifu.

Katika sahihi mbili; Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« اجتنبوا السبع الموبقات ... »

*“Epukeni mambo saba yenye kuangamiza..”*

Alitaja miongoni mwa hayo: kukashifu wanawake waliohifadhiwa, waumini, wenye kughafilika (wasiojihusisha na uchafu).

Kusingizia ni kumwambia mwanamke muungwana, mwenye kujichunga, na Muislamu: “Ewe mzinifu, au ewe kahaba, au ewe Malaya’, au Mtu amwambie mumewe, ‘Ewe mwanamume malaya’, au mtu kumwita mwanawe, ‘Ewe mtoto wa haramu’, au mtu kumwambia binti yake, ‘Ewe mtoto wa malaya’, kwani neno Malaya lina maana ya mzinzi na kahaba. Kwa hiyo mtu akimwambia mwingine maneno hayo juu basi itapasa juu yake adhabu ya bakora themanini, isipokuwa asimamishe ushahidi kwa hilo. Na ushahidi ni kama alivyosema Allah Taalaa; Mashahidi wanne wanao thibitisha ukweli wake, dhidi ya mwanamke aliyemsingizia, au mwanamume huyo, asipotoa uthibitisho basi atachapwa atakapodai kuambiwa maneno hayo aliyesingiziwa. Vile vile akimsingizia mtumwa, kama kumwambia mtumwa wake, “Ewe mzinifu, au ewe kahaba, au ewe mchafu.” Pia atapata hukumu hiyo ya kushikishwa adabu ya kuchapwa bakora themanini.

Imethibitika katika sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

« من قذف مملوكه بالزنا أقيم عليه الحد يوم القيامة إلا أن يكون كما قال »

*“Mwenye kumsingizia mjakazi wake kwa zina na hakuthibitisha atasimamishiwa haddi siku ya kiyama, ila iwe kama alivyosema”<sup>276</sup>.*

Wajinga wengi wanatumbukia kwenye maneno haya machafu ambayo yana adhabu katika dunia na akhera. Na hii ni kwa yaliyothibitika kutoka kwa Mtume ﷺ, kuwa amesema:

---

<sup>276</sup> Sahihi: Ameipokea Bukhari 6858, Muslim 1660, kutoka kwa Abu Hurairah.

« إن الرجل ليتكلم بالكلمة ما يتبين فيها يزل بها في النار أبعد مما بين المشرق  
والمغرب »

*“Hakika mtu atazungumza neno lisilokuwa na ukweli ndani yake,  
atateleza nalo motoni mbali zaidi kuliko mashariki na magharibi”<sup>277</sup>.*

Mu’adhi akamuuliza Mtume ﷺ: “Ewe Mtume wa Allah kwani sisi tutachukuliwa kutokana na maneno yetu?” Mtume ﷺ akasema:

« ثكلتك أمك يا معاذ ، وهل يكب الناس في النار على وجوههم إلا  
حصائد ألسنتهم؟ »

*“Akukose mama yako ewe Mu’adh, hivi ni kitu gani kitawaingiza  
watu motoni zaidi kuliko ndimi zao?”<sup>278</sup>*

Na katika hadithi nyingine:

« من كان يؤمن بالله واليوم الآخر فليقل خيرا أو ليصمت »

*“Mwenye kuwa anamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho  
basi na aseme kheri au anyamaze”<sup>279</sup>.*

Allah Tabaaraka wa Ta’ala amesema:

مَا يَلْفُظُ مِنْ قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٨﴾

**“Hatamki neno ila karibu yake yupo mwangalizi tayari.” (50:18)**

‘Uqbah bin `Aamir رضي الله عنه alimuuliza Mjumbe wa Allah تعالى: “Ewe Mjumbe wa Allah vipi nitaokoka?” Mtukufu Mtume ﷺ alijibu:

---

<sup>277</sup> Sahihi: Ameipokea Bukhari 6477, Muslim 2988, Pia kutoka kwa Abu Hurairah

<sup>278</sup> Sahihi: Ameipokea Tirmidhi 2616, Ibn Maajah 3973, Al Baani ameisahihisha, Al-Irwaa 413.

<sup>279</sup> Sahihi: Ameipokea Bukhari 6018, Muslim 47, Pia kutoka kwa Abu Hurairah



« أمسك عليك لسانك وليسعك بيتك ، وابتك على خطيئتك وإن أبعد الناس  
إلى الله القلب القاسي »

*“Jizuilie mwenyewe ulimi wako, na nyumba yako ikutoshe, na lia  
juu ya makosa yako, na hakika aliye mbali zaidi kwa Allah ni mwenye  
moyo msusuavu”<sup>280a</sup>.*

Na akasema: *“Hakika mchukiwa zaidi wa watu kwa Allah ni mchafu mwenye  
mdomo mchafu, ambaye anazungumza maneno machafu na maneno duni”*  
(Imepokewa sio katika lafdhi hii na Imam at Tirmidhy 92043 na Imam  
Ahmad 1:405)

Tunamuomba Allah Atukinge sisi na nyinyi, kutokana na shari za ndimi  
zetu, kwa Ukarimu Wake na Wema Wake, hakika Yeye ni Mpaji  
Mkarimu.

\*\*\*

---

<sup>280a</sup> Sahihi: Ameipokea Tirmidhi 2406, Ahmad 5/148,149,259. Swahiihil Jaami'i 1388

DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI NA MBILI

KUIBA KUTOKA KATIKA NGAWIRA ZA VITA

Nayo ni kutoka katika *Baitul Maal* na kutoka katika mali ya Zaka.

Allah تعالیٰ Anasema:  إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْخَائِبِينَ

“...*Hakika Allah hawapendi wenye kuhini..*” (8:58)

Akasema:

وَمَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَنْ يَغُلَّ وَمَنْ يَغُلَّ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ثُمَّ تُوْفَىٰ كُلُّ نَفْسٍ

“*Na haiwi kwa Nabii yeyote kufanya khiyana. Na atakaye fanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyo yafanyia khiyana..*” (3:161)

Katika sahihi Bukhari: Abu Hurairah رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa: “Mjumbe wa Allah ﷻ alisimama siku moja kati yetu na akataja hiana za ngawira za vita na akalikuza jambo lake, kisha akasema:

« لا ألفين أحدكم يجيء يوم القيامة على رقبته بعير له رغاء يقول : يا رسول الله أغثنى ، فأقول : لا أملك لك من الله شيئاً قد أبلغتك ، لا ألفين أحدكم يجيء يوم القيامة على رقبته فرس له حمحمة فيقول : يا رسول الله أغثنى ، فأقول : لا أملك لك من الله شيئاً قد أبلغتك . لا ألفين أحدكم يجيء يوم القيامة على رقبته شاة لها نغاء يقول : يا رسول الله أغثنى ، فأقول : لا أملك لك من الله شيئاً قد أبلغتك . لا ألفين أحدكم يجيء يوم القيامة على رقبته نفس لها صياح فيقول : يا رسول الله أغثنى ، فأقول : لا أملك من الله شيئاً قد أبلغتك . لا ألفين أحدكم يوم القيامة على رقبته رفاع تخفق ، فيقول : يا رسول الله أغثنى ، فأقول : لا أملك لك من الله شيئاً قد أبلغتك ، لا ألفين أحدكم يجيء يوم القيامة على رقبته صامت ، فيقول : يا رسول الله أغثنى ، فأقول : لا أملك لك من الله شيئاً قد أبلغتك »

*“ Sitopendelea kumuona yeyote miongoni mwenu siku ya kiyama anasema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah, niokoe’, Nitamwambia: ‘Similiki chochote kilichokufika kwa ajili yako kutoka kwa Allah’, sitapenda kumuona yoyote miongoni mwenu siku ya kiyama shingoni mwake kuna farasi huku analia, na huku anasema: “Ewe Mjumbe wa Allah niokoe’, Nitamwambia: ‘Similiki chochote kilichokufika kwa ajili yako kutoka kwa Allah’, Sitapenda kumuona yoyote miongoni mwenu siku ya kiyama shingoni mwake kuna mbuzi na huku analia, ‘Ewe Mjumbe wa Allah niokoe’. Nitamwambia: ‘Similiki chochote kilichokufika kwa ajili yako kutoka kwa Allah’. Sitapenda kumuona yoyote miongoni mwenu siku ya kiyama shingoni mwake kuna nafsi ina piga kelele na huku analia, ‘Ewe Mjumbe wa Allah niokoe’. Nitamwambia: ‘Similiki chochote kilichokufika kwa ajili yako kutoka kwa Allah’. Sitapenda kumuona yoyote miongoni mwenu siku ya kiyama shingoni mwake kuna nguo zinapeperuka na huku analia, ‘Ewe Mjumbe wa Allah niokoe’. Nitamwambia: ‘Similiki chochote kilichokufika kwa ajili yako kutoka kwa Allah’. Sitapenda kumuona yoyote miongoni mwenu siku ya kiyama shingoni mwake kuna dhahabu na fedha, huku analia na anasema, “Ewe Mjumbe wa Allah niokoe.’ Nitamwambia: ‘Similiki kwa ajili yako chochote kilichokufika kutoka kwa Allah”<sup>280b</sup>. Hadithi hii ameipokea Muslim.*

Hadithi hii inaonya wale wanaochukua kitu kutoka katika ngawira za vita. Kabla vitu hivyo havijagawanywa kati ya washindi, kutokana na hazina bila ya ruhusa ya kiongozi au kutoka fungu la Zaka ambayo imekusanywa kwa ajili ya wahitaji. Atakuja siku ya kiyama huku amebeba shingoni mwake kile alichokichukua, kama alivyotaja Allah Aliyetukuka:

وَمَنْ يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ<sup>ع</sup>

**“...Na atakaye fanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyo yafanyia khiyana...”. (3:161)**

---

<sup>280b</sup> Ameipokea Ahmad 2/426, Bukhari 3073, Muslim 1731.

## Al - Kabair

---

Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

« أدوا الخيط والمخيط وإياكم والغلول، فإنه عار على صاحبه يوم القيامة »

*“Lipeni (hata kama) uzi na jiepusheni na khiyana kwani hiyo ni aibu siku ya kiama”<sup>281</sup>.*

Alipomteua ibn Latbiyyah kukusanya Zaka, alipokuja, akasema: “Hii ni yenu na hii ni yangu nimepewa zawadi”. Mtume ﷺ alipanda juu ya mimbari na baada ya kumsifu Allah ﷻ alisema:

« والله لا يأخذ أحد منكم شيئاً بغير حقه إلا جاء يوم القيامة يحمله ، فلا أعرف رجلاً منكم لقي الله يحمل بغيراً له رغاء أو بقرة لها خوار أو شاة تيعر ، ثم رفع يده ﷻ فقال : «اللهم هل بلغت ؟ »

*“Wallaahi hachukui yoyote kati yenu chochote bila ya haki yake ila atakuja siku ya kiyama amekibeba, simjui mtu miongoni mwenu ambaye atakutana na Allah huku amembeba ngamia anayenung’unika, au ngombe anayelia, au kondoo anayelia”.*  
Mtume ﷺ alinyanyua mikono yake akasema: *“Ewe mola wangu, Je nimefikisha?”<sup>282</sup>*

Abu Huraira رضي الله عنه ametoa taarifa: “Tulikwenda kwa Mjumbe wa Allah ﷻ Khaibari na Allah ﷻ Alitupa ushindi hapakuwa na dhahabu au pesa kati ya ngawira, bali zilikuwepo nguo na chakula. Tukaenda bondeni (Al-Qura), pamoja na Mtume Mtukufu ﷺ alikuwepo mtumwa aliyepewa zawadi Mtume Mtukufu ﷺ na mtu mmoja wa Judhaam anaitwa Rifa’ah bin Yaziid kutokana na kabila la Banii Dhabiib. Tulipopiga kambi bondeni Mtumwa wa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa amesimama hapo, akifungua kipando chake Mtume ﷺ akarushiwa mshale ikawa ndio mauti yake. Sisi tukasema: “Furaha yake, amepata shahada Ewe Mjumbe wa Allah” . Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

---

<sup>281</sup> Sahihi: Ameipokea Ahmad 5/318,319, Tirmidhi 1561, Nasaai 7/131, Ibn Maajah 2852, kutoka kwa Ubbadah bin Swaamit. Al Baani amesahihisha isinadi yake katika Al Irwaa 5/74-75, As Silsilah As Swahihah 985.

<sup>282</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 2597 na Muslim 1832.

« كلا والذي نفسي بيده إن الشملة لتلتهب عليه نارا ، أخذها من الغنائم  
لم تصبها المقاسم » .

*"Hapana! Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake  
kilemba chake kinawaka moto, alikichukuwa kwenye ngawira ambayo  
hakikufikiwa na mgao".*

Basi watu wakafadhaika, Mtu mmoja akaja na kamba moja au mbili  
(akasema: Nimezipata siku ya vita vya Khaibar) Mtume ﷺ alisema:

« شركاء أو شركان من نار »

*" Kamba moja au mbili ni moto" ,<sup>283</sup>*

'Abdullah bin 'Amr anasimulia: "Palikuwa na mtu mmoja jina lake  
Karkara ambaye alikuwa akiangalia mzigo wa Mtume ﷺ, mtu huyo  
alikuwa na Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

« هو في النار »

*" Yeye yuko motoni."*

basi watu wakaenda kumuangalia wakamkuta na joho ambalo aliliiba  
kutoka katika ngawira ya vita." (Bukhari)<sup>284</sup>.

Zayd bin Khalid Juhani anataarifu kuwa mtu mmoja aliiba kitu kutoka  
katika ngawira ya vita vya Khaybar, wakati alipokufa, Mtukufu  
Mtume ﷺ alitukataza kumswalia Swala ya mazishi na alisema:

« إن صاحبكم غل في سبيل الله »

*"Hakika mwenzenu amekhini katika njia ya Allah".*

---

<sup>283</sup> Sahihi Al-Bukhari 4234-6077 na Muslim 115.

<sup>284</sup> Sahihi Al-Bukhari 3074 na Ahmad 2/160.

Zayd akasema: "Tukaangalia katika vitu vyake tukagundua Lulu kati ya Lulu za wayahudi (wa khaybar) thamani yake ni sawa na dirham mbili<sup>285</sup>.

Imam Ahmad alisema: "Sisi hatukujua Mtume ﷺ kujizuia kumswalia yoyote isipokuwa mtu aliyeiba ngawira katika vita, na yule aliyejiuwa mwenyewe.<sup>286</sup> Kuwa Mtume ﷺ alisema:

« هدايا العمال غلول »

*"Zawadi kwa watendaji ni khiyana".<sup>287</sup>*

Katika mlango huu kuna hadithi nyingi za Mtume ﷺ kuhusu huo wizi. Baadhi yake zitakuja katika mlango wa dhuluma. Na dhuluma ipo sehemu tatu; Kwanza, kula mali kwa batili; Pili, kudhulumu waja kwa kuua, au kupiga, au kuvunja na kujeruhi; Tatu, kudhulumu waja kwa kuwashutumu, kuwalani, kuwatukana, na au kuwasingizia. Mtukufu Mtume ﷺ alihutubia Mina akasema:

« ألا إن دماءكم وأموالكم وأعراضكم عليكم حرام كحرمة يومكم هذا في شهركم هذا في بلدكم هذا »

*"Sikilizeni, damu yenu, mali yenu, na heshima yenu ni haramu juu yenu, kama heshima ya siku yenu hii, katika mwezi wenu huu, na mji wenu huu." (Bukhari na Muslim)<sup>288</sup>*

---

<sup>285</sup> Sahihi Ameipokea Abu Dawud 2710, An-Nasaai 4/64, Ibn Maajah 2848, Al-bani ameisahishwa katika Ahkaamil Janaaiz: 79, Al-Irwaa 726, Na Taaliqur-Raghiib 2/189.

<sup>286</sup> Sahihi: Imepokewa kuwa Mtume kwamba Mtume amewacha kumswalia kwa sababu ya deni analodaiwa aliyefariki na jambo hili lilikuwa hapo mwanzoni kasha alipofunguliwa alisema: "Mimi ni wa mwanzo kwa waumini kuliko wao wenyewe hivyo atakayekufa akiwa na deni basi ni juu yangu kulipa. Na atakayeacha mali basi mali ile ni kwa warithi wake." Imepokewa na Ahmad 2/290, Muslim 1619 na Al-Bukhari amepokewa kwa mfano huo 5371.

<sup>287</sup> Imepokewa na Abu Dawud 2710, An-Nasai 4/64, Ibn Majah 2848 na kusahishwa na Al-Albani katika Ahkam Al-Janaiz 79, Al-Irwaa 726 na At-Ta'aliq Ar-Raghiyb 2/189.

<sup>288</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 105, 1741 na Muslim 1679.

## Al - Kabair

---

Na akasema:

« لا يقبل الله صلاة بغير طهور ولا صدقة من غلول »

*“Allah hakubali swadaqa yoyote bila tahara wala swadaqa ya khiyana”.*<sup>289</sup>

Tunamuomba Allah taufiqi katika Anayoyapenda na Anayoyaridhia,  
Hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu!.

\*\*\*

---

<sup>289</sup> Imepokewa na Muslim 224, At-Tirmidhi 1 na Ibn Majah 273 na 271.

## DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI NA TATU

### WIZI

Allah Aliyekuka Anasema:

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا جَزَاءً بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِّنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٣٨﴾

***“Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, kateni mikono yao, hayo ni malipo ya waliyo yachuma, ni adhabu ya mfano itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima”. (5:38)***

Ibn Shihaab alisema Allah تعالی Amehukumu adhabu ya kukata katika kuiba mali za watu. Na Yeye تعالی ni Mwenye Nguvu katika kuadhibu Kwake, Mwingi wa hekima, katika aliye mwajibisha kukatwa mkono wake. Mjumbe wa Allah تعالی alisema:

« لا يزني الزاني حين يزني وهو مؤمن ، ولا يسرق السارق حين يسرق وهو مؤمن ، ولكن التوبة معروضة »

*“Hazini mzinzi wakati anazini na huku ni muumin, wala haibi mwizi wakati anapoiba na huku ni muumin, lakini toba ni yenye kuonyeshwa”.<sup>290</sup>*

Ibn ‘Umar رضي الله عنهما anatoa taarifa kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alimkata mkono mwizi alipoiba kitu thamani yake dirham tatu.<sup>291</sup> na kutoka kwa Aisha akasema: ‘Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa anakata mkono wa mwizi katika robo dinari na zaidi’.<sup>292</sup> Katika riwaya nyingine Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>290</sup> Takhriji yake ishaelezwa.

<sup>291</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 95, 96 na 98 na Muslim 1686.

<sup>292</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6786, 6790 na Muslim 684.



## Al- Kabair

---

*“Usikate mkono wa mwizi chini ya ya thamani ya kikoti (al majni)”.*  
*‘Aisha alipoulizwa, ‘Nini thamani ya kikoti?’ Alijibu: ‘Robo ya dinari’<sup>293</sup>*

Katika riwaya nyingine Mtume ﷺ amesema,

*“ Kateni kwa Robo Dinari wala msikate chini ya hapo”<sup>294</sup>*

Dinari ni sawa na dirham tatu, kwani dinari moja ni sawa na dirham kumi na mbili na zaidi. Robo dinari wakati huo ilikuwa ni dirhamu tatu na dinari ni dirhamu kumi na mbili.

Abu Hurairah رضى الله عنه anatarifu kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

وقال النبي ﷺ: «لعن الله السارق يسرق الحبل فتقطع يده»

*“Allah amemlani mwizi anayeiba yai na anakatwa mkono wake, na anaiba kamba anakatwa mkono wake”<sup>295</sup>*

Al-A'mash amesema: “Watu walikuwa wanaona kuwa anatoa yai la chuma (kofia) na kamba walikuwa wanaona inalingana na dirhamu tatu.”  
Aisha amesema: “Mwanamke wa kimakhzuumi alikuwa anaazima vitu na anakanusha, basi Mtume ﷺ akaamrisha kukatwa mkono wake. Watu wake wakamjia Usamah bin Zaid wakaongea nae katika hilo, nae akaongea na Mjumbe wa Allah ﷺ. Naye akamwambia:

*“Ewe Usamah nakuona unatetea katika adhabu miongoni mwa adhabu za Allah Taalaa”.*

Kisha akasimama kuwahutubia watu akasema:

---

<sup>293</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 6792, 6793, 679 na Muslim 1685.

<sup>294</sup> Imepokewa na Ahmad 6/80 na At-Tabarani katika Al-Awsat 8/306

<sup>295</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 6793, 6799 na Muslim 1687.

« إنما أهلك من كان قبلكم أنهم كانوا إذا سرق فيهم الشريف تركوه ، وإذا سرق فيهم الضعيف قطعوه والذي نفسي بيده لو أن فاطمة بنت محمد سرقت لقطعت يدها »

*“Enyi watu! Si vingine wameangamia waliokuwa kabla yenu, kwani wao walikuwa akiiba kati yao mtukufu basi wanamuacha, na akiiba kati yao mnyonge wanamkata (mkono). Naapa kwa Ambaye nafsi yangu imo Mkononi Mwake lau Fatimah binti Muhammad angeiba ningekata mkono wake”.* Kwa hiyo akakata mkono wa yule binti wa Kimakhzumi. (Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6788 na Muslim 1688).

‘Abdulrahmaan bin Jariir alisema: “Tulimuuliza Fudhaalah bin ‘Ubaid kuning’iniza mkono wa mwizi shingoni mwake, ni katika Sunnah?”. Akasema: “Mwizi aliletwa mbele ya Mtume ﷺ akaamuru mkono wake ukatwe na uning’inizwe shingoni mwake.”<sup>296</sup> Wanazuoni wanasema: “Kujuta hakumnufaishi mwizi mpaka arudishe alichoiba, na akiwa amefilisika basi atajifungua kwa mwenye mali”. Allah ni Mjuzi zaidi.

\*\*\*

---

<sup>296</sup> Hadithi dhaifu: Imepokewa na Abu Dawud 4411, At-Tirmidhi 1447, An-Nasai 8/92, Ibn Majah 2587 na imedhoofishwa na Shaykh Al-Albani katika Al-Irwaa 2432.

## DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI NA NNE

### WIZI WA UHARAMIA

Allah Aliyetukuka Anasema:

إِنَّمَا جَزَأُ الَّذِينَ حُكِرُوا بِأَلْفِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَنْ يُقَتَّلُوا أَوْ يُصَلَّبُوا  
أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِمَّنْ خَلْفٍ أَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ ذَٰلِكَ لَهُمْ خِزْيٌ فِي  
الدُّنْيَا وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٥٣﴾

***“Basi malipo ya wale wanao mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wakawania kufanya uchafuzi katika nchi, ni kuuwawa, au kusalibiwa, au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kutolewa nchi. Hii ndiyo hizaya yao katika dunia; na katika Akhera watapata adhabu kubwa.” (5:33)***

Wahidi anasema: “Maana ya kupigana vita na Allah na Mjumbe Wake ﷺ: ‘Ni kuwaasi na kutowatii wao’. Kila asiye kutii amekupiga vita. Na wanakwenda katika ardhi kwa uharibifu, yani kwa kuu na kufanya wizi, na kuchukua mali. Na kila aliyetumia silaha juu ya waumini huyo ni mwenye kumpiga vita Allah na Mtume Wake. Na hii ni kauli ya Malik, Shafii na Awza’i. Kauli Yake Taalaa:

أَنْ يُقَتَّلُوا

***“Wauwawe”***

Hadi kauli yake:

***“ Au watolewe ardhini”***

Walibi amesema kutoka kwa Ibn Abbaas: (Neno au) Walibi limeingizwa kwa kuchagua, yaani mtawala akipenda ataua, na akipenda atasulubu,

na akitaka atamfukuza. Na hii ni kauli ya Hasan, Saiid bin Musayyib na Mujaahid.

Katika riwaya nyingine 'Atwiyyah amesema: 'Au' si kwa ajili ya kuruhusu, kwani hilo linategemea hukumu kwa kutofautiana na makosa. Ikiwa mtu akiuwa na akachukua mali, basi auliwe na asulubiwe; akiiba bila kuuwa, atakatwa mkono wake; na atakaye mwaga damu na hakuchukua mali atauwawa; na mwenye kutia hofu njia na hakuchukua mali atafukuzwa ardhini. Na huu mtazamo ni wa madhehebu ya Imam Shaafi.

Imam Shafii anasema kila mmoja ataadhibiwa kwa kadiri ya kitendo chake, ambaye anastahili kuuwawa na kusulubiwa, kwanza auwawe baadae asulubiwe (yaani asisulubiwe kabla- hali yu hai) kwa siku tatu na baadae ateremshwe; na yule ambaye amehukumiwa kuuwawa tu, basi auwawe na kiwiliwili chake wapewe jamaa zake kwa maziko.

Yule anayestahili kukatwa viungo vyake asiuliwe, mkono wake wa kulia ukatwe na sehemu iliyokatwa uchomwe ndani ya mafuta ya moto ili kuzuia kuvuja damu na kuuponesha, na akirejea wizi wake basi akatwe mguu wake wa kushoto. Na akiiba kwa mara ya tatu basi mkono wake wa kushoto ukatwe.

Kutokana na hadithi ya Mtume ﷺ amesema kuhusu mwizi:

*"Akiiba mkateni mkono wake, kisha akiiba mkateni mguu wake, kisha akiiba mkateni mkono wake, kisha akiiba mkateni mguu wake".<sup>297</sup>*

Kwa kuwa Abu Bakr na 'Umar رضي الله عنهما wamefanya hivyo, na wala hapakuwepo aliyetofautiana nao miongoni mwa maswahaba,<sup>298</sup> na njia

---

<sup>297</sup> Sahihi: Imepokewa na Abu Dawud 4410, An-Nasai 8/90 na Al-Baihaqi 8/272 na kusahihishwa na Al-Albani katika Al-Irwaa 2434.

<sup>298</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Abi Shaiba 11/61/2, Al-Baihaqi 8/273 na kusahihishwa na Al-Albani katika Al-Irwaa 2439.

## Al - Kabair

---

ya kuwa kwake kushoto ni maafikiano ya waliokwenda kwenye mguu baada ya kukata mkono, juu ya kuwa huo ni kushoto, na hiyo ndiyo maana ya Kauli Yake Taala:

مَنْ خَلَفَ

*'...kwa kutofautisha...'*

Kwa maelezo kuhusu Kauli Yake Ta'ala:

يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ

*"Kuhamishwa ardhini."*

Ibn Abbaas anasema: 'Ni mtawala kumwaga damu yake -kumuua'. Kwa kusema: Mwenye kukutana naye amuue, hii ni kwa ambaye anaweza hilo. Ama kwa aliyemkamata kwa kumfukuza kwake ni kumtia mahabusu na jela, kwa kuwa atakapofungwa na akazuiwa kuharibu ardhi basi anakuwa amemfukuza kwenye ardhi. Ibn Qutaybah ameandika mashairi kwa baadhi ya wafungwa:

*Tumetoka duniani na sisi ni katika watu wake,  
sisi sio katika walio hai ndani yake wala maiti.  
Anapotujia magereza siku moja kwa haja yoyote, tunastaajabu  
na tunasema; huyu amekuja kutoka duniani.*

Amesema: Kwa kukata tu njia na kutishia njia amefanya kosa kubwa, vipi basi atakapochukua mali, au akajeruhi au akaua, anakuwa amefanya madhambi makubwa mengi achilia mbali kuacha kwao Swala na kutumia wanayoyachukua katika pombe, zina na liwati na mengine yasiokuwa hayo.

Tunamuomba Allah تعالی Atuepushe kutokana na kila balaa, na mitihani, kwani Yeye ni Mpaji, Mkarimu, Msamehevu, Mwingi wa rehma.

## DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI NA TANO

### KIAPO CHA UWONGO

Allah Aliyetukuka Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا أُولَٰئِكَ لَا خَلْقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٧﴾

***“Hakika wanao uza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao thamani ndogo, hao hawatakuwa na sehemu ya kheri yoyote katika Akhera, wala Mwenyezi Mungu hatasema nao wala hatawatazama Siku ya Kiyama, wala hatawatakasana, nao watapata adhabu chungu.” (3:77)***

Wahidi anasema: “Watu wawili walishtakiana kwa Mtume ﷺ kuhusu ardhi. Mtukufu Mtume ﷺ akamtaka mdai kuchukua kiapo (kuthibitisha kuwa anasema ukweli) hapo Allah alimteremshia Mtume ﷺ aya hii akaitoa haki ya mdai kwa yamini, na akathibitisha haki ya mdai kwa haki yake.”<sup>299</sup> Abdullah amesema: Mtume amesema:

« من حلف على يمين وهو فيها فاجر ليقطع بها مال امرئ مسلم لقي الله تعالى وهو عليه غضبان »

*“Mwenye kuapa juu ya yamini na yeye ndani yake ni muovu ili apate kwayo mali ya mtu muislamu atakutana na Allah Taalaa akiwa amemkasirikia”.*

Ash’ath amesema: “Wallaahi aya hii iliteremshwa kuhusu mimi, palikuwa na kipande cha ardhi ambacho myahudi alinikatalia, “Nikamtangulia kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Akaniambia:

---

<sup>299</sup> Imepokewa na Ibn Jariir 7283 kutoka kwa Ash-Shiib.

«أَلَمْ يَبَيِّنْهُ؟»

“Una ushahidi?”

Nilisema: “Sina” Mtukufu Mtume ﷺ akamtaka Yahudi aape, Miye nikasema: “Ewe Mjumbe wa Allah endapo akiapa yamini, atachukuwa mali yangu. Hapo Allah تعالی aliteremsha Aya hii:

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا

**“Hakika ambao wananunua thamani ndogo kwa ahadi ya Allah na yamini zao...”. (3:77)** (Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 2516, 2357 na Muslim 138.)

Yaani: Faida ndogo ya kidunia hali wanaapa juu yake kwa uongo.

أُولَئِكَ لَا خَلَاقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ

**“hao hawatakuwa na sehemu ya kheri yoyote katika Akhera”**

وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ

**“wala Mwenyezi Mungu hatasema nao”.**

Yaani: kwa mazungumzo ya kuwafurahisha.

وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

**“wala hatawatazama”**

Muangalio utakaowafurahisha, yaani muono wa huruma

وَلَا يُزَكِّيهِمْ

**“wala hatawatakasa”**

Wala hatawazidishia kheri wala hatawasifu.

Abdullah bin Mas'uud anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

*“Mwenye kuapa juu ya yamini na yeye ndani yake ni muovu ili akate kwayo mali ya mtu muislamu atakutana na Allah Taalaa akiwa amemkasirikia”.*

Abdullahi akatusomea ukweli wake katika kitabu cha Allah:

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا

***“Hakika ambao wananunua thamani ndogo kwa ahadi ya Allah na yamini zao...” (3:77)***

Hadi mwisho wa aya, ameipokea Bukhari na Muslim<sup>300</sup> Abu Umamah alisema:

« من اقتطع حق امرئ مسلم بيمينه فقد أوجب الله له النار وحرم عليه الجنة »

*“Mwenye kujikatia juu ya haki ya mali ya mtu Muislamu bila haki kwa yamini yake, itakuwa hapana budi kwa Allah kumtia mtu huyo motoni na kumnyima pepo.”*

Mtu mmoja aliuliza: “Hata ikiwa ni kitu kidogo Ewe Mjumbe wa Allah?” Akasema:

« وإن كان قضيباً من أراك »

*“Hata ikiwa ni kipande cha mswaki”.* (Muslim)<sup>301</sup>.

---

<sup>300</sup> Sahihi: Al-Bukhari 7445 na Muslim 138

<sup>301</sup> Imepokea na Muslam 137 na Ahmad 5/260 na Ibn Majah 2324.



## Al - Kabair

---

Hafsi bin Maysarah alisema: "Hadithi hii ni kali mno.' Akasema: Kwani kauli hii haiko katika kitabu cha Allah?

أَوْلَيْكَ لَا خَلْقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ

**"...hao hawatakuwa na sehemu ya kheri yoyote katika Akhera..." (3:77)**

Abu Dhari رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah alisema: "Watu

« ثلاثة لا يكلمهم الله يوم القيامة ولا يذكهم ولهم عذاب أليم »

(wa aina) tatu Allah hatozungumza nao wala hatowatakasa siku ya kiyama na wana adhabu kali". Akaisoma mara tatu.

Abu Dhar رضي الله عنه akasema: "Wametoka kapa na kuhasirika Ewe Mjumbe wa Allah ﷺ, ni nani hao?" Mtume ﷺ akasema:

« المسبل ، والمتان ، والمنفق لسبعته بالخلف الكاذب »

"Mwenye kuburuza nguo kwa majivuno, mwenye kusimbulia, (anayesimulia wema aliyoufanya juu ya watu hadharani), na mwenye kutoa (anayeuzua) bidhaa zake kwa yamini ya uwongo."<sup>302</sup>

Mtukufu Mtume ﷺ alisema:

« الكبائر: الإشراف بالله ، وعقوق الوالدين ، وقتل النفس ، واليمين الغموس »

"Madhambi makubwa; ni kumshirikisha Allah, kuwaasi wazazi, kuuwa nafsi, na yamini ya uwongo." (Bukhari).<sup>303</sup>

---

<sup>302</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/148, 162 na Muslim 106.

<sup>303</sup> Sahihi: Al-Bukhari 6675 kutoka kwa Ibn 'Umar.

Yamini ya uwongo ni mtu kukusudia kudanganya katika kiapo chake, na imeitwa *al-Ghumuusi* kwa kuwa inamzamisha muapaji na madhambi; Na imesemwa, 'inamzamisha motoni.'"

### **KUAPA KWA KISICHOKUWA ALLAH**

Miongoni mwa hayo ni kuapa kwa kisichokuwa Allah Ta'ala kama vile kuapia Nabii 'Wanabi', Ka'abah, Malaika, Mbingu, maji, uhai, na amana, na hayo ndio mabaya zaidi yalio hapa. Roho, kichwa uhai wa sultani, neema ya mfalme, na udongo wa fulani.

Abdullah ibn 'Umar anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah Ta'ala amesema:

« إن الله ينهاكم أن تحلفوا بآبائكم ، فمن حلف فليحلف بالله أو ليصمت »

*"Hakika Allah amekataza kuapa kwa baba zenu, kwa hivyo mwenye kuapa basi aape kwa Allah au anyamaze."*<sup>304</sup>

Katika riwaya nyingine katika Sahihi:

« فمن كان حالفًا فلا يحلف إلا بالله أو ليسكت »

*"Basi mwenye kuapa na aape kwa Allah au anyamaze"*.<sup>305</sup>

'Abdur-Rahmaan bin Samurah anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« لا تحلفوا بالطواغي ولا بآبائكم »

*"Msiape kwa masanamu au kwa baba zenu."* (Muslim)<sup>306</sup>.

---

<sup>304</sup> Sahihi: Al-Bukhari 3836, 6108, 6646 na 6647 na Muslim 1646.

<sup>305</sup> Sahihi: Al-Bukhari 3836, 6108, 6646 na 6647 na Muslim 1646.

<sup>306</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 1648.

## Al- Kabair

---

Buraida رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa, Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« من حلف بالأمانة فليس منا »

*“Mwenye kuapa kwa amana siyo katika sisi.” (Abu Dawud)<sup>307</sup>.*

Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« من حلف فقال: إني بريء من الإسلام ، فإن كان كاذبًا فهو كما قال ، وإن كان صادقًا فلن يرجع إلى الإسلام سالمًا »

*“Mwenye kuapa akasema: mimi niko mbali na Uislamu. Basi akiwa ni muongo basi yeye ni kama alivyosema, na akiwa ni mkweli basi hata rejea kwenye Uislamu salama”.<sup>308</sup>*

Ibn ‘Umar alisikia mtu akisema: “Naapa kwa Ka’abal’, Akamwambia: ‘Usiape kwa asiyekuwa Allah kwani mimi nimemsikia Mtume wa Allah ﷺ anasema:

« من حلف بغير الله فقد كفر أو أشرك »

*“Mwenye kuapa kwa asiyekuwa Allaah hakika amekufuru au ameshirikisha..”*

Hadithi hii ameipokea Tirmidhi na ni Hassan kwa mujibu wa Ibn Hibaan katika sahihi yake na Al-Hakim, na akasema: sahihi katika masharti yao.<sup>309</sup>

Amesema: Baadhi ya wafasiri wamefasiri kauli yake:

---

<sup>307</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/352, Abu Dawud 3253 na kusahihishwa na Shaykh katika sahihi Al-Jami’ 6203.

<sup>308</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/335, 356, An-Nasai 2/140, Ibn Majah 200 na kusahihishwa na Shaykh Albani katika sahihi Al-Jami’ 6421.

<sup>309</sup> Imepokewa na Ahmad 2/125 Abu Dawud 3251, At-Tirmidhi 1535 na kusahihishwa na Shaykh katika sahihi al-Jami’ 2604.

«من حلف بغير الله فقد كفر أو أشرك»

*“Mwenye kuapa kwa asiyekuwa Allah amekufuru au ameshirikisha.”*

Juu ya kutilia uzito kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume wa Allah ﷺ kuwa anasema:

«الرياء شرك»

*“Ria ni shirki”*

Na akasema Mtume ﷺ: “Mwenye kuapa akasema katika yamini yake: Naapa kwa Laata na `Uzza, na aseme: “*Laa ilaaha illa Ilaahu*”<sup>310</sup> (Hakuna mola isipokuwa Allah).

Miongoni mwa maswahaba kuna waliokuwa wageni wa kuapa kabla ya Uislamu wake, pengine huteleza ulimi wake akaapia hivyo, Ndio maana Mtume ﷺ akaamuru kuharakisha kauli yake “*Laa ilaaha illa Ilaahu*” ili afute kwa hili yaliyotanguliwa na ulimi wake. Na taufiqi iko kwa Allah.

\*\*\*

---

<sup>310</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6107 na Muslim 1647.

## DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI NA SITA

### DHULUMA

Maana ya dhuluma ni kuzichukua mali za watu kwa dhuluma, na kuwadhulumu watu kwa kuwapiga na kuwashutumu na kuvuka mipaka na kuwakandamiza wanyonge. Allah Aliyetukuka Anasema:

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَفْلًا عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ ؕ إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ  
الْأَبْصَارُ ﴿٤٤﴾ مُهْطِعِينَ مُقْبِعِي رُءُوسِهِمْ لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ وَأَفْئِدَتُهُمْ هَوَاءٌ ﴿٤٥﴾  
وَأَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ فَيَقُولُ الَّذِينَ ظَلَمُوا رَبَّنَا أَخْرْنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ مِّنْ  
دَعْوَتِكَ وَتَتَّبِعِ الرَّسُولَ ۖ أُولَٰئِكَ تَكُونُوا آفَاسَتُمْ مِّنْ قَبْلُ مَا لَكُمْ مِّنْ زَوَالٍ ﴿٤٦﴾  
وَسَكَنتُمْ فِي مَسْكِينَ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ وَتَبَيَّنَ لَكُمْ كَيْفَ فَعَلْنَا بِهِمْ وَضَرَبْنَا  
لَكُمْ الْأَمْثَالَ ﴿٤٧﴾

**“ Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayo yafanya madhaalimu. Hakika Yeye anawaakhirisha tu mpaka siku yatapo kodoka macho yao. Nao wako mbioni, vichwa juu, na macho hayapepesi, na nyoyo zao tupu. Na waonye watu siku itapo wajia adhabu, na walio dhulumu waseme: Ewe Mola wetu Mlezi! Tuakhirishe muda kidogo tuitikie wito wako na tuwafuate Mitume. Kwani nyinyi si mliapa zamani kwamba hamtaondokewa? Na mkakaa katika maskani zile zile za walio zidhulumu nafsi zao. Na ikakudhihirikieni jinsi Tulivyo watendea. Nasi Tukakupigieni mifano mingi. ” (Ibrahim, 14:42-45)**

Akasema tena Allah:

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ ﴿٤٨﴾

**“Na wanao dhulumu watakuja jua mgeuko gani watakao geuka.” (26:227)**

Na Akasema tena Allah:

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ

**“Bali lawama ipo kwa wale wanao wadhulumu watu...” (42:42)**

Mjumbe wa Allah ﷻ Amesema:

« إن الله ليملئ للظالم حتى إذا أخذه لم يفلته . »

**“Hakika Allah humpa muda dhalimu mpaka atakapomkamata hamponyoki..”**

Kisha Mtume Mtukufu ﷻ akasoma:

وَكَذَلِكَ أَخْذُ رَبِّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخْذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿١٠٢﴾

**“Na ndio kama hivyo ndivyo inavyo kuwa Mola wako Mlezi anapo ikamata miji inapo kuwa imedhulumu. Hakika mkamato wake ni mchungu na mkali.”(11:102)<sup>311</sup>**

Mtukufu Mtume ﷻ amesema:

**“Ambae kwake kuna dhuluma ya nduguye (Muislamu) katika heshima au kitu, basi na ajifungue leo, kabla ya kuwa hakuna dinari wala dirhamu, endapo anayo matendo mema yatachukuliwa kwake kwa kiasi cha dhuluma yake, na kama hana mema basi huchukuliwa maovu ya wengine na hubebeshwa yeye” .<sup>312</sup>**

---

<sup>311</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 4686, Muslim 2583 kutoka kwa Abu Musa Al-Asha'ariy.

<sup>312</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 2449, Ahmad 2/435, 506 kutoka kwa Ibn 'Umar.

## Al- Kabair

---

Mtukufu Mtume ﷺ alisema akisimulia kuhusu Mola Wake:

*“Enyi watumishi wangu Mimi Nimeharamisha dhulma juu ya Nafsi Yangu, na Nikaifanya baina yenu kuwa imeharamishwa, kwa hivyo msidhulumiane.”<sup>313</sup>*

Mjumbe wa Allah ﷻ aliuliza:

*“Mnamjua aliyefilisika?”*

Wasikilizaji masahaba wakajibu: “Ewe Mjumbe wa Allah aliyefilisika kati yetu ni yule ambaye hana pesa wala mali.”

Mtukufu Mtume ﷺ akasema:

*“Hakika muflisi wa uma wangu ni ambaye atakuja siku ya kiyama na Swala zake, Funga zake, Zaka na Hija; na atakuja amemshutumu huyu, amechukua mali ya huyu, amefukua heshima ya huyu, na amempiga huyu, na kamwaga damu ya huyu, Kwa hiyo itachukuliwa kwa ajili ya huyu kutoka kwenye mema yake, na huyu kutoka kwenye mema yake. Na endapo matendo yake mazuri yakiisha kabla hajamaliza anayodaiwa, yatachukuliwa maovu yao na kutupiwa yeye kisha atatupwa motoni”.*

Hadithi zote hizi zimo katika Sahihi, na imetangulia hadithi:<sup>314</sup>

*“Hakika watu wanazama katika mali ya Allah bila ya haki, hakika wao wana adhabu ya moto siku ya kiama”.*<sup>315</sup>

Imetangulia kauli yake kwa Mu’adh alipomtuma Yemen:

---

<sup>313</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 2577, At-Tirmidhi 2495 na Ibn Majah 4257.

<sup>314</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/303, 334 Muslim 2581, At-Tirmidhi 2418 kutoka kwa Abu Huraira.

<sup>315</sup> Maelezo yake yametangulia.

## Al - Kabair

---

*“Ogopa dua ya aliye dhulumiwa, kwani hakuna pazia baina yake (hiyo dua) na baina ya Allah” (Bukhari).<sup>316</sup>*

Na katika sahihi:

« من ظلم قيد شبر من الأرض طوقه من سبع أرضين يوم القيامة »

*“Mwenye kudhulumu kadiri ya shubiri ya ardhi itamfunga shingoni mwake baina ya ardhi saba siku ya kiama.”<sup>317</sup>*

Katika baadhi ya vitabu Allah Anasema:

« اشتد غضبي على من ظلم من لم يجد له ناصرا غيري »

*“Ghadhabu yangu imekuwa kali juu ya mwenye kumdhulumu asiye pata wa kumunusuru isipokuwa Mimi”.*

Baadhi yao wameimba mashairi haya:

*Usidhulumu kamwe pindi uwapo mwenye uwezo,  
Kwani dhuluma inarejea mwisho wake kwenye majuto.  
Macho yako yanalala na mwenye kudhulumiwa amezinduka.  
Anakuapiza wewe na macho ya Allah hayalali.*

Baadhi ya salafi walikuwa wanasema: “Usidhulumu wanyonge kwani utakuwa miongoni mwa washari wenye nguvu”.

Abu Hurairah رضي الله عنه akasema: Hakika ng'ombe atakufa katika mahali pake akiwa amekonda kwa dhuluma ya mwenye kudhulumu.

Kukasemwa: Imeandikwa kwenye Taurati atanadi mwenye kunadi nyuma ya daraja (yaani *Swirati*) “Enyi kongamano la majabari waasi, enyi

---

<sup>316</sup> Maelezo yake yametangulia.

<sup>317</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/188, 189, na Al-Bukhari 2452 na Muslim 1610 kutoka kwa Sa'id bin Zaid.



## Al- Kabair

---

kongamano la wenye kustarehe waovu. Hakika Allah Ameapa kwa Utukufu Wake na Utisho Wake kutovuka daraja hili dhalimu yoyote leo”.

Jabir<sup>رضي الله عنه</sup> anatoa taarifa wakati wahajiri wa Uhabeshi walipofika Makka katika mwaka wa *Fat-hu* na kukutana na Mtume ﷺ, Mtume aliwauliza:

«ألا تخبروني بأعجب ما رأيتم بأرض الحبشة؟»

*“Kwanini hamniambii kuhusu kilichowavutieni zaidi mlichokiona katika ardhi ya habasha.”*

Vijana waliokuwemo miongoni mwao wakajibu: “Ewe mjumbe wa Allah wakati fulani tulikuwa tumekaa na tukamuona mwanamke mzee akitembea na mtungi wa maji kichwani mwake, alipita karibu na kijana mmoja ambaye aliweka mikono yake baina ya mabega yake, na akamsukuma kwa nguvu na yule kizee akaanguka na kuvunja ule mtungi wa maji. Tena kizee huyo alisimama na akamtazama kijana huyo na kumwambia: “Wewe kijana muovu, utaona Siku Allah تعالى atakapo weka Kiti cha Enzi na kuwakusanya wa kwanza na wa mwisho, na mikono na miguu ikasema juu ya waliokuwa wakiyachuma. Utajua siku jambo langu baina yako na mimi mbele yake kesho”.

Mjumbe wa Allah ﷺ akasema:

«صدقت كيف يقدر الله قوماً لا يؤخذ من شديدهم لضعيفهم»

*“Amesema kweli, vipi Allah atawatukuza watu ambao (haki) haichukuliwi kutoka kwa wenye nguvu wao kwa ajili ya wanyonge wao”.*<sup>318</sup>

Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

---

<sup>318</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Majah 4010, Ibn Hibaan 5058 na kusahihishwa na Albani katika Mukhtasar Al-'Uluwu 46/59 na sahihi Al-Jami' 4597 na 4598.

« خمسة غضب الله عليهم إن شاء أمضى غضبه عليهم في الدنيا وإلا أمر بهم في الآخرة إلى النار : أمير قوم يأخذ حقه من رعيته ولا ينصفهم من نفسه ولا يدفع الظلم عنهم وزعيم قوم يطيعونه ولا يساوي بين القوي والضعيف ويتكلم بالهوى ، ورجل لا يأمر أهله وولده بطاعة الله ولا يعلمهم أمر دينهم ، ورجل استأجر أجيراً فاستوفى منه العمل ولم يوفه أجرته ، ورجل ظلم امرأة صداقها »

*“(Watu) watano Allah Amewakasirikia Akitaka Atapitisha Ghababu Yake juu yao hapa duniani, la sivyo Ataamrisha watiwe motoni akhera: mtawala wa watu huchukua haki yake kwa raia wake wala hawafanyii sawasawa ndani ya nafsi yake, wala haondoi dhuluma kwao. Na kiongozi wa watu ambae wanamtii, wala hafanyi sawa kati ya mwenye nguvu na dhaifu, na husema kwa matamano (yake), na Mtu ambaye haamuru mkewe na watoto wake kumtii Allah, na wala hawafundishi mambo ya dini yao, mtu anaajiri mfanyakazi wala hamlipi ujira wake, na mtu amemdhulumu mwanamke mahari yake”.*<sup>319</sup>

‘Abdullah bin Salaam anasema: wakati Allah Aliyetukuka Alipoumba binaadamu walisimama kwa miguu yao wakainua nyuso zao mbinguni na kuuliza: “Ewe Mola uko pamoja na nani Wewe?” Akajibu: “Nipo na wale wanaodhulumiwa hadi wapewe haki zao.”

Wahb bin Munabbih alihadithia Hadithi ifuatayo: “Mfalme jabari miongoni mwa majabari alijenga kasiri kisha akaliimarisha, akaja maskini kizee wa kike alijenga kibanda chake kidogo upande mmoja wa kasiri hilo ili ajihifadhi.

Siku moja yule mfalme dhalimu alitembelea na kulizunguka kasiri lake hilo, akaona kibanda akauliza: ‘Ni cha nani hiki?’ Akaambiwa ni cha bibi

---

<sup>319</sup> Az-Zawaajir 2/122 na kupokea kwa tamshi imeelezwa (Ruwiya) ambacho kinathibitisha udhaifu wake.

## Al- Kabair

---

kizee mmoja fukara anajihifadhia hapo, akaamuru kivunjwe na kikavunjwa. Bibi kizee akaja akauliza: 'Ni nani amekivunja?', Akajibiwa: 'Mfalme amekiona akaamuru kivunjwe'.

Bibi kizee huyo akainua uso wake mbinguni akasema: "Ewe bwana, endapo mie sijakuwepo Wewe ulikuwa wapi?" Basi Allah akamtuma Sayyidina Jibril kupindua kasiri hiyo juu chini."

Imetolewa taarifa kuwa Khalid bin Barmak (Wazir Mkuu) wa Khalifa Harun Rashid na mwanawe wa kiume walipofungwa, mwanawe alisema: "Baba baada ya utukufu, tumeishia kwenye pingu na jela?, Khalid alimjibu: "Ewe mwanangu dua ya mwenye kudhulumiwa, hupanda juu usiku sisi tulikuwa tumeghafilika nayo, lakini Allah hakughafilika nayo."

Yaziid bin Hakiim alikuwa anasema: "Sikumuogopa yoyote kama uoga wangu kwa mtu niliyemdhulumu". Nami najua hana wa kumnusuru yeye isipokuwa ni Allaah anasema: "*Hasbiya LLahu Wallahi* baina yangu na yako"

Abu Umamah alisema; "Siku ya kiyama, dhalimu atakutana na aliyemdhulumu kwenye daraja la Jahannam, atamjua na alichomdhulumu, waliodhulumiwa hawatawaacha waliowadhulumu mpaka wawanyang'anye mema yalio mikononi mwao na endapo hawana mema watabebeshwa maovu yao mfano wa yale waliowadhulumu, hadi wafike tabaka la chini kabisa la moto."<sup>320</sup>

'Abdullah bin Unais رَضِيَ اللهُ عَنْهُ anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*"Watu watafufuliwa Siku ya kiyama wakiwa pekupeku, uchi, wenye magovi, wao watasikia sauti ambayo itasikiwa mbali na karibu ikisema:*

---

<sup>320</sup> Hassan: Imepokewa na At-Tabarani 5976 na Haithami amesema katika Majma' Az-Zawaid 10/354 watu wake ni waaminifu nayo ni Hassan in sha Allah.

*“Mimi ni Mfalme Mlipaji, haifai kwa yoyote miongoni mwa watu wa peponi kuingia peponi, na wala wakazi wa motoni kuingia motoni, madamu kwake kuna dhuluma hata kupiga kofi na zaidi, Wala mola wako hamdhulumu yoyote”.*

Tukasema: “Ewe Mtume wa Allah basi kwa vipi na sisi tunakuja pekupeku na magovi”. Akasema:

*“Kwa mema na mabaya na Mola Wako hamdhulumu yoyote.”<sup>321</sup>*

Mtukufu Mtume ﷺ amesema:

*“Aliyepiga fimbo kwa dhuluma atalipiziwa siku ya kiama”.<sup>322</sup>*

## HADITHI

Inahadithiwa kuwa mfalme Kaisari alimteua mwalimu kwa ajili ya kumsomesha mwanawe, mrithi wa kiti cha ufalme. Mwalimu alimfundisha tabia njema na kila fani ya elimu, mwana mfalme akawa amesoma vizuri. Siku moja mwalimu bila ya sababu wala kosa alimpiga mwana mfalme, kijana akamuekea kinyongo mwalimu wake kutokana na hilo mpaka alipokuja kuwa mkubwa.

Baada ya kifo cha baba yake, mwana wa mfalme akawa mfalme, alimwita aliyekuwa mwalimu wake na kumkumbusha siku fulani ulinichapa bila sababu. Mwalimu akajibu: “Sikiliza ewe mfalme, baada ya wewe kukhitimu niliyokusomesha elimu na adabu njema mie nilijua kuwa iko siku moja baada ya kifo cha baba yako utatawala kiti cha baba yako, nilitaka kukufunza maumivu ya kupigwa na mateso ya kutendewa yasio

---

<sup>321</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 3/495, Al-Bukhari katika Al-Adab al-Mufrad 185 na kusahihishwa na Albani katika As-Swahiha 5351 na Al-Adab al-Mufrad 137.

<sup>322</sup> Sahihi: Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Awsat 1468, Al-Bukhari katika Al-Adab al-Mufrad 185 na kusahihishwa na Albani katika As-Swahiha 5351 na Al-Adab Al-Mufrad 137.

## Al- Kabair

---

ya haki, ili usimdhulumu yoyote. Mwana mfalme akasema: 'Allah akulipe kheri' Kisha akaamuru apewe zawadi.

Miongoni mwa dhuluma ni kuchukua mali ya yatima. Na imetangulia hadithi ya Mu`adh wakati Mtume ﷺ alipomwambia:

*"Na ogopa dua ya mwenye kudhulumiwa kwani hakuna kizuizi baina yake na baina ya Allah"*<sup>323</sup>

Katika riwaya nyingine:

*"Kuwa dua ya mwenye kudhulumiwa inainuliwa juu ya mawingu na mola anasema Tabaaraka wa Taalaa: Naapa kwa Utukufu Wangu na Uisho Wangu nitakunusuru japo baada ya muda"*.<sup>324</sup>

Baadhi ya malenga wameimba mashairi haya:

*Ogopa dua ya mwenye kudhulumiwa kwa dua yake,  
Inainuliwa juu ya mawingu kisha inajibiwa.  
Ogopa dua ya ambae hakuna baina ya dua yake,  
Na baina ya mola wa walimwengu kizuizi.  
Wala usidhani kuwa Allah ni mwenye kuitupa  
Wala kuwa yeye maneno yanafichika kwake  
Imeswihi kuwa Allah amesema: Naapa kwa utukufu wangu,  
Nitamnusuru mdhulumiwa hali anapata thawabu.  
Basi mwenye kutosadiki hadithi hiyo bila shaka yeye  
Ni mjinga la sivyo akili yake imeharibika.*

---

<sup>323</sup> Sahihi: Maelezo yake yametangulia.

<sup>324</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/305, At-Tirmidhi 3598, Ibn Majah 1752 na kusahihisha na Albani katika As-Silsilah 1211.

## FASILI

Miongoni mwa dhuluma kubwa ni kuchelewesha kulipa pamoja na uwezo wa kulipa. Kwani imethibiti katika sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

مَطْلُ الْغَنِيِّ ظَلَمٌ

*"Tajiri kuchelewesha kulipa deni ni dhuluma".<sup>325</sup>*

Na katika riwaya nyingine:

*"Mwenye kukutwa na dhuluma ni halali kwangu cheo chake na kumwadhibu."*

Miongoni mwa dhuluma ni kumdhulumu mwanamke kutompa mwanamke mahari yake, matumizi yake na mavazi yake.

Ibn Masu'ud amesema: "Siku ya kiyama, utachukuliwa mkono wa mjakazi au mtumwa, na mwito utanadiwa juu ya vichwa vya watu, mtu huyo ni fulani bin fulani yeyote anayemdai aje achukue haki yake. Kwa hiyo mwanamke atafurahi kuwa na haki juu ya baba yake, kaka yake, au mumewe, kisha akasoma:

إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَذَكَرُوا اللَّهَ كَثِيرًا وَانْتَصَرُوا مِنْ بَعْدِ مَا ظَلَمُوا<sup>4</sup>  
وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ ﴿١٠١﴾

***"...Hakutakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana." (23:101)***

Aliendelea kusema Allah atamsamehe amtakaye madhambi yake, lakini Yeye تعالٰى hatosamehe haki za watu. Kwa hivyo, mtu atasimamishwa mbele

---

<sup>325</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/279 na Al-Bukhari 2287 na Muslim 1564.

## Al- Kabair

---

ya watu, na Allah Aliyetukuka atawaambia wadai: “Chukueni haki zenu.’ Allah تعالیٰ Aliyetukuka atawaamuru Malaika: “Chukueni mema yake, na wapeni wanaomdai kwa kadiri ya madai yao. Endapo akiwa ni walii (rafiki) wa Allah basi Allah Atamuongezea chembe cha matendo ya mema hadi imuingize peponi. Lakini akiwa ni mtu muovu, na hakuna kitu kilichobaki cha matendo yake mema, malaika watasema:

“Ewe bwana wetu, matendo yake mema yote yamekwisha gawiwa na bado madai juu yake yamebaki. Allah atawaambia malaika: ‘Basi yaongezeeni juu ya maovu yake’. Kisha atavurumishwa motoni”.<sup>326</sup>

Hadithi hii imethibitishwa na kauli iliyotangulia kutajwa ya Mtume ﷺ:

*“Je mnajua muflisi? Akataja kuwa muflisi wa uma wangu, ni yule ambaye atakuja siku ya kiyama na Swala zake, Funga zake, Zaka na Hija zake, atakuja amemtukana huyu, na kumpiga huyu, na kuchukua mali ya huyu, kwa hiyo mema yake yatachukuliwa kwa ajili ya huyu, na huyu, endapo matendo yake mema yamemalizika kabla ya kulipa anayodaiwa, yatachukuliwa maovu yao na kutupiwa yeye kisha atatupwa motoni”.<sup>327</sup>*

## FASILI

Na miongoni mwa dhulma ni mtu kumuajiri mtu kisha asimpe ujira wa kazi yake. Kwa kilichothibiti katika Hadithi ya Mtume ﷺ katika sahihi Al-Bukhari kuwa Mtume ﷺ amesema:

*“ Allah anasema kuwa: Watu watatu Mimi ni mgomvi wao siku ya kiama na yule Nitakayekuwa mgomvi wake Nitagombana naye: Mtu aliyepewa kisha hakutekeleza ahadi, mtu aliyemuza muungwana*

---

<sup>326</sup> Imepokewa na Ibn Jarir 18/42 na Abu Nu’aym 4/202

<sup>327</sup> Maelezo yake yametangulia.

## Al - Kabair

---

*na akala thamani yake, na mtu aliyemkodi mtu amfanyie kazi na akamaliza kazi yake na asimpe ujira wake.*"<sup>328</sup>

Vivyo hivyo akidhulumiwa myahudi au mnasara au kama atakuwa amempa kazi zaidi ya uwezo wake au amechukua kitu kwake bila ridhaa yake huyo anaingia katika Kauli ya Allaah: "Hatoniona" au kusema: "Nitagombana naye" siku ya kiama. Mfano wake ni amesema: Mwenye kuapia dini yake na huku ni muongo muovu kama ilivyothibiti katika Al-Bukhari na Muslim kuwa Mtume ﷺ amesema:

وقال [رسول الله] <sup>(٢)</sup> ﷺ: «من اقتطعَ حقَّ امرئٍ مسلمٍ يمينه فقد أوجب الله له النارَ»، قيل: يا رسولَ الله! وإن كان شيئاً يسيراً؟ قال: «وإن كان قضييماً من أراك» <sup>(٣)</sup> رواه مسلم.

*"Mwenye kukata haki ya mtu Muislamu kwa yamini yake basi Allah amepasa juu yake moto na kumharamishia pepo."*

Ikasemwa: Ewe Mtume wa Allah hata kama kitu chenyewe ni kidogo? Mtume ﷺ akasema:

*'Hata kama ni kipande cha mswaki.'"<sup>329</sup>  
Kisasi ni pungufu kesho utakapotekeleza,  
Kitakachochumwa na mkono wako kwa uadilifu,  
Katika kisimamo chetu baina yatu isipokuwa mwenye kujijenga,  
Au mwenye kutoa au mwenye kushawishi kichwa,  
Viungo vyao humo ni mashahidi ni jela yao,  
Ni moto na hakimu wao ni mwenye nguvu kubwa,  
Haki zikichelewa leo kwa tajiri  
Kesho zitatekelezwa pamoja na ufilisi.*

---

<sup>328</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 2227 na 2270

<sup>329</sup> Maelezo yake yametangulia.



## Al - Kabair

---

Na imehadithiwa kuwa haichukizi kwa mja kulazimishwa siku ya kiama amuone anayemjua akihofia atamdai alichomdhulumu huku duniani kama alivyosema Mtume ﷺ:

*"Mtarejesha haki za watu kwa wenyewe siku ya kiama kiasi cha mbuzi asiye na pembe atataka haki yake kwa mbuzi mwenye mapembe."*<sup>330</sup>

Na amesema tena Mtume ﷺ:

*"Mwenye kuwa na dhuluma kwa nduguye ya cheo au kitu aifungulie leo kabla haijawa dinari au dirham. Akiwa na amali njema, itachukuliwa kwa kadiri ya dhuluma yake. Asipokuwa na mema yatachukuliwa maovu ya mwenzake na kubebeshwa yeye, halafu atatupiwa motoni."*

Abdullah bin Abu Dunya amesimulia na ametegemeza isnadi yake kwa Abu Ayyub Ansari kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*"Wa mwanzo watakaohasimiana siku ya kiama: ni mume na mkewe; Wallaahi ulimi wake hautasema, lakini mikono na miguu itashuhudia dhidi ya mume kwa alivyokuwa akimfanyia mkewe miongoni mwa kheri au shari, kisha ataitwa mwanamume kwa mfanyakazi wake mfano huo, hakutachukuliwa kwao pesa wala hazina. Lakini mema ya huyu dhalimu kupewa mdhulumiwa, kisha kutaletwa majabari katika pingu za chuma na kutasemwa: waswageni motoni".*<sup>331</sup>

Qadhi Shuraih alisema: "Madhalimu watajua haki ya waliowadhulumu, kuwa dhalimu anangojea adhabu na aliyedhulumiwa anangojea nusura na thawabu".

---

<sup>330</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 2582 na At-Tirmidhi 2420.

<sup>331</sup> Dhaifu mno: Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Kabir 3969 na ipo ndani ya Adh-Dhahabi katika Al-Mizani hadithi hii akasema ni batili.

## Al - Kabair

---

Imepokewa kuwa Allah anapompendea mja wake kheri anampelekea dhalimu.

Tawuus Yamani aliingia kwa Khalifa Hisham bin 'Abdul-Malik na akamwambia: "Muogope Allah تعالی siku ya wito (kiama)." Hishaam alimuuliza; 'Nini maana ya siku ya wito" Tawuus akasema:

Allah Aliyetukuka Anasema:

فَأَذِّنْ مُؤَدِّنٌ بَيْنَهُمْ أَنْ لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿٧٤﴾

**"...Ndiyo! Basi mtangazaji atawatangazia: Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate walio dhulumu" (7:44)**

Hishaam akazimia Tawuus akasema: "Huku ni kudhalilisha kwa sifa tu. Basi vipi kudhalilisha kunakoonekana".

Ewe mwenye kuridhia jina la dhalimu! Hivi una dhuluma ngapi?. Jela ni Jahannam na haki ndio hakimu.

## FASILI

Katika kutahadharisha dhidi ya kuingia katika dhuluma, kuchanganyika nao na kusaidiana nao.

Allah Aliyetukuka Anasema:

وَلَا تَرْكَبُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ

**"Wala msiwategemea wanao dhulumu, usije ukakuguseni Moto". (11:113)**

Kutegemea huku kunamaanisha kupenda na kukipondokea zaidi, amesema Ibn 'Abass: 'Yaani usipondokee sana kwenye mahaba na ulaini

## Al - Kabair

---

wa maneno.' Sudi na Ibn Zaid wamesema: "Msipambiane na madhalimu".  
Ikrimah amesema: "Hilo ni kuwatii na kuwapenda" na Abul `Aaliyaa  
amesema: "Msiridhie matendo yao".

فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ

**"...usije ukakuguseni Moto".**

Kwa hiyo mtapatwa na joto lake

وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ

**"Na nyinyi hamtakuwa na marafiki wowote zaidi ya Allah".**

Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: 'Nyinyi hamna kizuizi chochote, dhidi ya  
adhabu ya Allah',

ثُمَّ لَا تَنْصُرُونَ

**"Kisha hamtanusuriwa".**

Hamzuii adhabu ya Allah, Allah Amesema:

\* أَحْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ

**"Wakusanyeni waliodhulumu na wenza wao...". (37:22)**

Yaani na mfano wao na wafuasi wao.

Ibn Masuud رضي الله عنهما anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

« سيكون أمراء يغشاهم غواش أو حواش من الناس يظلمون ويكذبون ، فمن  
دخل عليهم وصدقهم بكذبهم وأعانهم على ظلمهم فليس مني ولست منه ،  
ومن لم يدخل عليهم ولم يعينهم على ظلمهم فهو مني وأنا منه »

## Al - Kabair

---

*“Kutakuwa na watawala watakaowakandamiza watu na kusema uongo na watazungukwa na watu wa hali ya chini, yoyote atayekuwa nao na akashuhudia uongo wao, na akawasaidia wao katika dhuluma yao, basi hayuko nami, wala siko nae, na asiyeingia kwao na hakuwasaidia juu ya dhuluma yao, basi huyo ni katika mimi na mimi ni katika yeye huyo ni wangu nami ni wake”.*<sup>332</sup>

Imepokewa tena kutoka kwake (Ibn Masuud) kuwa Mtume ﷺ, amesema:

« من أعان ظالماً سلط »

*“Mwenye kumsaidia dhalimu naye atasalitiwa”.*<sup>333</sup>

Said bin Musayyib alisema: “Daima msifurahishwe na wenye kusaidia wenye kudhulumu isipokuwa kwa kuchukua nyoyoni mwenu, ili matendo yenu mema yasije yakaporomoka”.

Makhuul Dimishqi alisema: ‘Siku ya kiyama mwitaji ataita wako wapi madhalimu na wasaidizi wao?’, Hatabakia yeyote aliyewasaidia japo wino tu, au alijaza chupa zao wino, au alichonga kalamu zao au aliwafanyia jambo lolote kubwa kushinda hilo, huyo atakusanywa pamoja nao. Akauliza: ‘Mimi nilishona nguo ya sultani, Je na mimi ni katika wasaidizi wa dhulma?’ Sufyan alimjibu: “Wewe ni katika madhalimu hasa, wasaidizi wa madhalimu ni wale wanaokuuzia sindano na nyuzi”. Mtume ﷺ amesema:

« أول من يدخل النار يوم القيامة السواطون الذين يكون معهم الأسواط  
يضربون بها الناس بين يدي الظلمة »

---

<sup>332</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 3/24, Ibn Hibaan 286 na At-Tirmidhi 614 kwa tamshi linalokaribiana na imesahihishwa na Al-Albaan katika riwaya ya Tirmidhi katika At-Ta’aliq Ar-Raghiib 3/15, 150.

<sup>333</sup> Hadithi maudhui imepokewa na Abu Hafsi Kashafi katika sehemu ya Mazungumzo yake 141-142 na Shaikh Al-Albani ameiweka katika silsila Adh-Dhwa’ifa 1937.

## Al- Kabair

---

*“Siku ya kiyama watu wa kwanza watakaoingia motoni, wachapaji wenye mijeledi ambao wanawachapa nayo watu mbele ya madhalimu”.*<sup>334</sup>

Ibn ‘Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا alisema: “Wasaidizi wa madhalimu na polisi ni mbwa wa motoni siku ya kiyama”.<sup>335</sup>

Imepokewa kuwa Allah alimfunulia Musa عَلَيْهِ السَّلَامُ kuwa: “Waamuru Banii Israili kuwa wasisome utajo wangu, kwani mimi ninamkumbuka aliyenitaja, na kuwa utajo wangu kwao ni kuwalaani wao”, na katika riwaya: “Kwani mimi ninamtaja aliyenitaja miongoni mwao kwa laana”. Mtukufu Mtume ﷺ amesema:

« لا يقف أحدكم في موقف يقتل فيه رجل ظلما ، فإن اللعنة تنزل على من حضر ذلك المكان إذا لم يدفعوا عنه »

*“Asisimame yeyote kati yenu mahali ambapo panapouawa mtu kwa dhuluma, kwani laana inashuka juu ya aliyehudhuria mahali hapo na bila kumtetea”.*<sup>336</sup>

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« أتني رجل في قبره فقيل له : إنا ضاربوك مائة ضربة لم يزل يستشفع إليهم حتى صاروا إلى ضربة واحدة فضربوه ، فالتهب القبر عليه نارا فقال : لم ضربتموني هذه الضربة ؟ فقالوا : إنك صليت صلاة بغير طهور ومررت برجل مظلوم فلم تنصره »

---

<sup>334</sup> Dhaifu: Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Awsat 6635, Ibn ‘Adiy 7/267 na akasema: Hadithi isiyohifadhiwa.

<sup>335</sup> Dhaifu: Imepokewa na Abu Nu’aim katika Al-Hilya 4/21 imedhoofisha na Albani katika Dhaifu Al-Jami’ 6341 na A-Dha’ifa 3472.

<sup>336</sup> Dhaifu: Imepokewa na At-Tabarani 11675, Al-Kabir na akasema Al-Haithami 6/282 na kuna Asad bin ‘Atwaa amesema kuwa Al-Azdiy hajulikani na Mandal alimuona kuwa ni mwaminifu na Abu Hatim alimuona hivyo hivyo na Ahmad ameiona kuwa ni dhaifu na wengineo na watu waliobakia ni waaminifu.

## Al - Kabair

---

“Mtu mmoja alijiwa kaburini kwake akaambiwa, (na malaika wa kisasi) sisi tutakupiga mijeledi mia moja, akawa anaomba hadi ukabaki mjeledi mmoja. Basi wakampiga nao, kaburi lake likalipuka moto.’ Akauliza: ‘Kwanini mmenipiga pigo hili?’ Wakamjibu: ‘Wewe uliswali bila ya tohara, na ulipita karibu na mtu anayedhulumiwa na wewe hukumnusuru”.<sup>337</sup>

Hii ni hali ya mtu aliyeshindwa kumnusuru mwenye kudhulumiwa pamoja na kuweza, basi vipi hali ya mwenye kudhulumu?’ Imethibiti katika sahihi mbili kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« انصر أخاك ظالماً أو مظلوماً »

“Mnusuru nduguyo dhalimu na mwenye kudhulumiwa”

Kukaulizwa: “Ewe Mtume wa Allah! Nitamnusuru akiwa ni mwenye kudhulumiwa, vipi nitamnusuru akiwa ni dhalimu?” akasema:

« تمنعه من الظلم فإن ذلك نصره »

“Unamzuia kudhulumu kwani hiyo ni nusura yake”.<sup>338</sup>

Kilielezwa kisa na mmoja wa wajuzi: Nilimuota mtu mmoja miongoni mwa watumishi wa madhalimu baada ya kifo chake kwa muda akiwa katika hali mbaya. Nikamuuliza: ‘Umefikia wapi?’ Akajibu: ‘Katika adhabu ya Allah.’ Nikamuuliza: ‘Vipi hali ya madhalimu?’ Akajibu: ‘Ni hali mbaya, hakupata kuisikia.’

الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيُّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ ﴿٢٢٧﴾

“Na wanao dhulumu watakuja jua mgeuko gani watakao geuka.” (26:227).

---

<sup>337</sup> Dhaifu: Imepokewa na At-Tabarani 12/339 na kudhoofishwa na Albani katika dhaifu Al-Jami’ 257.

<sup>338</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 2443, 2444, Ahmad 3/92 na At-Tirmidhi 2282 kutoka kwa Anas na Muslim kutoka kwa Jabir 2584.

## KISA

Mtu mmoja alihadithia kisa hicho: "Nilimuota mtu ambaye mkono wake mmoja umekatwa begani mwake alikuwa anasema: "Mwenye kuniona mimi, basi asimdhulumu yeyote."

Nilimsogelea huyo mtu na kumuuliza: "Ndugu yangu ni nini kisa chako? Yeye alisema: "Ewe ndugu yangu kisa changu ni cha ajabu, miye nilikuwa msaidizi wa madhalimu siku moja nilimuona mvuvi ambaye alikuwa amevua samaki mkubwa, niliwaza moyoni, nilitamani kumpata samaki huyo, na mie nikamwambia: "Nipe huyo samaki." Yeye akaniambia, 'kwanini nikupe wewe? Miye ninauza ili nipate chakula cha watoto wangu', Hapo nilimpiga kwa nguvu nikachukua samaki kutoka kwake kwa nguvu na kwenda zangu. Wakati ninakwenda zangu, samaki akaning`ata kidole gumba changu, mng`ato mkali, nilipokuja naye nyumbani, nikamdondosha kutoka mkononi mwangu akanigonga kidole gumba changu, nikapata maumivu makali, sikuweza kulala usiku kucha kwa maumivu niliyo kuwa nayo. Kitu cha mwanzo asubuhi nilimwendea daktari, nikamueleza maumivu nilionayo. Daktari akaniambia jeraha lilifanya sumu na kuoza lazima nikate kidole, akakata kidole, usiku kucha sikuweza kulala wala kutulia. Siku ya pili yake nilirudi kwa daktari akanieleza kuwa: nakata kiganja chako, akakikata, maumivu yakaenea hadi kwenye mkono, sikuweza kutulia, nikawa naomboleza kwa maumivu makali. Nikaambiwa mkono itabidi ukatwe kwenye kisukusuku ukakatwa, maumivu yakaenea hadi kwenye paja la mkono kuliko maumivu ya mwanzo. Nikaambiwa; nakata mkono wako kwenye bega lako, la sivyo utaenea kwenye mwili wako wote, basi ukakatwa.

Tena watu wakaniuliza sababu ya maumivu yangu, nikawahadithia kisa cha samaki. Wao wakaninasihi nimtafute yule mvuvi haraka na nimuombe msamaha kabla sumu haijatambaa mwilini mzima. Nikawa siachi kumtafuta mjini mvuvi hadi nikampata, nikamuangukia miguuni na huku nikimbusu miguu yake, nikilia kwa uchungu na nikamwambia "Ewe bwana tafadhali kwa ajili ya Allah nisamehe." Akaniuliza, 'Wewe

## Al - Kabair

---

nani?’ Nikamwambia, ‘Miye ndiye nilimchukua samaki wako kwa dhuluma”. Na nikamkumbusha kile kisa. Nikamuonesha mkono, akalia baada ya kuona. Akaniambia ndugu yangu, miye nimekusamehe nimekufungulia kwako kwa jinsi nilivyokuona na balaa hili.

Nikamuuliza, ‘Ewe bwana wangu, nakuomba kwa Allah, niambie uliniapiza kwa Allah nilipomchukua (samaki wako)?’ Akanijibu, ‘Naam nilisema: Ewe Allah huyu amenizidi kwa nguvu zake, na akachukua ulichoniruzuku kwa dhuluma. Basi nionyeshe uwezo wako kwake.’ Nikasema: ‘Ewe bwana wangu hakika Allah amekuonyesha Nguvu Zake kwangu, na mimi ninatubia kwa Allah, yale niliyokuwa nikiyafanya ya kusaidia madhalimu, wala sitarudi kusimama kwenye mlango wowote kwa ajili yao, wala sitakuwa msaidizi wao muda wa kuishi kwangu. Inshaa Allaah.” Wabillaahi Ttawfiiq.

\*\*\*



DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI NA SABA

WATOZA KODI

Allah Aliyetukuka Anasema:

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ  
أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٢﴾

***“Bali lawama ipo kwa wale wanao wadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Hao watapata adhabu iliyo chungu” (42:42)***

Al-Makaas ‘mtoza ushuru’ ni miongoni mwa madhalimu wasaidizi wakubwa, bali mwenyewe ni dhalimu. Anachukua kisichostahiki na anawapa wasiostahiki.

Kwa ajili hii Mtume ﷺ amesema: “Mkusanyaji kodi hataingia peponi”.

Na akasema: “Haingii peponi mkusanya kodi”.

Ameipokea Abu Dawud.<sup>339</sup> Na hilo ni kwa sababu yeye anasimamia dhuluma za waja.

Na ni kutoka wapi mkusanyaji kodi atawalipa watu siku ya kiyama, kodi alizozichukua kwao? Bila shaka watachukua mema yake, na hii inaingia katika kauli ya Mtume ﷺ akisema: “Mnajua ni nani muflisi?”

Wakasema: “Ewe Mjumbe wa Allah! Muflis katika sisi ni asiye na dirhamu wala vitu.” Mtume ﷺ akasema:

---

<sup>339</sup> Dhaifu: Imepokewa na Ahmad 4/143 na 150,

## Al - Kabair

---

*"Hakika muflis katika Ummati wangu ni yule anayekuja na Swala, Zakka, Saumu na Hijja, na anakuja ilhali amemtukana huyu na kampiga huyu na akachukua mali ya huyu, yatachukuliwa katika mema yake na huyu katika mema yake, na yakisha mema yake kabla ya kulipa anayodaiwa yatachukuliwa mabaya yake na kutupiwa yeye kisha kutupwa motoni."*<sup>340</sup>

Na katika hadithi ya mwanamke ambaye ameitupa nafsi yake katika rajmi, 'kuhukumiwa kupigwa mawe:

*"Hakika ametubu toba lau angeitubu mtoza ushuru angesamehewa, au ingekubaliwa kwake".*

Kutoza ushuru ndani kuna aina inayofanana na uny'ang'anyi, nao ni katika wizi. Mkusanya kodi, mwandishi, shahidi, mbebaji wake miongoni mwa askari wake, Shaykh, na mwenye bendera ni washirika katika madhambi, na ni wenye kula haramu.

Imeswihi hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

*"Haingii peponi nyama yoyote iliyoota kwa haramu, na moto ni aula kwake"*.<sup>341</sup>

Wahidi amesema katika maelezo ya Kauli Yake Taalaa:

قُلْ لَا يَسْتَوِي الْحَبِيبُ وَالطَّيِّبُ

**"Sema: Haviwi sawa viovu na vyema..." (5:100)**

Jabir<sup>340</sup> رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa mtu mmoja alimuuliza mjumbe wa Allah ﷻ: "Ewe Mjumbe wa Allah pombe ilikuwa ndio biashara yangu,

---

<sup>340</sup> Mapokezi yake yametangulia.

<sup>341</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Shi'b 5373, 5374 na kusahihishwa na Al-Albani kwa tamshi, 'Haingii peponi nyama iliyokula haramu.' Al-Mishkat 2887 kupitia njia ya Abu Bakr.

## Al- Kabair

---

nami niliweza kukusanya mali kutokana na mauzo yake, ninaweza kunufaika kutokana na mali hiyo kwa kuzitumia kwa matendo mema kwa utii wa Allah Mtukuka?' Mtume wa Allah ﷺ alimjibu:

« إن أنفقته في حج أو جهاد أو صدقة لم يعدل عند الله جناح بعوضة . إن  
الله لا يقبل إلا الطيب »

*“Ukizitumia kwa ajili ya Hija, au Jihadi, au sadaka, haitalingana thamani yake mbele ya Allah na bawa la mbu, hakika Allah hapokei isipokuwa kizuri.”*

Allah Taalaa akateremsha aya kwa ajili kuswadikisha kauli ya Mtume ﷺ :

قُلْ لَا يَسْتَوِي الْحَيْثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْحَيْثِ

***“Sema: Haviwi sawa viovu na vyema ujapo kupendeza wingi wa viovu. ...” (5:100)<sup>342</sup>***

‘Ata na Al-Hasan wamesema: “Ni halali na haramu”. Tunamuomba Allah msamaha.

\*\*\*

---

<sup>342</sup> Hadithi dhaifu: Kitabu *Asbaab Nuzuul* cha Wahidi uk 121 na Suyyuti amesema: “Mlango wa kauli katika sababu za kuteremshwa” kwa sanadi dhaifu.

## DHAMBI KUBWA YA ISHIRINI NA NANE

### KULA HARAMU NA KUITUMIA KWA NJIA YOYOTE IWAYO

Allah تعالیٰ Anasema:

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ

**“Wala msile mali zenu baina yenu kwa batili...” (2:188)**

Yaani baadhi yenu wasile mali za baadhi kwa batili.

Ibn ‘Abbaas anasema: ‘Yaani kuapa yamini ya batili ya uongo, ili mtu ajipatie mali ya nduguye kwa batili.’ Kula kwa batili kuko aina nne:

Kwanza: ni kwa njia ya dhuluma, mfano kunyan’ganya, khiana, na wizi.

Pili: kujipatia hiyo mali kwa michezo, kama kamari, na anasa. Na mfano wake.

Mjumbe wa Allah تعالیٰ amesema:

« إن رجالاً يتخوضون في مال الله بغير حق فلهم النار يوم القيامة »

*“Hakika watu wanaokula katika mali ya Allah bila haki, basi wao wana moto siku ya kiama”.*<sup>343</sup>

Katika Sahihi Muslim Mtume ﷺ alipotaja:

«الرجل يطيل السفر أشعث أغبر يمد يديه إلى السماء يا رب يا رب ومطعمه حرام ومشربه حرام وملبسه حرام ، وغذي بالحرام فأنى يستجاب لذلك »

---

<sup>343</sup> Mapokezi yake yametangulia hapo nyuma.

## Al- Kabair

---

*“Mtu anayefanya safari akiwa ni mwenye vumbi, ananyanyua mikono yake mbinguni, na kusema: Ewe bwana wangu, ewe bwana wangu ilhali chakula chake ni haramu, na kinywaji chake ni haramu, na mavazi yake ni haramu, na amelelewa kwa haramu basi vipi atajibiwa kwa hilo”.*<sup>344</sup>

Anas anasema: nilimwambia Mtume ﷺ: “Ewe Mtume wa Allah niombe kwa Allah anifanye mwenye kujibiwa dua”. Mtume ﷺ: Akasema:

« يا أنس أظب كسبك تحب دعوتك، فإن الرجل ليرفع اللقمة من الحرام إلى فيه فلا يستجاب له دعوة أربعين يوماً »

*“Ewe Anas fanya vizuri chumo lako utakuwa mwenye kujibiwa dua, kwani mtu anapoinua tonge la haramu mdomoni mwake, basi hatajibiwa dua siku arubaini”.*<sup>345</sup>

Imepokewa na Al-Baihaqi kwa Sanad hadi kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

*“Allah amependa kugawa tabia zenu kama alivyogawa riziki zenu, na hakika Allah Anampa dunia Ampendae na Asiyempenda, Lakini hampini dini isipokuwa Anayempenda, kwa hiyo ambaye Atampa dini hakika huyo Amempenda, wala mja hachumi mali ya haramu na akatoa kutokana na mali hiyo akabarikiwa, au sadaka akakubaliwa, wala haiachi nyuma ya mgongo wake isipokuwa pato lake hilo ni la motoni. Hakika Allah hafuti baya kwa baya, lakini hufuta baya kwa zuri.”*<sup>346</sup>

Ibn ‘Umar رضي الله عنهما anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

---

<sup>344</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 1015 na At-Tirmidhi 2929.

<sup>345</sup> Dhwaifu: Hadithi kuhusu kuombwa kwa Dua ni Hadithi ya S’ad bin Abi Waqasw na sio ya Anas. Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Awsat 6495 kutoka kwa Ibn ‘Abass na imepokewa tena na Al-Munridhiy kwa tamshi dogo zaidi ‘Imepokewa’.

<sup>346</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/387, Al-Hakam 1/34, Al-Baihaqi katika Ash-Shi’b 599 na Al-Bukhari katika Al-Adab al-Mufrad 274 na ikasahihishwa na Shaikh Al-Albani katika As-Swahiha 2714 ikiwa ni marfuu’ na ikasahihishwa ikiwa ni mawqaf katika sahihi Al-Adab Al-Mufrad 209.

## Al - Kabair

---

« الدنيا حلوة نضرة من اكتسب فيها مالا من حله وأنفقه في حقه أتأبه الله وأورثه جنته ، ومن اكتسب فيها مالا من حله وأنفقه في غير حقه أدخله الله تعالى دار الهوان . ورب متخوض ( فيما اشتهدت نفسه من الحرام ) له النار يوم القيامة »

*“Dunia ni tamu inayong`aa, mwenye kuchuma ndani yake mali kutoka kwa uhalali wake, akaitumia kwa haki yake, Allah Atamuingiza Pepo Yake, na mwenye kuchuma ndani yake mali bila ya haki yake, Allah Atamuingiza nyumba ya udhalilifu. Pengine mwenye kuzama (katika matamanio ya nafsi yake katika yaliyo ya haramu) atakawa katika moto siku ya kiama”.*<sup>347</sup>

Vile vile imetolewa taarifa kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

« من لم يبال من أين اكتسب المال لم يبال الله من أي باب أدخله النار »

*“Ambaye hajali mali yake ameichuma wapi, Allah hatajali ni mlango gani atamtia motoni”.*<sup>348</sup>

Abu Hurairah رضي الله عنه amesema:

« لأن يجعل أحدكم في فيه تراباً خيراً من أن يجعل في فيه حراماً »

*“Mtu kutia mdomoni mwake udongo ni bora kwake kuliko kutia mdomoni mwake haramu.”*<sup>349</sup>

---

<sup>347</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 5139 na imehakikiwa na Al-Albani katika Hadithi 1103 kutoka kwa Ibn Umara na kusahihishwa na Shaikh katika As-Swahiha 1592 na Sahihi Al-Jami' 3410 ikiwa ni muhtasari.

<sup>348</sup> Hassan: Imepokewa na At-Twabarani 1770, 1661 na 1662 kutoka kwa Jundub ikiwa ni marfu' 'Atakayeweza miongoni mwenu asifanye wala asile ya haramu wala mahjama katika damu ya haramu hafiki katika milango miongoni mwa milango ya peponi isipokuwa baina yake na kuiingia.' Isnadi yake haina neno.

<sup>349</sup> Dhwaifu: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi'b 5379 na kudhoofishwa na Al-Albani katika Dhwaif Al-Jami' 446.

## Al- Kabair

---

Yusuf bin Asbaat alisema: 'Kijana akiwa anamuabudu Mungu shetani anawaambia wasaidizi wake, angalieni wapi kinatoka chakula chake, ikiwa chakula chake ni kibaya, basi huwaambia: mwacheni ataabike na kujisumbua nafsi yake imekutosheni.'

Kwa hakika jitahada zake huku akiendelea kula ya haramu haitomnufaisha. Maneno haya yameungwa mkono katika maneno ya Mtume ﷺ kuhusu mtu ambaye chakula chake ni cha haramu na kinywaji chake ni cha haramu na mavazi yake ni ya haramu na anakula kutokana na haramu

«فأنى يستجاب لذلك؟»

“..Basi vipi atajibiwa kwa hilo?”<sup>350</sup>

Imepatikana taarifa katika hadithi kuwa kila asubuhi na kila jioni katika Baytil Maqdis kuna malaika ananadi:

«من أكل حراما لم يقبل الله منه صرفا ولا عدلا»

“Mwenye kula haramu Allah hakubali kwake sunna wala faradhi”

‘Abdullah ibn Mubaarak alisema: “Kukataa dirham moja yenye mashaka ni bora kwangu kuliko kutoa sadaka dirham mia moja elfu na mia”. Na imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

« من حج بمال حرام فقال لبيك ، قال ملك : لا لبيك ولا سعديك حجك  
مردود عليك »

“Mwenye kuhiji kwa mali ya haramu na akasema: (Labbayka Allaahumma labbayk) na malaika wanasema: “Hapana! Hujaitika wala hujafurahi, Hija yako umerudishiwa mwenyewe”.<sup>351</sup>

---

<sup>350</sup> Angalia Sahihi Muslim 5101.

<sup>351</sup> Dhwaifu: Imepokewa na Ibn Al-Jawziy katika Al-'Ilal Al-Mutanahiyat 2/930 angalia Adh-Dwahifa 1091.

## Al - Kabair

---

Imepokewa na Imam Ahmad katika Musnad yake kutoka kwa Mtume Mtukufu ﷺ kuwa amesema:

« من اشترى ثوبا بعشرة دراهم وفي ثمنه درهم من حرام لم يقبل الله له صلاة  
ما دام عليه »

*“Mwenye kununua nguo kwa dirham kumi, na ndani yake kuna dirhamu ya haramu, basi Allah hatakubali Swala yake madamu iko juu yake (nguo hiyo).”*<sup>352</sup>

Wahib ibn Ward amesema: hata ukisimama kikakamavu sawa sawa kama mlingoti wa meli katika Swala, haitakunufaisha mpaka uangalie kinachoingia tumboni mwako, ni halali au haramu.<sup>353</sup>

Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا amesema: “Allah hakubali Swala ya mtu ambaye tumboni mwake kuna haramu, hadi atubu kwa Allah Mtukuka kutokana nayo”. Sufyan Thauri amesema: Mtu anayetumia haramu katika utii, ni kama aliyesafisha nguo kwa mkojo. Nguo hazisafishwi isipokuwa kwa maji, na dhambi haisamehewi isipokuwa kwa halali”. ‘Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُ amesema, Mtume ﷺ amesema:

« لا يدخل الجنة جسد غذي بالحرام »

*“Hauingii peponi mwili (kiwiliwili) uliolishwa haramu.”*<sup>354</sup>

Zayd ibn Arqam amesema: “Abu Bakr رَضِيَ اللهُ عَنْهُ alikuwa na Mtumwa aliyekuwa anamletea kipato, (Amemuandika kwa ajili ya mali) na Abu Bakr alikuwa akimuuliza: “Wapi umepata hii?” Endapo Abu Bakr akiridhia basi atakula la sivyo, atakiacha. Usiku mmoja mtu huyo alimtelea chakula na Abu Bakr رَضِيَ اللهُ عَنْهُ, alikuwa amefunga, alisahau

---

<sup>352</sup> Dhwaifu: Imepokewa na Ahmad 2/98 kwa sanad dhaifu kama ilivyo katika dhaifu Al-Jami’ 5428.

<sup>353</sup> Sahihi: Imepokewa na Abu Nua’im 8/154.

<sup>354</sup> Hassan: Imepokewa na Ahmad 3/399, Ibn Hibaan 5567 na Al-Baihaqi katika Ash-Shi’b 5377



## Al- Kabair

---

kumuuliza suali la kila siku, akamega hicho chakula kidogo. Akakumbuka na kamuuliza: “Umekipata wapi?”, Mtumwa huyo akamjibu, ‘Nilijidai kuwa mtabiri wa baadhi ya watu nami sikuwa hodari, niliwadanganya’ Abu Bakr رضي الله عنه akasema ole wako, kidogo uniangamize, Abu Bakr akatia vidole mdomoni mwake akawa anajitapisha, lakini hakikutoka, akaambiwa: ‘Hakitoki isipokuwa kwa maji.’ Akanywa maji huku anajitapisha akasema: ‘Lau isingetoka isipokuwa kwa nafsi yangu ningeitoa”. Kisha akasema: Nimemsikia Mjumbe wa Allah ﷻ akisema:

« كل جسد نبت من سحت فالنار أولى به »

*“Kila kiwiliwili kilichomea (kimekuwa) kutokana na haramu moto ni aula kwake”.*

Kwa hivyo nikaogopa kumea katika mwili wangu kutokana na tonge hilo.<sup>355</sup> Imetangulia kutoka kwa Mtume ﷺ

« لا يدخل الجنة جسد غذي بحرام »

*“Hautaingia peponi mwili uliokuzwa kwa haramu”.*<sup>356</sup> Na Isinadi yake ni sahihi.

Wanazuoni Allah Awarehemu wamesema: Anaingia katika mlango huu mtoza ushuru, khaini, mwenye kughushi, mwizi, mvivu, mla riba, mwakilishi wake, mla mali ya yatima, anayeshuhudia uongo, aliyekopa na akakanusha, mla rushwa, anayepunguza mizani na kilo, anayeuzua kitu ambacho kina dosari akaifunika, mcheza kamari, mchawi, mtengeneza picha, mzinzi, malaya, dalali anayechukua ujira wake bila idhini ya muuzaji, na mwenye kumwambia mnunuzi zaidi, na anayeuzua mtu huru akala thamani yake.

---

<sup>355</sup> Sahihi: Kisa hiki ni sahihi na kipo katika Al-Bukhari 2483 hadi kauli yake, “ Akatapika kila kitu katika tumbo lake” Hadithi imepokewa na Al-Baihaqi 5735 na Abu Nua’im 1/ 31 kwa mfano wake kwa Sanad dhaifu sana na ndani yake kuna Ibn Zaid ambae An-Nasai amemtaja kama Matruuk.

<sup>356</sup> Maelezo yake yametangulia.

## FASILI

Mtume ﷺ amesema:

« يؤتى يوم القيامة بأناس معهم من الحسنات كأمثال جبل تهامة ، حتى إذا جيء بهم جعلها الله هباء منثورا ثم يقذف بهم في النار » .

*“Siku ya kiyama watu wataletwa na matendo mema kama mfano wa mlima wa Tihaamah, mpaka watakapofika nayo Allah ataifanya vumbi lilotawanywa na watatumbikizwa motoni.”*

Kukasemwa: “Ewe Mjumbe wa Allah, kwa sababu gani hiyo?”

Mtume ﷺ akasema:

« كانوا يصلون ، ويصومون ، ريزكون ، ويحجون وغير أنهم كانوا إذا عرض لهم شيء من الحرام أخذوه فأحبط الله أعمالهم »

*“Wao walikuwa wakifunga, wakitoa Zaka, wanahiji, isipokuwa wao walikuwa wakionyeshwa haramu wanaichukua, kwa hiyo Allah Akapomoshia matendo yao”.*<sup>357</sup>

Imesimuliwa kutoka kwa baadhi ya waja wema kuwa mcha mungu mmoja alionekana katika ndoto baada ya kifo chake, akaulizwa ‘Allah amekufanya nini?’ Akajibu: “Kheri, Isipokuwa nimezuiwa pepo kwa sababu ya sindano niliyoiazima na sikuirudisha”.

Tunamuomba Allah Taalaa msamaha na uzima, na taufiki, kwa Anayoyapenda, Hakika yeye ni Mpaji, Mkarimu Mwingi wa huruma Mwingi wa kurehemu.

---

<sup>357</sup> Sahihi: ni sahihi kwa ushahidi mwingineo, amesema Suyuti katika Ad-Dur 5/122 imepokewa kutoka kwa Samuwaih katika Fawaid yake kutoka kwa Salim Mawla wa Abu Hudhaifa na Ibn Majah 4245 na kusahihishwa na Al-Albani katika As-Swahiha 505.

DHAMBIB KUBWA YA ISHIRINI NA TISA

MTU KUJIUA MWENYEWB

Allah Aliyetukuka Anasema:

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ؕ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٠٨﴾ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ عَدُوًّا وَظُلْمًا  
فَسَوْفَ نُصَلِّيهِ نَارًا ؕ وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٢٠٩﴾

**“Wala msijiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwarehemuni. Na mwenye kutenda hayo kwa uadui na udhaalimu, basi huyo Tutamwingiza Motoni. Na hilo ni jepesi kwa Mwenyezi Mungu.” (4:29:30)**

Waahidi katika kueleza aya hiyo anasema:

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ؕ

**“Msijiuwe wenyewe;**

Inamaanisha msiuane baadhi yenu, kwani nyote mnatokana na dini moja, kwa hivyo nyinyi ni kama nafsi moja.’ Maelezo haya vile vile ameyatoa Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا na wanazuoni wengi. Hata hivyo kuna baadhi ya wanazuoni wanatoa tafsiri yao kuwa katazo hili ni mtu kujiua mwenyewe, kuswihi kwa habari hii kunatokana na aliyotuambia Abu Mansuur Muhammad bin Muhammad Al-Mansuuri kwa isinadi yake kutoka kwa ‘Amr binil `Aas alisema: ‘Niliota ndoto (nikapata janaba) usiku wa baridi kali wakati wa vita vya *Dhaatis-As-Salaasil* nikahofia kuwa kama nikioga nitakufa, hivyo nikatayamamu na kuswali swala ya alfajiri pamoja na wenzangu, nikamsimulia kisa hiki Mtume ﷺ akaniambia:

**“Ewe ‘Umar umewaswalisha wenzako ukiwa na janaba?”**

Nilimuambia jambo lililonizuia kukoga nikasema: Nimemsikia Allah akisema: kisha akasoma aya hii:

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٠٨﴾

**“...Wala msjiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwarehemuni.” (4:29)**

Mjumbe wa Allah ﷺ alicheka na hakuniambia lolote.<sup>358</sup>

Hadithi hii ni ushahidi kuwa ‘Amr alitafsiri aya hii kwa kuangamia nafsi yake siyo wengine, na Mtume ﷺ hakumpinga, Kauli yake:

وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ عُدْوَانًا

**“Na mwenye kufanya hivyo”.**

Ibn ‘Abbaas alikuwa anasema: Ishara inarudi kwenye kila alichokikataza Allah kutoka mwanzo wa sura hadi kwenye maudhui haya. Watu wengine wakasema: ‘Kamio linarudi kwa wenye kula mali kwa batili na kuua nafsi iliyoharamishwa’, Na Kauli Yake:

عُدْوَانًا وَظُلْمًا

**“Kwa uadui na dhuluma”**

Na miongoni mwa dhuluma ni kufanyia uadui aliyoyaamrisha Allah.

وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٢٠٩﴾

**“Na hilo likawa kwa Allah ni jepesi”.**

---

<sup>358</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 4/203-204, Abu Dawud 334 na kusahihishwa na Shaykh Albani katika As-Silsilah 154.

## Al- Kabair

Kuwa Yeye ni Muweza kuyafanya aliyoyaahidi kama vile kuingiza motoni. Kutoka kwa Jundub ibn 'Abdullah anatoa taarifa kuwa Mtume ﷺ amesema:

وعن جُنْدُب بن عبد الله -رضي الله عنه-، عن النبي ﷺ قال: «كان ممن كان قبلكم رجلٌ به جرحٌ فيجزع، فأخذ سكيناً فحزَّ بها يده، فما رقا الدم حتى مات، قال الله -تعالى-: -بادرتني عبدي بنفسه؛ حرمتُ عليه الجنة»<sup>(3)</sup> متفق عليه.

*“Ilikuwa katika waliokuwa kabla yenu, mtu ambaye alikuwa na jeraha akafazaika akachukua kisu akajikata nacho mkono wake, kwa hiyo damu haikukoma, hadi akafa. Allah Aliyetukuka Akasema: “Mja wangu ameniharakisha basi Nimemharamishia pepo.” Imepokewa katika sahihi mbili.<sup>359</sup>*

Na kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah تعالى amesema:

وعن أبي هريرة -رضي الله عنه-، قال: قال رسولُ الله ﷺ: «من قتل نفسه بحديدةٍ فحديدته في يده يتوجأ<sup>(4)</sup> بها في بطنه في نار جهنم خالداً مخلداً فيها أبداً، ومن قتل نفسه بسهمٍ فسمه في يده يتحسأه في نار جهنم خالداً مخلداً فيها أبداً»<sup>(5)</sup> متفق عليه.

*“Mwenye kujiua mwenyewe kwa chuma, basi ndani ya Jahannam silaha yake ile ya chuma chake kitakuwa mkononi mwake akijichoma nayo tumbo lake katika mto wa Jahannam milele, atawekwa humo milele, na mwenye kujiua mwenyewe kwa sumu, basi sumu yake itakuwa mkononi mwake, akijichoma katika moto wa Jahannam daima milele, na mwenye kujiua mwenyewe kwa kujirusha jabalini, basi atakuwa akijirusha jabalini ndani ya Jahannam daima milele.”. Imepokewa kutoka katika sahihi mbili<sup>360</sup>*

<sup>359</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 3463 na Muslim 113.

<sup>360</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 5778 na Muslim 109.

## Al - Kabair

---

Katika hadithi ya Thabit bin Dhahhaak anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

عن يحيى بن أبي كثير<sup>(٣)</sup>، عن أبي قلابة، عن ثابت بن الضحَّك، عن النبي ﷺ قال: «لعنُ المؤمنُ قَتْلَهُ، وَمَنْ قَذَفَ مُؤْمِنًا بِكُفْرٍ فَهُوَ كَقَاتِلِهِ، وَمَنْ قَتَلَ نَفْسَهُ بِشَيْءٍ عَذَّبَهُ اللهُ بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»<sup>(٤)</sup> [حديث] صحیح<sup>(٥)</sup>.

*“Kumlaani muumini ni kama kumuua, na mwenye kumsingizia muumini ni kama kumuua kwake, na mwenye kujiua mwenyewe kwa kitu ataadhibiwa nacho siku ya kiyama.”<sup>361</sup>*

Katika hadithi sahihi:

وفي الحديث الصحيح<sup>(١)</sup>: الذي آلمته الجراحُ فاستعجلَ الموتَ فقتل نفسه بذبابٍ سيفه، فقال النبي ﷺ: «هو من أهل النار»<sup>(٢)</sup>.

Kutoka kwa mtu ambaye jeraha lilimsumbua akafanya haraka kufa kwa kujiua kwa panga lake, Mtume ﷺ akasema: “Mtu Yule ni katika watu wa motoni.”<sup>362</sup>

Tunamuomba Allah Atuongoze katika njia ya haki na Atukinge na shari za nafsi zetu, na uovu wa matendo yetu. Hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu, Msamehevu na Mrehemevu.

\*\*\*

---

<sup>361</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6105 na Muslim 110.

<sup>362</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6607 na Muslim 112.

**DHAMBI KUBWA YA THELATHINI**  
**UONGO KATIKA KAULI ZETU NYINGI**

Allah تعالیٰ Aliyetukuka Anasema:

ثُمَّ نَبْتَلُ فَنَجْعَل لَّعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكٰذِبِينَ ﴿٦١﴾

**“...kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo. ”(31:61)**

Akasema tena katika aya nyingine:

قُتِلَ الْخٰرِصُونَ ﴿١٠﴾

**“Wazushi wameangamizwa.” (51:10)**

Yaani: Waongo. Kisha Akasema tena:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ كٰذِبٌ

**“Hakika Mwenyezi Mungu hamwongoi apindukiaye mipaka, mwongo mkubwa. ” (40:28)**

Katika sahihi mbili ‘Abdullah ibn Masuud anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

وقال النبي ﷺ: «إِنَّ الْكٰذِبَ يَهْدِي إِلَى الْفَجْوَرِ، وَإِنَّ الْفَجْوَرَ يَهْدِي إِلَى النَّارِ، وَلَا يَزَالُ الرَّجُلُ يَكْذِبُ حَتَّى يُكْتَبَ عِنْدَ اللَّهِ كٰذِبًا»<sup>(٤)</sup> متفق عليه.

**“Ukweli huongoza kwenye wema, na wema huongoza kwenye pepo, na mtu hataacha kusema ukweli na kutafuta ukweli hadi aandikwe mbele ya Allah kuwa mkweli, Na mtu hataacha kusema uwongo na kuchagua uongo hadi aandikwe mbele ya Allah kuwa muongo”.**<sup>363</sup>

---

<sup>363</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 6094 na Muslim 2707 kutoka kwa Ibn Mas’uud.

## Al - Kabair

---

Katika sahihi mbili vile vile kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

وقال ﷺ: «آية المنافق ثلاث: إذا حدث كذب، وإذا وعد أخلف، وإذا  
أتمن خان»<sup>(6)</sup>.

*“Alama za mnaifiki ni tatu hata kama atakuwa anafunga (saumu),  
anaswali na anadai kuwa ni Muislamu: (nazo ni) wakati  
akizungumza husema uongo, akitoa ahadi huivunja na akiaminiwa  
hugeuka (hufanya khiana).”<sup>364</sup>*

Na akasema Mtume ﷺ:

وقال: «أربع من كن فيه كان منافقاً خالصاً، ومن كانت فيه خصلة منهن  
كانت فيه خصلة من النفاق حتى يدعها: إذا أتمن خان، وإذا حدث كذب، وإذا  
عاهد غدر، وإذا خاصم فجر»<sup>(6)</sup> متفق عليه.

*“Mambo mane mwenye kuwa nayo anakuwa mnaifiki halisi na  
anapokuwa na moja wapo anakuwa na sehemu ya unafiki hadi aiache,  
ni kuwa anapoaminiwa anahalifu, na anapoahidi anahini, na  
anapogombana anafanya uovu, na anaposema anadanganya.”<sup>365</sup>*

Katika Sahihi Bukhari kuna hadithi juu ya ndoto za Mtume ﷺ anasema:

*“Tulikwenda tukamkuta mtu amelala chali na mtu mwingine  
amesimama karibu naye ameshika koleo za chuma mkononi mwake,  
na humchana nayo mdomo wake hadi kichogoni mwake, na kuchana  
pua zake hadi shingoni mwake, na kuchana macho yake hadi shingoni  
mwake, kisha atamgeukia upande mwingine na kufanya hivyo  
hivyo. Hafanyi hivyo isipokuwa upande ule wa mwanzo utakuwa  
umeshakuwa kama ulivyokuwa mwanzo, kwa hiyo atafanyiwa hivyo  
hadi siku ya kiama. Kwa hiyo nikawauliza: “Ni nani huyu?, (Jibril*

---

<sup>364</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 33 na Muslim 59 kutoka kwa Abu Hurayrah.

<sup>365</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 34 na Muslim 58 kutoka kwa Ibn Mas'ud.



## Al - Kabair

---

na Mikail) Wakasema: Alikuwa anarauka asubuhi nyumbani kwake na kutengeneza uongo unaofika pambizo (za dunia)".<sup>366</sup>

Mtume ﷺ amesema:

«يُطِيعُ الْمُؤْمِنُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ لَيْسَ الْخِيَانَةُ وَالْكَذِبُ»

"Kila kitu kinamfuata muumini isipokuwa khiana na uongo."<sup>367</sup>

Katika hadithi nyingine:

"Tahadharini na kudhania kwani kudhania, ni mazungumzo yaliyo ya uongo zaidi."<sup>368</sup>

Katika hadithi nyingine:

"Watu wa tatu Allah hatazungumza nao wala hatawaangalia siku ya kiama, mzee mzinifu, mfalme muongo, na maskini mwenye kiburi".<sup>369</sup>

Mtume ﷺ amesema:

"Ole wake ambae anasema neno ili kuwachekesha nalo watu, kwa hiyo anadanganya, Ole wake Ole wake Ole wake".<sup>370</sup>

Uongo mkubwa zaidi kuliko huo ni kuapa, kama alivyosema Allah kuhusu wanafiki kwa Kauli Yake:

وَيَحْلِفُونَ عَلَى الْكُذِبِ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٥٨﴾

"...Na huapa kwa uwongo, na hali kuwa wanajua." (58:14)

---

<sup>366</sup> Angalia rejea za nyuma.

<sup>367</sup> Angalia rejea za nyuma.

<sup>368</sup> Imepokewa na Ahmad 2/465, 517, Al-Bukhari 6066, Muslim 2563 kutoka kwa Abu Hurayrah.

<sup>369</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 2347, Muslim 108 na Abu Dawud 3474.

<sup>370</sup> Imepokewa na Abu Dawud 4990, Tirmidhi 2315 na imefanywa Hassan na Shaikh katika Ghayatul Maram 376 na Al-Mishkaat 4737 na Sahihi Al-Jami' 8013.

## Al - Kabair

---

Mtume ﷺ amesema katika Hadithi sahihi:

*“Watu watatu; Allah hatozungumza nao Siku ya kiyama wala kutawatakasa na wana adhabu iumizayo, mtu mwenye maji ya ziada anamnyima mpita njia, mtu amenunua bidhaa kwa mtu akaapa kwa Allah kuwa ataichukua kwa kadha wa kadha, kwa hivyo akamswadikisha, kumbe yeye yuko kinyume na hivyo, na mtu amembai kiongozi hakumbai isipokuwa kwa ajili ya dunia, akimpa kutokana nayo humtekelezea, na asipompa hamtekelezei.”<sup>371</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

*“Ni khiana kubwa kumuambia jambo nduguyo, ambaye anakuamini kwa hilo na wewe unamdanganya.”<sup>372</sup>*

Katika hadithi nyingine:

وقال ﷺ: «من تحلّم بحلّم لم يرّه، كُلفَ أن يعقدَ بين شعيرتين يوم القيامة، ولن يفعل»<sup>(٧)</sup> رواه البخاري - أيضاً.

*“Mwenye kuhadithia ndoto asiyojota atalazimishwa kufunga (fundo) baina ya nywele mbili, naye siye mwenye kufunga (fundo hilo).”<sup>373</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

[وقال ﷺ: «إن أفرى أفرى أن يُرى الرجلُ عينيه ما لم ترّياً»<sup>(١١)</sup> رواه البخاري - أيضاً]<sup>(١٢)</sup>.

*“Uzushi mkubwa kwa Allah ni mtu (kudai) macho yake yameona ambacho hayakuona.”<sup>374</sup>*

---

<sup>371</sup> Dhwaifu: Ahmad 4/183, Al-Baihaq katika Ash-Shi'b 4479 na kudhoofishwa na Shaikh katika As-Silsilah Adh-Dwaifa 1251.

<sup>372</sup> Sahihi: Ahmad 1/616, 359, na Al-Bukhari 7042.

<sup>373</sup> Sahihi: Ahmad 4/106, na Al-Bukhari 7043.

<sup>374</sup> Sahihi: Al-Bukhari 7043.

## Al-Kabair

---

Maana yake ni kudai kuwa ameona katika ndoto kadha wa kadha, na yeye hakuwa ameona chochote. Ibn Masuud amesema:

*“Mtu huendelea kusema uwongo na kuchagua uongo hadi atiwe nukta nyeusi ndani ya moyo wake, moyo wake uwe mweusi, na hivyo kuandikwa mbele ya Allah miongoni mwa waongo”.*

Inatakiwa Muislamu kuhifadhi ulimi wake na maneno, isipokuwa maneno yaliyodhihirika masilahi yake, kwani katika kunyamaza kuna amani na amani hailingani na chochote.

Katika Sahihi Bukhari kutoka kwa Abu Huraira رَضِيَ اللهُ عَنْهُ anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

*“Mwenye kumuamini Allah na siku ya mwisho na aseme kheri au anyamaze”.* (Bukhari).<sup>375</sup>

Hadithi hii ni sahihi ni andiko la wazi kuwa mtu hatakiwi kuzungumza ila itakapokuwa mazungumzo yake yale ni sahihi, nayo ni maneno yenye kudhihirisha maslahi yake kwa muongejaji. Anasema Abu Musa رَضِيَ اللهُ عَنْهُ alimuuliza Mtume ﷺ: ‘Ewe Mjumbe wa Allah Muislamu yupi ni bora?’

Mtume ﷺ akasema:

*“Ni yule ambaye waislamu wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake”.*<sup>376</sup>

Katika sahihi mbili imetolewa taarifa kuwa Mtume ﷺ alisema:

*“Hakika mtu atatamka maneno bila ya kufikiri (hafikiri kuwa hayo ni haramu) basi mtu huyo atatiwa motoni masafa mfano wa mashariki na magharibi.”*<sup>377</sup>

---

<sup>375</sup> Sahihi: Al-Bukhari 6018 na Muslim 42.

<sup>376</sup> Rejea yake ilishaoneshwa.

<sup>377</sup> Sahihi: Imepokewa na At-Tirmidhi 92319, Ibn Majah 3969 na Al-Baihaqi katika Ash'ib 4606, imesahihishwa na Shaikh Al-Albani katika Silsila As-Swahiha 886.

## Al - Kabair

---

Katika Muwattwa ya Imam Maalik kuna riwaya ya Bilal ibn Al-Haarith Al-Muzni anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*“Hakika mtu atasema neno ili kumridhisha Allah, na hakuwa anadhania kuwa neno hilo litamfikisha lilipomfikisha. Allah Aliyetukuka Atamwandikia kwalo radhi hadi siku ya kukutana naye, na mtu (mwengine) atasema neno la kumchukiza Allah, na hakuwa anadhania kuwa litamfikisha lilipomfikisha, na Allah Aliyetukuka Atamwandikia hasira zake hadi siku ya kiama.”*

Zipo hadithi nyingi kuhusu hayo, lakini hizi tulizozisimulia zinatoshleza. Baadhi yao waliulizwa: “Umeona aibu ngapi za mwanadamu?” Akasema: ‘Zipo nyingi zisizo hesabika. Nilizohesabu ni aibu elfu nane, na ninaona jambo moja akilifanya mtu, litaficha aibu zote, nalo ni kuhifadhi ulimi.”

Allah Atuepushie kumwasi kwa maasi aliyokataza, na tufanye katika yanayomridhisha, hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu.

\*\*\*

DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA MOJA

HAKIMU MUOVU

Allah Mtukuka Anasema:

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٥٤﴾

**“...Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.” (5:44)**

Allah Aliyetukuka Anasema:

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٥٥﴾

**“...Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu.” (5:45)**

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفٰسِقُونَ ﴿٥٦﴾

**“...Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu.” (5:47)**

Amepokea Al-Hakim katika sahihi yake kutoka kwa Talha bin ‘Ubaidullah رضي الله عنه kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ anasema:

لا يقبلُ اللهُ صلاةَ إمامٍ حَكَمَ بِغَيْرِ ما أَنزَلَ اللهُ

**“Allah haikubali Swala ya kiongozi anayehukumu kinyume na alivyoteremsha Allah”.<sup>378</sup>**

---

<sup>378</sup> Dhaifu: Ameipokea Al-Hakim 4/89 na akasema sahihi sanad yake na ikafuatiwa na kauli ya Adh-Dhahabi, ‘Kuashiria Madhalama na ndani yake yupo Abdullah bin Muhammad na Muslim Al-‘Adwi na Muslim na ametaja Al-Mundhiri katika At-Targhiib 3/169 na akasema ‘Abdullah huyu ni Waahin Jiddah

## Al - Kabair

---

Al-Hakim ameisahihisha pia katika masimulizi ya Buraida رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

وصحح الحاكم - أيضاً - والعهد عليه - من حديث بُريدة، عن النبي ﷺ  
قال: «قاضي في الجنة وقاضيان في النار، قاض عرف الحق فقتضى به فهو في الجنة،  
وقاض عرف الحق فجار متعمداً فهو في النار، وقاض قضى بغير علم فهو في النار»<sup>(1)</sup>.

*“Mahakimu ni watatu: hakimu mmoja peponi, na mahakimu wawili motoni, hakimu aliyejua haki akaifanyia haki huyo yuko peponi, na hakimu anayeijua haki akafanya jeuri kwa ujeuri basi huyo ni wa motoni, na hakimu amehukumu bila elimu, Basi huyo ni wa motoni”.*  
Wasikilizaji wakauliza: “Ni nini dhambi ya asiyejua?”  
Mtume ﷻ akasema: “Dhambi yake ni kutohukumu hadi ajue”<sup>379</sup>

Na kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema: “Aliyefanywa hakimu amechinjwa bila kisu.”<sup>380</sup>

Fudhail bin Iyaadh رحمه الله تعالى amesema: “Inatakiwa kwa hakimu ahukumu siku moja, na siku moja aililie nafsi yake”.

Muhammad bin Wasi'i رحمه الله تعالى alisema: “Siku ya kiyama wa mwanzo watakaoitwa kwenye hesabu ni Mahakimu”.

Aisha رضي الله عنها alitoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*“Ataletwa hakimu mwadilifu Siku ya kiama, na kwa sababu ya uzito wa hesabu atatamani kuwa yeye (hakimu) hakuhukumu baina ya watu wawili kuhusu tende moja.”* (Ahmad).<sup>381</sup>

---

<sup>379</sup> Sahihi: Imepokewa na Abu Dawuud 3573, At-Tirmidhi 1325, Ibn Majah 2315, na kusahihishwa na Shaikh Al-Albani katika Al-Arwaa 23614 na Sahihi Al-Jami' 4446, 4447.

<sup>380</sup> Sahihi: Imepokewa na Abu Dawuud 3571, 3572, At-Tirmidhi 1323, na ni Hassan kulingana na Shaikh Al-Albani katika Ar-Rawdh An-Nadhiir 1137, Al-Mishkaat 3733 na Swahihi Al-Jami' 6594.

<sup>381</sup> Dhwaifu: Imepokewa na Ahmad 6/75, Ibn Hibaan 5055 na Dhwaifu Al-Jami' 1516.

## Al-Kabair

---

Mu'adh bin Jabal anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*"Hakimu atateleza katika (shimo) la Jahannam kwa umbali zaidi ya Adeni."*<sup>382</sup>

'Ali bin Abi Talib رضي الله عنه anasema nimefikia Mjumbe wa Allah ﷺ akisema:

*"Si liwali wala hakimu isipokuwa ataletwa Siku ya kiama asimamishwe mbele ya Allah Mwenye nguvu Mwenye kushinda, hadi asimamishwe juu ya Swirati, kisha siri zake zitasomwa juu ya vichwa vya watu. Endapo alikuwa mwadilifu, Allah Atamuokoa kwa uadilifu wake, vinginevyo daraja lile litatetemeshwa mtetemeko mkali, kila kiungo katika viungo vyake vitapeperuka mwendo wa kadha na kadha, kisha daraja litamrushia Jahannam."*<sup>383</sup>

Makhuul amesema: "Endapo ningechaguliwa ni chagua baina ya ukadhi na kukatwa shingo yangu, ningechagua kukatwa shingo badala ya ukadhi."

Ayuub Sikhitiyani alisema: Mimi nimegundua kuwa wasomi wakubwa ndio wanaoukimbia zaidi. Sufyan Thawri aliambiwa: kuwa Shuraih amechaguliwa kuwa hakimu. (Sufyan) akasema: "Aa! wamekwishamharibu"

Malik bin Mundhir alimuita Muhammad bin Wasi amfanye kuwa kadhi wa Basra akakataa, akambembeleza akamwambia: 'Utakaa kwenye ukadhi au nitakuchapa'. Muhammad bin Wasi alimjibu: 'Ukifanya hivyo wewe ni mfalme, lakini ni bora kudhalilika hapa duniani, kuliko kudhalilika hapo kesho akhera.' Wahb bin Munabbih alisema: "Wakati mtawala akiwa jeuri au akautumia ujeuri wake Allah hutia upungufu juu ya watu wa mamlaka yake, hadi katika masoko, riziki, mazao, na chuchu (za maziwa kama vile ng'ombe, n.k) na kila kitu. Na atakapotamani kheri au uadilifu Allah atatia baraka katika watu wa mamlaka yake vile vile."

---

<sup>382</sup> Dhwaifu: Imepokewa na 'Abdul bin Hamid katika Al-Muntakhab 108 na sanad yake dhaifu.

<sup>383</sup> Dhwaifu: Az-Zawajir 2/187 na dhaifu al-Jami' 2253.

## Al - Kabair

---

Gavana wa Hims alimwandikia Khalifa 'Umar bin 'Abdul 'Aziz: " *Ama Ba'adu*: Mji wa Hims umeangamia na unahitaji matengenezo." Khalifa 'Umar alimjibu: "Uhifadhi kwa kutumia uadilifu na njia zake zisafishe mbali na ujeuri". Wasalaam.

Akasema: "Ni haramu kwa kadhi kuhukumu akiwa na ghadhabu,<sup>384</sup> na yanapokusanyika kwa kadhi; uchache wa elimu, dhamira mbaya, tabia mbaya basi hasara yake imetimia, na ni wajibu juu yake kujiuzulu nafasi hiyo, na kuharakisha ikhilasi."

Tunamuomba Allah تعالی msamaha na uzima, na taufiki kwa anayo yapenda na kuyaridhia, Hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu.

\*\*\*

---

<sup>384</sup> Imepokewa na Al-Bukhari 7158 na Muslim kwa tamshi 'Kadhi hahukumu kati ya watu akiwa amekasirika.'



## DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA MBILI

### UTOAJI NA UPOKEAJI RUSHWA

Allah Aliyetukuka Anasema:

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ وَتُدْخِلُوا بِهَا إِلَى الْحُكْمِ لِتَأْكُلُوا فَرِيقًا

مِنْ أَمْوَالِ النَّاسِ بِالْإِثْمِ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٨﴾

***"Wala msiliane mali zenu kwa baa'tili na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua" (2:188)***

Yaani: Msitumie mali zenu kwa mahakimu wala msiwape rushwa ili wakukatieni haki za wengine, hali mnajua kuwa hayo si halali. Abu Hurairah رضي الله عنه amesema: Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*"Allah amemlaani mtoa rushwa na mpokea rushwa katika hukumu".*  
Imepokewa na At-Tirmidhi na akasema ni hadithi Hasan.<sup>385</sup>

'Abdullah bin 'Amr anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amemlaani mwenye kutoa na mwenye kupokea rushwa".<sup>386</sup>

Wanazuoni wanasema: 'Ar-Raash' Mwenye kutoa ni yule anayetoa rushwa, na 'Al-Murtashi' ni yule anayepokea rushwa, ambaye hulaaniwa kwa sababu amekusudia kusababisha matatizo kwa waislamu, au kwa sababu yeye anataka kumiliki kisichomstahiki. Ikiwa anatoa rushwa kwa ajili ya kupata haki yake au kuondoa dhuluma kwa nafsi yake yeye haingii katika laana.

---

<sup>385</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/387, 388, At-Tirmidhi 1336 na kusahihishwa na Shaikh Al-Albani katika sahihi At-Tirmidhi na sahihi Ibn Majah na sahihi Al-Jami' 5093.

<sup>386</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/164, 190, 212, Abu Dawuud 3580, At-Tirmidhi 1337, Ibn Majah 2313, na kusahihishwa na Shaikh Al-Albani katika sahihi At-Tirmidhi na sahihi Ibn Majah angalia marejeo yaliyotangulia.

Ama hakimu kuchukua rushwa ni haramu, kwani kwa rushwa hiyo atakuwa amebatilisha haki. Imepokewa katika hadithi:

« إن اللعنة على الرائش أيضاً »

*“Hakika laana ni juu ya mtu wa kati wa kutoa rushwa vile vile.”<sup>387</sup>*

### FASILI

Katika hayo, Abu Dawud ameandika katika Sunan yake kuwa Abu Umaamah Bahili رضي الله عنه amesema: Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« من شفع لرجل شفاعه فأهدى له عليها هدية فقد أتى باباً كبيراً من أبواب الربا »

*“Mwenye kumuomba mtu shufaa na yule aliyembewa akampa zawadi aliyemuomba na akaikubali basi ameendea milango mingi katika milango ya riba”.*<sup>388</sup>

Ibn Masuud amesema: “As-Suhtu ni kutaka haja kwa nduguyo akakukidhia nawe ukampa zawadi na yeye akaikubali”.<sup>389</sup>

Masruuq alimuomba mtu haki yake kwa Ibn Ziyaad naye akamrudishia haki yake. Yule mtu akamtuma mtumishi wake ampelekee zawadi Masruuq lakini Masruuq alikataa na hakuikubali. Akasema: Nilimsikia Ibn Mas’ud anasema: “Mtu yoyote akimsaidia Muislam na Muislam huyo akamtunukia zawadi juu ya hilo iwe ndogo au kubwa, basi hiyo ni As Suhtu.’ Mtu huyo akasema: “Ewe Abu ‘Abdur Rahmaan, sisi tulikuwa tunadhania kuwa *suhti* ni rushwa katika hukumu peke yake.’ Masruuq akamjibu: “Hiyo ni kufuru” Tunajilinda kwa Allah kutokana nayo. na tunamuomba Allah msamaha na uzima katika balaa zote na machukizo.

---

<sup>387</sup> Dhafu: Imepokewa na Ibn Abi Shaybah 6/549, 587, At-Tabarani 2/94/1415 imedhoofishwa na Shaikh katika dhwaifu al-Jami’ 4687.

<sup>388</sup> Sahihi: imepokewa na Ahmad 5/261, Abu Dawud 3524 na sahihi Al-Jami’ 6316.

<sup>389</sup> Hassan: Imepokewa na Abdu Razzaq 8/147, 148, Al-Baihaqi katika Al-Kubra 10/139, 5116 katika Ash-Shi’b na watu wake ni madhubuti.

**KISA**

Kutoka kwa Imam Abu 'Umar Al-Awzai' aliyekuwa akikaa Beirut- kuwa wakati mmoja mkristo alikwenda kwake na kusema: Gavana wa Ba'alabak amenidhulumu, kwa hiyo nakuomba umuandikie kwa niaba yangu na akampa chungu la asali. Imam Awza'i alimwambia: Ikiwa unataka miye nipokee jagi hilo kama zawadi bila kukuandikia barua kwa Gavana, au ukitaka nitamuandikia barua Gavana lakini sitopokea jagi la asali na ulichukue mwenyewe. Imamu alimuandikia barua gavana huyo na kuomba awapunguzie kodi wakristo, mkristo huyo alichukua barua na jagi hilo la asali ambalo alilileta kama zawadi na akaondoka nalo. Baadaye alipopata barua ya Imam, Gavana wa Ba'alabak alipunguza kodi juu ya wakristo kwa kiwango cha dirham thelathini kwa ombi la kiongozi. Mwenyezi Mungu Amrehemu na atufufue katika kundi lake.

\*\*\*

## DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA TATU

### WANAWAKE KUJIFANANISHA NA WANAUME NA WANAUME KUJIFANANISHA NA WANAWAKE

Katika sahihi kumenakiliwa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

قال ابن عباس [-رضي الله عنهما-]<sup>(١)</sup>: «لعن رسول الله ﷺ  
المختئين من الرجال والمترجلات من النساء»<sup>(٢)</sup> صحيح<sup>(٣)</sup>.

*“Allah amewalaani wanawake wanaojifanisha na wanaume na  
wanaume wanaojifanisha na wanawake.” (Bukhari)<sup>390</sup>*

Katika ripoti nyingine amesema:

وعن النبي ﷺ قال: «لعن الله الرُّجُلَةَ من النساء»

*“Allah amemlaani mwanamke anayejifanya mwanaume.”<sup>391</sup>*

Katika riwaya nyingine Mtukufu Mtume ﷺ amesema:

*“Allah amewalaani wanaume wanaojifanya wanawake, na wanawake  
wanaojifanya wanaume.”<sup>392</sup>*

Yaani, wenye kujifanisha na wanaume katika kuvaa kwao na mazungumzo yao.

Na Abu Hurairah رضي الله عنه anatoa ripoti akisema:

وقال أبو هريرة [-رضي الله عنه-]<sup>(١)</sup>: «لعن رسول الله ﷺ الرجلَ  
يَلْبَسُ لِيْسَةَ المرأة، والمرأة تَلْبَسُ لِيْسَةَ الرَّجُلِ»

---

<sup>390</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 5885, 6834, At-Tirmidhi 2784, na Abu Dawud 4097.

<sup>391</sup> Sahihi: Imepokewa na Abu Dawud 4099 na sahihi Al-Jami' 5096.

<sup>392</sup> Imepokewa na Ahmad 1/252, 227, 254, Al-Bukhari 5886, At-Tirmidhi 2785.

## Al - Kabair

---

*"Allah amewalaani wanawake wanaovaa mavazi ya wanaume na wanaume wanaovaa mavazi ya wanawake."*<sup>393</sup>

Kwa hivyo endapo mwanamke akivaa nguo za kiume basi ajue analaaniwa na amepata laana ya Allah ﷻ na Mjumbe wake, na mume wake akimwezesha hilo yaani anamridhia na hamkatazi kwani yeye ameamriwa kumnyoosha juu ya kumtii Allah na kumkataza kumuasi, kwa kauli ya Allah ﷻ

قُوا أَنْفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ

***"Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe..." (66:6)***

Yaani watieni adabu na wafundisheni na waamrisheni utii wa Allah na wakatazeni dhidi ya kumuasi Allah kama hilo linavyopasa juu yenu, katika haki za nafsi zenu, na kauli ya Mtume ﷺ:

*"Kila mmoja wenu ni mchungu na kila mmoja wenu ni mwenye kuulizwa anachokichunga, mwanamume ni mchungaji na ni mwenye kuulizwa kuhusu wao siku ya kiama"*<sup>394</sup>

Imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

« أَلَا هَلَكْتَ الرِّجَالُ حِينَ أَطَاعُوا النِّسَاءَ »

*"Wanaume wameangamia pindi wanapowatii wanawake"*<sup>395</sup>

---

<sup>393</sup> Imepokewa na Ahmad 2/327, Abu Dawud 4097, Ibn Majah 3903

<sup>394</sup> Sahihi: Al-Bukhari 5188 na Muslim 1829.

<sup>395</sup> Dhaifu: Imepokewa na Al-Hakam 4/291, At-Tabarani katika Al-Awsat 427, imedhoofishwa na Shaikh katika silsila Adh-Dhwaifa 436 na dhaif al-Jami 6110 na imekuwa sahihi kwa tamshi 'Hawatofaulu watu wanaomilikiwa na mwanamke.' Imepokewa na Al-Bukhari 4427 na At-Tirmidhi 2262.

## Al - Kabair

---

Al-Hasan amesema: Wallahi hakuna siku yoyote mwanamume amemtii mkewe katika anayoyatamani isipokuwa Allah Aliyetukuka atamzamisha ndani ya moto. Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« صنفان من أهل النار لم أرهما . قوم معهم سياط كأذناب البقر يضربون بها الناس ، ونساء كاسيات عاريات مائلات رؤوسهن كأسنمة البخت المائلة لا يدخلن الجنة ولا يجدن ريحها، وإن ريحها ليوجد من مسيرة كذا وكذا»

*“Aina mbili (za watu) ni katika watu wa motoni ambao sikuwahi kuwaona. Watu wenye mijeledi kama mikia ya ng’ombe, wanawapiga nayo watu, na wanawake ambao japokuwa wamevaa nguo lakini wako uchi, wanawashawishi na mung’ao wa nywele zao ni kama nundu za ngamia. Hao hawataingia peponi wala hawatapa harufu yake, na hakika harufu yake (pepo) inapatikana kwa masafa kadha wa kadha.”<sup>396</sup> Imepokewa na Muslim.*

Ama kauli ya: *“ Na wanawake ambao japokuwa wamevaa nguo”* yaani katika neema za Allah, waliokuwa uchi, yaani ambao hawashukuru, imesemwa japo wanawake hao wamevaa lakini wako uchi, kwani nguo zao zinaonyesha ndani na rangi ya ngozi zao. Amefananisha muundo wa nywele zao sawa na nundu iliyoinama ya ngamia ya aina ya ‘Bagtrian’ ambao wana nundu mbili kubwa, kwani hutengeza nywele zao kama sega la nyuki kimuundo na kuzikoza kwa kilemba au mfano wake.

Naafi amesema: Ibn ‘Umar alikuwa na Abdullahi bin Amri kutoka kwa Zubair bin ‘Abdul Mutwalib pindi alipotokea mwanamke anaswaga mbuzi amebeba upinde. Ibn ‘Umar akamuuliza wewe ni mwanamke au mwanamume? Akasema: Mwanamke. Akamgeukia Ibn ‘Amri akasema: “Allah amewalaani juu ya ulimi wa Mtume wake ﷺ wenye kujifananisha na wanaume katika wanawake na wanaume wenye kujifananisha na wanawake”.

---

<sup>396</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 2128 na Ahmad 2/356, 440.

## Al - Kabair

---

Miongoni mwa matendo ambayo mwanamke analaaniwa kudhihirisha mapambo kama vile dhahabu na lulu kutoka ndani ya nikabu, na kujitia kwake manukato ya miski na ambari na manukato mengine anapotoka, na kuvaa hariri na nguo zenye kuonesha ndani na kurefusha nguo na kupanua mikono ya kanzu na kurefusha na mengine anapotoka.

Yote hayo ni katika kwenda uchi ambako Allah anamkasirikia mfanyaji wake na anamkasirikia katika dunia na akhera, matendo haya ambayo yamekuwa mengi kwa wanawake. Mtume ﷺ amesema kuhusu wao:

*“Nilichungulia motoni nikaona wakazi wake wengi ni wanawake”.*<sup>397</sup>

Mjumbe wa Allah ﷻ akasema:

*“Sijaacha baada yangu fitina ambayo ni madhara zaidi juu ya wanaume kuliko wanawake”.*<sup>398</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 5096 na Muslim 2740.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Atuepueshe na fitna zao na watengamae pamoja nasi kwa neema na ukarimu wake.

\*\*\*

---

<sup>397</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 5198 na Muslim 2737.

<sup>398</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 5096 na Muslim 2740.

DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA NNE

DAYYUTH MWENYE KUFURAHIA MATENDO YA MKEWE NA  
KUWADI MWENYE KUPITA BAINA YA WATU  
WAWILI KWA AJILI YA KU HARIBU

Allah تعالیٰ Aliyetukuka Anasema:

الزَّانِي لَا يَنْكِحُ إِلَّا زَانِيَةً أَوْ مُشْرِكَةً وَالزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ أَوْ مُشْرِكٌ وَحُرْمٌ ذَلِكَ  
عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

***"Mwanamume mzinifu hamwoi ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina. Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mshirikina. Na hayo yameharimishwa kwa Waumini."*** (24:3)

Kutoka kwa 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما anaripoti kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema kuwa:

«ثلاثة لا يدخلون الجنة: العاق والديه، والدُّيُوثُ، ورجُلَةُ النساءِ»

*"Watu wa aina tatu hawatoingia peponi, mwenye kuwaasi wazazi wake, na Dayyuthi ambaye anakiri uchafu katika familia yake na mwanamke anayejifananisha na mwanamume".*<sup>399</sup>

Kutoka kwa An-Nasai kuwa Mtume ﷺ amesema:

*"Watatu Mwenyezi Mungu amewaharamishia pepo: Mnywa pombe, Mwenye kuwakata wazazi wake na Dayyuthi ambaye anakiri uchafu katika familia yake."*<sup>400</sup>

---

<sup>399</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/79, 128, Al-Hakim 1/72, Al-Baihaqi 10/226 na imesahihishwa na Shaikh Albani katika sahihi Al-Jami' 3052.

<sup>400</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/134, An-Nasai 5/80, At-Tabarani 13180 na kusahihishwa na Shaykh katika sahihi Al-Jami' 3063 na angalia Hadithi namba 3062.



## **Al - Kabair**

---

---

Yaani ambaye anaona ni mazuri machafu ya mkewe. Allah atuhifadhi na hilo.

Mwandishi amesema: Mwenye kudhania uchafu kwa mkewe naye akajighafilisha nao kwa mahaba yake, na kuwa yeye ana deni haliwezi, au ana mahari kubwa au ana watoto wadogo kwa hiyo mwanamke akampeleka kwa kadhi na akataka matumizi yao, na yeye hawezi kulitimiza hilo. Wala hakuna kheri katika asiyekuwa na wivu.

Tunamuomba Allah uzima katika balaa zote na mitihani hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu.

\*\*\*

**DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA TANO**  
**(MUHALILI NA MUHALLALU LAHU)**  
**MWENYE KUMUOA MWANAMKE ALIYEACHWA**  
**KWA AJILI YA KUMHALALISHA KWA MUME**  
**WAKE WA KWANZA**

Ibn Mas'ud anatoa taarifa kuwa Mtume wa Allah ﷺ amesema:

صَحَّحَ مِنْ حَدِيثِ ابْنِ مَسْعُودٍ - رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ - : «أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ  
لَعَنَ الْمُحَلِّلَ وَالْمُحَلَّلَ لَهُ»<sup>(41)</sup> رَوَاهُ النَّسَائِيُّ وَالتِّرْمِذِيُّ.

*"Muhallil na muhallalahu wamelaaniwa".<sup>401</sup>*

Ibn Abbaas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ anatoa taarifa kuwa wakati Mtukufu Mtume ﷺ alipoulizwa kuhusu *Muhallil* akajibu:

*"Hapana, bali ndoa ni utashi, na si udanganyifu, wala isitihizai kwa kitabu cha Allah `Azza wa Jalla, mpaka aonje asali yake".<sup>402</sup>*

Ameipokea Abu Ishaq Jawzjaani kutoka kwa 'Uqba bin 'Aamir anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*"Nikuambieni kuhusu beberu lililoazimwa?".*

Wasikilizaji walimjibu, 'Ndio ewe Mjumbe wa Allah', Yeye akasema:

«هو المحلل ، لعن الله المحلل والمحلل له»

---

<sup>401</sup> Sahihi: Imepokewa na An-Nasai 2/98, Ahmad 1/448, Al-Baihaqi 7/208 na kusahihishwa na Shaikh Albani katika Al-Irwaa 1897.

<sup>402</sup> Dhwaifu: Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Kabiiir 11567 kwa sanad dhaifu na ipo sawa kwa tamshi iliyokaribiana na ya Al-Bukhari 5265, Muslim 1433.

## Al - Kabair

---

*"Huyo ni Muhallil, Allah Amemlaani Muhallil na Muhallal-lahu."*  
(Ameipokea Ibn Maajah kwa isnadi sahihi).<sup>403</sup>

Ibn 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَانَاtoa ripoti kuwa mtu alimuuliza: Unasemaje kuhusu mwanamke nimemuoa ili kumhalalisha kwa mumewe aliyemuacha, yeye hakuniomba wala hajui? Ibn 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَانAKamjibu "Hapana! Isipokuwa ndoa ya kupenda, akikuvutia utamshikilia na ukimchukia utamuacha, kwani sisi tulikuwa tunahesabu jambo hili katika zama za Mtume ﷺ kuwa ni uchafu".<sup>404</sup>

Uthram na Ibn Mundhir wanatoa taarifa kuwa 'Umar binil-Khattaab amesema: "Sikutani na *Muhallil* na *Muhallal-lahu* isipokuwa nitawapiga mawe"

Na alipoulizwa 'Umar binil Khattaab رَضِيَ اللهُ عَنْهُ kuhusu kumfanyia mwanamke *Tahallul* (kumhalalisha) kwa mumewe, akasema: "Huo ni uzinzi".<sup>405</sup>

Abdullah bin Shariik 'Amiri anatoa taarifa kuwa Ibn 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَانAliulizwa kutoa uamuzi kwa hali ifuatayo: "Mtu mmoja alimuacha binamu yake baadaye alisikitika kwa kufanya hivyo na akataka mtu mwingine kumrudia, kwa niaba yake. Ibn 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَانakasema: "Wote wawili watakuwa ni wazinifu, hata wakiwa wameishi pamoja kwa miaka ishirini, madamu yeye anajua kuwa alimuoa kwa ajili ya kumhalalisha kwa mumewe wa kwanza".<sup>406</sup>

Mtu mmoja alimwambia Ibn 'Abbaas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَانbinamu yangu, alimtaliki mkewe mara tatu akajuta sasa afanye nini? Ibn 'Abbaas akamjibu binamu

---

<sup>403</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Majah 1936, Al-Hakim 2/198, Al-Baihaqi 7/208 na kusahihishwa na Shaikh katika Al-Irwaa 6/309, 310.

<sup>404</sup> Sahihi: Imepokewa na At-Tabarani katika Al-Awsat 2/174 na kusahihishwa na Shaikh katika Al-Irwaa 1898.

<sup>405</sup> Sahihi: 'AbduRazzaq 10776, Ibn Abi Shaybah 4/294 kwa sanad sahihi.

<sup>406</sup> Sahihi: 'AbduRazzaq 10778

## Al - Kabair

---

yako amemuasi mola wake, hivyo anamjutisha na amemtii shetani na hakumpatia pakutokea, Mtu huyo tena akamuuliza wewe unasemaje kwa mwanamume anayefanya *Tahlil* kwa ajili yake?" Ibn 'Abbas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُم akamjibu: " Ambaye anamuhadaa Allah na yeye anamhadaa" .<sup>407</sup>

Ibrahim Nakhai amesema: "Ikiwa nia ya mmoja wa hao watatu, mume wa kwanza au mume wa mwisho au mke ni *Tahlil*, basi ndoa ya mwisho ni batili, wala haiwi halali kwa wa mwanzo" .<sup>408</sup>

Hassan Al-Basri amesema: "Mmoja wa watatu akidhamiria *Tahlil* ameharibu (ndoa)" .<sup>409</sup>

Saiid binil Musayyib Imamu wa taabiina amesema kuhusu mtu amemuoa mwanamke ili amhalalishe kwa ajili ya mumewe wa mwanzo, akasema: 'Hahalaliki" .<sup>410</sup>

Maalik bin Anas ni katika waliosema hivyo, na Laith bin S'ad, Sufyaan Thawri na Imam Ahmad bin Hanbal. Na Ismail bin Saiid amesema: nimemuuliza Imamu Ahmad kuhusu mtu anamuoa mwanamke na katika nafsi yake ana lengo la amhalalishe kwa mumewe wa mwanzo na mke hakujua hilo, akasema huyo ni *Muhallil* na anapotaka kwa hilo kuhalalisha basi yeye amelaaniwa. Na katika madhehebu ya Shafi: Anaposhurutisha *Tahlili* katika ndoa basi ndoa itabatilika, kwa vile ni sharti iliokatika kabla ya kukamilika kwake, kama vile ndoa ya mutaa. Ikipatikana sharti kabla ya ndoa basi ni sahihi. Na wakiifunga hivyo na wasiweke sharti kabla yake ndoa haitaharibika, na akimuoa kwa sharti kuwa akimfanyia *Tahlili* atampa talaka, kuna kauli mbili: Sahihi ni kuwa hiyo ni batili, na njia ya kubatilika kwake ni kuwa hiyo ni sharti inazuia kuswihi kwake kudumu ndoa kwa hiyo ikafanana na kuweka wakati. Rai hii ndio sahihi zaidi

---

<sup>407</sup> Sahihi: Imepokewa na 'AbduRazzaq 10779 na ameitaja Shaykh katika Al-Irwaa 1899.

<sup>408</sup> Imepokewa na Ibn Abi Shaybah 4/295 na Said bin Mansur 1994

<sup>409</sup> Imepokewa na Ibn Abi Shaybah 4/295 na Said bin Mansur 1995

<sup>410</sup> Imepokewa Said bin Mansur 1989

## **Al - Kabair**

---

---

kwa Raafi. Njia ya pili ni sharti lenye kuharibu iliounganika na kifungo haibatiliki kama vile lau atamuoa kwa sharti ya kutooa juu yake wala kusafiri nae. Allah ndie anayejua zaidi. Tunamuomba Allah Atuwafikishe katika Anayoridhia na kutuepusha Aliyotukataza, Yeye ni Mkarimu, Mkwasi na Mpole.

\*\*\*

**DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA SITA**  
**KUTOJILINDA NA MIKOJO NA HIYO NI**  
**ALAMA YA MANASARA**

Allah Aliyetukuka Amesema:

وَيُتَابِكُ فَطَهِّرْ ﴿٧٤﴾

**"Na nguo zako, zisafishe ". (74:4)**

Ibn 'Abbaas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا anasimulia kuwa Mtukufu Mtume ﷺ Alipofika kwenye makaburi mawili akasema:

وقال النبي ﷺ، ومر بقبرين: «إنهما يعذبان»<sup>(٤)</sup>، وما يعذبان في كبير<sup>(٥)</sup>؛ أمّا أحدهما: فكان لا يستتره<sup>(١)</sup> من بوله، وأمّا الآخر: فكان يمشي بالنميمة»

*"Hakika hao wanaadhibiwa, wala hawaadhibiwi katika jambo kubwa, mmoja wao alikuwa anatembea kwa kuchonganisha, ama mwingine alikuwa hajichungi dhidi ya mkojo." (Bukhari na Muslim)<sup>411</sup>  
Yaani: Alikuwa hajichungi na mkojo.*

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

وعن أنس -رضي الله عنه-، عن النبي ﷺ قال: «تَسْرَهُوا مِنَ الْبَوْلِ؛ فَإِنَّ عَامَّةَ عَذَابِ الْقَبْرِ مِنْهُ»<sup>(٤)</sup> رواه الدارقطني.

*"Jilindeni na (athari mabaki ya) mkojo (nguoni na mwilini mwako), Kwa sababu adhabu za kaburi ni kutokana nayo." (Daraqutni)<sup>412</sup>*

Kisha mtu ambaye hajichungi mwili wake na nguo zake kutokana na mkojo Swala yake haikubaliki.

---

<sup>411</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 1378, 352, 1361, Muslim 292, Abu Dawud 20

<sup>412</sup> Sahihi: Imepokewa na Ibn Aby Shay 2/44/1; Ibn Majah 348; Al-Hakim 1/183; Daraqtuny 1/128.

## Al- Kabair

---

Imepokewa na Hafidh Abu Nua'im katika kitabu Al-Hilyah kutoka kwa Shaqiy bin Mati' Al-Asbahi kutoka kwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema: "Watu wanne watawaudhi wakazi wa motoni, juu ya maudhi waliyokuwa nayo, wanakwenda baina ya maji yanayochemka na moto, na kulia kwa maumivu na mateso. Wakazi wa motoni watasemezana wenyewe: "Wana nini hao wanatuudhi juu ya mateso yetu tunayopata?" Akasema: "Mtu ambaye juu yake kuna sanduku la kaa la moto, na mtu anakokota matumbo yake, mtu ambaye mdomoni mwake kuna chirizika usaha na damu, na mtu anayekula nyama yake. Mwenye sanduku ataulizwa, 'Ana nini hadi anatuudhi juu ya maudhi tulio nayo.' Atasema: 'Mtu huyo alikufa na mizigo ya mali za watu shingoni mwake.' Kisha atamwambia ambaye anakokota matumbo yake, 'Ana nini hadi anatuudhi juu ya maudhi tulio nayo.' Atasema: 'Hakika huyo alikuwa hajali kupatwa na mkojo (wala hauoshi).' Kisha ataambiwa ambaye mdomoni mwake kunachiririka usaha na damu, 'Ana nini hadi anatuudhi juu ya maudhi tulio nayo.' Kutasemwa: 'Huyo alikuwa anaangalia kila neno baya na analifurahia".

Na katika riwaya nyingine: "Alikuwa anakula nyama za watu na anatembea kwa lengo la kuchonganisha watu.' Kisha ataambiwa ambaye anakula nyama yake, 'Ana nini anatuudhi juu ya maudhi tuliokuwa nayo.' Atasema: "Hakika alikuwa anakula nyama za watu, yaani kusengenya".<sup>413</sup>

Tunamuomba Allah msamaha na uzima kwa Wema Wake na Ukarimu Wake hakika Yeye ni Mrehemevu wa wenye kurehemu.

\*\*\*

---

<sup>413</sup> Dhaifu: Imepokewa na Ibn Abi Dunya katika Mlango wa Ghiyba 49; al-Haythamiy 186; Abu Na'im 5/ 167; na Attabarany fyl Kabiir 7226

## DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA SABA

### KUJIONYESHA - RIYA

Allah Aliyetukuka Anasema kuhusu wanafiki:

يُرَاءُونَ النَّاسَ وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّهَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٤١٢﴾

**"...wanajionyesha kwa watu tu, wala hawamdhukuru Mwenyezi Mungu ila kidogo tu." (4:142)**

Allah Aliyetukuka Amesema tena:

فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ ﴿٤١٣﴾ الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٤١٤﴾ الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ﴿٤١٥﴾  
وَيَمْتَعُونَ الْمَاعُونَ ﴿٤١٦﴾

**"Basi, ole wao wanao swali, Ambao wanapuuza Swala zao; wanajionyesha, na huku wanazuia msaada." (107:4-7). Na,**

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَبْطُلُوا صَدَقَاتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَى كَالَّذِي يُنفِقُ مَالَهُ رِثَاءَ النَّاسِ

**"Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi, kama anaye toa mali yake kwa kuwaonyesha watu..." (2:264)**

Kadhalika katika Surat Al-Kahf:

فَمَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا ﴿١١٠﴾

**"Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi." (18:110)**



Yaani hajioneshi kwa matendo yake.

Abu Huraira رضي الله عنه anatoa taarifa kwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

وقال النبي ﷺ: «أَوَّلُ النَّاسِ يُقْضَىٰ عَلَيْهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ: رَجُلٌ اسْتَشْهَدَ، فَأُتِيَ بِهِ، فَعَرَّفَهُ اللَّهُ نِعْمَتَهُ، فَعَرَفَهَا، فَقَالَ: مَا عَمَلْتُ فِيهَا؟ قَالَ: قَاتَلْتُ فِيكَ حَتَّى اسْتَشْهَدْتُ، قَالَ: كَذَبْتَ، وَلَكِنَّكَ قَاتَلْتَ لِيُقَالَ: جَرِيءٌ، فَقَدْ قِيلَ، قَم، ثُمَّ أُمِرَ بِهِ فَسُحِبَ عَلَىٰ وَجْهِهِ حَتَّى أُلْقِيَ فِي النَّارِ.

ورجل تعلم العلم وعلمه، وقرأ القرآن، فأُتِيَ بِهِ، فَعَرَّفَهُ اللَّهُ نِعْمَتَهُ، فَعَرَفَهَا، قَالَ: فَمَا عَمَلْتُ فِيهَا؟ قَالَ: تَعَلَّمْتُ الْعِلْمَ وَعَلَّمْتُهُ، وَقَرَأْتُ فِيكَ الْقُرْآنَ، قَالَ: كَذَبْتَ، وَلَكِنَّكَ تَعَلَّمْتَ<sup>(١)</sup> لِيُقَالَ: عَالِمٌ، وَقَرَأْتَ الْقُرْآنَ لِيُقَالَ: قَارِئٌ، فَقَدْ قِيلَ<sup>(٢)</sup>، قِيلَ، ثُمَّ أُمِرَ بِهِ فَسُحِبَ عَلَىٰ وَجْهِهِ حَتَّى أُلْقِيَ فِي النَّارِ.

ورجلٌ وسَّعَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَأَعْطَاهُ مِنْ أَصْنَافِ الْمَالِ، فَأُتِيَ بِهِ، فَعَرَّفَهُ نِعْمَتَهُ، فَعَرَفَهَا، فَقَالَ: مَا عَمَلْتُ فِيهَا؟ قَالَ: مَا تَرَكْتُ مِنْ سَبِيلٍ تُحِبُّ أَنْ يُنْفَقَ فِيهِ إِلَّا أَنْفَقْتُ فِيهِ لَكَ، قَالَ: كَذَبْتَ، وَلَكِنَّكَ<sup>(٣)</sup> فَعَلْتَ لِيُقَالَ: هُوَ جَوَادٌ، فَقَدْ قِيلَ، ثُمَّ أُمِرَ بِهِ فَسُحِبَ عَلَىٰ وَجْهِهِ حَتَّى أُلْقِيَ فِي النَّارِ<sup>(٤)</sup> رواه مسلم<sup>(٥)</sup>.

*“Hakika mtu wa kwanza kuhukumiwa siku ya kiama ni mtu aliyekufa Shahidi katika njia ya Allah. Yeye ataletwa. Allah atamkumbusha neema yake atajua, Atamuuliza, “Ulifanya nini ndani yake?” Atasema: ‘Nilipigana ndani yake hadi nikafa shahidi.’ Atamwambia: ‘Umedanganya bali ulipigana ili isemwe yu shujaa, na imesemwa.’ Kisha itaamriwa ataburuzwa juu ya uso wake na kutupwa motoni. na mtu Allah amempa aina za mali. Allah atamkumbusha neema yake atajua, Atamuuliza: “Ulifanya nini ndani yake?” Atasema: “Sikuacha njia yoyote unayopenda itolewe isipokuwa nilitoa ndani yake kwa ajili yako.’ Atasema: ‘Umedanganya bali ulifanya hivyo ili isemwe umkarimu na imesemwa. Kisha itaamriwa ataburuzwa juu ya uso wake na kutupwa motoni. Aliyefunza elimu na akaisomesha, kisha akasoma Qur’an na akaisomesha kwa hiyo ataletwa nayo atajua*

## Al - Kabair

---

neema yake na atamkumbusha yeye fadhila zake. Atamuuliza: "Umefanya nini ndani yake." Atajibu: "Nimejifunza elimu na nimeisomesha na nimesoma Qur'an kwa ajili yako." Atasema: 'Muongo bali umefanya hivyo ili isemwe u msomi, na imesemwa.' Kisha itaamriwa ataburuzwa juu ya uso wake na kutupwa motoni" (Imepokewa na Muslim 1905)

Katika riwaya nyingine: Mtukufu Mtume ﷺ amesema:

وقال النبي ﷺ: «مَنْ سَمِعَ سَمْعَ اللَّهِ بِهِ، وَمَنْ يُرَائِي يُرَائِي اللَّهَ بِهِ»  
متفق عليه.

"Mwenye kujisikizisha (kufanya ili asikike) Allah atamsikizisha, na mwenye kujionesha Allah atamuonesha." (Bukhari na Muslim)

Al-Khattabi amesema: "Maana yake: Mwenye kufanya matendo bila ikhlasi isipokuwa kujionesha kwa watu kwa ajili ya sifa na umaarufu, basi yatafichuka aliyokuwa akiyaficha". Wallaahu A`alam

Mtume ﷺ amesema:

وعن معاذ [-رضي الله عنه-] <sup>(٢)</sup>، عن النبي ﷺ قال: «اليسيرُ من  
الرِّياءِ شركٌ» <sup>(٣)</sup> صححه الحاكم.

"Kidogo kinachotokana na Ria ni shirki." (Hakim).<sup>414</sup>

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

"Khofu kubwa ninayokuhofieni nyie ni shirki ndogo".

Kukasemwa: 'Ewe mjumbe wa Allah nini hiyo?' Mtume ﷻ alijibu,

---

<sup>414</sup> Rejea hapo nyuma.

## Al - Kabair

---

« الرياء . يقول الله تعالى يوم يجازى العباد بأعمالهم : اذهبوا إلى الذين كنتم ترءونهم بأعمالكم فانظروا هل تجدون عندهم جزاء؟ »

*“Ria, ni siku ambayo Allah Mtukuka atawalipa watu matendo yao, atawaambia nendeni kwa wale ambao mlilionyesha kwao matendo yenu, basi angalieni mtapata kwao chochote?”<sup>415</sup>*

Na imesemwa kuhusu Kauli Yake Allah Mtukufu:

وَبَدَأَ هُمْ مِنْ اللَّهِ مَا لَمْ يَكُونُوا يَحْتَسِبُونَ ﴿٤٧﴾

**“...Na yatawadhihirikia kwa Mwenyezi Mungu wasiyo kuwa wakiyatarajia.” (39:47)**

Inasemekana kuwa walikuwa wakifanya matendo wakiyaona katika dunia kuwa ni mazuri lakini siku ya kiama yataonekana kuwa ni mabaya. Baadhi ya *Salaf* walipokuwa wakisoma aya hii walisema:

**“Ole wenu nyinyi watu mnaotenda matendo mema kwa kujionesha.”**

Na ikasemwa hakika mwenye kujionesha huitwa siku ya kiama kwa majina manne: ‘Ewe mwenye kupenda kujionesha, ewe mdanganyifu, ewe muovu, ewe mwenye hasara nenda ukachukue zawadi yako kwao hao uliowafanyia kazi hiyo na matendo hayo, huna ujira kwetu.’

Al-Hasan amesema: Yule anayependa kujionesha na akaficha maovu yake mwenyewe binafsi na akataka watu wamuamini kuwa yeye ni mtu mzuri mwema, lakini vipi watu watamfikiria wakati atawekwa mbele ya bwana wake kati ya wale watakaogharikishwa?. Hakika nyoyo za waumini watamtambua huyo mtu kwa hali hiyo aliyonayo.

---

<sup>415</sup> Rejea hapo nyuma.

## Al - Kabair

---

Qatadah alisema: "Mtu akifanya ria Allah Anasema: angalieni ni namna gani mja wangu ananikejeli."

Imesimuliwa kuwa 'Umar ibn Khattab' رضي الله عنه alimuona mtu anayetembea na huku ameinamisha kichwa chake: "'Umar akamwambia: "Nyanyua kichwa chako ewe mtu! Unyenyekevu au unyonge wa mtu haupo shingoni bali upo moyoni?."

Inasemekana kuwa Abu Umamah Al-Bahili رضي الله عنه alikwenda msikitini na akamuona mtu katika sijda akilia kwa kwikwi huku akimuomba Allah تعالى, Abu Umamah alimwambia yule mtu: 'Wewe! wewe, ikikubidi kufanya hivyo basi fanya nyumbani kwako!'

Muhammad bin Mubarak As-Swauri aliongeza: ni bora zaidi kutekeleza aina hizo za ukweli wa dini muda wa usiku kuliko mchana, kuonesha vitendo kama hivyo mchana ni kwa ajili ya kiumbe lakini vikitendwa usiku ni kwa ajili ya bwana wa dunia.

Ali bin Abu Talib رضي الله عنه alisema: "Zipo dalili tatu za kujionesha? Mtu huwa mvivu akiwa peke yake, lakini anapochanganyika na watu hufanya kazi, na akisifiwa huzidisha kazi hiyo na akilaumiwa hupunguza."

Fudhail bin 'Iyyadh رحمه الله تعالى alisema: "Kujizuia kufanya jambo kwa ajili ya watu ni *Riya* (kujionesha) na kufanya kitu au jambo kwa ajili ya kukubalika na watu ni shirki (kumshirikisha Allah تعالى) na wakati ukweli ni kuomba ulinzi kutoka kwa Allah تعالى juu ya yote mawili."

Sisi tunamuomba Allah تعالى Atupe msaada na utakasifu katika matendo, maneno, mienendo na mapumziko, hakika Yeye تعالى ni Mpaji Mkarimu.

\*\*\*

**DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA NANE**

**KUJIFUNZA ELIMU YA DINI KWA AJILI YA DUNIA NA  
KUIFICHA ELIMU HIYO**

Allah Mtukuka Anasema:

إِنَّمَا نَحْنُ لِلَّهِ مِن عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ

**"...Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni  
mwa waja wake ni wanazuoni..." (35:28)**

Yaani wanaomjua Allah Mtukuka. 'Abdulla Bin 'Abbas amesema: Maana yake: (Allah amesema), "Wanaonihofu katika viumbe Wangu ni kwa kujua Kudra Zangu na kuwa Mimi Ndiye Allah Pekee, Utukufu Wangu na Milki Yangu.' Mujahid na Sha`abi wamesema: "Mwanazuoni ni ambaye anamuogopa Allah'. Rabii bin Anas amesema: 'Asiye muogopa Allah si mwanazuoni'. Allah Mtukuka Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنزَلْنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَأَهْدَىٰ مِنْ بَعْدِ مَا بَيَّنَّاهُ لِلنَّاسِ فِي الْكِتَابِ  
أُولَٰئِكَ يَلْعَنُهُمُ اللَّهُ وَيَلْعَنُهُمُ اللَّعْنُونَ ﴿٢٥٩﴾

**" Hakika wale wanao ficha Tuliyo yateremsha -nazo ni hoja  
zilizo wazi na uwongofu baada ya Sisi kuzibainisha kwa  
watu Kitabuni - hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na  
wanawalaani kila wenye kulaani." (2:159)**

Aya hii imeteremka kuhusu wanazuoni wa kiyahudi, na makusudio ya aya:

الْبَيِّنَاتِ ،

**" zilizo wazi"**

Ar Rajm (kupigwa mawe), Adhabu (huduud) na hukumu.

وَأَهْدَى

"na uwongofu"

Yaani suala la Muhammad, na sifa zake,

مِنْ بَعْدِ مَا بَيْنَهُ لِلنَّاسِ

"..baada ya Sisi kuzibainisha kwa watu.."

Yaani: Wana wa Israili

فِي الْكِتَابِ

"..ndani ya kitabu.."

yaani ndani ya Taurati.

أُولَئِكَ

"..Hao.."

Yaani: ambao wanaficha

أُولَئِكَ يَلْعَنُهُمُ اللَّهُ وَيَلْعَنُهُمُ اللَّعِنُونَ ﴿١٦١﴾

"..hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani kila wenye kulaani".

Ibn Abbaas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا amesema: kila kitu kisicho majini na binadamu. Ibn Masuud amesema: 'Waislamu wawili hawalaaniani isipokuwa laana hiyo hurudi kwa mayahudi na wakristo ambao wameficha habari za Mtume ﷺ na sifa zake.'

Allah Mtukuka Anasema:

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْفُرُونَهُ فَبَدُوهُ وَرَاءَ

ظُهُورِهِمْ وَأَشْرَوْا بِهِم مِمَّا قَلِيلًا فَبُئْسَ مَا يَشْتَرُونَ ﴿١٦٢﴾

**"Na pale Mwenyezi Mungu alipo fungamana na walio pewa Kitabu kuwa: Lazima mtawabainishia watu, wala hamtokificha, walikitupa nyuma ya migongo yao, na wakanunua kwacho thamani duni. Basi ni kiovu hicho walicho nunua." (3:187).**

Al-Wahidi amesema: "Aya hii iliteremshwa kuhusu mayahudi wa Madina, Allah alichukua ahadi kwao katika Taurati kuwa watawabainishia watu habari ya Muhammad ﷺ, tabia zake, utume wake, wala hawataificha, na hiyo Kauli Yake Taalaa:

لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ

**"Lazima mtawabainishia watu, wala hamtokificha"**

Al-Hassan anasema: 'Hii ni ahadi ya Allah kwa wanazuoni wa kiyahudi kuwa watawabainishia watu katika vitabu vyao, na ndani yake kuna utajo wa Mtume ﷺ. " Na Kauli Yake: **'Walikitupa nyuma ya migongo yao'**

Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: Yaani: 'Ahadi hiyo wakaitupa nyuma ya migongo yao.'

وَأَشْتَرُوا بِهِ مِمَّا قَلِيلًا

**'Na wakanunua kwacho thamani duni'**

Yaani: 'Walivyokuwa wanavichukua kwenye biashara zao kwa ukubwa wao katika elimu." Na Kauli Yake:

فَبِئْسَ مَا يَشْتَرُونَ

**'Basi ni kiovu hicho walicho nunua'**

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema: 'Kumekuwa kuovu kununua kwao, kumekuwa kuovu na wamepata khasara. Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

## Al - Kabair

---

وقال النبي ﷺ: «مَنْ تَعَلَّمَ عِلْمًا مِمَّا يُبْتَغَى بِهِ وَجْهُ اللَّهِ، لَا يَتَعَلَّمُهُ إِلَّا لِيَصِيبَ بِهِ عَرَضًا مِنَ الدُّنْيَا، لَمْ يَجِدْ عَرَفَ الْجَنَّةَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»<sup>(٥)</sup>؛ يعني: ربحها. رواه أبو داود بإسناد صحيح.

*“Mwenye kujifunza elimu katika ambayo inatafutwa kutokana nayo kumridhisha Mwenyezi Mungu, hajifundishi isipokuwa apate nayo mapato ya duniani basi mtu huyo hatopata harufu ya pepo”.*  
Imepokewa na Abu Dawud<sup>416</sup>

Hadithi ya Abu Huraira رضي الله عنه imetangulia kuhusu watu watatu wanaoburuzwa motoni, mmoja wao ni anayeambiwa:

إنما تعلمت ليقال: عالمٌ، وقد قيل

*“Umejifunza elimu ili isemwe u-msomi, na imesemwa”.*<sup>417</sup>

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

«مَنْ ابْتَغَى الْعِلْمَ لِيَاهِي بِهِ الْعُلَمَاءُ، أَوْ يُمَارِي بِهِ السُّفَهَاءَ، أَوْ تُقْبَلُ أَفْتِدَةُ النَّاسِ إِلَيْهِ فَإِلَى النَّارِ».

*“Mwenye kutafuta elimu ili kushindana nayo na wanazuoni, au ashindane na wajinga au kuvutia kwake nyoyo za watu basi huyo ni wa motoni.”*

Na katika riwaya:

وفي لفظ: «أَدْخَلَهُ اللَّهُ النَّارَ»<sup>(٣)</sup> أخرجه الترمذي، لكن إسحاق وإيه<sup>(٤)</sup>

*“Allah atamtia motoni”.* (Tirmidhi)<sup>418</sup>

---

<sup>416</sup> Imepokewa na Ahmad 2/338, Abu Dawud 3664, Ibn Majah 252 na kusahihishwa na Shaikh katika sahihi Al-Jami' 6159.

<sup>417</sup> Maelezo yake yametangulia.

<sup>418</sup> Sahihi: At-Tirmidhi 2654 na Sahihi Al-Jami' 5930



## Al - Kabair

---

Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

وقال النبي ﷺ: «مَنْ سَأَلَ عَنْ عِلْمٍ فَكَتَمَهُ، أَجْمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِلِجَامٍ مِنْ نَارٍ»<sup>(1)</sup> إسناده صحيح، رواه عطاء عن أبي هريرة.

*"Mwenye kuulizwa juu ya elimu na akaificha basi atatiwa lijamu ya moto siku ya kiyama."*<sup>419</sup>

Mtume ﷺ alikuwa anaomba dua:

«اللهم إني أعوذُ بك من علمٍ لا ينفع»

*"Najilinda dhidi ya elimu isionufaisha"*<sup>420</sup>

Mjumbe wa Allah ﷺ amesema

« من تعلم علما لم يعمل به لم يزد العلم إلا كبيرا »

*"Mwenye kujifunza elimu na asiitumie elimu haimtamzidishia isipokuwa kiburi"*.<sup>421</sup>

Abu Umamah anatoa taarifa kwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

«يجاء بالعالم السوء يوم القيامة فيسقى في النار فيدور بقضبه كما يدور الحمار بالرحا فيقال له : بما لقيت هذا وإنما اهتدينا بك فيقول : كنت أخالفكم إلى ما أنهاكم عنه»

---

<sup>419</sup> Sahihi: Abu Dawud 3658, At-Tirmidhi 2649, Ibn Majah 166 na kusahihishwa na Shaikh katika sahihi Al-Jami' 6284.

<sup>420</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 2722, An-Nasai 5551, Ibn Majah 250 na At-Tirmidhi 3482.

<sup>421</sup> Dhwaifu: Imepokewa kwa mfano huo na Ibn Majah 258 na kudhoofishwa na Shaikh katika Adh-Dhwaifa 5017.

## Al - Kabair

---

*“Ataletwa mwanazuoni muovu siku ya kiama na atavurumishwa motoni na atazunguka na kalamu yake kama punda anavyozunguka na jiwe la kusagia”, Ataulizwa, ‘Nini kimekusibu? Kwani sisi tumeongozwa nawe’, Yule bwana atasema: ‘Nilikuwa nikifanya kinyume cha ninayo kukatazeni’.*<sup>422</sup>

Hilal Ibn ‘Alaa amesema: Kutafua elimu ni kazi ngumu na kuihifadhi ni ngumu zaidi kuliko kuitafuta, na kusalimika nayo ni ngumu zaidi kuliko kuitumia. Tunamuomba Allah Atusalimishe dhidi ya kila matatizo na Atuwafikishe kwenye yanayo mpendeza. Hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu.

\*\*\*

---

<sup>422</sup> Dhwaifu: Imepokewa na Al-Asbahani katika At-Targhiib 2136 na sanadi yake ni dhaifu na maana yake yamekuja katika Al-Bukhari 3267 na Muslim 2989.

## DHAMBI KUBWA YA THELATHINI NA TISA

### KHIANA

Allah Amesema:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَخُونُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ وَتَخُونُوا أَمْنِيَّتِكُمْ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٧٧﴾

***“Enyi mlio amini! Msimfanyie khiana Mwenyezi Mungu na Mtume, wala msikhini amana zenu, nanyi mnajua.” (8:27)***

Al-Waahidi amesema: Ayah imeshuka kwa Abu Lubaabah pale Mtume ﷺ alipomtuma kwa Bani Quraydhah walipo wazingira, na watoto wake walikuwa katika wao, wakamwambia: ‘Ewe Abu Lubaabah! Unaonaje kama tukikubali hukumu ya Sa’ad kwa ajili yetu?’ Abu Lubaabah akawaashiria kwenye koo lake kuwa msifanye hivyo kwani hukumu yake ni kuchinjwa. Na hilo likawa ni kumkhini Allah na Mtume wake\*. Abu Lubaabah akasema: “Miguu yangu haikuondoka mahali pangu hadi nikajua kuwa mimi nimemkhini Allah na Mtume Wake” Na Kauli Yake,

وَتَخُونُوا أَمْنِيَّتِكُمْ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٧٧﴾

***“Na mnakhini amana zenu na hali mnajua”***

Ni muunganisho wa katazo la mwanzo, yaani: Wala msikhini amana zenu. Ibn Abbaas amesema: “Amana ni matendo ambayo Allah Amewaamini nayo waja”. Yaani faradhi. anasema: Msizipunguze. Kalbi amesema: Kumkhini Allah na Mtume wake ni kumuasi kwake. Khiana ya amana: kila mmoja ni mwaminiwa juu ya alichofaradhisha Allah juu yake, akitaka atayakhini na akitaka atayatekeleza hakuna yeyote aonae isipokuwa Allah Taalaa. Kauli Yake:

وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٧٧﴾

***“Na nyie mnajua”***

## Al - Kabair

---

Kuwa hiyo ni amana bila utata Allah Amesema:

﴿وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي كَيْدَ الْخَائِبِينَ﴾

**“Na kuwa Allah haongozi vitimbi vya wenye khiana.”**

Yaani: haongozi vitimbwi vya mwenye kukhini amana yake, anamfedhehesha mwishoni kwa kunyimwa uongofu.

Mtume ﷺ amesema:

وقال: «آيةُ المنافقِ ثلاثٌ: إذا حدثَ كذبَ، وإذا وعَدَ أخلفَ، وإذا اتَّبعَ خَانَ»<sup>(1)</sup>.

*“Alama za mnafiki ni tatu anapozungumza anadanganya, na anapoahidi anakhalifu, na anapo aminiwa anakhini.”<sup>423</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

لا إيمانَ لمن لا أمانةَ له، ولا دينَ لمن لا عهدَ له

*“Hakuna imani kwa asie na Imani, wala dini kwa asiye na ahadi.”<sup>424</sup>*

Khiana ni mbaya katika kila jambo na nyingine ni shari zaidi kuliko nyingine. Aliyekuhini si kama aliyekuhini katika mke wako, na akafanya dhambi kubwa.

Mtume ﷺ akasema:

*“Tekeleza amana kwa aliyekuamini wala usimkhini aliyekufanyia khiana.”<sup>425</sup>*

---

<sup>423</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>424</sup> Hasan: Ibn Abu Shaybah katika Al iiman 7 Al Muntaqaa 11/11

<sup>425</sup> Sahihi: Tirmidhi 1264 Al baani ameisahihisha katika As Swahiihah 4230 Ar-Rawdhun Nadhiir 16 265 Al-Mishkaat 2934

## Al - Kabair

---

Na katika hadithi pia;

*“Humtii Muumini kila kitu isipokuwa khiana na uongo.”<sup>426</sup>*

Mtume ﷺ amesema: Kuwa Allah anasema:

*“Mimi ni watatu katika washirika wawili madam mmoja wao hajamkhini mwenziwe”.<sup>427</sup>*

Na ndani yake pia kuna:

*“Cha kwanza kitakacho ondolewa kwa watu ni amana, na cha mwisho kitakachobakia ni Swala na huenda mwenye kuswali hana kheri ndani yake.”<sup>428</sup>*

Mtume ﷺ akasema:

*“Jihadharini na khiana kwani ni mshirika mbaya sana”<sup>429</sup>.*

Na Mtume ﷺ akasema:

*“Hivi ndivyo watu wa motoni, akataja mtu miongoni mwao ambaye hafichi tamaa japo ndogo isipokuwa atafanya khiana.”<sup>430a</sup>*

Ibn Mas’uud رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا amesema: “Ataletwa mwenye amana ambaye ameifanyia khiana na ataambiwa: ‘Tekeleza amana yako’, atasema: ‘Kivipi Ewe Mola wangu na dunia imeshaondoka?’, Itatengenezwa kama umbo

---

<sup>426</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>427</sup> Dhaifu: Abu Dawud 3383 Al Khatwiib katika At Taariikh 4/316 Al Baani ameidhoofisha katika Dhaiiful Jaami’i 1748

<sup>428</sup> Sahihi: Ameipokea Al Kharaaiti katika Makaarimil Akhlaaqi ukurasa 28 Abu Nuaim katika Al Hilyah 6/265 Shaykh ameisahihisha katika As Silsilah as Sahiihah 1739

<sup>429</sup> Sahihi: Abu Dawud 1548 An Nasaai 8/263 Ibn Maajah 3354 Shaykh ameifanya Hasan katika Swahihil Jaami’i 1283

<sup>430a</sup> Maelezo yake yametangulia

## **Al - Kabair**

---

---

lake la siku alipoichukua ilhali angali Jahannamu. Ataambiwa: "Teremka na nitoe'. Atateremka ataibeba kwenye shingo yake na ni nzito kuliko majabali ya duniani, mpaka anapodhania kuwa ameokoka anapomoka nayo tangu siku alipoichukua na yeye yuko juu ya athari yake milele na milele, kisha akasema' Swala ni amana, na udhu ni amana, kuosha ni amana, uzito amana, mizani ni amana. Na kubwa kuliko la hayo yote ni ahadi."

Ewe Mola amiliana nasi kwa Upole Wako na utudiriki sisi kwa Msamaha Wako.

\*\*\*

## DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI

### KUSIMANGA

Allah Taalaa Amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُبْطَلُوا صَدَقَاتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَى

***“Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi” (2:264)***

Al-Waahidi amesema: “Huko ni kusimanga kwa anachotoa”. Kalbi amesema: “Kwa kumsimanga Allah kwa sadaka yake, na kumuudhi mwenyewe”. Katika Sahihi ni kuwa Mtume ﷺ amesema:

وفي الحديث الصحيح: «ثلاثة لا يكلمهم الله، ولا ينظر إليهم يوم القيامة، ولا يزكيهم، ولهم عذاب أليم: المسبل إزاره، والمنان، والمنفق سلعته بالخلف الكاذب»<sup>(1)</sup>.

*“Watatu Allah hatawasemesha wala hatawaangalia Siku ya Kiama wala hatawatakasa na wao wana adhabu iumizayo: Mwenye kuburuza kikoi, mwenye kusimbulia na mwenye kutoa bidhaa yake kwa yamini ya uongo”<sup>430b</sup>*

‘(Al-Musbilu)’ mwenye kuburuza kikoi chake au suruali yake hadi kwenye nyayo zake, au kanzu yake kwani Mtume ﷺ amesema:

*“Kilicho chini ya fundo mbili za mguu kutokana na kikoi hicho ni motoni”<sup>431</sup>.*

Na katika hadithi nyingine:

---

<sup>430b</sup> Maelezo yake yametangulia

[عمر بن يزيد الشامي، عن أبي سلام<sup>(٤١)</sup>، عن أبي أمامة [الباهلي -رضي الله عنه-] قال: قال رسول الله ﷺ: «ثلاثة لا يقبل الله منهم صرفاً ولا عدلاً: عاق، ومنان، ومكذب بالقدر»<sup>(٤٢)</sup> [عمر: صويلح]<sup>(٤٣)</sup>.

*“Watatu hawaingii peponi: mwenye kugombana na wazazi wawili, na mwenye kudumu kunywa pombe na mwenye kusimanga”.  
Ameipokea An Nasaai<sup>432</sup>*

Hadaa ni hila na ulaghai, kusimanga ni kutoa kitu au anatoa sadaka kisha anaisimangia. Imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

*“Tahadharini na kusimanga kwa wema kwani kunabatilisha shukrani na kunafuta ujira.”<sup>433</sup>*

Kisha Mtume ﷺ akasoma kauli ya Allah Taalaa.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَبْطُلُوا صَدَقَتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَى

***“Enyi ambao mmeamini msibatilishe sadaka zenu kwa kusimanga na udhia”. (2:264)<sup>434</sup>***

Ibn Siirin alimsikia mtu anamwambia mwingine: “Nimekufanyia wema na nimekufanyia hiki na hiki”. Ibn Sirin akasema: “Nyamaza kwani hakuna kheri kwa wema unapohesabiwa”. Wengine walikuwa wakisema: “Mwenye kusimanga kwa mema, mema yake yanaanguka kutokana na kushukuriwa kwake, na mwenye kujiona kwa amali yake ujira wake huporomoka”. Shafii aliimba mashairi haya:

---

<sup>431</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>432</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>433</sup> Sijaiona kwa tamshi hili.

<sup>434</sup> Al-Baqarah (2:264)



**Al - Kabair**

---

---

*Usiwafanye watu wakusimange kwa wema.*

*Ichagulie nafsi yako hadhi yake.*

*Na subiri kwani kusubiri ni kinga.*

*Masimango ya watu nyoyoni ni makali zaidi kuliko michomo ya mshale*

Mwingine aliimba mashairi haya:

*Na swahibu ametanguliza (wema) mkononi (mwangu)*

*Malipo yangu yamechelewa kwake akanifanyia uadui*

*Alipoyakinisha kuwa dahari imenipiga*

*Alidhirisha majuto kwenye alivyo nitawalisha*

*Umeharibu kwa kusimanga wema uliutanguliza*

*Mkarimu anapopeana kamwe hawi msimangaji*

**\*\*\***

DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA MOJA

KUKANUSHA KUDURA

Allah Taalaa Amesema:

إِنَّا كُلُّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥٤﴾

**“Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo”(54:49)**

Ibnul –Jawzi anasema katika tafsiri yake: “Kuhusu sababu ya kushuka aya hii kuna kauli mbili: Mojawapo: Ni kuwa washirikina wa Makkah walimjia Mtume wa Allah ﷺ wakabishana naye katika kudura, ndipo ikashuka aya hii. Na Muslim peke yake aliiandika<sup>435</sup>.

Abu Umaamah amesema kuwa aya hii ni katika *Al-Qadiriyah*<sup>436</sup>. Na kauli ya pili kuwa Askofu wa Najraan alikuja kwa Mtume ﷺ akasema: “Ewe Muhammad unadai kuwa maasi ni kwa kadari, ilhali sivyo.’ Mtume ﷺ akasema: “Nyinyi ni watesi wa Allah?”.

Ikashuka aya hii:

إِنَّ الْمَجْرِمِينَ فِي ضَلَالٍ وَسُعُرٍ ﴿٥٧﴾ يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ ذُقُوا مَسًّا

سَقَرًا ﴿٥٨﴾ إِنَّا كُلُّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥٩﴾

**“Hakika wakosefu wamo katika upotofu na wazimu. Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu!, Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo”<sup>437</sup>. (54:47-49)**

---

<sup>435</sup> Sahihi: Ahmad 2/444 Muslim 9/2606

<sup>436</sup> Dhaifu: Ibn Adiy 5/38 Al Waahidi katika Asbaabun-Nuzuul 827 kutokana na njia ya Afiir bin Ma’adaan na yeye ni dhaifu. Al-Haythami amesema katika Al-Majma’ 7/26, imepokewa na At-Tabarani katika al-Awsat kutoka katika riwaya ya Baqiya naye ni Mudlis (si mkweli) Habii bin Muhammad na Majhul.

<sup>437</sup> Dhaifu: Al-Waahidi 828 na isinadi yake ni dhaifu

## Al - Kabair

---

Umar ibnil Khattwaab amepokea kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

« إذا جمع الله الأولين والآخرين يوم القيامة أمر مناديا فنادى نداء يسمعه الأولون والآخرون : أين خصماء الله ؟ فتقوم القدرية فيؤمر بهم إلى النار »

*"Allah Atakapowakusanya wa mwanzo na wa mwisho Siku ya kياما atamuamrisha mtangazaji atatangaza tangazo atakalolisikia wa mwanzo na wa mwisho: 'Wako wapi watesi wa Allah?', Watasimama Qadariya na wataamrisha kwenda motoni"*<sup>438</sup>.

Allah Anasema:

ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ ﴿٥٨﴾ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥٩﴾

***"Onjeni adhabu kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo"***.

Na wameitwa watesi wa Allah kwa vile wao wanabisha kuwa haifai kukadiria maasi kwa mja kisha amuadhibu kwa hayo.<sup>439</sup>

Hishaam bin Hassaan amepokea kutoka kwa Al-Hasan amesema: Wallahi lau Qadariya atafunga Saumu na akawa kama kamba, na akaswali akawa kama upinde Allah Atamtia motoni kwa uso wake, kisha ataambiwa:

ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ ﴿٥٨﴾ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥٩﴾

***"Onjeni mguso wa Jahannamu. Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo."***<sup>440</sup>

---

<sup>438</sup> Dhaifu: Ibn Abi Aaswim 336 Twabarani katika Al Aswat 6510 Al Bani ameidhoofisha katika Dhillalil Jannah

<sup>439</sup> Dhaifu: Twabarani katika Al Kabiir 11163 Al Haythami Aswat 6510 Al Bani ameidhoofisha katika Dhillalil Jannah

<sup>440</sup> Dhaifu: ibnul Jawzi katika Tafsiri yake 102 kwa isinadi ambayo ndani yake kuna udhaifu

## Al - Kabair

---

Muslim amepokea katika Sahihi yake kutokana na hadithi ya Ibn Umar, Mtume ﷺ amesema:

« كل شيء بقدر حتى العجز والكيس »

*“Kila kitu ni kwa kadari hadi uvivu na uwerevu”.*

Ibn Abbaas رضي الله عنهم amesema: “Kila kitu Tumekiumba kwa Qudura iliyoandikwa katika ubao uliohifadhiwa (*Allawhul-Mahfuudh*) kabla ya kutokea kwake”<sup>441</sup>.

Allah Ta’alaa Amesema:

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٣٧﴾

**“Na Allah Amekuumbeni na mnayoyafanya.” (37:96).**

Ibn Jariir amesema: Humo kuna njia mbili; Moja wapo: Allah Amekuumbeni na matendo yenu; na ya Pili: Allah Amekuumbeni na yale masanamu mnayoyaumba kwa mikono yenu. Na katika aya hii kuna dalili kuwa matendo ya waja yameumbwa. *Wallahu-A`alam.*

Allah Amesema:

**“Fa-alhamahaa fujuuraha wataqwaaha.”**

Ilhaam ni kutia kitu katika nafsi. Said ibin Jubayr amesema: Ameilazimisha uovu wake na wema wake. Ibn Zayd Amesema: Amelifanya hilo kwa Taufiki Yake kwa ajili ya ucha-Mungu na kutelekeza kwake kwa ajili ya uovu.” *Wallah A`alam.*

Katika hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ:

---

<sup>441a</sup> Sahihi, Ameipokea Al-Bukhaari katika ‘Khalqi af`aalil`ibaad’ uk: 26 kwa tamshi: “Kila kitu ni kwa kipimo hadi kuweka mkono wako juu ya shavu lako”..

« إن الله منَّ على قوم فألهمهم الخير فأدخلهم في رحمته ، وابتلى قوماً  
فخذلهم وذمهم على أفعالهم ولم يستطيعوا غير ما ابتلاهم فعذبهم  
وهو عادل »

*" Hakika Allah Amewatendea wema na Akawapa ilhaam ya kheri na Akawatia katika Rehema Yake, na Akawatahini watu Akawatelekeza (wengine) na Akawatia hatiani juu ya matendo na hawakuweza isipokuwa lile Alilowatahini nalo, kwa hiyo Atawaadhibu nalo na Yeye ni Muadilifu".*

لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ ﴿٦٦﴾

**"Haulizwi anayoyafanya na wao wanaulizwa."**<sup>441b</sup>

Mu'adh bin Jabal amesema, Mtume ﷺ amesema:

« ما بعث الله نبياً قط إلا وفي أمته قدرية ومرجئة، إن الله لعن القدرية والمرجئة  
على لسان سبعين نبياً »

*"Allah hakumtuma Mtume yeyote isipokuwa katika ummah wake kuna Qadariya na Murjiah, Hakika Allah Amewalani Qadariyah juu ya ndimi za mitume sabini"*.<sup>442</sup>

Imepokewa kutoka kwa Aisha amesema: Mtume ﷺ amesema:

« القدرية مجوس هذه الأمة »

**"Qadariyah ni Majusi wa ummah huu"**.<sup>443</sup>

Imepokewa kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما amesema: Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>441b</sup> (Dhaif: addaruqutny fyl Ifrad 2/64, na ameitaja al-baniy katika Dhaifa 1740, na katika Dhaifil jamii 1663)

<sup>442</sup> Dhaifu: Ibn Abi Aaswim 325, na Sheikh Al-Baani ameidhoofisha katika Dhililil-Jannah

## Al - Kabair

---

لكل أمة مجوس ومجوس هذه الأمة « الذين يزعمون أن لا قدر ،  
أن الأمر أنف . قال : فإذا لقيتهم فأخبرهم أنني منهم بريء وأنهم براء  
نبي »

*“Kila Ummah una majusi wake<sup>444</sup>, na majusi wa ummah huu ni watu  
wanaodai kuwa hakuna Qadari na kuwa amri ni lazima, na unapokutana  
nao waambieni mimi niko mbali nao na wao wako mbali nami”.*

Kisha akasema:

« والذي نفسي بيده لو أن لأحدهم مثل أحد ذهباً فأنفقه في سبيل الله ما  
قبل حتى يؤمن بالقدر خيره وشره »

*“Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake lau mmoja  
wao atakuwa na dhahabu kama mlima Uhud na akaitoa katika njia  
ya Allah hatakubaliwa hadi aamini kadari - kheri yake na shari yake”.*

Kisha akataja hadithi ya Jibrili na maswali yake kwa Mtume ﷺ Aliuliza:  
‘Ni nini Imani?’ Akamjibu:

« قال : ما الإيمان ؟ قال : أن تؤمن بالله وملائكته وكتبه ورسله وتؤمن بالقدر  
خيره وشره » .

*“Umwamini Allah na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Mitume  
Wake na uamini Qadari - kheri yake na shari yake.”<sup>445</sup>*

Kauli yake:

« أن تؤمن بالله »

*“Umwamini Allah”.*

---

<sup>443</sup> Hasan: Abu Dawud 4691 Ibn Abu Aaswim 338,339,34,231 Al-Baani ameifanya Hasan katika Swahihil Jaamii 4442

<sup>444</sup> Hasan: Abu Dawud 4691, 4695, Attirmidhy 2738, Swahihil Jaamii 5163, na Al-Mishkaat 107

<sup>445</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 8.

## Al - Kabair

---

Kumuamini Allah ni mtu kuswadikisha kuwa Yeye تعالى Yupo, Mwenye kusifika kwa Utukufu na Ukamilifu. Ametakasika na sifa za upungufu, na kuwa Yeye ni Peke Yake, Mtegemewa, na Muumbaji wa viumbe wote, Mwenye Kupanga Atakacho na Anafanya Atakacho katika Ufalme Wake.

Na mtu kuamini Malaika ni kuswadikisha uja wao kwa Allah.

بَلْ عِبَادٌ مُّكْرَمُونَ ﴿٢٦﴾ لَا يَسْبِقُونَهُ بِالْقَوْلِ وَهُمْ بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾  
يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ أَرْتَضَىٰ وَهُمْ مِنَ  
خَشْيَتِهِ مُشْفِقُونَ ﴿٢٨﴾

***“Bali hao (wanao waita wana) ni watumwa walio tukuzwa. awamtangulii kwa neno, nao wanafanya Amri Zake. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala hawamwombei yeyote ila yule anaye mridhia Yeye, nao kwa ajili ya kumwogopa wananyenyekea”. (21:26-28)***

Na Mtu kuamini Mitume ﷺ ni kuamini kuwa wao ni wa kweli katika waliyoeleza kutoka kwa Allah Taalaa. Allah Amewatia nguvu kwa miujiza yenye kuonyesha ukweli wao, na kuwa wao wamefikisha ujumbe katika ujumbe Wake na wamewabainishia wenye kukalifishwa na sheria. Na kuwa inapasa kuwaheshimu na kutotofautisha yeyote miongoni mwao.

Kuamini siku ya mwisho ni kusadikisha Siku ya Kiama na iliyoyakusanya kama vile kurejea baada ya mauti, kufufuliwa, kukusanywa, hesabu, mizani, njia, pepo na moto na kuwa hizi mbili ni Nyumba za thawabu yake na adhabu yake kwa wema na waovu na yasiokuwa hayo miongoni mwa nukuu zilizoswihi. Na kuamini Qadari: Ni kuamini yale yaliotangulia kutajwa, na matokeo yake ni kile kilichoonyeshwa.

Na kauli Yake Taalaa:

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٣٦﴾

**“Na Allah Amekuumbeni na mnayoyafanya”.(37:96) Na,**

إِنَّا كُلُّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٣٧﴾

**“Hakika Sisi kila kitu Tumekiumba kwa kipimo ‘Qadari’”.**

Katika hayo ni kauli yake katika hadithi ya Ibn Abbaas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا

« واعلم أن الأمة لو اجتمعوا على أن ينفعوك بشيء لم ينفعوك إلا بشيء  
قد كتبه الله عليك، ولو اجتمعوا على أن يضروك بشيء لم  
يضروك إلا بشيء قد كتبه الله عليك رفعت الأقلام وجفت الصحف »

*“Jua lau umma utakusanyika juu ya kukunufaisha kwa kitu  
hawatakunufaisha isipokuwa kwa ambalo Allah Amekwisha  
kukuandikia, na lau watakusanyika ili wakudhuru kwa kitu  
hawatakudhuru isipokuwa kwa jambo alilokwishakukuandikia Allah  
juu yako. Kalamu imeinuliwa na wino umekauka”<sup>446</sup>.*

Madhehebu ya Salaf na maimamu wa Khalaf wana mtazamo kuwa mwenye kusadikisha mambo haya kabisa bila kuwa na shaka wala kusita anakuwa muumini wa haki. Ni sawa hilo liwe ni kutokana na dalili za wazi au kabisa kabisa za kukata. *Wallahu A’alam.*

## FASILI

Wamewafikiana watu sabini miongoni mwa Taabiina, Maimamu na Fuqahaa wa Waislamu kuwa Sunnah ambayo amefishwa nayo Mtume ﷺ mwanzo wake ni kuridhia hukumu ya Allah na Qadari yake,

---

<sup>446</sup> Swahihi: Ahmad 1/293,303 Tirmidhi 2516 Shaykh ameisahihisha katika Sahiihil Jaami’i 7957



## Al - Kabair

---

kusalimu amri yake na kusubiri chini ya hukumu yake, na kuacha aliyoyakataza na kumtakasia amali. Kuamini Qadari - kheri yake na shari yake, na kuacha kushindana (kubishana), kujadiliana na kuhasimiana katika Dini, na kufuta juu ya khofu mbili na jihadi pamoja na kila Khalifa mwema na muovu, na kuwaswalia waliokufa miongoni mwa watu wa Qibla.

Imani: Ni kauli, amali na nia. Inazidi kwa utii na inapungua kwa maasi. Na Qur'an ni maneno ya Allah, kupitia Jibrili, ambayo amemteremshia Mtume Wake Muhammad ﷺ bila ya kuumbwa. Subira iko chini ya bendera ya mtawala, vyovyote alivyo, muadilifu au jeuri, wala hatuwang'oi watawala kwa upanga hata wakiwa jeuri. Wala hatumkufurishi mtu yoyote wa Qibla hata akitenda dhambi katika madhambi makubwa, isipokuwa akiyahalalisha. Wala hatumshuhudii yoyote pepo kwa mema aliyoyafanya isipokuwa aliyeshuhudiwa na Mtume ﷺ. Na tunajizuia kwa yaliyotokea kutokana na migogoro baina ya sahaba wa Mtume ﷺ. Na kiumbe bora baada ya Mtume ﷺ ni Abu Bakr kisha Umar kisha Uthmaan kisha Al-Rَضِيَّ اللهُ عَنْهُمْ, na tunawatakia rehema wake wote wa Mtume ﷺ na watoto wake na sahaba zake رَضِيَ اللهُ عَنْهُمْ.

## FAIDA

Kuna maneno ya watu ambayo ni ukafiri, wanazuoni wameyaweka wazi. Miongoni mwa hayo ni kama vile mwenye kukejeli Jina la Allah, au Amri Yake, au Ahadi Yake, au Kamio Lake, mtu anayefanya haya amekufuru. Lau atasema: 'Allah angeniamrisha kadha nisingefanya', hivyo amekufuru maamrisha ya Allah.' Maneno mengine yenye kumtia mtu katika ukafiri ni kusema, 'Qibla kingekuwa upande huu nisingeswali wala kukielekea'. Lau ataambiwa: 'Usiache Swala kwani Allah atakuadhibu akasema: 'Lau ataniadhibu kwa hilo pamoja na maradhi niliyonayo amenidhulumu' kwa maneno haya atakuwa amekufuru. Lau atasema: 'Lau Malaika na Mitume wangeshuhudia nisingesadiki', kwa maneno haya atakuwa amekufuru. Na lau aliambiwa: 'Punguza kucha zako kwani ni Sunna', akasema: 'Sifanyi hata kama ni sunna', atakuwa

## Al - Kabair

---

amekufuru. Akisema: Fulani namuona kama myahudi, atakuwa amekufuru. Lau atasema kuwa Allah amekaa kwa ajili ya Insafu au amesimama kwa ajili ya insafu amekufuru. Na imekuja vingine kuwa: Atakayemwambia Muislamu: 'Allah asikuhitimishie kwa kheri au atakunyang'anya imani, imeelezwa pia kuwa mwenye kutaka yamini kwa mtu na akamtaka aape kwa Allah, akamwambia aapie kwa talaka atakuwa amekufuru. Wametofautiana kuhusu maneno yafuatayo yatakayosemwa: "Nakuona kama mfu, baadhi wamesema amekufuru. Lau atasema: 'Lau fulani angekuwa Mtume nisingemuamini', atakuwa amekufuru. Lau atasema: 'Ikiwa aliyoyasema ni kweli', basi tumenusurika, atakuwa amekufuru.

Lau ataswali bila udhu kwa stihizai au kwa kuhalalisha atakufuru. Lau watu wawili watagombana na mmoja wao akasema: '*Laa Hawla wala Quwwata Ila Billahi.*' Na mwingine akasema: '*Laa Hawla wala Quwwata haishibishi*', atakua amekufuru. Lau atasikia adhana akasema, 'muongo' amekufuru. Akisema: 'Siogopi kiama', amekufuru. Akiweka bidhaa zake akasema: "Nimezisalimisha kwa Allah' na mtu mwingine akasema, 'umezisalimisha kwa asiyekimbiza mwizi', amekufuru. Lau mmoja wao atakaa mahali palipoinuka kama hatibu na watu wanamuuliza maswali huku wanacheka au mmoja wao akasema: 'Kipande cha mkate ni bora kuliko elimu' amekufuru. Lau atapatwa na matukio mabaya kisha akasema, 'imechukua mali yangu na mwanangu, utafanya nini', atakuwa amekufuru.

Lau atampiga mtoto wake au kijana wake na mtu akamwambia: "Je, wewe si Muislamu?" Akasema: 'Hapana' kwa makusudi atakuwa amekufuru. Lau atatamani Allah asingeharamisha zina au kuua au dhuluma atakuwa amekufuru. (Lau atafungwa kamba kiunoni mwake akaulizwa hilo akasema: huu ni mshipi). Lau Mwalimu atamwambia mtoto: 'Yahudi ni bora kuliko Waislamu kwani wanawapa walimu wa (watoto wao' atakafuru.) Lau atasema: 'Mkristo ni bora kuliko majusi.' Atakufuru. 'Lau mtu ataulizwa Imani ni nini?' Akajibu, 'Sijui' atakuwa amekufuru. Na miongoni mwa hayo kuna matamshi yanayokuwa karaha yasiyofaa.

## **Al - Kabair**

---

---

Nayo ni: 'Huna dini!' 'Huna Imani', 'Huna yakini', 'Wewe ni muovu', 'Wewe ni mnafiki', 'Wewe ni mzandiki', 'Wewe ni fasiki', hayo na mfano wake yote ni haramu na inaogopewa kwa mja kwa hayo kunyang`anywa Imani, na kukaa milele motoni.

Tunamuomba Allah تعالیٰ kwa Upole Wake Atufishe tukiwa waislamu juu ya kitabu na Sunnah. Hakika Yeye ni Mrehemevu wa wenye kurehemu.

\*\*\*

DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA MBILI

KUJISIKIZISHA KWA WATU WANAYOYAFICHA

Allah Anasema

وَلَا تَجَسَّسُوا ﴿٤٩﴾

**“Msifanye ujasusi” (49:13)**

Ibnul-Jawzi anasema: Abu Razin, Hasan, Dhahaak na Ibn Siiriin wamesoma kwa Haa, **“Walaah tahassasuu”**. Abu Ubaidah amesema *at-Tajassasu* na *at-Tahassasu* maana yake ni moja, nayo ni kutafuta. Yahya ibn Ibn Abi Kathiir amesema: *At-Tajassasu* ni kuchimbua aibu za watu, na *at-Tahassasu* ni kusikiliza mazungumzo ya watu. Wafasiri wanasema: ‘Ujasusi ni kuchimbua aibu za Waislamu’.

Maana ya aya ni kuwa: Yeyote asichimbue aibu ya ndugu yake ili ajue Allah alichokisitiri kwake.

Ibn Mas-uud aliambiwa: Huyu Waliid bin ‘Uqbah ndevu zake zinavuja pombe akasema: ‘Tumekatazwa kufanya ujasusi kama likidhihirika jambo kwake tutamchukulia kwa jambo hilo.<sup>447</sup> Mtume ﷺ amesema:

« من استمع إلى حديث قوم وهم له كارهون صب في أذنيه الآنك يوم القيامة » .

*“Mwenye kusikiliza mazungumzo ya watu na wao wanamchukia atamiminiwa risasi iliyoyayushwa sikioni mwake Siku ya Kiama.”*  
Ameipokea Bukhari.<sup>448</sup>

Tunamuomba Allah Taufiqi kwa Anayo yapenda na Kuyaridhia hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu.

---

<sup>447</sup> Sahihi: Zaadul Masiir 7/471; Kauli ya Ibn Masuud ameipokea 479 na Isinadi yake ni sahihi

<sup>448</sup> Sahihi: Bukhari 7042 Humaidi 531 Ibn Hibbaan 5685 Twabarani: 1855 Al bayhaqi 7/269, Ahmad 1/359

## DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA TATU

### MWENYE KUFITINI

Huyo ni mtu anayesambaza mazungumzo baina ya watu kwa ajili ya kuleta uharibifu baina yao. Huu ndio ubainifu wake.

Ama hukumu yake ni haramu kwa makubaliano ya waislamu. Katika uharamu wake kumedhihirika dalili nyingi za kisheria kutokana na Kitabu na Sunnah. Allah Amesema:

وَلَا تُطِيعُ كُلَّ حَلَّافٍ مَّهِينٍ ﴿١٠﴾ هَمَّازٍ مَشَاءٍ بِنَمِيمٍ ﴿١١﴾

***“Wala usimt’ii kila mwingi wa kuapa wa kudharauliwa, Mtapitapi, apitaye akifitini.” (Al-Qalam, 68:10-11)***

Katika sahihi mbili Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« لا يدخل الجنة نمام »

*“Hataingia peponi mfitinishi”<sup>449</sup>.*

Kuna Hadithi Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما anahadithia kuwa Mtume ﷺ alipita kwenye makaburi mawili akasema:

« إنهما ليعذبان وما يعذبان في كبير ، أما أنه كبير . أما أحدهما فكان لا يستبرئ من بوله ، وأما الآخر فكان يمشي بالنميمة . »

*“Wakazi wa makaburi hayo wanaadhibiwa wala hawaadhibiwi kwa kosa kubwa, mmoja wao anatembea kwa kuchonganisha, na mwingine alikuwa hajisafishi vizuri na mkojo.”*

---

<sup>449</sup> Sahihi: Ahmad 5/391; 396 Muslim; 105 Bukhari 6056 kwa tamshi la Fattaatun

## Al - Kabair

---

Kisha Mtume ﷺ alichukuwa tawi bichi la mtende akalichana sehemu mbili na akapanda kila moja katika kaburi moja. Alipoulizwa kwa nini alifanya hivyo .’ Mtume ﷺ alisema:

« لعله أن يخنف عنهما ما لم يبسا »

*“Huenda adhabu yao ikapunguzwa madamu matawi haya hayajakauka.”*

Na kauli yake: وما يعذبان في كبير ،

*‘Wala hawaadhibiwi kwa kosa kubwa’,<sup>450</sup>*

yaani sio kubwa kwa madai yao. Na ndio maana katika riwaya nyingine amesema:

« بلى إنه كبير »

*“Bali ni kubwa.”*

Kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنهما anatoa ripoti kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« تجدون شر الناس ذا الوجهين الذي يأتي هؤلاء بوجه وهؤلاء بوجه »

*“Mtamkuta mtapitapi muovu zaidi wa watu ni mwenye nyuso mbili: huonesha uso mmoja kwa mtu na uso mwingine kwa mwingine”<sup>451</sup>*

*“Na mwenye kuwa na ndimi mbili katika Dunia Allah atamfanyia ndimi mbili za moto siku ya kiama”<sup>452</sup>*

Maana ya mwenye ndimi mbili ni kuzungumza na hawa kwa maneno mengine na hawa kwa maneno mengine na hiyo ndio maana ya mwenye nyuso mbili.

---

<sup>450</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>451</sup> Sahihi: Bukhari 3493, 3494,3495 Muslim 2526

<sup>452</sup> Sahihi: Bukhari 1310, Twayaalisi 644; Ibn Hibaan 5756

## Al - Kabair

---

Imam Abu Haamid–Al Ghazali amesema: Mara nyingi hutumiwa juu ya mwenye kuhamisha maneno ya mmoja hadi kwa mwingine. Kwa kauli yake: ‘Fulani anasema kuhusu wewe kadha, na kuchonganisha sio mahususi kwa hilo tu, bali ukomo wake ni kudhihirisha kuchukia mwenye kuhamishiwa au mwenye kuhamishwa kwake au yule wa tatu. Ni sawasawa iwe kwa kauli au kwa maandishi, ishara au mfano wake.

Kiini cha kuchonganisha ni kufichua siri na kupasua sitara ambayo inachukiza kuidhihirisha. Inatakiwa mwanadamu kunyamaza kwa kila hali za watu anazoziona, isipokuwa katika ambayo kuyazungumza kuna faida kwa waislamu, au kuzuia kwao maasi.

Amesema: Mwenye kuletewa uchonganishi, na akaambiwa: Fulani amekusema kuwa kadha wa kadha yatamlazimu mambo sita:

La Kwanza: Asimsadiki kwa sababu ni m-beya, maelezo yake ni yenye kukataliwa.

La Pili: Amkataze jambo hilo, kumnasihi na kumkemea.

La Tatu: Amkasirikie kwa ajili ya Allah تعالی, Mwenye Nguvu, kwani ni mwenye kukasirikiwa mbele ya Allah تعالی na kukasirika kwa ajili ya Allah ni wajibu.

La Nne: Wala asimdhania vibaya mwenye kusemwa kwa Kauli Yake:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَأٍ فَتَبَيَّنُوا

***“Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi...” (49:12).***

La Tano: Aliyoambiwa yasimpelekee kwenye kufanya ujasusi na kufuatilia aibu za watu. Allah تعالی Amesema:

وَلَا تَجَسَّسُوا

**“Wala msipelelezane..”**

La Sita: Asiridhie nafsi mwake aliyokatazwa mfitinshi kwa hiyo asisimulie fitina yake. Imekuja kuwa mtu mmoja alikwenda kwa Khalifa ‘Umar bin ‘Abdul-Aziiz na akamtaja mtu kwa jambo. ‘Umar akamwambia: ‘Wewe ndugu yangu ukitaka tutachunguza mambo, ukiwa mkweli basi utaingia katika aya hii:

يَتَأْتِيَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْ جَاءِكُمْ فَاسْقُوا بِنَبَأٍ فَتَبَيَّنُوا

**“Enyi mlio amini! Akikujieni mpotovu na khabari, ichunguzeni...” (49:6)**

Na ikiwa wewe ni muongo basi wewe ni watu wa aya hii.

هَمَّازٌ مَّشَاءٌ بِنَمِيمٍ

**“Mtapitapi, apitaye akifitini” (68:11)**

Na ukitaka tutakusamehe. Yule mtu akasema: “Naomba msamaha ewe kiongozi wa waumini, sitorudia tena milele”.

Mtu mmoja alimletea maneno Saahib bin ‘Ubbaad, akimshawishi achukue mali ya yatima ambayo ilikuwa nyingi mno. Hapo, Sahib akaandika nyuma ya kikaratasi hicho, “Kumsema mtu (uchonganishi) ni uovu hata ukiwa sahihi, maiti (Allah atamrehemu), yatima Allah Atamuunga, mali ni matunda ya Allah, na mchonganisha Allah Atamlaani.’

Hassan al-Basri amesema: “Mwenye kukuletea mazungumzo ya mwingine jua kuwa atapeleka kwa mwingine mazungumzo yako, na hili ni kama kauli ya watu, Mwenye kukuhamishia wewe, atahamisha kutoka kwako vilevile - tahadhari nae.”



## Al - Kabair

---

Abdullah Ibn Mubarak amesema: "Mtoto wa zina hawezi kuficha siri. Haya yameashiriwa kwa Kauli ya Allah: lakini badala yake huenda na kusambaza na huo ni ushahidi kuwa yeye ni mwanaharamu kutokana na Kauli ya Allah Ta'ala:

عُتِلَّ بَعْدَ ذَلِكَ زَيْمٍ ﴿٦٨﴾

**"Mkavu, na juu ya hayo, mshari, amejipachika tu." (68:12)**

Na maana ya *Zaniim* ni mwanaharamu.

Imepokewa kuwa mmoja wa *Salaf* alimtembelea mmoja wa ndugu yake akamwambia mambo ya baadhi ya ndugu zake anayoyachukia akamwambia: "Ewe ndugu yangu, umerefusha kusengenywa na umekuja kwangu na madhambi matatu: Umenichukiza juu ya ndugu yangu, umeshughulisha moyo wangu kwa sababu yake, na umejituhumu." Wengine wamesema: "Mwenye kukupa habari za kumshutumu nduguyo, huyo amekushutumu wewe."

Mtu mmoja alikwenda kwa Ali bin Al-Husain akamwambia: "Fulani amekutukana na amesema hivi na hivi juu yako." Akasema: 'Twende kwake', akaenda nae na huku anaangalia namna ya kujinusu akamwambia: "Ndugu yangu, ikiwa uliyoyasema kunihusu ni kweli basi Allah Anisamehe, na ikiwa ni uwongo basi Allah Akusamehe". Imesemwa katika maelezo ya aya hii:

حَمَّالَةَ الْحَطَبِ ﴿١١١﴾

**"Na mkewe, mchukuzi wa kuni" (111:4)**

Yaani, mke wa Abu Lahabi. Inasemekana alikuwa anasambaza habari za kufitinisha. Kufitinisha katika (aya hiyo) kumeitwa kuni kwa sababu ni sababu ya uadui. Kama ambavyo kuni ni sababu ya kuwasha moto. Husemwa: Kufitinisha ni madhara makubwa zaidi kuliko matendo ya shetani. Kwa kuwa matendo ya shetani ni kwa wasiwasi na matendo ya mfitinishi ni uso kwa uso.

## KISA

Mtu mmoja aliona mtumwa anauzwa anatangazwa kuwa hana baya lolote isipokuwa ni mfitinishi tu. Akaona aibu hiyo ni ndogo akamnunua. Siku chache zikapita na yule mtumwa akamwambia bibi yake: “Bwana wangu anadhamiria kuoa mke mwingine, na amesema kuwa hakupendi na kama unataka akuonee huruma na kuacha yale aliyoazimia basi akilala usiku chukua kiwembe na umnyoe nywele zake kidogo chini ya kidevu chake pindi akishalala.” Yeye (mke) akasema nafsini mwake: “Nitafanya hivyo.” Mwenye nyumba aliporudi mtumwa huyo alikwenda kwa bwana huyo na kumwambia: “Ewe bwana wangu mkeo anampenda mtu mwingine na anataka kujiokoa kwako, na ameazimia kukuchinja leo usiku. Ikiwa huamini basi jifanye umelala atapokuja kitandani angalia kitu atakacho kuja nacho mkononi anataka kukuchinja nacho.” Bwana wake akamsadiki.

Usiku ulipoingia mwanamke akaja na kiwembe ili anyoe nywele za chini ya kidevu ilhali mwanaume amejifanya kalala. Akasema nafsini mwake, Wallahi yule kijana amesema kweli. Alipoweka kiwembe na kutaka kuanza kumnyoa, mume alisimama, akachukua kiwembe na kumchinja nacho. Jamaa zake walipokuja na kumuona (mke) ameuawa, na wao wakamuua yule mtu. Basi kukatokea vita baina ya makundi mawili kwa sababu ya ukorofi wa kijana yule mkorofi<sup>453</sup>. Kwa sababu hiyo Allah akamuita mfitinishi - Fasiqi katika Kauli Yake Taalaa:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اِنْ جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِّنَا فَتَّبِعُوْهُ اَنْ تُصِيْبُوْا قَوْمًا مَّجْهَلًا

فَتُصْحَبُوْا عَلٰٓى مَا فَعَلْتُمْ نٰذِرِيْنَ ﴿٤٥٤﴾

***“ Enyi mlio amini! Akikujieni mpotovu na khabari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kuto jua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyo yatenda.”***<sup>454</sup> (49:6)

---

<sup>453</sup> Ibn Abi Dunyaa katika Al Ghiibah 133 na katika As Swamt 271

<sup>454</sup> Al Hujuraati (49:6)

DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA NNE

KULAANI

Mtume ﷺ amesema:

«سِيَابُ الْمُسْلِمِ فُسُوقٌ وَقِتَالُهُ كُفْرٌ»

“Kumtukana muislam ni ufasiqi na kupigana naye ni ukafiri<sup>455</sup>”.

Mtume ﷺ amesema:

أَلْعَنُ الْمُؤْمِنُ كَقَتْلِهِ

“Kumlaani muumini ni kama kumuua.”.

Abu Dardaa anatoa taarifa kuwa Mtume wa Allah ﷺ amesema:

وقال: «لا يكونُ اللّعانُ شفعاء ولا شهداء يومَ القيامةِ

“Walaanifu (wenye kulaani sana) hawatokuwa waombezi wala mashahidi siku ya kiyama.”<sup>456</sup> (Muslim).

Na akasema Mtume ﷺ :

لا ينبغي لصديق أن يكون لعاناً

“Haifai kwa mtu mkweli kuwa mlaanifu<sup>457</sup>”.

Ibn Mas’uud anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

وعنه قال: «ليس المؤمنُ بالطَّعَانِ، ولا اللَّعَانَ، ولا الفاحشِ، ولا

البذيءِ»<sup>(1)</sup> حسنه الترمذي.

---

<sup>455</sup> Sahihi: Bukhari 6044,6048 Muslim 64

<sup>456</sup> Sahihi: Bukhari 6047 Muslim 110

<sup>457</sup> Sahihi: Muslim 2098

## Al - Kabair

---

*“Muumini hana tabia ya kukosoa au kulaani wengine wala kwa uchafu wala kuzungumza maneno machafu.”<sup>458</sup>*

Abu Dardaa رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

[وعنه ﷻ قال<sup>(3)</sup>: «إِنَّ الْعَبْدَ إِذَا لَعَنَ شَيْئًا صَعِدَتِ اللَّعْنَةُ إِلَى السَّمَاءِ، فَتُغْلَقُ أَبْوَابُ السَّمَاءِ دُونَهَا<sup>(4)</sup>، ثُمَّ تَأْخُذُ يَمِينًا وَشِمَالًا، فَإِذَا لَمْ تَجِدْ مَسَاحًا رَجَعَتْ إِلَى الَّذِي لُعِنَ إِنْ كَانَ أَهْلًا لَذَلِكَ، وَإِلَّا رَجَعَتْ إِلَى قَاتِلِهَا<sup>(5)</sup>» رواه أبو داود.

*“Mja akilaani kitu hicho kilicholaaniwa hupaa mbinguni na milango ya pepo hufungwa dhidi ya laana hiyo, kisha laana hiyo hurudi ardhini na milango ya ardhi hufungwa, hivyo huenda kulia na kushoto, isipopata mapito hurudi kwa aliyelaaniwa ikiwa ni mstahiki (itampata) vinginevyo hurudi kwa msemaji wake”<sup>459</sup>.*

Mtume ﷻ alimuadhibu mtu aliyemlaani ngamia wake, kwa kumpokonya ngamia yule kutoka kwake.

‘Imraan bin Hiswain amesema: “Mtume ﷻ alipokuwa safarini akiwa na Ansari juu ya ngamia, alikuwepo mwanamke mmoja wa ki-Ansaar alikuwa akimuendesha ngamia na kutokana na hasira yule mwanamke akamlaani yule ngamia, Mtume ﷻ akamsikia akasema:

«خذوا ما عليها ودعوها؛ فإنها ملعونة.»

*“Ondoeni kila kitu juu yake (ngamia huyo) na mwacheni kwani amelaaniwa”.*

Imraan akasema: ‘Nikana kwamba namuona hivi sasa anatembea katika watu hakuna yoyote anaye mjali.’<sup>460</sup>

---

<sup>458</sup> Maelezo yake yametangulia.

<sup>459</sup> Sahihi: Abu Dawud 4905 Ibn Abi Dunya katika As Swamti 202 Shaykhameisahihisha katika As Silsilah as Swahiihah 1269 na katika Sahihil Jaami’i 1672 Sahihi: Muslim 2097

<sup>460</sup> Sahihi: muslim 2595

## Al - Kabair

---

Abu Hurairah amesema: Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ أَرَبَى الرُّبَا اسْتَطَالَهُ<sup>(٢)</sup> المرء في عِرْضِ أُخِيهِ الْمُسْلِمِ»

*"Hakika riba kubwa kabisa ni mtu kukashifu heshima ya ndugu yake Muislamu."*<sup>461</sup>

Kutoka kwa 'Amr bin Qais amesema: "Wakati mtu akipanda kipando chake (yule mnyama) anasema: "Ewe Allah mjaalie huyu bwana wangu awe rafiki yangu mwenye huruma na anipende. Lakini mtu yule akimlaani. Mnyama yule husema: 'Ametuasi kwa mafundisho ya Mjumbe wake ﷺ, basi laana ya Allah iwe juu yake".

## FASILI

### KURUHUSIWA KULAANI WATU WA MAASIA

Allah Mtukuka Anasema:

أَلَا لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٨﴾

*"Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate walio dhulumu."*(11:18)

ثُمَّ نَبَّهَالٍ فَتَجْعَلُ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكَاذِبِينَ ﴿٦١﴾

*"...kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo."*(3:61)

Imethibiti kuwa mjumbe wa Allah amesema:

*"Allah Amemlani mla riba, na mwakilishi wake, na shahidi wake na mwandishi wake"*.<sup>462</sup>

---

<sup>461</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>462</sup> Maelezo yake yametangulia

## Al - Kabair

---

Na kuwa amesema:

*"Allah amlaani mwenye kuhalalisha na mwenye kuhalalishiwa."*<sup>463</sup>

Na amesema tena Mjumbe wa Allah katika Hadithi nyingine:

*"Allah amemlaani mwenye kuunganisha nywele zake na mwenye kumuunganishia nywele zake, anayechonga meno, na mwenye kumchongea meno, mwenye kunyoo nyusi, na mwenye kumnyoo nyusi"*.<sup>464</sup>

Na kuwa Mtume ﷺ amemlani, 'Mwenye kuomboleza kwenye misiba, na mwenye kunyoo nywele katika misiba, na mwenye kuchana nguo katika misiba.'<sup>465</sup>

Na kuwa amewalani wenye kutengeneza picha,<sup>466</sup> na kuwa Mtume ﷺ amemlaani mwenye kubadilisha minara ya ardhi"<sup>467</sup>. Yaani mipaka yake.

*"Allah amemlani mwenye kutukana wazazi wake, na amemlani mwenye kumtukana mama yake."*<sup>468</sup>

Na katika As-Sunan amesema:

*"Allah amemlaani mwenye kumpoteza njia kipofu"*.<sup>469</sup> "Na amemlani mwenye kumingilia mnyama"<sup>470</sup>, "Na amemlani mwenye kufanya

---

<sup>463</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>464</sup> Sahihi: Bukhari 5931; Muslim 2125

<sup>465</sup> Sahihi: Al-Bukhari 1296; Muslim 104

<sup>466</sup> Sahihi: Al-Bukhari 2086.

<sup>467</sup> Sahihi: Ahmad 1/188,152. Muslim 1978

<sup>468</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>469</sup> Sahihi: Ahmad 1/217,317 Abu Yaalaa 212 Baihaqi katika As Shiib 4988 katika As Sunan 8/231 Sahiihil Jaami'i 5767

<sup>470</sup> Sahihi: Ahmad 1/217,317 Abu Yaalaa 212 Baihaqi katika As Shiib 4988 katika As Sunan 8/231 Sahiihil Jaami'i 5767

*matendo ya watu wa Luti".<sup>471</sup> "Au kumuendea kuhani<sup>472</sup>, au mwanamke kwenye duburi yake,<sup>473</sup> na amemlani mwenye kuomboleza na wanaomzunguka<sup>474</sup>". Na amemlani mtu anayeswalisha watu na huku wanamchukia<sup>475</sup>". Na "amemlani mwanamke anayelala na huku mumewe amemkasirikia<sup>476</sup>". Na "amemlani mwanammume amesikia Hayya 'ala Swalat, Hayya 'alal falaah na asijibu". Na "Amemlani mwenye kuchinja kwa asiyekuwa Allah<sup>477</sup>", "na amemlani mwizi<sup>478</sup>". Na "Amemlani mwenye kutukana sahaba<sup>479</sup>" Na, "Amemlani mwanamume anayeiga wanaume na wanawake wanaoiga wanaume<sup>480</sup>" "Na amemlani Mwanaume wenye kujifanisha na wanawake, na wanawake wenye kujifanisha na wanaume".<sup>481</sup>*

*"Na amemlani mwanamke anavaa nguo za kiume na mwanamume mwenye kuvaa nguo za kike<sup>482</sup>". "Na amemlani mwenye kujisaidia haja kubwa katika njia (ya watu)<sup>483</sup>". "Na amemlani mwanamke Sulataau (asiyepaka waja, hina, wala kujipamba). Na amemlani mwenye kumshawishi mke dhidi ya mumewe au mtumwa dhidi ya bwana wake<sup>484</sup>". "Na amemlani mwenye kumuingilia mwenye hedhi au mwanamke kwenye duburi yake<sup>485</sup>". Na, "Amemlani mwenye*

---

<sup>471</sup> Maelezo yake yametangulia katika 470 hapo juu.

<sup>472</sup> Maelezo yake yametangulia.

<sup>473</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>474</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad na Abu Dawud angalia katika al-Jami' 4693.

<sup>475</sup> Sahihi: Imekuja bila tamshi la laana kutoka kwa Abu Umaamah kwa Tirmidhi angalia Sahihil Jaami 3057.

<sup>476</sup> Sahihi: Bukhari 3237 Muslim 1426

<sup>477</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>478</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>479</sup> Hasan: Twabarani na Al Baani ameifanya Hasan katika as Swahiihah 2340 Swahiihul Jaamii 5111

<sup>480</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>481</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>482</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>483</sup> Sahihi: kwa tamshi jingine

<sup>484</sup> Sahihi: Sahihi: Ahmad "Kwa tamshi Mwenye kutaka kumshawishi mtu katika watu basi huyo sio katika sisi"

<sup>485</sup> Maelezo yake yametangulia

## Al - Kabair

---

*kumuashiria ndugu yake na chuma (silaha)<sup>486</sup>". Na "Amemlani mwenye kuzuia sadaka,(yani: Zaka) <sup>487</sup>". Na, "Amemlani mwenye kujinasibisha na asie baba yake, au kujinasibisha kwa wasio wamiliki wake<sup>488</sup>". "Na amemlani mwenye kumtia alama mnyama usoni mwake<sup>489</sup>". "Na amemlani mwenye kutetea na mwenye kutetewa adhabu ya Allah inapofika kwa hakimu"*

*"Na amemlani mke anayetoka nyumbani mwake bila ruhusa ya mumewe."<sup>490</sup> Na, "Akamlani anapolala kwa kumhama mumewe mpaka arudi".<sup>491</sup> Na, "Amemlani mwenye kuacha kuamrisha mema na kukataza mabaya ikiwezekana kwake", "Na amemlani mwenye kufanya na kufanywa (Yaani: mwenye kulawiti na mwenye kulawitiwa)."<sup>492</sup>. Na, "Amelani pombe, na anayeinywa, na anayemnyweshwa, na mnunuzi wake, na muuzaji wake, na mchujaji na mchujiwa na anayebeba na anayebebewa na anaye kula thamani yake, na mwenye kuelekezea".*

Na akasema Mtume ﷺ:

*"Watu sita nimewalani na Allah amewalani, na wamelaaniwa na kila Mtume mwenye kujibiwa dua; mwenye kukanusha Qudura ya Allah, mwenye kuongeza kitu ndani ya kitabu cha Allah, mwenye kusalitiwa nguvu. Ili kumtukuza aliyemdhalisha Allah, na kumdhalilisha aliyemtukuza, mwenye kuhalalisha (vita) katika msikiti (haramu) wa Makkah. Na mwenye kuhalalisha katika familia yangu,*

---

<sup>486</sup> Sahihi: Muslim 2616 Tirmidhi 2162

<sup>487</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>488</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>489</sup> Sahihi: Muslim na Ibn Hibbaan 3002, 2005 Abu dawud 2564 tabarani katika 2/140 angalia As Swahihah 2149

<sup>490</sup> Maudhui: Al Khatib katika at - taariikh 200, 201 Al Baani amesema: ni maudhuu katika As-Silsilah Dhahifah 1020

<sup>491</sup> Swahih: Ameipokea Bukhari 3237, Muslim 1436 bila tamshi la laana

<sup>492</sup> Maelezo yake yametangulia



*aliloiharamisha Allah, na mwenye kuacha Suna yangu<sup>493</sup>". Na, 'Amemlani mwenye kuzini na mke wa jirani yake<sup>494</sup>". "Na amemlani mwenye kuoa mkono wake<sup>495</sup>". "Na amemlani mwenye kuoa mwanamke na binti yake<sup>496</sup>". "Na amemlani mwenye kutoa rushwa, na anayechukua rushwa na muunganishi baina yao"<sup>497</sup>. "Na amemlani mwenye kuficha elimu<sup>498</sup>". "Na amemlani mwenye kulimbikiza nafaka<sup>499</sup>" "Na amemlani mwenye kumtelekeza Muislamu - yaani amemdhaliisha wala hakumnusuru<sup>500</sup>" "Na amemlani mtawala asiye na huruma<sup>501</sup>". "Na amewalani waseja miongoni mwa wanaume na wanaosema hawataoa" na wanawake wasiotaka kuolewa, na amemlaani anayepanda jangwani peke yake kwenda katika ardhi isiyo na kitu na amemlaani mwenye kumuingilia mnyama."<sup>502</sup>*

Tunajilinda kwa Allah kutokana na Laana Yake na ya Mtume Wake.

## **FASILI**

Kumlaani Muislam aliyehifadhika ni haramu kwa ijmai ya waislamu. Inaruhusiwa kuwalaani wenye sifa mbaya kwa jumla kama kusema: "Allah awalaani madhalimu". "Allah Awalaani makafiri." "Allah Awalaani mayahudi na manasara." "Allah Awalaani watendaji maovu." "Allah Awalaani watengeneza picha na mfano wake kama ilivyotangulia. Ama kumlaani anayejulikana kama vile dhalimu, mwizi au mzinifu au mla

---

<sup>493</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>494</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>495</sup> Imekuja bila tamshi la laana

<sup>496</sup> haikuja na tamshi la laana

<sup>497</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>498</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>499</sup> Zimekuja hadithi nyingi katika kulimbikiza chakula na zote ni dhaifu, angalia Dhaiiful Jaamii 5355,5355,5357.

<sup>500</sup> Sahihi: Bukhari 1870, 3172, 3179; Muslim 3170

<sup>501</sup> Imepokewa na Muslim 1828 kwa tamshi, "Ewe Mwenyezi Mungu utakayemtawalisha katika jambo la Umma wangu kisha akawafanyia ugumu nawe mfanyie ugumu."

<sup>502</sup> Dhaifu: Ahmad 2/287,289 Al Haythami katika Majma'a Az Zawaaid

## Al - Kabair

---

riba, kwa dhahiri ya hadithi ni kuwa hiyo sio haramu. Al-Ghazali amesainisha kuharamishwa hilo isipokuwa wale ambao tumejua kuwa wamefariki wakiwa makafiri, kama vile Abu Lahab, Abu Jahl, Firauni, Hamana na watu kama hao. (Al-Ghazaal) alisema: Kulaani ni kuamini kuwa huyo (aliyelaaniwa) ameondolewa katika rehema ya Allah تعالی lakini hatuwezi kujua kuwa mtu huyo anakufa akiwa kafiri au fasiqi.

Akasema: Ama ambao Mjumbe wa Allah ﷺ amewalaani kwa majina kama vile alivyosema:

*"Ewe Allah mlani Ra`alaa, na Dhaq`waani na 'Aswiyyah waliomuasi Allah na Mtume wake<sup>503</sup>".*

Makabila haya matatu ya waarabu inafaa kuwalani kwao kwani Mtume ﷺ amejua kufa kwao juu ya ukafiri. Amesema: Inakaribia kwenye laana kumuomba mtu shari, hata kumuomba dhalimu kama vile kauli ya mtu: 'Wala Allah asikupe uzima kiwiliwili chako, wala asikisalimishe wala asikipitishhe mapito yake, yote hayo ni mabaya.' Na vile vile kulaani wanyama wote na vitu visivyona roho haya yote ni haramu.

Inafaa kwa mwenye kuamrisha mema na kukataza maovu kusema na kila mwenye kufundisha adabu kumwambia anaye mwambia hivyo: "Ole wako, au wewe dhaifu wa hali." au 'Ewe mchache wa kuangalia nafsi yako, au mwenye kudhulumu nafsi yako', na mfano wake, kwa namna ambayo haifiki kwenye uwongo, wala hakuna ndani yake tamshi lenye singizio la wazi au ishara, hata akiwa mkweli katika hilo. Na inafaa tulioyatanguliza, na inakuwa lengo lake ni kufundisha na kukemea, na maneno huingia zaidi katika nafsi. *Allah 'Aalam.*

Ewe Allah epusha nyoyo zetu dhidi ya kufungamana na walio dhidi Yako na tujalie miongoni mwa Unaowapenda na wanaokupenda na tusamehe sisi na wazazi wetu na waislamu wote.

---

<sup>503</sup> Sahihi: Muslim 675

**MAWAIDHA**

Enyi wenye chakula kidogo ilhali safari ni ndefu, ewe mwenye kuelekea yanayo kudhuru na kuacha yenye kunufaisha, unaonekana umepitwa na jambo jema, mpaka lini utapoteza wakati hesabu yako ipo kwa malaika walinzi *Raqiib* na *Atiid*.

\*\*\*

## DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA TANO

### UHAINI WA KUTOTEKELEZA AHADI

Allah Mtukuka zaidi Anasema:

وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ إِنَّ الْعَهْدَ كَاتِبٌ مَسْئُولًا ﴿٣٤﴾

**"Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itasailiwa." (17:34)**

Zajaaj amesema: 'Lolote Allah تعالی aliloliamuru au alilolikataza ni miongoni mwa ahadi.'

Allah Mtukuka Amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَوْفُوا بِالْعُقُودِ

**"Enyi mlio amini! Timizeni ahadi" . (5:1)**

Al-Wahidi amesema: Ibn 'Abbaas anaelezea katika riwaya ya al-Waalibi: '(Uhuud); ina maana ya aliyohalalisha na aliyoharamisha, na aliyofaradhisha na aliyowekea adhabu katika Qur`an.' Dhahaak amesema: 'kwa ahadi ambazo Allah amechukua kwa umma huu kuzitekeleza katika aliyoyaharamisha na aliyoyakataza, kama vile Swala na faradhi nyingine na ahadi.'

'Uquud maana yake ni kile alichohukumu miongoni mwa Alivyofaradhisha Allah juu yetu. Kwa hakika amehukumu hilo. Wala hakuna njia yoyote ya kuivunja kwa hali yoyote ile.

Muqaatil bin Hayaan رضي الله عنه amesema:

وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ

**'Timizeni ahadi'.**

## Al - Kabair

---

Alichokuahidini Allah kwenye Qur'an, katika aliyokuamrisheni, kama vile kumtii na kuufanyia kazi na makatazo yake na ahadi iliyokuwa baina yenu na baina ya washirikina na baina ya watu." Allah Ndiye Mwenye kujua zaidi. Mtume ﷺ amesema:

« أربع من كن فيه كان منافقاً خالصاً ، ومن كانت فيه خصلة منهن كانت فيه خصلة من النفاق حتى يدعها: إذا حدث كذب، وإذا أُوْتِمَن خان وإذا عاهد غدر ، وإذا خاصم فجر »

*"Tabia nne akiwa nazo mtu humfanya kuwa mnafiki, na mwenye tabia moja katika hizo huwa mnafiki mpaka aziache: akizungumza husema uongo, akiaminiwa hufanya hiana, na anapo ahidi hufanya vitimbi, na anapogombana anafanya uovu". Imetolewa katika Swahihii mbili<sup>504</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

*"Kila mhaini atakuwa na bendera siku ya kياما inaitwa: hii ni khiana ya fulani mtoto wa fulani<sup>505</sup>."*

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« يقول الله عز وجل ثلاثة أنا خصمهم يوم القيامة: رجل أعطى بي ثم غدر ، ورجل باع حراً فأكل ثمنه ، ورجل استأجر أجيراً فاستوفى منه العمل ولم يعطه أجره »

*"Allah Mtukuka anasema: "(Watu) wa tatu mimi ni mgomvi wao siku ya kياما; mtu anayetoa ahadi Kwangu kisha akafanya khiana, na mtu anayemuza mtu huru na kula thamani yake, na mtu anayemuajiri mfanyakazi na akamaliza kazi asimlipe ujira wake." (Bukhari)<sup>506</sup>.*

---

<sup>504</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>505</sup> Sahihi: Bukhari 3186 Muslim 1736, 2227, 2270 Ahmad 2/242

<sup>506</sup> Sahihi: Bukhari 3186 Muslim 1736, 2227, 2270 Ahmad 2/241

Katika hadithi nyingine Mtume wa Allah ﷺ amesema:

*“Mwenye kuvua mkono wa utii atakutana na Allah siku ya kiama akiwa hana hoja, na mwenye kufa na shingoni mwake hakuna bay`ah anakufa kifo cha kijahilia”. (Muslim)<sup>507</sup>.*

Mtume wa Allah ﷺ amesema:

« من أحب أن يزحزح عن النار ويدخل الجنة فلتأته منيته وهو يؤمن بالله واليوم الآخر ، وليأت إلى الناس الذي يحب أن يؤتى إليه ومن باع إماماً فأعطاء صفقة يده وثمرة قلبه فليطعه إن استطاع ، فإن جاء أحد ينازعه فاضربوا عنق الآخر »

*“Mwenye kutaka kunusurika na moto na kuingia peponi basi mauti yake yamjie huku anamuamini Allah na siku ya kiyama, na awajie watu kwa lile analopenda kujiwa yeye, na mwenye kum`bai kiongozi kwa hiyo akampa bishara (nguvu) ya mkono wake na matunda ya moyo wake, basi na amtii akiweza, kwa hiyo akija mwingine anampokonya basi kateni shingo ya huyo mwingine<sup>508</sup>”.*

\*\*\*

---

<sup>507</sup> Sahihi: Muslim 1851

<sup>508</sup> Sahihi: Muslim 1488; Abu Dawud 4248: An Nasaai 7/152,154: Ibn Maajah 4956, Ibn Hibaan 5916.

**DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA SITA**

**KUAMINI MAKUHANI NA WANAJIMU**

Allah Mtukuka Anasema:

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ أُولَئِكَ كَانَ

عَنْهُ مَسْئُولًا ﴿٣٦﴾

**“Wala usiyafuate usiyo na ujuzi nayo. Hakika masikio, na macho, na moyo - hivyo vyote vitasailiwa.” (17:36)**

Al-Waahidi amesema katika tafsiri ya kauli yake Taalaa:

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ ﴿٣٦﴾

**“Wala usiyafuate usiyo na ujuzi nayo”**

Al-Kalbi amesema: ‘Usiseme usilo na elimu nalo’. Qatadah amesema: “Usiseme ‘nimesikia’ wala hukusikia, au ‘nimeona’ wala hujaona, au ‘nimejua’ wala hujui<sup>509</sup>.”

Al-Walibi kutoka kwa Ibn ‘Abbaas: Allah anawauliza waja namna gani walivitumia na katika nini, katika hili kuna kemeo la kuangalia yasiyo halali, na kusikiliza yasiyo halali, na kutaka yasiyo faa. *Walaahu A`alam.*

Allah Mtukuka Anasema:

عَلِيمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿٢٦﴾ إِلَّا مَن آرْتَضَىٰ مِن رَّسُولٍ

**“Yeye Ndiye Mwenye kujua ya siri, wala hamdhihirishii yeyote siri Yake, Isipo kuwa Mtume wake aliye mridhia.” (72:26-27)**

---

<sup>509</sup>Sahihi: Twabarani: 15/86 kutoka kwa Qatadah kwa isinadi sahihi

## Al - Kabair

---

Ibn Al-Jawzi alisema: Mwenye kujua yasiyoonekana ni Allah Mwenye nguvu na Mwenye uwezo, na ni Yeye Pekee hana mshirika, katika milki Yake. 'Haidhihirishi': yaani hamuonyeshi Ghaibu Yake yoyote miongoni mwa watu:

إِلَّا مَنْ أَرْتَضَىٰ مِنْ رَسُولٍ ﴿٦٧﴾

**"Isipo kuwa Mtume Wake aliye mridhia.."**

Kwa kuwa dalili ya ukweli wa Mitume ni habari zao za ghaibu. Na maana ya: 'Hakika aliye mridhia kwa utume atamuonyesha ghaibu atakayo', hili ni dalili kuwa mwenye kudai kuwa nyota inaonyesha ghaibu basi huyo ni kafiri. Wallaahu A'alam<sup>510</sup>

Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

«مَنْ أَتَىٰ عَرَافًا<sup>(٣)</sup> أَوْ كَاهِنًا فَصَدَّقَهُ بِمَا يَقُولُ، فَقَدْ كَفَرَ بِمَا أَنْزَلَ عَلَيَّ مُحَمَّدٌ ﷺ»

*"Mwenye kumuendea mpiga ramli au kuhani akamswadikisha basi amekufuru yaliteremshwa kwa Muhammad".<sup>511</sup>*

Tumesimuliwa katika sahihi mbili kuwa Zaid bin Khalid al-Juhani amesimulia kuwa: "Mjumbe wa Allah ﷺ aliswalisha Swala ya Alfajiri na mvua inanyesha baada ya kumaliza Swala akawaelekea watu akasema: "Mnajua bwana wenu amesema nini?"

Wao wakamjibu: 'Allah na Mjumbe Wake wanajua zaidi.' Mtume ﷺ akasema: Kuwa Allah amesema:

وقال ﷺ صَبِيحَةَ لَيْلَةٍ مَطِيرَةٍ: «يقول الله [-تعالى-] <sup>(١)</sup>: أَصْبَحَ مِنْ عِبَادِي مُؤْمِنٌ، وَكَافِرٌ، فَمَنْ قَالَ: مُطَرْنَا بِفَضْلِ اللَّهِ، فَذَلِكَ مُؤْمِنٌ بِي، كَافِرٌ بِالْكَوْكَبِ، وَمَنْ قَالَ: مُطَرْنَا بِنَوْءٍ <sup>(٢)</sup> كَذَا، فَذَلِكَ كَافِرٌ بِي، مُؤْمِنٌ بِالْكَوْكَبِ» <sup>(٣)</sup> رواه البخاري

<sup>510</sup> Zaadul Masiir 8/385

<sup>511</sup> Sahihi: Ahmad 2/429 ; Haakim 1/8 Sahiihil Jaamii 5639



## Al - Kabair

---

*“Hii asubuhi baadhi ya waja wangu waliamka wakiniamini, na baadhi yao ni makafiri: Aliyesema imenyeshwa mvua kwa Fadhila ya Allah na Rehema Yake, amepambazuka akiwa Ameniamini Mimi na kukufuru nyota, Ama aliyesema: imenyeshwa mvua kwa nyota kadha wa kadha, basi huyo kanikufuru na ni muumini wa nyota”.*<sup>512</sup>

Wanazuoni wanasema: “Ikiwa Muislam anasema inanyesha kwa ajili ya dhuruba kadha wa kadha na ikiwa huyo mtu ameamini dharuba kuwa ndio chanzo cha kuleta mvua, basi huyo ni kafiri, murtadi bila shaka”. Ikiwa amemaanisha kuwa dharuba ndio alama ya kushuka kwa mvua na mvua inashuka wakati wa alama hii, na kushuka kwake ni kwa tendo la Allah Muumba Wake, atakuwa hajakufuru.” Wakatofautiana kuhusu ukaraha wake. Iliyochaguliwa ni kuwa, hiyo ni makuruhu, katika maneno ya makafiri. Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

وقال ﷺ: «مَنْ أَتَى عِرْفَانَ فَسَأَلَهُ عَنْ شَيْءٍ فَصَدَّقَهُ؛ لَمْ تُقْبَلْ لَهُ صَلَاةٌ أَرْبَعِينَ يَوْمًا»<sup>(2)</sup> رواه مسلم.

*“Mwenye kwenda kwa mpiga ramli na akamuamini basi Swala yake haitokubaliwa siku arobaini.”*<sup>513</sup>

‘Aisha رضي الله عنها amesema: Nilimuuliza Mtume ﷺ juu ya watabiri alijibu:

*“Hao hawana lolote.”*

Mtume ﷺ akaambiwa:

*“Ewe Mjumbe wa Allah wao si walisema vile na vile (na utabiri wao ukawa kweli).”*

Akajibu:

---

<sup>512</sup> Sahihi: Bukhari 846, Muslim 71

<sup>513</sup> Sahihi: Muslim 223, na Ahmad 5/380.

## Al - Kabair

---

*"Hilo ni neno la ukweli ambalo jini amelisikia akalithibitisha kwenye sikio la sahibu wake kwa hiyo analihifadhi hilo pamoja na ya uwongo mia moja". Imetolewa katika Sahihi mbili<sup>514</sup>*

Aisha رضي الله عنها anatoa taarifa kuwa mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

*"Malaika huteremka mawinguni kwa hiyo hutaja kitu ambacho kimehukumiwa mbinguni, na shetani huibia kusikiliza kwa hiyo anasikia, na huielekeza kwa makuhani (watabiri) na wao wanadanganya pamoja nayo uongo mia wa kwao wenyewe." (Bukhari)<sup>515</sup>*

Kutoka kwa Qubaisah bin Abil Mukharriq anatoa taarifa kuwa mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« العيافة والطيرة والطرق من الجبت »

*"Kuchora vijistari na ndege na kufukuza ndege ni katika ushirikina." (Abu Dawud).<sup>516</sup>*

Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema:

[وقال ﷺ]: «مَنْ اقْتَبَسَ شَعْبَةً مِنَ النُّجُومِ اقْتَبَسَ شَعْبَةً مِنَ السَّحَرِ»<sup>(٤)</sup> رواه أبو داود بسند صحيح.

*"Mwenye kuchukua sehemu katika nyota hakika amechukua sehemu katika uchawi na atazidisha anacho zidisha".<sup>517</sup>*

Ali bin Abi Talib رضي الله عنه amesema: "Mpiga ramli ni mchawi na mchawi ni kafiri".

Tunamuomba Allah uzima na hifadhi katika dunia na akhera.

---

<sup>514</sup> Sahihi: Muslim 2228; Bukhari 5762

<sup>515</sup> Sahihi: Bukhari 2210

<sup>516</sup> Dhaifu: Abdur Razzak 19502; Ibn Sa'ad 7/35; Ahmad 3/477; Abu Daud 3907; na ameidhoofisha Sheikh katika kitabu Dhaifu za Abu Daud 842

<sup>517</sup> Sahihi: Ahmad 1/311; Abu Daud 3905; Ibn Majah 3726; na ameisahihisha Sheikh katika kitabu cha Silsilatu Sahihah 793 na katika Sahihil Jamii 6074

DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA SABA

MWANAMKE KUTOMTII MUMEWE

Allah Mtukuka Anasema:

وَأَلَّتِي تَخَافُونَ نُشُوزَهُمْ فَعِظُوهُمْ ۖ وَاهْجُرُوهُمْ فِي الْمَضَاجِعِ وَأَضْرِبُوهُمْ ۗ  
فَإِنْ أَطَعْتَكُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِمْ سَبِيلًا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَرِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤﴾

***"Na ambao mnachelea kutoka katika ut'iifu wanasihini, muwahame katika malazi na wapigeni. Wakikut'iini msiwatafutie njia ya kuwaudhi bure. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye aliye juu na Mkuu".(Annisaa: 24)***

Al-Waahidi amesema: "Kutotii hapa kunamaanisha kumuasi mume, na hiyo ni kujikweza juu yake kwa ubishi."

'Ata alisema: Kutojitia manukato kwa ajili yake na (mumewe) kumnyima nafsi yake na kubadili utii aliokuwa akimfanyia".

فَعِظُوهُمْ ۖ

***"Wanasihini"***

Kwa kitabu cha Allah na wakumbusheni yale aliyowaamrisha Allah ndani yake.

وَاهْجُرُوهُمْ فِي الْمَضَاجِعِ

***"Muwahame katika malazi"***

Ibn 'Abbas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا amesema: 'Maana yake ni mume ampe mgongo kitandani wala asizungumze naye.' Sha'abi na Mujaahid wamesema: 'Hiyo ni kuhama kulala naye, kwa hiyo asilale naye.'

وَأَضْرِبُوهُنَّ

**“Wapigeni”**

Inamaanisha pigo lisiloumiza, Ibn Abbaas amesema: Kutia adabu mfano wa **lakzati**, (kipigo kidogo tu cha kuashiria) na mume anatakiwa kukabiliana na ujeuri wa mkewe kwa yale aliyoyaruhusu Allah na kuyataja katika aya hii.

فَإِنْ أَطَعْتَكُمْ

**“Wakikut’iini”.**

Katika yanayotakiwa kwao

فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِنَّ سَبِيلًا

**“msiwatafutie njia ya kuwaudhi bure”.**

Ibn Abbaas amesema: Msiwatafutie sababu, katika sahihi mbili: Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*“Mume akimwita mkewe kitandani (kwa mapenzi), akakataa malaika wanamlani hadi asubuhi<sup>521</sup>”.*

Na katika tamshi jingine:

« فَبَاتَ وَهُوَ عَلَيْهَا غَضَبَانِ لِعَنْتِهَا الْمَلَائِكَةُ حَتَّى تَصْبِحَ »

*“...Kwa hiyo akapitisha usiku huku akiwa amemkasirikia, Malaika wanamlani hadi asubuhi”.*

Katika tamshi jingine la Sahihi mbili:

---

<sup>521</sup> Sahihi: Bukhari 3237 Muslim 1436

## Al- Kabair

---

« إذا باتت المرأة هاجرة فراش زوجها فتأبى عليه إلا كان الذي في السماء  
ساخطا عليها حتى يرضى عنها زوجها »

*“Mwanamke akilala kwa kuhama godoro la mumewe kwa hiyo  
anamkatalia, isipokuwa yule wa aliyekuwa mbinguni humkasirikia  
hadi mumewe amridhie<sup>522</sup>”.*

Jabir bin ‘Abdullah anatoa taarifa kuwa mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« ثلاثة لا يقبل الله لهم صلاة ، ولا ترفع لهم إلى السماء حسنة : العبد الآبق  
حتى يرجع إلى مواليه فيضع يده في أيديهم ، والمرأة الساخط عليها  
زوجها حتى يرضى عنها ، والسكران حتى يصحو »

*“(Watu) watatu Allah hakubali Swala zao wala jema lao lolote  
haliinuliwi mbinguni, mtumwa aliyetoroka mpaka arudi kwa bwana  
wake, kwa hiyo ataweka mkono wake juu ya mikono yao, na  
mwanamke ambaye mumewe amemkasirikia hadi amridhishe, na  
mlevi hadi azinduke<sup>523</sup>”.*

Al-Hasan amesema: Amenihadithia aliyemsikia Mjumbe wa Allah ﷺ  
anasema:

*“Suala la kwanza atakaloulizwa mwanamke siku ya kiama ni kuhusu  
Swala yake na kuhusu mumewe ”.<sup>524</sup>*

Na katika hadithi nyingine:

وقال ﷺ: «لا يحل لامرأة<sup>(٥)</sup> أن تصومَ وزوجها شاهدٌ إلا بإذنه، ولا  
تأذن في بيته إلا بإذنه»<sup>(٦)</sup> رواه البخاري.

---

<sup>522</sup> Sahihi: Bukhari 5194 Muslim 1436

<sup>523</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>524</sup> Dhaifu: Abu Sheikh katika *Thawaabul A'amaal* nayo ni mursal. Nazo ni miongoni mwa Mursal za Al-Hassan.

## Al - Kabair

---

*“Hairuhusiwi kwa mwanamke ambaye anamuamini Allah na siku ya mwisho, kufunga na mume wake yupo isipokuwa kwa ruhusa yake wala kumruhusu yeyote ndani ya nyumba isipokuwa kwa ruhusa yake”. (Bukhari)<sup>525</sup>*

Maana ya kuwa yupo, ni kutokuwa mbali, na hilo ni katika saumu ya Suna asifunge mpaka amuombe idhini mumewe kwa ajili ya wajibu wa haki yake na utii wake. Amesema Mtume ﷺ,

وقال ﷺ: «لو كنت امرأةً أحداً أن يسجدَ لأحدٍ؛ لأمرتُ المرأةَ أن تسجدَ لزوجها»<sup>(٧)</sup> صححه الترمذي.

*“Ningekuwa ni mwenye kumuamuru yeyote kumsujudia mtu mwengine basi ningemuamrisha mwanamke kumsujudia mumewe.” (Tirmidhi).<sup>526</sup>*

Shangazi wa Hiswain bin Muhsan alimtaja mumewe kwa Mtume ﷺ akasema:

وقالت عمّة ابن محصن<sup>(١)</sup>، ودَكَرَتْ زوجها للنبي ﷺ، فقال: «انظري أين أنت منه؛ فإنه جنتك ونارك»<sup>(٢)</sup> رواه النسائي.

*“Angalia hali yako kwake, kwani yeye ndio pepo yako na moto wako.” (Nasaai)<sup>527</sup>*

Abdullah bin Umar رضي الله عنهما anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*“Allah hamtazami mwanamke ambaye hamshukuru mumewe na wala hajitoshi naye”.<sup>528</sup>*

---

<sup>525</sup> Sahihi: Bukhari 5195; Muslim 1026

<sup>526</sup> Tirmidhi 1159 Ibn Hibbaan 4162; Swahihil Jaami'i 5294

<sup>527</sup> Sahihi: Ahmad 4/341, 6/419; Twabarani katika Al Awsat 532; Al Baani ameisahihisha katika As Silsilah As Swahihah

<sup>528</sup> Sahihi Mawquuf: An Nasaai katika 'Asharatun Nisaai 251 ni Mawquuf na isinadi yake ni sahihi

## Al - Kabair

---

Mtume ﷺ vile vile amesema:

وَيُرَوَّى عَنِ النَّبِيِّ ﷺ أَنَّهُ قَالَ: «مَنْ خَرَجَتْ مِنْ بَيْتِ زَوْجِهَا لِعَمَتِهَا  
الْمَلَائِكَةُ حَتَّى تَرْجِعَ أَوْ تَتُوبَ»<sup>(2)</sup>.

*“Mwanamke anapotoka nyumbani kwa mumewe (bila ya ruhusa)  
Malaika humlaani hadi arudi au atubu.”<sup>529</sup>*

Ummu Salamah رضي الله عنها amesema: Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*“Mwanamke yeyote atayekufa huku mumewe amemridhia basi  
ataingia peponi<sup>530</sup>.”* (Tirmidhi).

Wajibu ni mwanamke kutafuta radhi, na kuepuka hasira wala asijizuie kwake wakati wowote anaomtaka, asimkatalie mumewe akimtaka kama alivyosema Mtume ﷺ :

« إِذَا دَعَا الرَّجُلَ امْرَأَتَهُ إِلَى فِرَاشِهِ فَلْتَأْتِهِ وَإِنْ كَانَتْ عَلَى التَّنُورِ »

*“Wakati mume anamwita mkewe kitandani basi na amuendee hata  
kama ni ndani ya tanuri la moto<sup>531</sup>”* (Tirmidhi).

Wanazuoni wamesema: “Lazima akubali wito wa mumewe isipokuwa akiwa na hedhi au nifasi (kipindi cha uzazi) kwa hali hiyo inakatazwa kujamiiana, basi si halali kwake kumuitikia, wala mume kumuita mkewe wakati wa hedhi na nifasi, wala asijamiiane naye hadi aoge. Kwa Kauli ya Allah تعالى:

فَاعْتَرِلُوا الْبَيْتَ فِي الْمَحِيضِ وَلَا تَقْرُبُوهُنَّ حَتَّى يَطْهُرْنَ ﴿٢٢٢﴾

***“Waepukeni wanawake wala msiwakaribie mpaka  
wajitoharisha”. (2:222)***

---

<sup>529</sup> Ni maudhuu: Al Khatib katika at Taariikh 6/200, 1/221; Al Baani amesema katika Ad-Dhaiifah hiyo ni maudhuu 1020 na ameidhoofisha

<sup>530</sup> Dhaifu: Abu Shaibah 7/48/1 Tirmidhi 1171 Ibn Maajah 1854; Al-Baani katika dhaiifal Jaamii' 2226

## Al - Kabair

---

Ibn Qutaibah amesema:

يَطْهَرْنَ

'...wajitoharisha...".

Mpaka damu ikatike, inamaanisha yaani anapojitoharisha yaani wakaoga kwa maji. Wallahu 'Alam.

Imetangulia kauli ya Mtume ﷺ :

« من أتى حائضاً أو امرأة من دبرها فقد كفر بما أنزل على محمد »

"Mwenye kumingilia mwanamke mwenye hedhi au kwenye duburi yake amekufuru yaliyoteremshwa juu ya Muhammad<sup>532</sup>".

Katika hadithi nyingine:

« ملعون من أتى حائضاً أو امرأة في دبرها »

"Amelaaniwa mwenye kumingilia mwenye hedhi au mwanamke katika duburi yake<sup>533</sup>".

Nifasi ni kama hedhi, muda wake ni siku arobaini, kwa hivyo mwanamke hapaswi kumridhia mumewe endapo akitaka kumingilia akiwa na hedhi au nifasi, na amtii katika hali isiyokuwa hiyo (mwanamke haruhusiwi kumkatalia mumewe.)

Mwanamke anatakiwa ajue kuwa yeye yuko chini ya mume, hivyo anatakiwa kupata idhini ya mumewe katika utumiaji mali, anatakiwa awape fursa jamaa za mumewe kushinda jamaa zake. Ajiandae kumpumzisha (kustarehe na) mumewe kwa namna zote za usafi, wala

---

<sup>531</sup> Sahihi: Ahmad 4/22,23, At-Tirmidhi 1160, angalia As-Swahihah 1202 na Al Mishkaat 3257

<sup>532</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>533</sup> Maelezo yake yametangulia



## Al- Kabair

---

asijifakharishe dhidi yake kwa uzuri wake, wala asimtie aibu mumewe kwa ubaya wake (wa sura).

Al-Asma'iyy amesema: "Mie niliingia ndani ya nyumba ya wafugaji nikamuona mwanamke mzuri akiwa na mume mwenye sura mbaya nikamuuliza: "Unakubali vipi kuishi na mume kama huyo?" Akajibu: "Sikiliza wewe! Labda alifanya jambo zuri baina yake na Muumba Wake; kwa hiyo akanifanya mimi ndio zawadi yake, au pengine mimi nimefanya baya akanifanya kuwa ndio adhabu yangu."

Aisha رضي الله عنها amesema: "Enyi wanawake lau mngejua haki za waume wenu juu yenu basi mwanamke miongoni mwenu angefuta vumbi nyayo za mumewe kwa mashavu yake." Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« نساؤكم من أهل الجنة الودود التي اذت أو أذيت أتت زوجها حتى تضع يدها في كفه فتقول : لا أذوق غمضاً حتى ترضى »

*"Wake zenu wanaokuwa Peponi ni wenye upendo ambaye akiudhi au akiudhiwa huja kwa mumewe, hadi anaweka mkono wake na anamwambia: Sitolala hadi umeniridhia<sup>534</sup>."*

Inapasa kwa mke kudumu na haya mbele ya mumewe na kuinamisha kufumbia jicho lake mbele yake, lazima aonyeshe utiifu kwa mume, aache kumtazama mumewe kwa kejeli, amtii akimuamrisha, akae kimya anapozungumza, amkaribishe anapoingia na ampokee akiingia nyumbani, aepukane na lolote litakalomuudhi. Asimame kumuaga wakati anatoka nyumbani, amtiii wakati anamuita kitandani, awe mkweli kwake kuhusu yeye na mali yake ikiwa hayupo. Aweke mwili wake manukato, asafishe mdomo kwa mswaki na manukato, adumu na mapambo mbele yake, na aache kumsengenya. Awe mkarimu kwa jamaa zake na kidogo akione kingi."

---

<sup>534</sup> Sahihi: Imepokewa na An-Nasai katika kuingiliana na wanawake 257. At-Twabarani 19/140/307 katika Al Awswat 5648; Al Baani ameisahihisha katika swahihi Al-Jami' 2604.

## FADHILA YA MKE MTIIFU KWA MUMWE NA ADHABU KALI YA MKE MUASI

Inatakiwa mwanamke anayemuogopa Allah ﷻ kujitahidi kumtii Allah na kumtii mumewe na ajaribu kumfurahisha kwa sababu yeye ndiye pepo na moto wake kama alivyosema Mtukufu Mtume ﷺ:

*“ Mwanamke yeyote anayekufa ilhali mumewe wake amefurahikiwa naye ataingia peponi<sup>535</sup>. ”*

Vile vile ﷺ amesema:

*“ Mwanamke akiswali Swala zake tano, akafunga mwezi wake, (Ramadhani). Akajitunza heshima yake na anamtii mumewe basi anaingia peponi kwa mlango wowote autakao<sup>536</sup>. ”*

Vile vile imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

*“ Ndege hewani na samaki baharini, Malaika mbinguni, Jua na Mwezi wanamuomba msamaha mke mtiifu madamu yuko katika radhi ya mumewe<sup>537</sup>. Mke yeyote mwenye kumuasi mumewe yupo katika laana ya Allah na malaika wake, na watu wote. Mwanamke yeyote anayemkunja uso mumewe yumo katika hasira za Allah hadi amchekeshe na amridhishe. Mwanamke yeyote aliyetoka nyumbani kwake bila ya ruhusa ya mumewe Malaika wanamlaani hadi arudi ”<sup>538</sup>.*

Mtukufu Mtume ﷺ amesema:

*“ Wanawake wane wataingia peponi, na wane wataingia motoni; Ama wane ambao ni wa peponi, ni mwanamke mwenye kujihifadhi,*

---

<sup>535</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>536</sup> Sahihi: Ibn Hibbaan 4163 twabarani katika Al Awswat 4598; Al Baani amesahihisha katika Swahihil Jaamii 661

<sup>537</sup> Sijaiona Hadithi hii.

<sup>538</sup> Sijaiona

*mwenye kumtii Allah na mumewe, Mwenye kizazi, mwenye subira mwenye kutosheka na kichache pamoja na mumewe, ana haya. Mumewe akiwa mbali naye anahifadhi nafsi yake na mali yake, na akiwa yupo anazuia ulimi wake dhidi yake. Wane; Mwanamke ambaye mumewe amefariki na akamwachia watoto wadogo basi hujishughulisha kuwalea watoto na kuwafanyia wema haolewi kwa kuhofia kupotezwa (watoto wake). Ama wanne wa motoni: ni mwanamke mwenye ulimi mchafu wa maneno, mumewe akiwa hayupo nyumbani, halindi heshima yake na akiwepo anamuudhi kwa ulimi wake. Wa pili: Mwanamke anayemlazimisha mumewe asiyoyaweza. Wa Tatu: mwanamke asiyeficha nafsi yake kwa wanaume na anatoka nje ya nyumba yake bila kujisitiri. Wa Nne: Mwanamke ambaye hamu yake ni kula na kulala na kuvaa na hana hamu ya Swala, wala kumtii Allah, wala Mjumbe Wake, wala katika kumtiiii mumewe". "Mwanamke mwenye sifa hizi na anatoka kwenye nyumba yake bila idhini ya mumewe analaaniwa. Naye ni miongoni mwa watu wa motoni isipokuwa atubie kwa Allah" <sup>539</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

*"Niliangalia motoni nikaona wengi wa wakazi wake ni wanawake<sup>540</sup>."*

Sababu yake ni uchache wa kumtii kwao Allah, Mjumbe wake ﷺ na mumewe na wingi wao wa kutoka nje hovyoyote na kudhihirisha mapambo.

*Tabbarruj* ni anapotaka kutoka anavaa nguo za fahari na kujipamba na anatoka kuvutia watu, kama akisalimika na watu na nafsi yake basi watu hawasalimiki nae.

Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>539</sup> Sahihi: na Imepokewa na Sa'ad kwa lafdhi nyingine, angalia Sahihil Jamii 887

<sup>540</sup> Al-Bukhari 3241 Muslim 2737

« المرأة عورة فإذا خرجت من بيتها استشرفها الشيطان »

*“Mwanamke ni uchi anapotoka nyumbani mwake shetani anamuangalia” (Sahih: At-Tirmidhy 1173; Ibn Hibban 5598; 5599; Sahihil Jami’i 6690*

Kubwa zaidi kwa mwanamke kutoka kwa Allah ni kuwa nyumbani, na katika hadithi:

« المرأة عورة فاحبسوها في البيوت »

*“Mwanamke ni uchi basi mfunjeni nyumbani”<sup>541</sup> .*

Mwanamke anapotoka watu wake wanamuuliza: Unaelekea wapi? Anasema nazuru mgonjwa, nasindikiza jeneza, basi shetani haachi kuwa naye hivyo mpaka anatoka nyumbani mwake, ilhali hajatafuta radhi za Allah kama vile kukaa kwake nyumbani, na kumuabudu Mola Wake, na kumtii mumewe.

Ali bin Abu Talib alimuuliza mkewe Fatimah binti wa Mtume ﷺ: “Ewe Fatimah nini kheri ya mwanamke?.” Yeye alijibu: “Asiwaone wanaume wala wao wasimuone”. Ali alikuwa anasema: ‘Hivi hamuoni haya, wala hamuoni wivu ikiwa mmoja wenu anamuachia mkewe kwenda kati ya wanaume anawaangalia.”

Na kubwa zaidi linalokuwa kwa mwanamke mbele ya Allah ni anapokuwa nyumbani kwake. Na katika hadithi:

Siku moja Aisha na Hafsah walikuwa wamekaa kwa Mtume ﷺ Akaingia Ibn Ummu Maktuum akasema:

« احتجبا منه »

*“Jificheni dhidi yake”.*

---

<sup>541</sup> Sijaiona

Wakasema: “Yeye ni kipofu hatuoni wala hatujui” ,

«أفعمياوان أنتما ألتما تبصرانه ؟ »

“Kwani nyinyi ni vipofu hamumuoni yeye?<sup>542</sup>”.

Kama ambavyo inapasa kwa mwanamume kufumba jicho lake kwa wanawake vile vile inapasa kwa mwanamke kufumba jicho lake kwa wanaume. Kama ilivyotangulia kwenye kauli ya Fatimah kuwa kheri kwa mwanamke ni kutoona wanaume wala wasimuone yeye”. Kama akilazimika kutoka kumtembelea mzazi wake na jamaa zake na maliwato na mfano wake katika asiyo na budi nayo basi atoke kwa idhini ya mumewe pasina kudhihirisha mapambo, wala nguo za kubana wala chafu na ainamishe macho yake katika kutembea kwake. Aangalie ardhini si kulia wala kushoto, na asipofanya hivyo anakuwa mwenye kuasi. Kimeelezwa kisa kuwa kulikuwa na mwanamke mmoja ambaye alikuwa hajisitiri, na alikuwa anatoka katika nyumba yake *mutabbarrijah* akafa, baadhi ya ndugu zake wakamuona usingizini amepelekwa mbele ya Allah akiwa na nguo laini basi upepo ukavuma Allah akampa mgongo, akasema: “Mchukueni upande wa kushoto hadi motoni kwani yeye alikuwa miongoni mwa *mutabbarrijah* katika dunia.”

Ali bin Abu Talib alisema: Mimi na Fatmah tuliingia kwa Mtume ﷺ tukamkuta analia sana kwa uchungu. Nikamwambia: Baba yangu na mama yangu wawe muhanga kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Allah, ni kitu gani kinachokuliza?’ Mtume ﷺ akajibu:

« يا علي ليلة أسرى بي إلى السماء رأيت نساء من أمي يعذبن بأنواع العذاب ،  
فبكيت لما رأيت من شدة عذابهن ، ورأيت امرأة معلقة بشعرها يغلي دماغها ،  
ورأيت امرأة معلقة بلسانها والحميم يصب في حلقها ، ورأيت امرأة قد شددت

---

<sup>542</sup> Dhaifu: Abu Dawud 4112 Tirmidhi 2778; Al Baani ameidhoofisha katika Al Irwaa 1806 na Al Mishakaat 3116.

رجلاها إلى تدييها ويداها إلى ناصيتها ، ورأيت امرأة معلقة بتدييها ، ورأيت امرأة رأسها رأس خنزير وبدنها بدن حمار عليها ألف ألف لون من العذاب ، ورأيت امرأة على صورة الكلب والنار تدخل من فيها وتخرج من دبرها والملائكة يضربون رأسها بمقامع من نار «

*“Ewe ‘Ali wakati wa safari yangu ya usiku kwenda mbinguni niliwaona wanawake wa uma wangu wanaadhibiwa adhabu aina za adhabu, kwa hiyo nikalia kutokana na adhabu kali niliyoiona. Nilimuona mwanamke akining’inizwa kwa nywele zake na ubongo wake unachemka, mwanamke mwingine akining’inizwa kwa ulimi wake na anamiminiwa maji ya moto katika koromeo lake, na nimemuona mwanamke amefungwa miguu yake kwenye matiti yake na mikono yake imefungwa utosi mwake. Na nimemuona mwanamke ananing’inizwa kwa matiti yake. Nimemuona mwanamke kichwa chake cha nguruwe na kiwiliwili cha Punda, na juu yake kuna aina elfu za adhabu. Nimemuona mwanamke akiwa na sura ya mbwa na moto unaingia mdomoni mwake na ukitoka katika duburi yake malaika walikuwa wakimtandika kichwani mwake kwa nyundo za moto”.*

Fatimah akasimama akasema: “Ewe baba yangu mpenzi ni vitendo gani vya wanawake hao walivyovifanya vilivyo sabababisha adhabu hizo?”

Mtume ﷺ akasema:

« يا بنية أما المعلقة بشعرها فإنها كانت لا تغطي شعرها من الرجال، وأما التي كانت معلقة بلسانها فإنها كانت تؤذي زوجها ، وأما المعلقة بتدييها فإنها كانت تفسد فراش زوجها ، وأما التي تشد رجلاها إلى تدييها ويداها إلى ناصيتها وقد سلط عليها الحيات والعقارب فإنها كانت لا تنظف بدننها من الجنابة والحيض وتستهنئ بالصلاة ، وأما التي رأسها رأس خنزير وبدنها بدن حمار فإنها كانت نمامة كذابة ، وأما التي على صورة الكلب والنار تدخل من فيها وتخرج من دبرها فإنها كانت منانة حسادة ، ويا بنية الويل لامرأة تعصي زوجها»

*“Ewe binti yangu, aliyening’inizwa kwa nywele zake alikuwa hajifuniki nywele zake mbele ya wanaume, aliyening’inizwa kwa ulimi wake, alikuwa akimuudhi mumewe, yule aliyening’inizwa kwa matiti yake alikuwa akifisidi tandiko la mumewe, aliyekuwa miguu yake imefungwa kwenye matiti yake utosini mwake, na mikono yake kwenye utosi wake na amesalitishiwa nyoka na ng’e alikuwa hasafishi mwili wake kutokana na janaba na hedhi, na alikuwa akikejeli Swala, na mwenye uso wa nguruwe na kiwiliwili cha punda alikuwa akisambaza maneno ya kashfa, na yule aliyekuwa na sura ya mbwa na moto ukiingia mdomoni mwake na kutoka duburini mwake alikuwa msimbulizi hasidi. Ewe binti yangu ole wake mwanamke anayemuasi mumewe<sup>543</sup>”*

Mu’adh bin Jabal رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« لا تُوذِي المرأة زوجها في الدنيا إلا قالت زوجته من الحور العين : لا تُوذيه قاتلك الله »

*“Mwanamke hamuudhi mumewe hapa duniani isipokuwa Huuril`ain watamwambia: “Usimuudhi huyo Allah atakuangamiza<sup>544</sup>”*

### **WAJIBU WA MWANAMUME KWA MKEWE**

Ikiwa mke anaamriwa kumtii mumewe na kutafuta radhi yake, mume pia anaamriwa kumfanyia hisani, upole, subira kwa mabaya yanayojitokeza kwake na mengine, na kumpa haki yake kama vile matumizi na mavazi, na tangamano zuri kwa Kauli Yake Allah Aliyetukuka:

وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ

**“Na kaeni nao kwa wema”(4:19)**

---

<sup>543</sup> Sijaiona japokuwa uongo wake uko wazi

<sup>544</sup> Sahihi: Ahmad 5/242; At Tirmidhy 1184; Ibn Majah 2014; Sahihah 1/513

Na kauli ya Mtume ﷺ :

« استوصوا بالنساء ، ألا إن لكم على نساءكم حقاً ولنساءكم عليكم حقاً  
فحقهن عليكم أن تحسنوا إليهن في كسوتهن وطعامهن ، وحقكم عليهن  
أن لا يوطئن فرشكم من تكرهون ، ولا يأذن في بيوتكم لمن تكرهون»

*“Nakuusieni kuhusu wanawake! hakika nyiye mna haki juu ya wanawake wenu, na wao wana haki juu yenu, haki zao juu yenu ni kuwafanyia vizuri katika mavazi yao na chakula chao. Na haki yenu juu yao kutomlaza kwenye godoro lenu mnayemchukia wala wasimkaribishe nyumbani kwenu mnaowachukia.”<sup>545</sup>*

Mtume ﷺ akasema:

« خيركم خيركم لأهله »

*“Mbora wenu ni aliye mbora kwa mkewe”<sup>546</sup>.*

Katika maelezo mengine:

« خيركم أطفلكم بأهله »

*“Mbora wenu ni mpole wenu zaidi kwa watoto wake”.*

ni yule atakayekuwa mwenye huruma juu ya mkewe zaidi. Mtukufu Mtume ﷺ mwenyewe alikuwa ni mwenye huruma kwa wanawake.

Mtume ﷺ vile vile alisema:

« أيما رجل صبر على سوء خلق امرأته أعطاه الله الأجر مثل ما أعطى أيوب  
عليه السلام على بلائه ، وأيما امرأة صبرت على سوء خلق زوجها أعطاه  
الله من الأجر مثل ما أعطى آسية بنت مزاحم امرأة فرعون»

---

<sup>545</sup> Muslim 1218

<sup>546</sup> Tirmidhi 3895; Daarami 260; Ibn hibbaan 4177; As Swahihah 1/513



*“Ikiwa mwanamume ataonyesha ustahamilivu juu ya mkewe mwenye tabia mbaya Allah atamtunukia zawadi sawasawa na aliyompa Ayyub kwa subira yake. Na mwanamke akifanya subira kwa mumewe mwenye hasira mbaya Allah atampa zawadi sawasawa na aliyopewa Asiyah binti Muzahim, mke wa Firauni<sup>547</sup>”.*

Imetolewa taarifa kuwa mtu alikwenda kwa ‘Umar ibn al-Khattab na kumlalamikia kuhusu mkewe. Akasimama mlangoni kwa ‘Umar akamsikia mke wa ‘Umar akimgombeza ‘Umar na ‘Umar alikaa kimya akimsikiliza mkewe wala hakumjibu. Mtu yule aligeuka na akaanza kwenda zake huku akijisemea mwenyewe: ikiwa hali ni hiyo kwa ‘Umar kiongozi wa waumini na aliyekuwa akisifika kwa ukakamavu wake na umadhubuti itakuwa hali gani miye maskini dhaifu?. ‘Umar alipotoka nje na kumuona yule mtu anakwenda zake alimwita na akamwambia ni jambo gani ulilokuja nalo?

Akamjibu: “Ewe kiongozi wa waumini nimekuja kulalamika kwako kuhusu tabia mbaya ya mke wangu ya kuwa ana ghadhabu mbaya na namna anavyonung’unika kwangu, lakini nilipofika hapa nikamsikia mkeo akifanya hivyo hivyo kwako, basi nikarejea huku nikijisemea: “Ikiwa hivyo ndivyo hali kwa kiongozi wa waumini je, itakuwa vipi kwangu?”

‘Umar akajibu: “Ewe ndugu yangu miye ninamstahamia kwa kuwa yeye anazo haki zake juu yangu: ananipikia, ananiokea mikate, ananifulia nguo zangu, anawanyonyesha watoto wangu...yote hayo si wajibu kwake na zaidi yeye ni kiburudisho wangu na huniweka mbali na matendo yaliyokatazwa ndiyo maana nastahamili. Yule mtu akasema ni sawa sawa kisa chako na changu ewe kiongozi wa waumini: ‘Umar akamwambia sasa ndugu yangu kuwa na subra naye kwani ni kwa muda mfupi tu (yaani maisha mafupi).

---

<sup>547</sup> Sijaiona

### HADITHI (KISA)

Kisa kinasimuliwa kuwa kulikuwa na mmojawapo katika waja wema alikuwa na ndugu yake kwa ajili ya Allah, na mja yule vile vile ni katika waja wema, alikuwa akimtembelea kila mwaka mara moja. Alikwenda katika ziara moja na akagonga mlango, mwanamama mwenye nyumba akauliza, 'Nani wewe?' Yeye akajibu (nduguyo) wa mume wako miye nimekuja kumzuru.

Yule mwanamke akamjibu: "Amekwenda kutafuta kuni, inshallah Allah asimrudishe na Allah ﷻ amvunje mifupa yake amenifanyia kadha wa kadha.' na akaendelea kumkashifu mumewe, rafiki yake akasimama mlango na kumsikiliza namna anavyoropokwa, wakati akiwa katika hali hiyo rafiki yake alirudi kutoka mlimani na alikuwa akimuongoza simba aliyebeba huo mzigo wa kuni na huku akifuatana na huyo bwana. Alipofika alimsalimu rafiki yake na kumkaribisha ndani, akaingia ndani na akautua mzigo wake wa kuni na akamwambia simba: 'Nenda Mwenyezi Mungu akubariki." Baada ya hapo akamkaribisha ndugu yake na mwanamke akiendelea kusumbuka na kukashifu lakini yeye hakumwambia hata neno moja. Mgeni alikaa kwa muda na baada kupata chakula akaondoka huku akimhusudu rafiki yake kwa ustahamilivu aliokuwa nao juu mwanamke mwenye gubu.

Amesema: Ulipofika mwaka wa pili alikwenda tena kumtembelea ndugu yake yule kama ilivyo ada yake, alipofika kwake akagonga mlango na kutoka kule ndani ya nyumba mwanamke akauliza: 'Nani?' akamjibu: "Ndugu wa mume wako fulani-bin-fulani' Akamjibu, 'karibu tafadhali pita ukae, In sha Allah mume wangu atarudi karibuni tu.' Mwanamume akashangaa kwa tabia ilikuwa nzuri, sifa ya mazungumzo, mapokezi mazuri, baada ya muda mfupi mumewe akarudi huku amebeba mzigo wa kuni mgongoni mwake na kitendo hicho kilimzidisha kustajaabu.

Walikaa na wakizungumza kwa raha wakati mkewe akiwaandalia na kuwapa chakula chenye ladha na kujumuika katika mazungumzo yao

ulipofika wakati wa kuondoka mgeni hakuweza kustahmili na akamuuliza mwenyeji wake, 'Ndugu yangu ninaweza kukuuliza kitu?' Mwenyeji akamwambia: "Ni kitu gani ndugu yangu?" Akasema: "Mwaka jana nilipokuja mkeo alikuwa na kauli chafu na tabia mbaya na nikakuona unakuja kutoka mlimani huku simba amebeba mzigo wa kuni, mwaka huu ninamuona mkeo ana nidhamu na mtaratibu na siyo mwenye hasira na wewe mwenyewe umebeba mzigo wa kuni mgongoni mwako. Je, ni nini sababu yake?' Mwenyeji wake akatabasamu na akamwambia ndugu yake: "Mke wangu wa kwanza amefariki kama unavyojua alikuwa na hasira mbaya na mwenye matusi lakini nilimstahamia zawadi ya stahamala yangu Allah ﷻ alinipa uwezo wa kumdhibiti simba na nikawa ninamtumia simba kama punda. Alipofariki mke wangu wa kwanza nilimuoa mwanamke mwema na nipo katika amani naye Allah akampa uhuru simba katika udhibiti na nikawa ninabeba mzigo wangu mwenyewe kwa amani na raha ninayoipata kutoka kwa mke huyu, mwenye tabia njema, aliyebarikiwa, mtiifu.

Tunamuomba Allah Aturuzuku subira katika yanayopasa na kuridhia, hakika Yeye ni Mkwasi.

\*\*\*

DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA NANE

MASANAMU

KUFANYA PICHA KATIKA NGUO, KUTA, MAWE NA  
VITU VINGINE KWA MSHUMAA, NTA, RANGI AU  
KITU KIPYA KAMA SHABA, SUFU N.K  
NA AMRI ZA KUZIHARIBU

Kutokana na nguo au mawe, au sarafu au kitu chochote, kutokana na nta au chuma au kuchora, au ubao au kitu chengine, amri iliyopo ni kuiharibu. Allah تعالیٰ Aliyetukuka Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يُؤْذُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَأَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا مُهِينًا ﴿٥٧﴾

***“Hakika wanao muudhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Mwenyezi Mungu Amewalaani duniani na Akhera, na amewaandalia adhabu ya kufedhehi” . (33:57)***

Ikrimah anasema: “Hao wanaofanya masanamu na picha”. Ibn ‘Umar anatoa taarifa kutoka kwa Mjumbe wa Allah kuwa amesema:

رَقَالَ [النَّبِيُّ ﷺ] <sup>(٣)</sup>: «أَشَدُّ النَّاسِ عَذَابًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ الْمُصَوَّرُونَ، يُقَالُ لَهُمْ: أَحْيُوا مَا خَلَقْتُمْ» <sup>(١)</sup> متفق عليه.

*“Siku ya kufufuliwa kiyama wale wanaotengeneza masanamu au picha watapewa adhabu na wao wataambiwa vitieni uhai hivyo mlivyovitengeneza.” (Bukhari na Muslim). <sup>548</sup>*

Aisha رضي الله عنها amesema: Mtume wa Allah ﷺ alirudi safari niliweka pazia ndani yake kuna picha, alipoiona uso wake ulibadilika rangi akasema:

---

<sup>548</sup> Bukhari 5951,7558; Muslim 2108

## Al- Kabair

---

« يا عائشة : أشد الناس عذاباً يوم القيامة الذين يضاهئون بخلق الله عز وجل »

*“Ewe Aisha, wenye adhabu kali siku ya kiama ni wanaojifananisha na uumbaji wa Allah Taalaa”. Aishah akasema: ‘Nikalikata na kufanyia mito miwili.” (Bukhari na Muslim)<sup>549</sup>*

Ibn ‘Abbas anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« كل مصور في النار ، يجعل له بكل صورة صورها نفس يعذب بها في نار جهنم »

*“Kila mtengeneza picha ataingia motoni, atafanyiwa picha anaadhibiwa nayo katika moto wa Jahannamu”. Sahihi mbili<sup>550</sup>*

Imepokewa tena kwake amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ anasema:

« من صور صورة في الدنيا كلف أن ينفخ فيها الروح يوم القيامة وليس ينفخ فيها أبداً »

*“Mwenye kutengeneza picha duniani atalazimishwa kuzipulizia roho naye si mwenye kupuliza humo abadan<sup>551</sup>”.*

Amesema tena Mtume ﷺ :

« يقول الله عز وجل : ومن أظلم ممن ذهب يخلق كخلقي ، فليخلقوا حبة ، أو ليخلقوا شعيرة ، أو ليخلقوا ذرة »

*“Ni nani dhalimu mkubwa kuliko anayenda huku anaumba kama uumbaji wangu, basi na waumbe japo punje moja, na waumbe japo ngano, au waumbe japo punje ya mtama”. Imepokewa na Bukhari na Muslim<sup>552</sup>.*

---

<sup>549</sup> Bukhari 5954; Muslim 2106

<sup>550</sup> Bukhari 2225; Muslim 2110

<sup>551</sup> Bukhari 5963; Muslim 2110

<sup>552</sup> Bukhari 5953,7559; Muslim 2111

## Al - Kabair

---

Mtume ﷺ anasema:

« يخرج عنق من النار يوم القيامة فيقول : إني وكلت بثلاثة : بكل من دعا مع الله آلهما آخر ، وبكل جبار عنيد ، وبالمصورين »

*“Siku ya kiama kutatoka shingo motoni itasema: nimewakilishwa kwa watatu; kwa kila aliyeomba Allah pamoja na miungu mwingine, na kila jabari mwenye inadi, na watengeneza picha<sup>553</sup>”.*

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema:

« لا تدخل الملائكة بيتا فيه كلب ولا صورة »

*“Malaika hawaingii nyumba ndani yake kuna mbwa au picha<sup>554</sup>”.*  
Bukhari na Muslim.

Katika Sunan Abu Dawud kutoka kwa Ali bin Abi Twaalib amesema:  
Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« لا تدخل الملائكة بيتا فيه كلب ولا صورة ولا جنب »

*“Malaika hawaingii nyumba ndani yake kuna mbwa au picha au mwenye janaba<sup>555</sup>”.*

Al-Khattwabi رحمه الله تعالى amesema: Kauli yake Mtume ﷺ:

« لا تدخل الملائكة بيتا فيه كلب ولا صورة ولا جنب »

*“Malaika hawaingii nyumba ndani yake kuna mbwa au picha au mwenye janaba”*

---

<sup>553</sup> Ahmad 2/336; Tirmidhi 2574; Swahiihil Jaami'i 8051

<sup>554</sup> Bukhari 5948,5958 Muslim 2106

<sup>555</sup> Dhaifu: Ahmad 1/83,104, 139, 150, Abu Dawud 227 Nasaai 1/141 Shaykh ameidhoofisha katika dhaiifil Jaami'i 6203

## Al- Kabair

---

Anakusudia wale Malaika wanaoteremka na rehema na baraka na sio wale malaika wenye kuhifadhi amali za watu, hawatofautishi awe ni mtu mwenye janaba na asiye na janaba, na inasemekana: kuwa haikusudiwi mwenye janaba aliyepatwa na janaba na akachelewesha kukoga hadi inapofikia muda wa Swala, lakini ni yule anayepatwa na janaba wala haogi na huzembea kuoga na hiyo imekuwa ni tabia yake, kwani Mtume ﷺ alikuwa akiwatembelea wake zake kwa joshu moja tu<sup>556</sup>.” Na huku ni kuchelewesha kukoga wakati wake wa mwanzo inapokuwa ni wajibu kufanya hivyo. Mama ‘Aisha رضي الله عنها amesema: “Mtume ﷺ alikuwa akilala akiwa na janaba wala hagusi maji<sup>557</sup>.”

Ama kuhusu mbwa, ni kumfuga mbwa si kwa ajili ya kilimo wala kuwinda, ama atakaposongeka kwenye hilo hakuna kosa kwake katika baadhi ya mambo, au kwa ajili ya kulinda nyumba yake, hakuna kosa kwake in shaa Allah.

Ama picha, ni picha ya chenye roho, ni sawa iwe ni ya mtu aliyesimamishwa au iliyonakishiwa sakafuni au ukuta au ikawekwa katika mtindo, au ikafumwa katika nguo au mahali, kwani hukumu ya ujumla inakuwa kwake basi na aiepuke. Wabillaahit–Tawfiqi.

Inapasa kuharibu picha kwa mwenye kuweza na kuziondoa. Muslim amepokea katika Sahihi yake kutoka kwa Hayyaan bin Huswain amesema: Ali bin Abi Twaalib ameniambia: “Nikutume juu ya lile alilonituma juu yake Mtume? Usiache picha yoyote ila utafuta, wala kaburi lililoinuka isipokuwa ulisawazishe”.<sup>558</sup>

Tunamuomba Allah Taufiqi kwa anayo yapenda na kuyaridhia hakika Yeye ni Mpaji Mkarimu.

\*\*\*

---

<sup>556</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 109.

<sup>557</sup> Abu Dawud 228; Tirmidhi 118,119; Ibn Maajah 581; Swahihil Jaami'i 5019

<sup>558</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 1/96, 128 na Muslim 669.

**DHAMBI KUBWA YA ARUBAINI NA TISA**

**KUJIPIGA MAKOFI, KUOMBOLEZA, KUCHANA NGUO, KUNYOA  
KICHWA, MENGINE YA HAYO, NA KUOMBA MAANGAMIVU  
WAKATI WA MSIBA**

Abdullah Bin Mas'uud anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ anasema:

« ليس منا من لطم الخدود وشق الجيوب ودعا بدعوى الجاهلية »

*“Si katika mimi mwenye kujipiga mashavu yake, anayechana mifuko yake, na akaomba dua za kijahilia<sup>559</sup>”.*

Imepokewa katika sahihi mbili kutoka kwa Abu Musa Al-Ash'ary kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« بريء من الصالفة والخالقة والشاقة »

*“Yuko mbali na mwenye kupiga mayowe (katika msiba) na mwenye kunyoa kichwa chake upara (kwa msiba), na mwenye kuchana nguo zake (wakati wa msiba)<sup>560</sup>”*

Pia ni haramu kutimua nywele, kujipiga mashavu, kukwaruza uso na kuomboleza. Imepokewa kutoka kwa Ummu 'Attwiyyah kuwa amesema: “Mtume ﷺ amechukua kwetu ahadi katika Al-Bay`ah kuwa hatutaomboleza.”<sup>561</sup> Ameipokea Bukhari

Abu Hurairah رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mtume wa Allah ﷺ amesema:

---

<sup>559</sup> Ameipokea Ahmad 1/432,456, Bukhari 1297, 2197. Muslim 103

<sup>560</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>561</sup> Sahihi ameipokea Ibn Abu Shaybah 3/389. Ahmad 6/496. Bukhari 1306, 3892,7215. Muslim 936.



## Al-Kabair

---

« اثنتان في الناس بهما كفر: الطعن في الأنساب والنياحه على الميت »

*"Mambo mawili kwa watu ni ukafiri: kukosoa nasaba na kuomboleza maiti."* (Muslim)<sup>562</sup>.

Abu Said Al-Khudhri رضى الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amemlaani mwenye kuomboleza na mwenye kumsikiliza. Abu Dawud<sup>563</sup>

Abu Burda رضى الله عنه alisema kuwa Abu Musa Ash'ari aliugua akazimia na kichwa chake kiko katika chumba cha mkewe mmojawapo, yule mkewe akawa anaomboleza kwa kilio. Abu Musa Ash'ari hakuweza kumzuia, alipozinduka akasema: "Mimi nimejitenga na alichojitenga nacho Mtume wa Allah ﷺ, Mtume wa Allah ﷺ alikuwa mbali na wanawake wanaomboleza na wanaonyoa vipara vichwa vyao na wanaochana nguo zao."<sup>564</sup>

Nu'man bin Bashiir amesema kuwa wakati Abdullah bin Rawahah alipozimia, dada yake akaanza kulia na kupiga kelele, 'Ahh!! Kadha, Ahh kadha!!' Alipozinduka Alisema:

*"Hukusema chochote isipokuwa niliambiwa, wewe uko kadha, wewe uko kadha."* (Bukhari).<sup>565</sup>

Katika sahihi mbili kuwa Mjumbe wa Allah alisema:

« الميت يعذب في قبره بما نوح عليه »

*"Maiti huadhibiwa kaburini kwa aliyoombolezewa."*<sup>566</sup>

---

<sup>562</sup> Sahihi ameipokea Ibn Abu Shaybah 3/39. Ahmad 2/496. Muslim 67

<sup>563</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>564</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>565</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 4267

<sup>566</sup> Sahihi: Al-Bukhari 1292 na Muslim 927

## Al - Kabair

---

Abu Musa amesema: Hakuna maiti anayekufa na akasimama mliaji akasema: 'Ewe bwana wangu, ewe jabali langu, na kadha wa kadha, na mfano wake na kunakuwa na malaika wanamwambia: Hivyo ndivyo ulivyo?' (Tirmidhi)<sup>567</sup>

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« النائحة إذا لم تتب قبل موتها تقام يوم القيامة وعليها سربال من قطران ودرع من جرب »

*"Ikiwa mwanamke aliyeomboleza na hakutubia kabla ya kifo chake basi siku ya kiama atakuwa na nguo za lami na shati la lami."*<sup>568</sup>

Akasema Mtume ﷺ :

« إنما نهيت عن صوتين أحمرتين فأجرين: صوت عند نعمة ولهو ولعب ومزامير شيطان ، وصوت عند مصيبة خمش في وجوه وشق في جيوب ورنه شيطان »

*"Nimekatazwa sauti mbili za kipumbavu na ovu: sauti wakati wa kuimba, pumbao mchezo na zumari za shetani, na sauti wakati wa msiba, kurarua nyuso, kuchana mifuko, na kuimba kwa mlio wa shetani"*<sup>569</sup>.

Al-Hasan alisema: "Sauti mbili zimelaaniwa – zumari wakati wa kuimba, na maombolezo wakati wa msiba."

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« إن هذه النوائح يجعلن صفتين في النار فينبحن في أهل النار كما تنبح الكلاب »

---

<sup>567</sup> Hasan Tirmidhi 1003, Ibn Majah 1594, Al- Baani ameifanya Hasan katika sahihi al Jaami'i 801.

<sup>568</sup> Sahihi Muslim 934, Ahmad 5/342, 343.

<sup>569</sup> Hasan: Al Haakim 4/40 na ina ushahidi wa hadithi: 'Sauti mbli zimelaaniwa.' na Shaykh ameifanya Hasan katika Sahihi 427, na sahihi Al Jaamii 3801.

## Al - Kabair

---

*“Hakika maombolezo haya yatafanya mistari miwili ndani ya moto na yatabweka kwa wakazi hao kama mbwa wanavyobweka.”<sup>570</sup>*  
(Twabarani)

Awzai amesema: “Umar Ibn Al-Khattab alisikia sauti ya kuomboleza (inayotokea ndani ya nyumba) akaingia humo pamoja na watu wengine. Akawapiga hadi akamfikia mwenye kuomboleza akampiga mpaka mtandio wake ukaanguka. Akasema: Mpige kwa kuwa yeye ni muombolezaji hakuna kumhurumia, halii kwa msiba wenu bali anamwaga machozi achukue dirihamu zenu, na anawaudhi maiti zenu kaburini mwenu, na wahai wenu katika nyumba zenu kwani anakataza subira ambayo Allah تعالٰيameiamuru, na anakuamuruni kubabaika wakati Allah تعالٰيamekataza.

Tambua ya kuwa kuomboleza: ‘ni kupaza sauti kwa manung’uniko, na muombolezaji kutaja mazuri ya maiti.’ Kumesemwa pia: ‘ni kumlilia na kutaja mema yake.’

Wanazuoni wamesema: ‘Ni haramu kupaza sauti kwa kupitiliza katika kulia. Ama kulia kimya kimya bila ya kutoa sauti au kuomboleza si haramu.’

Katika sahihi Bukhari na Muslim kumesimuliwa kuwa Abdullah bin ‘Umar amesema: Wakati Sa’ad bin ‘Ubaadah alipolalamika (kuhusu) tabu (fulani) Mjumbe wa Allah ﷺ alikwenda kumzuru yeye na alifuatana na ‘Abdu Rahman bin ‘Auf, Sa’ad bin Abi Waqqaas na ‘Abdullah bin Mas`uud wakaingia na walipomuona (Sa’ad bin ‘Ubaadah) amepoteza fahamu Mtume ﷺ akalia na watu walipoona kilio cha Mtume ﷺ wakalia, Mtume ﷺ akasema:

« أَلَا تَسْمَعُونَ إِنَّ اللَّهَ لَا يُعَذِّبُ بِدَمْعِ الْعَيْنِ وَلَا بِحُزْنِ الْقَلْبِ ، وَلَكِنْ يُعَذِّبُ  
بِهَذَا أَوْ يَرْحَمُ »

---

<sup>570</sup> Dhaifu ameipokea Twabarani katika Al Awswat 5229 na isinadi yake ni dhaifu.

## Al - Kabair

---

*“Sikilizeni kwani hamkusikia kuwa Allah haadhibu kwa machozi ya macho wala kwa huzuni ya moyo, lakini huadhibu kwa huu au anarehemu’.* Akaashiria kwa ulimi wake.<sup>571</sup>

Tumesoma katika sahihi mbili kwa Usamah bin Zaid رضي الله عنه Mjumbe wa Allah ﷺ alimnyanyua mtoto wa bint yake, Ibrahim anaugulia nafsi yake, macho ya Mtume ﷺ yakabubujika machozi. Sa’ad akauliza: “Nini hiki ewe Mjumbe wa Allah?”.

Akamjibu:

« هذه رحمة جعلها الله في قلوب عباده ، وإنما يرحم الله من عباده الرحماء »

*“Hii ni rehema Allah ameiweka ndani ya nyoyo za waja wake, si vinginevyo Allah huwarehemu miongoni mwa waja wake walio warehemevu”<sup>572</sup>.*

Sahihi mbili zimeandika kuwa Anas رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa wakati Mjumbe wa Allah ﷺ alipokwenda kumzuru mtoto wake Ibrahim wakati akiugulia nafsi yake, machozi yalimdongoka machoni mwake, ‘Abdu Rahman bin ‘Auf akahoji: “Hata wewe ewe Mjumbe wa Allah?”.

Mjumbe wa Allah ﷺ akasema:

« يا بن عوف إنها رحمة »

*“Ewe Ibn ‘Auf, hii ni rehema”.*

Kisha akabubujika chozi jingine akasema:

« إن العين لتدمع والقلب يحزن ، ولا نقول إلا ما يرضي ربنا وإنما بفراقك يا إبراهيم لمحزونون »

---

<sup>571</sup> Sahihi Bukhari 1304, Muslim 924

<sup>572</sup> Ameipokea Ibn Abu Shaybah 3/392 Ahmad 5/204 Bukhari 1284, Muslim 923.

## Al - Kabair

---

*"Hakika macho yabubujika na moyo unahuzunika, wala hatusemi isipokuwa linalomridhisha Mola Wetu, na sisi kwa kuachana nawe Ibrahim tunahuzunika"<sup>573</sup>.*

Ama katika hadithi Sahihi: Ni kuwa maiti anaadhibiwa kwa kulia watu wake, hiyo si katika dhahiri yake isipokuwa hiyo ni *Taawili* (tafsiri ya ndani) na wanazuoni wakatofautiana juu ya *Taawili* yake kwa kauli kadhaa, ya dhahiri ni kuwa hiyo inabebwa kama yeye akiwa ni sababu ya kulia huko, au akiwa ameusia kuliliwa na ghairi ya hayo. *Wallaahu a'alam.*

Wafuasi wa Shafii wakasema: Inafaa kulia kabla au baada ya kifo, lakini kabla yake ni bora, kwa hadithi Sahihi:

« فإذا وجبت فلا تبكين باكية »

*"Kwa hiyo ikiwajibika (akishakufa) asilie mliaji yeyote"<sup>574</sup>.*

Shaafi na wafuasi wake wamesema kuwa ni karaha kulia baada ya mauti karaha ya '*Tanziihi*' kusafisha wala si haramu.

## SUBIRA

Mwenye kuomboleza amekuwa na laana na adhabu kwa sababu inaamuru babaiko. Allah na Mjumbe wake wameamuru subira na kujipima na wamekataza kubabaika na kukasirika.

Allah Mtukuka Amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اسْتَعِينُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاةِ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿١٥٣﴾

***"Enyi mlio amini! Takeni msaada kwa subira na Swala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri." (2:153)***

---

<sup>573</sup> Sahihi Bukhari 1303, Muslim 23/10

<sup>574</sup> Sahihi Ahmad 5/446; Abu Dawud 3111; An Nasaai 4/13; Ibn Maajah 2703 na Al Baani ameisahihisha katika Sahihi Abu Dawud.

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ ۗ وَنَبِّئِ  
الَّذِينَ إِذَا أَصَابْتَهُمْ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٦﴾

***“Hapana shaka Tutakujaribuni kwa chembe ya khofu, na njaa, na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wabashirie wanao subiri. Wale ambao ukiwasibu msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake Yeye hakika tutarejea.” (2:155-156)***

‘Ata amesema kuwa Ibn ‘Abbas amesema: ‘Mimi niko pamoja na nanyi nitakunusuruni wala sitakutelekezeni.’ Allah Aliyetukuka amesema:

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ

***“Na Tutakujaribuni”.***

Yaani: Tutaamiliana nanyi muamala wa mwenye kupewa mtihani, kwani Allah Anajua matokeo ya mambo kwa hiyo hahitaji kujaribu ili kujua mwisho, lakini Anaamiliana muamala wa anayemjaribu. Mwenye kusubiri Atamlipa thawabu kwa kusubiri kwake, na asiye subiri hatastahiki thawabu. Na Kauli Yake Taalaa:

مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ

***“Kwa chembe ya khofu, na njaa”***

Ibn Abaas amesema: “Kumhofia adui na njaa kutokana na ukame:

وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ

***“...na upungufu wa mali na watu”,***

Yaani: hasara na upungufu katika mali, na kuangamia mifugo.

وَالْأَنْفُسِ

**“Na watu”,**

Kwa mauti, kuuawa, maradhi na mvi.

وَالثَّمَرَاتِ

**“Na matunda”.**

Yaani: Mahitaji, na kutokutoa matunda kama yalivyokuwa yanatoka. Kisha aya inamalizia kwa kuwabashiria wenye kusubiri, ili kuonyesha kuwa mwenye kusubiri wakati wa misiba hii atakuwa juu ya ahadi ya thawabu kutoka kwa Allah. Allah Ta’alaa Akasema:

وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ

**“Na wabashirie wanao subiri”,**

Kisha Akawasifu kwa kusema:

الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ

**“Wale ambao ukiwasibu msiba”**

Yaani: Wakipata maafa katika yaliyotajwa, wala hakusemwi katika ya kheri kuwa ni msiba,

إِنَّا لِلَّهِ

**“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu”,**

Yaani sisi ni waja wa Allah kwa hiyo atakufanyia akitakacho,

وَأِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

**“Na Kwake Yeye hakika tutarejea.”**

## Al - Kabair

---

Kwa kufa na kwisha. Na maana ya kurejea kwa Allah ni kwa kurejea Kwake kwa hukumu, kwani hakika Amewamilikisha watu hukumu, kwa hiyo hukumu za waja zikiondoka hukumu itarudi kwa Allah Azza Wajalla. Aishah anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« ما من مصيبة يصاب بها المؤمن إلا كفر الله بها عنه حتى الشوكة يشاكها »

*“Hakuna msiba wowote unaompata Muumini isipokuwa Allah Atamfutia madhambi yake hata mwiba unaomchoma.” (Muslim)<sup>575</sup>.*

Al-Qamah bin Marthad bin Saabit kutoka kwa baba yake anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema,

« من أصيب بمصيبة فليذكر مصيبته بي فإنها أعظم المصائب »

*“Mwenye kupata msiba basi na akumbuke msiba wake kwangu, kwani huo ni msiba mkubwa zaidi”<sup>576</sup>.*

Amesema tena Mtume ﷺ:

« إذا مات ولد العبد يقول الله للملائكة : قبضتم ولد عبدي ؟ قالوا : نعم

قال : قبضتم ثمرة فؤاده . قالوا : نعم . قال : فما قال ؟ قالوا : حمدك

واسترجع . فيقول الله : ابنوا لعبدي بيتا في الجنة وسموه بيت الحمد »

*“Atakapokufa mtoto wa mja wangu Allah Atawaambia malaika: ‘Mmekamata mtoto wa mja wangu?’ Watasema: ‘Ndiyo.’ Atasema: ‘Mmekamata tunda la moyo wake.’ Watasema: ‘Ndiyo.’ Atasema: ‘Amesema nini?’ Wakasema: ‘Ameshukuru na kusema Inna Lillahi wainna Ilayhi Rajiu’un.’ Allah Atasema: ‘Mjengeeni mja wangu nyumba peponi na ipeni jina la Baitul Hamd.”<sup>577</sup>*

---

<sup>575</sup> Sahihi Bukhari 5640, Muslim 2572

<sup>576</sup> Sahihi Daarimi 1/40; Ibn Saad 2/75; Twabarani 6718 na Al- Baani ameisahihisha katika Silsilah As Swahihah 1106.

<sup>577</sup> Hassan: Imepokewa na Ahmad 4/415, At-Tirmidhi 1026, Ibn Hibaan 2948 na kwa mujibu wa Al-Bani ni Hassan katika Silsila As-Swahihah 1106.



## Al- Kabair

---

Abu Huraira رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« يقول الله تعالى : ما لعبيدي عندي جزاء إذا قبضت صفيه من أهل الدنيا  
ثم احتسب إلا الجنة »

*“Allah Taalaa anasema: Mja hana malipo ninapomchukua kipenzi chake, katika watu wa duniani kisha akatarajia (akajizua) isipokuwa peponi.”<sup>578</sup>*

Na amesema:

« من سعادة ابن آدم رضاه بما قضى الله ، ومن شقاوة ابن آدم سخطه بما  
قضى الله تعالى »

*“Miongoni mwa wema wa binadamu ni kuridhika kwake alioyahukumu Allah, na miongoni mwa uovu wa binadamu ni kuchukia kwake alioyahukumu Allah Taalaa”<sup>579</sup>.*

‘Umar Ibn al-Khattaab رضي الله عنه amesema wakati malaika wa kifo anapochukua roho ya muumini yeye husimama mlangoni na watu wa nyumba yake wanalia kwa sauti. Wengine wakijipiga mashavu yao makofi na wengine wakivuta na kunyambua nywele zao na kuomboleza, basi malaika wa mauti husema: “Ni la nini babaiko hili, ni la nini fazaiko hili? Wallahi sijafupisha maisha ya mtu yeyote, wala sijampunguzi mtu riziki yake, wala sikufanya kosa lolote kwenu, wala sijamdhulumu yeyote, ikiwa madai yenu na hasira zenu ni juu yangu mimi, wallaahi mimi nimeamriwa tu, na ikiwa ni kwa ajili ya maiti wenu basi huyo ametenzwa nguvu (na Allah) na ikiwa ni juu ya Mola wenu basi nyinyi mmemkufuru, na hakika mimi nitarudi tena na tena mpaka hatobaki hata mmoja miongoni mwenu”.

---

<sup>578</sup> Sahihi Bukhari 6424

<sup>579</sup> Dhaifu Ahmad 1444: Tirmidhi 2151 Al-Baani ameidhoofisha katika Silsilah Dhailah 1906.

## Al - Kabair

---

Mtume ﷺ amesema:

« والذي نفسي بيده لو يرون مكانه ويسمعون كلامه لذهلوا عن ميتهم ولبكوا  
على أنفسهم »

*“Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake, lau wangeona mahali pake na wangesikia maneno yake wangesinyaa kuhusu maiti wao na wangelilia nafsi zao.”<sup>580</sup>.*

Ameshuhudia ushuba wake na Akambashiria utulivu na Akampamba kwa *thaaniyaythnain* kama alivyosema ‘Umar رضي الله عنه: ‘Ni nani atakuwa bora kuliko wa pili wa wawili Allah ni watatu wao?’

### FASILI KATIKA RAMBI RAMBI

Abdullah bin Mas‘uud رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah amesema:

« من عزى مصابا فله مثل أجره »

*“Mwenye kumpa pole mwenye msiba basi yeye ana ujira mfano wa ujira wake, (aliyefiwa).”<sup>381, 582</sup>*

Abu Burdah anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ alimwambia (binti yake) Fatmah:

« من عزى ثكلى كسى بردا من الجنة »

*“Mwenye kumpa pole mama mwenye kufiwa basi atavalishwa nguo peponi.” (Tirmidhi)<sup>583</sup>*

---

<sup>580</sup> Sijaiona

<sup>381, 582</sup> Dhaifu: Imepokewa na At-Tirmidhi 1073, Ibn Maajah 1602 na Al Baani ameidhoofisha katika Dhaiifal Jaamii 5708.

<sup>583</sup> Dhaifu: Tirmidhi 1076; Al Baani ameidhoofisha katika Dhaiifah Al Jaamii 5707

## Al- Kabair

---

'Abdullah bin 'Amri bin Al-'As amesema; Mtume ﷺ alimuuliza mwanaye Fatma: "Nini kilichokutoa ndani ya nyumba yako?" Fatma akajibu: Nimekwenda katika nyumba hii ili kutoa pole ya msiba.<sup>584</sup>

'Amri bin Hazmi anatoa ripoti kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« ما من مؤمن يعزي أخاه بمصيبة إلا كساه الله من حلل الكرامة يوم القيامة »

*"Hakuna muumini yoyote anayempa rambi rambi nduguye katika msiba ila Allah atamvalisha yeye joho la heshima siku ya kياما."*<sup>585</sup>  
(Tirmidhi).

Jua kuwa rambirambi ni kumnasihi subira na kutaja yenye kufariji jamaa wa maiti, kupunguza huzuni yake, na kulainisha msiba wake, nacho ni kitu kinachopendeza, na kinaingia katika kuamrisha mema na kukataza mabaya, na linaingia katika Kauli Yake Taalaa:

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَى

**"Na saidianeni juu ya wema na uchamungu". (5:2)**

Aya hii ni katika mazuri zaidi yanayotolewa dalili katika rambirambi.

Na ujue kuwa rambirambi ni kuamrisha subira na inapendekezwa kabla ya kuzika na baada yake, watu wa Shaafi wamesema: "Ni tangu anapofariki maiti na inabakia baada ya kuzika kwa siku tatu". Na watu wetu wamesema: ni karaha rambirambi baada ya siku tatu, kwa kuwa rambirambi ni kutuliza moyo wa mwenye msiba, na mara nyingi kutulia moyo ni siku tatu, kwa hivyo hakuna kuanzisha upya huzuni. Hivi ndivyo walivyosema wengi kati ya watu wetu.

---

<sup>584</sup> Dhaifu: Abu Dawud 3123, An-Nasai 4/27 na kudhoofishwa na Shaykh katika Dhaif Abu Dawud 684.

<sup>585</sup> Dhaifu: Ibn Majah 1601, Al-Baihaqi 4/59 na Al- Baani ameidhoofisha katika Silsilah Al Irwaa 764

## Al - Kabair

---

Abul Abbaas katika wafuasi wetu amesema: “Hakuna ubaya kwa rambirambi baada ya siku tatu bali inabakia milele hata muda ukiwa mrefu”.

Nawawi amesema: “Lililochaguliwa ni kuwa rambirambi haifanywi baada ya siku tatu isipokuwa kwa sura mbili, walizozichagua watu wetu, nazo ni kuwa iwapo mwenye kutoa rambirambi au aliyefiwa hakuwepo wakati wa mazishi na kurudi kwake kukaafikiana baada ya siku tatu, na rambirambi baada ya kuzika. Ni vizuri zaidi kumuhani mtu baada ya kuzika kuliko kabla ya kuzika, kwa sababu jamaa wa marehemu wanashughulishwa na kumuandaa kwake. Na kuwa kutengana naye baada ya kuzika kunakuwa kukubwa zaidi na kuhuzunisha zaidi. Kwa hiyo kama akiona babaiko atatanguliza rambirambi ili kuwatuliza. *Wallaahu A`alam.*

Ni karaha kukaa kwa ajili ya rambi rambi, yaani watu wa nyumba kukusanyika katika nyumba mojawapo ili wakusudiwe na watoa rambi rambi. Matamshi ya rambirambi ni maarufu, Maneno mazuri zaidi ya rambirambi ni yaliyopokewa katika Sahihi mbili kutoka kwa Usama bin Zaid amesema: wakati binti wa Mtume ﷺ alipomwita akimtaarifu kuwa mwanae wa kiume yumo katika *Sakaratil mauti*.

Mtume ﷺ alimwambia Usama:

*“Rudi kwake na mwambie kuwa Allah ni Chake Alichochukua na Alichotoa na kila kitu Kwake Yeye kina muda maalumu na muamrishe asubiri na ajipime”.*<sup>586</sup> Akataja ukamilifu wa hadithi.

Nawawi amesema: Hadithi hii ni katika nguzo kubwa za Uislamu iliyokusanya mengi ya muhimu katika misingi ya dini, matawi yake, adabu, kusubiri juu ya maafa yote, ugonjwa, na malengo mengine.

---

<sup>586</sup> Sahihi Bukhari 1283, 7377, 7448 Muslim 923

## Al - Kabair

---

Maana ya maneno ya Mtume ﷺ:

*'Ni cha Allah Alichochukua.'*

Ni kuwa ulimwengu mzima ni Miliki Yake. Hachukui chenu bali anachukua chake kilicho kwenu na hii ina maana ya kuazima.

Na Kauli Yake:

*'...na ni Chake Alichotoa...'*

Alichokupeni hakiko nje ya Miliki Yake, bali hicho ni Chake Taalaa Anakifanya Anavyotaka,

*'...na kila kitu Kwake Yeye ni kwa muda maalumu...'*

Kwa hiyo msibabaike kwani aliyefishwa muda wake umekwisha basi muhali kumchelewesha au kumtanguliza nao. Kwa hiyo mkijua hivi basi subirini na tarajieni kwa yaliyokuteremkieni.

Mu'awia bin Iyas anatoa taarifa kutokana na hadithi ya baba yake kuwa Mtume ﷺ aliuliza baada ya kutomuona Sahaba wake mmoja, wakasema: "Ewe Mjumbe wa Allah mwanawe ambaye uliyemuona amefariki?"

Mtume ﷺ akampa rambi rambi akamwambia:

*"Ewe fulani bin fulani ni kipi kipendezacho zaidi kwako, uneemeke naye kwa umri wako, au la, uje kesho mlango wowote miongoni mwa milango ya peponi, umkute amekutangulia anakufungulia?"*

Akamjibu: "Ewe Mtume wa Allah mimi ningependelea kuwa yeye anitangulie peponi anifungulie hilo linapendeza zaidi kwangu." Mtume ﷺ akasema:

*"Hilo ni lako".*

## Al - Kabair

---

Pakasemwa: "Ewe Mtume wa Allah hilo ni lake haswa au ni kwa waislamu wote?"

Mtume ﷺ akasema:

*"Bali ni kwa waislamu wote"<sup>587</sup>.*

Abu Hurairah رضى الله عنه amepokea kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alitoka kuzuru makaburi ya Al-Baqii akakutana na mwanamke aliyekuwa akilia kwenye kaburi akamwambia:

*"Ewe kijakazi cha Allah muogope Allah na subiri".*

(Mwanamke) akasema: "Ewe mja wa Allah! Ungekuwa umepata msiba ungeniacha na hali yangu." Mtume ﷺ akasema:

*"Ewe kijakazi cha Allah Muogope Allah na usubiri".*

Yeye akajibu: "Ewe mja wa Allah umenisikia, basi ondoka". Mtume ﷺ akaondoka. Mtu mmoja alimuona akamwambia: 'Bwana yule amekuambia nini?' Akamwambia alichosema na alichomjibu yeye. Akamwambia: 'Unamjua?' Mwanamke akasema: 'Wallahi simjui.' Yule bwana akamwambia, 'Yule ni Mtume wa Allah' Hapo mwanamke akamkimbilia Mtume ﷺ akamwambia: "Ewe Mjumbe wa Allah nitasubiri." Mtume ﷺ akamjibu:

*"Hakika Subira ni kwenye pigo la kwanza."<sup>588</sup>*

Yaani; subra inakuwa nzuri wakati wa kutokewa na msiba, Ama baada ya hapo kwa kawaida hutokea liwazo. Katika Sahihi Muslim: Anatoa

---

<sup>587</sup> Sahihi: Ahmad 5/35 An-Nasaai 4/22 na Ibn Hibbaan 2947

<sup>588</sup> Dhaifu: Abu Ya'ala 6041, Isinadi yake ni dhaifu na asili yake ni katika Bukhari 1283; Muslim 926.

## Al- Kabair

---

taarifa kuwa mtoto wa kiume wa Abu Talha mwanaye Ummu Sulaim alipofariki, Ummu Sulaim aliiambia familia yake: 'Msimwambie Abu Talha juu ya mwanawe na niachieni miye nitamwambia.' Abu Talha aliporudi nyumbani alimuandalia chakula cha usiku na akajipamba, Abu Twalha akamuingilia. (Mke) akamwambia: "Ewe Abu Talha ikiwa watu waliazima kitu kwa watu wa familia nyingine, wakataka kitu chao je watawakatalia?'. Akajibu, 'Hapana.' Tena akamwambia, 'Sikiliza mwanao amefariki'. Abu Twalhah alikasirika na akasema, 'Umeniacha mpaka nimejichafua ndio unaniambia kuhusu mwanangu! Wallaahi hutanishinda juu ya subira.' Akatoka kwenda kwa Mjumbe wa Allah ﷺ kumueleza kilichotokea, Mjumbe wa Allah ﷺ akasema:

*" Allah Akubarikini katika usiku wenu".*

Akataja hadithi<sup>589</sup>, na katika hadithi nyingine:

*"Hakupewa yeyote kipaji bora na kipana zaidi kuliko subira"<sup>590</sup>.*

Ali رضي الله عنه<sup>589</sup> amesema: "Hakika wewe ukisubiri kwa imani na matarajio utafanikiwa vinginevyo utakunya kama wanavyo kunya wanyama".

Hakimu mmoja alimwandikia mtu aliyepatwa na msiba: "Hakika wewe kimekuondokea ulichoruzukiwa kwa hivyo usipoteze mbadala uliopewa, nao ni ujira'. Mwingine akasema: "Mwenye akili anafanya siku ya kwanza ya msiba anayoyafanya mjinga baada ya siku tano". Nimesema: Imejulikana kuwa mapito ya zama na zama yanaliwaza mwenye msiba, kwa hiyo ndiyo maana Mtume ﷺ akaamrisha subira wakati wa pigo la kwanza la msiba.

Imam Shafi alipata taarifa ya kifo cha mtoto wa 'Abdur-Rahmaan bin Mahdi رضي الله عنه<sup>589</sup> na hivyo 'Abdur Rahman alikuwa na huzuni kubwa.

---

<sup>589</sup> Swahili: Al-Bukhari 5470 na Muslim 23, 2144

<sup>590</sup> Swahili Bukhari 1469 Muslim 1053

## Al - Kabair

---

Kutokana na hayo Shafii alimuandikia na kumueleza: “Ndugu yangu jipoze nafsi yako kama wewe unavyo wapoza wengine, na chukia kitendo chako kiovu kama unavyochukia kwa wengine, na jua kuwa mapito ya misiba ni kukosa furaha na kunyimwa ujira. Basi ni vipi itakapojumuika pamoja na kuchuma dhambi? Kwa hiyo jipatie hadhi yako ewe ndugu yangu pindi ikikaribia kwako kabla ya kuitafuta ikiwa iko mbali nawe. Allah Akufunulie subira wakati wa msiba na Atuhifadhi sisi kwa subira wakati wa msiba, na akamwandikia mashairi akisema:

*Hakika mimi ninakupa rambirambi si kwa kuwa  
mimi niko katika uthibitiko, wa kuishi lakini hiyo ni suna ya dini.  
Mwenye kupewa rambirambi si mwenye kubakia baada ya maiti wake,  
wala mwenye kutoa rambirambi hata akiishi muda mrefu.*

Mtu mmoja aliwaandikia nduguze Waislam kama rambi rambi kwa kifo cha mwanawe. Hakika kwa baba yake mzazi ni mitihani na huzuni. Anapotangulia (kwenye haki) anakuwa swala yake na rehema yake, kwa hivyo usihuzunike kwa kumpoteza kutokana na fitina yake na huzuni yake, wala usipoteze mbadala aliokupa Allah kutokana na swala yake na rehema yake.

Musa binil Mahdi alimwambia Ibrahim bin Salamah: na akampa rambirambi kwa ajili ya mwanawe: “Allah akupe furaha na hilo ni jaribio na fitina, na amekupa huzuni na hiyo ni swala na rehema”. Mtu mmoja alimpa rambi rambi mtu mwingine akamwambia:

‘Hakika atakayekuwa na ujira kwako akhera ni bora kuliko atakayekuwa na furaha yako duniani”.

‘Abdullah bin ‘Umar baada ya kumzika mwanawe kisha akacheka kwenye kaburi, watu wakamuuliza: ‘Unacheka kaburini?’ Akasema: “Nilitaka kumnyong’onyesha shetani”.

Ibn Juraij amesema: “Ambaye hatapata mbadala wa msiba wake kwa ujira na matarajio basi ni bora aende kama anavyokwenda mnyama”.



## Al- Kabair

---

Humaidil A'araj amesema: Nimemuona Saidi bin Jubayr رضي الله عنه anasema huku akimuangalia mwanawe, 'Hakika mimi ninafanya urafiki wa kheri ndani yako.' Kukasemwa: "Ni upi huo?". Akasema: "Anakufa na ninatarajia".<sup>591</sup>

Mtu mmoja alikwenda kwa Hasan Al-Basri na akamlalamikia huzuni aliyokuwa nayo kutokana na kifo cha mtoto wake wa kiume, Hassan akamuuliza: "Mtoto wako alikuwa anakuwa mbali nawe?" akamjibu: "Ndio." Alikuwa akifanya hivyo mara kwa mara.

Hasan Al-Basri akamwambia: "Basi mwache awe mbali nawe, kwani hajakuwa mbali nawe isipokuwa unakuwa na ujira mkubwa kuliko hili". Akasema: "Ewe Abu Said umerahisisha huzuni yangu kwa mwanangu".

'Umar bin Abdil Aziiz aliingia kwa mwanawe katika ugonjwa wake akasema: "Ewe mwanagu unaonaje?" Akasema: "Najisikia niko juu ya haki." Akasema: 'Ewe mwanangu wewe kuwa katika mizani yangu inapendeza zaidi kuliko mimi kuwa katika mizani yako" Akasema: "Ewe baba yangu kuwa unayoyapenda yanapendeza zaidi kwangu kuliko yawe ninayoyapenda"<sup>592</sup>.

Mtoto wa imamu Shafi alipokufa, Imamu Shaafi akasoma mashairi haya:

*"Hivi ndivyo maisha yalivyo yasubirie,  
maafa ya mali au kufarikiana na mpendwa".*

Urwah alipatwa na jeraha la mguu, kwa hiyo mguu ukakatwa, hakuna yeyote aliyemzuia na huku yeye ni mzee sana, na hakuacha uradi wake wa usiku ule, Ila alisema:

لَقَدْ لَقِينَا مِنْ سَفَرِنَا هَذَا نَصَبًا

---

<sup>591</sup> Ameipokea Baihaqi katika Shi`ib 9768, na Abu Nuaim 4/275

<sup>92</sup> Ibn Abi Duniyaa katika Kitabu: Al-Muhtadhwiriin, 2155. Taarikh Dimishq 15/202

**“...Kwa hakika tumepata machofu kweli kwa hii safari yetu.”(Al Kahf, 18:62)**

Naakajifananisha kwa beti hizi:

*Naapia umri wangu sikuipeleka mikono yangu kwenye shaka,  
Wala miguu yangu haikuniamishia kwenye uchafu  
Wala hayakuniongoza masikio yangu wala macho yangu,  
Wala rai na akili yangu haikunielekeza juu yake  
Nami ninajua kuwa haukunipata msiba duniani,  
Isipokuwa umempata kijana yoyote mfano wangu.*

Akasema: “Ewe Alah ikiwa umenijaribu kwa hakika wewe umenipa afya, na ukiwa umechukua (kitu chochote) bila shaka umebakisha, umechukua kiungo kimoja na umebakisha viungo, na umechukua mtoto mmoja na umebakisha watoto”.

Usiku mmoja mtu kipofu kutoka kabila ya Banu ‘Abs alikwenda kumzuru Waliid (khalifa wa Bani Umayyah) Waliid akamuuliza kuhusu macho yake. Akasema:

“Nilikuwa tajiri mkubwa, siku moja wakati tukiwa tumelala ndani ya nyumba yetu katika bonde, mvua kubwa ilinyesha na bonde lilifurika mafuriko yaliburuza nyumba yangu na kuisomba, familia yangu na mali yangu yote, isipokuwa nilibakiwa na ngamia na mtoto wangu mdogo, ngamia alicharuka na kukimbia nikamfuata, alikuwa anakimbia huku na huku, nikasikia sauti ya mwanangu nikaenda nilipomfikia kichwa cha mwanangu kiko tumboni mwake akamuua, kisha nikamfuata ngamia, ili nimchukue akanipiga teke usoni na kupofua macho yangu, nikaamka sina familia, mali, mtoto, wala ngamia”.

Waliid akasema: Nendeni na huyu kwa Urwah ili ajue kuwa katika ardhi kuna mtu ana balaa kubwa kuliko yeye”.

Imepokewa kuwa wakati ‘Uthman bin ‘Affaan رضي الله عنه alipopigwa na wauaji na damu yake ikawa inachuruzika hadi kwenye ndevu zake,

## Al- Kabair

---

alisema: “Hakuna Mola isipokuwa wewe, umetakasika hakika mimi nilikuwa miongoni mwa madhalimu, Oh Allah hakika mimi najilinda kwako dhidi yao (wauaji) na ninakuomba msaada kwa mambo yangu yote, na ninakuomba subira kwa uliyonijaribu nayo.”<sup>593</sup>

Madaini alisema: “Nilimuona mwanamke jangwani mwenye uso mzuri na unaong’ara nikamwambia: “Wallahi inaonyesha kuwa wewe una maisha mazuri na ya furaha” mwanamke alimjibu ni kinyume cha unavyofikiri miye nimekutana na majonzi na msiba acha nikueleze yaliyonikuta. Nilikuwa na mume na kutoka kwake nilipata watoto wa kiume wawili. Siku ya *Al-Adh-haa*, mume wangu alichinja mbuzi, watoto walikuwa wakicheza, mtoto mkubwa akamwambia mdogo wake unataka nikuoneshe namna gani baba yetu anamchinja mbuzi wake akasema ndiyo, yule kaka mtu akamchinja nduguye alipoona damu alifadhaika akakimbilia mlimani akaliwa na mbwa mwitu.

Baba yake akatoka kumtafuta mwanawe akapotea jangwani akafa kwa kiu, mwisho nikabaki peke yangu duniani”. Nikasema: “Vipi wewe kuhusu kusubiri?” Mwanamke akasema: “Lau ingedumu kwangu ningedumu nayo, lakini ilikuwa ni jeraha limepona”.

Ibn Abbas رضي الله عنهما anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« من كان له فرطان من أمتي أدخله الله بهما الجنة »

*“Mwenye kuwa na vitangulizi viwili (watoto wawili waliofariki) katika umati wangu Allah Atamtia peponi”.*

Aisha رضي الله عنها akasema: “Je, ikiwa ni mtoto mmoja.” Akasema:

« ومن كان له فرط يا موفقة ! »

*“Na mwenye kuwa na mtoto mmoja ewe mwenye kuafikiwa”*

---

<sup>593</sup> Ibn Abi Duniyaa katika Kitabu: Al-Muhtadhwiriin, 49.

## Al - Kabair

---

Aisha رضي الله عنها akasema: "Na asiyekuwa na kitangulizi katika uma wako?"  
Akasema:

« أنا فرط أمتي لن يصابوا بمثلي »

*"Mimi ni kitangulizi cha uma wangu kamwe hawapatwi (na msiba)  
mfano wangu"<sup>594</sup>.*

Kutoka kwa Abu 'Ubaydah رضي الله عنه kutoka kwa baba yake amesema:  
Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« من قدم ثلاثة من الولد لم يبلغوا الحنث كانوا له حصنًا من النار »

*"Mwenye kutanguliza watoto watatu, hawajafikia baleghe, basi  
watakuwa ngome yake dhidi ya moto."*

Abu Dharr رضي الله عنه akasema: "Nimetanguliza watoto wawili" Akasema:

« واثنين »

*"Na wawili"*

Ubayy bin Ka'ab, mkuu na bwana wa wasomaji Qur-aan akasema:  
"Nimetanguliza mmoja". Akasema ﷺ:

« وواحدًا ولكن ذلك في أول صدمة »

*"Na mmoja lakini hayo ni katika pigo la mwanzo la msiba"<sup>595</sup>.*

Waki' anatoa taarifa kuwa Ibrahim Al-Harbi alikuwa na mtoto wa kiume umri wa miaka kumi na moja ambaye alihifadhi Qur-aan na alisoma Fiqh na hadithi na mambo mengi, alikufa na nilikwenda kumpa rambi

---

<sup>594</sup> Dhaifu: Tirmidhi 1068, Ahmad 2/334; Twabarani 12880; Shaykh ameidhoofisha katika Dhaiifil Jaami'i 5813.

<sup>595</sup> Dhaifu: At-Tirmidhi 1076, Ibn Maajah 1606 na Shaykh ameidhoofisha katika Dhaiifi Ibn Maajah 351 na Al-Mishkaat 1755.

rambi, akaniambia; "Nilikuwa natamani kifo cha mtoto wangu huyu." Nikasema: "Ewe Abu Ishaq wewe ni mwanazuoni mkubwa wa dunia unasema hivyo? Mwanao alikuwa Hafidh Qur'an, fiqhi na hadithi." Akasema: "Ndiyo, Sikiliza! Usiku mmoja niliota kuwa ilikuwa siku ya kiama na watoto wamesimama na majagi ya maji baridi wakiwapa watu, na siku hiyo ilikuwa ni ya joto kali, nikamwambia mmoja wao: ninyweshwe katika maji haya, akanitazama akasema: "Wewe sio baba yangu", Nikamuuliza: "Nyinyi ni nani? Akasema: "Sisi ni watoto tuliokufa ndani ya Uislam kabla ya baba zetu kwa hiyo tunawapokea na tunawanyweshwa maji". Ibrahim akasema: "Kwa ajili ya hili nimetamani mauti yake'.

Muhsin amepokea kuwa Abu Hasan amesema: "Nilimwambia Abu Huraira رضي الله عنه: "Tusimulie hadithi itakayofurahisha nafsi zetu, kuhusu mauti yetu". Akasema: "Ndiyo, wadogo wetu ni wadogo wa peponi, mmoja wao anampokea baba yake au alisema: wazazi wake, basi anamshika nguo yake au alisema mkono wake kwa hiyo hasimami mpaka amuingize peponi."<sup>596</sup>.

### **KISA CHA MALIK BIN DIINAAR**

Malik bin Dinar رضي الله عنه alisimulia kisa juu yake akisema nilikuwa nikipenda starehe na kunywa pombe, nilinunua mtumwa wa kike na nilimpenda sana akanizalia mtoto wa kike mzuri na mimi nikampenda sana.

Hadi akafikia kutambaa na kutembea kila ninapokuwa nikikaa kwa ajili ya kunywa pombe huja mikononi mwangu na kuimwaga ardhini. Wakati ametimiza miaka miwili akafariki na akaniacha katika majonzi, ulipofika usiku wa tarehe 15 wa Shaabani nililewa sana na usingizi ukanichukua niliota ndani yake kuwa ni siku ya kiama nimetoka kaburini lakini nyoka mkubwa wa bahari alikuwa akinifukuza akitaka kunimeza nikaanza

---

<sup>596</sup> Sahihi: Muslim 2635 Ahmad 2/488 Bukhari katika Adabul Mufrad 145

kukimbia lakini alikuwa akinikaribia miguuni mwangu, kila nikiimbia mbio zaidi ananikaribia, miye nilimpita mzee mmoja aliyekuwa amevaa joho mdhaifu nikampigia kelele nikamuomba: “Ewe Sheikh tafadhali niokoe na jambo hili la kutisha.’ Akasema: ‘Ewe mwanangu mimi ni mzee na dudu hili lina nguvu kuliko mimi siliwezi, lakini pita na fanya haraka pengine Allah atakuokoa nalo’.

Niliendelea kukimbia nalo liko nyuma yangu nikaona mashimo ya moto yanaroroma, nikakaribia kuangukia ndani yake, lakini mtu mmoja aliniambia wewe siyo mkazi wao’. Nikageuka kukimbia kuelekea mlimani na joka liko nyuma yangu, nikatokea mlimani niliona milango mingi ndani yake na kila mlango ulikuwa na walinzi nikasikia sauti ya mtu ikisema: “Muwahini huyu mwenye kusumbuka kabla adui yake hajampata, milango ikafunguliwa na nikaona kikundi cha watoto nyuso zao zilikuwa zinang’ara kama mwezi na kati yao alikuwepo mwanangu, akanijia kama mwanga wa taa na kwa mkono wake wa kulia akalipiga lile joka malo likageuka kukimbia, nikakaa kwenye chumba changu akasema: Ewe baba yangu..

﴿ أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ ﴾

***“ Je! Wakati haujafika bado kwa walio amini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyo teremka?” (57:16)***

Nikamwambia: “Ewe mwanangu, nanyi mnajua Qur’an?”, Akajibu: “Sisi tunajua zaidi yenu.’ Nikamuuliza: ‘Mwanangu mnafanya nini hapa?’ Akajibu: “Sisi ni watoto wa Waislamu tulikufa na tunaishi hapa hadi siku ya kiama na tunawapokea wazee wetu.”

Miye nilimwuliza, “Ewe binti yangu ni dudu gani lile linalonitisha lilikuwa likinifukuza?’ Akanijibu, “Ewe baba yangu yalikuwa matendo yako maovu yamekuwa na nguvu yakataka kukuangamiza.’ Nikamuuliza: “Ni nani yule mzee mnyonge niliyekutana naye?’

## Al- Kabair

---

Akamjibu: “Yale yalikuwa matendo yako mema ambayo ni dhaifu yalikuwa hayana nguvu ya kukulinda kutokana na matendo yako maovu uliyotenda, kwa hivyo ewe baba yangu tubia na rudi kwa Allah na usiwe kati ya wenye kuangamia”. Nikainua macho yangu, nikazinduka nikatubia saa hiyo hiyo”<sup>597</sup>.

Angalia na Allah Akurehemu, Baraka za watoto waliokufa wakiwa watoto wadogo wanaume au wanawake na manufaa yatapatikana akhera kwa wazazi waliosubiri na kujipima, na wakasema: ‘Kuhimidiwa ni kwa Allah, hakika sisi ni wa Allah na hakika sisi Kwake tutarudi.’ Na yatapatikana aliyoyaahidi Allah Ta’alaa kwa Kauli Yake:

الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمْ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ

**“Ambao wanapopata msiba wanasema: Sisi ni wa Mwenyezi Mungu”.**

Yaani: Sisi na mali zetu Anafanya Atakavyo.

وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿٢٠٦﴾

**“Na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea”.**

Thauban anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*“Mja hapatwi na msiba isipokuwa kwa moja ya mambo mawili; Ima kwa dhambi ambayo Allah hataisamehe ila kwa msiba huo, au kwa daraja ambayo Allah hakumpandisha isipokuwa kwa msiba huo.”<sup>598a</sup>*

Said bin Jubair amesema: ‘Umma huu umepewa wakati wa msiba ambacho hawakupewa Mitume kabla yao, nacho ni kusema:

---

<sup>597</sup> Ameitaja Ibn Quddaamah katika kitabu cha At-Tawwaabiin ukurasa 104.

<sup>598a</sup> Sahihi Al Bayhaqi 9854 katika Shi’ibi na imekuja kwa tamshi “Hairudishi kudura isipokuwa dua wala haizidishi umri isipokuwa wema na hakika mtu atanyimwa riziki kwa dhambi”. Ahmad 5/ 287, 280, Ibn Maajah 4022 Al Baani katika As Silsilah As Swahiihah 154

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

**“Sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea”.**

Lau wangepewa Mitume عليه السلام anangepewa Ya'aqub aliposema:

يَتَأَسَفُ عَلَى يُوسُفَ

**“Ee! huzuni yangu kwa Yusuf”**

Ummu Salama رضي الله عنها amesema: “Nimemsikia Mjumbe wa Allah ﷺ anasema:

« من قال عند المصيبة

“Mwenye kusema wakati wa msiba:

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

**“Sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea” “**

اللهم أجرني في مصيبتى واخلف لي خيرا منها إلا أجره الله وأخلف له خيرا منها «

*Ewe mola nikinge katika msiba wangu na nibadilishie kheri kuliko huo, isipokuwa Allah Atamlinda na Atampa mbadala bora kuliko huo”.*

Ummu Salama amesema: “Wakati Abu Salamah alipofariki nilijisemea, “Ni nani bora kuliko Abu Salamah?”, Kisha baada ya hapo Allah alinibadilishia kwa Mjumbe wa Allah ﷺ.” (Muslim)<sup>598b</sup>

---

<sup>598b</sup> Sahihi Muslim 918



## Al- Kabair

---

Sha'abi amesema kuwa Shuraih amesema: "Msiba ukinifika humhimidi Allah ﷻ mara nne, ninamhimidi ukiwa si mkubwa kuliko huo, ninamhimidi akiniruzuku subira juu yake, na ninamhimidi akiniafikia kusema (*Inna lillaahi wa inna ilaihi raajiuun*), na hakuufanya katika dini yangu."<sup>599</sup>

Na kauli yake: **أَوْلَيْتِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ**

**"Hao wana Swala ya mola wao na Rehema".**

Swala kutoka kwa mola wao ni rehema na maghufira

**وَأَوْلَيْتِكَ هُمُ الْمُتَّهَتُونَ**

**"Na wao ni wenye kuongoka".**

Anakusudia waliongoka kwa kurejea, na Imesemwa: "Kwenye pepo na thawabu"

Saidi ibnul Musayyib kutoka kwa 'Umar Ibn Khattab رضى الله عنه amesema: "Neema ya usawa na neema ya malipo".

**أَوْلَيْتِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ**

**"Hao wana Swala ya mola wao na Rehema".** Na neema mbili

**"Na wao hao ni wenye kuongoka."**

Neema ya usawa na neema ya malipo.<sup>600</sup>

Ama mwenye msiba akikasirika na akaomboleza kwa maangamivu, au kujipiga mashavu na kuchana mifuko ya nguo zake, au kutimua nywele

---

<sup>599</sup> Ameipokea Al-Bayhaqi 9980

<sup>600</sup> Al-Haakim 2/270, Al -Bayhaqi 9688

## Al - Kabair

---

zake, akanyoa kipara, na vitendo vinavyofuatana na hivyo basi ana laana za Allah awe mwanamume au mwanamke.

Imepokewa kuwa mwenye kupiga paja kwenye msiba kunapomoshwa thawabu. Imepokewa kuwa mwenye kupatwa na msiba akachana nguo zake, au akapiga kofi au akachana mfuko wa nguo, au akanyofoa nywele ni kana kwamba amechukua mkuki kumpiga nao Mola Wake. Imetangulia kuwa Allah haadhibu kwa kulia macho, wala kwa huzuni ya moyo, lakini anaadhibu kwa huu. Yaani anachosema mwenye msiba kwa ulimi wake – Yaani; kutokana na malalamiko na kuomboleza.

Imetangulia kuwa maiti anaadhibiwa kaburini mwake, kwa kile alichombolezwa nacho, muombolezaji anaposema: 'Ewe tegemeo langu, Ewe mnusuru wangu, Ewe msaidizi wangu, Ewe mkuu wangu.' Huvutwa maiti na malaika wanamuuliza, 'Wewe ndio msadizi wake? Wewe ndio tegemeo lake?, Wewe ndio mvishaji wake?.'

Kwa hiyo kuomboleza ni haramu kwa sababu kunaamsha huzuni na inazuia subira, na ndani yake kuna kuhalifu kujisalimisha katika hukumu ya Allah, na kunyenyekea amri ya Allah Taalaa.

## KISA

Saleh Al-Mari anasimulia kisa kifuatacho:

Nilifanya ziara makaburini siku ya usiku wa ijumaa, nikapitiwa na usingizi nikalala, niliota kuwa makaburi yamefunguka na maiti walikuwa wakitoka makaburini wamekaaa kwa duara duara. Sahani zilizofunikwa ziliteremka kwao kutoka mbinguni, lakini palikuwa na mtoto mdogo mwenye mvi ambaye alikuwa anaadhibiwa adhabu za kila aina. Nilikwenda kwake nikamuuliza: 'Ewe mtoto kwanini unaadhibiwa kati ya kikundi hiki?' Akasema:

"Ewe Saleh kwa ajili ya Allaah fikisha ninayo kutuma, na tekeleza amana, na hurumia upweke wangu, huenda Allah `Azza Wajalla akanijalia mimi juu ya mikono yako pa kutokea.

## Al- Kabair

---

Nilipofariki mama yangu alikusanya walijaji na waombolezaji, na kulia kila siku, na mimi ninaadhibiwa kwa sababu ya vitendo hivyo. Kuna moto mbele yangu, nyuma yangu, kulia kwangu na kushoto kwangu kwa sababu ya manung'uniko ya mama yangu. Basi Allah asimlipe kheri kwa ajili yangu.' Kisha akalia mpaka nikalia kwa kilio chake. Akasema:

'Ewe Saleh kwa jina la Allah nenda kwake (mama yangu) yupo mahali fulani akanijulisha mahali alipo, na muulize kwa nini mwanao anaadhibiwa.? "Ewe mama yangu, umenilea, na umenilinda na maovu yote nilipokuwa hai, lakini baada ya kufa kwangu umenitupa kwenye adhabu. ewe mama yangu lau ungeona minyororo shingoni mwangu, na miguuni mwangu, malaika wa adhabu ananipiga na kunifokea, lau ungeona ubaya wa adhabu yangu ungenionea huruma, endapo hutoacha kulalamika na kuomboleza basi nitamuomba Allah ﷻawe hakimu baina yangu na wewe kwenye siku mbingu zitapasuliwa, na watu waletwe mbele kwa ajili ya upambanuzi wa hukumu.'

Saleh akasema: 'Nikazinduka kwa mshituko, nikakaa katika mahali pangu kwa kuogopa hadi asubuhi, nikaingia mjini na sikuwa na hamu isipokuwa kwenye nyumba ya mama wa mtoto mwenye mvi, mtu mmoja akanielekeza nyumba nilipofika nikaona mlango wa nyumba una rangi nyeusi na sauti za maombolezo zilikuwa zikitoka humo ndani ya nyumba hiyo nilipogonga mlango mwanamke mzee alinifungulia, na akaniuliza: 'Unataka nini wewe?' Nikamwambie, 'Ninataka kumuona mama ambaye mwanawe amefariki.' Akaniambia, 'Unamtaka wa nini? Kwani yeye ameshughulishwa na huzuni yake.'

Nikamwambia: "Tafadhali niletee huyo mama kwani ninazo salamu zitokazo kwa mwanawe.' Alikwenda ndani akamwita mama. Yule mama akaja na alikuwa amevaa nguo nyeusi na uso wake umekuwa mweusi kwa kulia, na kujipiga makofi, akaniuliza, "Wewe ni nani?" Nikamwambia:

"Mimi ni Saleh. Miye nilipitisha sehemu ya usiku makaburini na mwanao alikuwa akiteseka na kanieleza nikueleze kwa niaba yake hivi: "Ewe

## Al - Kabair

---

mama yangu, umenilea, na umenilinda na maovu yote nilipokuwa hai, lakini baada ya kufa kwangu umenitupa kwenye adhabu, ewe mama yangu lau ungeona minyororo shingoni mwangu, na minyororo miguuni mwangu, malaika wa adhabu ananipiga na kunifokea, lau ungeona ubaya wa adhabu yangu ungenionea huruma, endapo hutoacha kulalamika na kuomboleza basi nitamuomba Allah تعالیawe hakimu baina yangu na wewe kwenye siku ya siku mbingu zitapasuliwa, na watu waletwe mbele kwa ajili ya upambanuzi wa hukumu”.

Aliposikia maneno hayo kutoka kwangu alizimia na kuanguka, alipopata fahamu alilia kwa uchungu na kusema: “Ewe mwanangu ingekuwa nimejua kama ni hivyo nisingefanya hivyo, ninatubia kwa Allah تعالیkutokana na haya akaingia nyumbani na akawafurusha wanawake waliokuwa wakiomboleza akabadili nguo badala ya nyeusi akaniletea pesa akasema: “Ewe Saleh toa pesa nyingi hizi sadaka kwa niaba ya mwanangu”.

Nikaondoka hapo nyumbani na nikazigawa pesa hizo kwa masikini na wanaostahiki. Usiku wa Ijumaa nyingine nilikwenda sehemu ile ile hapo makaburini kama mazoea yangu nikalala, nikawaona maiti wametoka makaburini mwao na kukaa kama ada yao, wakaletewa mabakuli, nikamuona yule kijana akiwa mwenye furaha naye akaletewa bakuli akachukua, aliponiona alinjia akasema: “Ewe Saleh Allah akulipe kheri kwa ajili yangu, Allah amenipunguzia adhabu, na hilo ni kwa sababu ya kuacha mama yangu aliyokuwa akiyafanya.’ Saleh akauliza ‘Haya mabakuli ni ya nini?’ Akasema: ‘Ni swadaqa za walio hai wanazotutolea, kisomo<sup>601</sup> na dua, huwateremkia kila usiku wa Ijumaa na huambiwa hizi wao kuwa zawadi kutoka kwa fulani.

Nenda kwa mama yangu na umpe salamu zangu, na umwambie Allah Atakulipa thawabu kwa uliyonifanyia, sadaka zako zimenifikia na kuwa

---

<sup>601</sup> Hili ndani yake hakuna dalili ya kufaa kusoma Qur’aan juu ya maiti hili halifai. Ama kuitoa thawabu ya kisomo ndani yake kuna mvutano.

## Al- Kabair

---

wewe hivi karibuni utakuwa nami jiandae.' Saleh akasema: 'Baada ya hapo niliamka baada ya siku chache kupita nilikwenda nyumbani kwa mama wa yule mtoto nikaona jenzeza limewekwa mlangoni. Nikauliza: 'Ni la nani hili?' Wakasema: 'Ni la mama wa yule mtoto". Basi nikahudhuria Swala yake, na akazikwa pembeni mwa mtoto wake kwenye hayo makaburi. Nikawaombea dua na nikaondoka.

Tunamuomba Allah kutujaalia kutufisha katika Uislamu na Atukutanishe na wema, na Atulinde dhidi ya moto, hakika Yeye ni Mpaji, Mkarimu, Mpole, Mwingi wa rehema.

\*\*\*

## DHAMBI KUBWA YA HAMSINI

### UASI

Amesema Allah Ta'ala:

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ أُولَئِكَ لَهُمْ  
عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٢﴾

***“Bali lawama ni kwa wale wanao wadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Hao watapata adhabu iliyo chungu”.*** (42:42)<sup>602</sup>

Mtume wa Allah ﷺ:

« إن الله أوحى إلي أن تواضعوا حتى لا يبغى أحد على أحد ولا يفخر أحد  
على أحد »

***“Hakika Allah ametoa wahyi kuwa nyenyekeeni mpaka mmoja wenu asimdhulumu mwingine wala asijifakhiri yeyote juu ya mwingine.”***  
(Muslim)<sup>603</sup>.

Katika Athari: Lau jabali lingelifanyia ujeuri jabali jingine basi Allah Angelifanya lililofanya ujeuri miongoni mwao vipande vipande.<sup>604</sup>

Mtume ﷺ amesema:

« ما من ذنب أجدر أن يعجل الله لصاحبه العقوبة في الدنيا مع ما يدخره له  
في الآخرة من البغي وقطيعة الرحم »

---

<sup>602</sup>(42:42)

<sup>603</sup> Sahihi: Muslim 2865; Abu Dawud 4895

<sup>604</sup> Sahihi: Bukhari katika Adabul Mufradi 588; Baihaqi katika As hi'ibi 6693 Al Baani amesahihisha katika Sahihil Adabul Mufrad 457

## Al - Kabair

---

*“Hakuna dhambi Allah Anaharakisha adhabu kwa mtendaji wake katika dunia pamoja na kumwekea (adhabu nyingine) akhera kuliko jeuri na kukata udugu.”<sup>605</sup>*

Allah Alimdidimiza Qaruni ardhini wakati alipofanya ujeuri juu ya watu wake. Allah Ta’alaa Amemuelezea kwa Kauli Yake:

﴿ إِنَّ قُرُونًا كَانَتْ مِنْ قَوْمِ مُوسَىٰ فَبَغَىٰ عَلَيْهِمْ ط

***“Hakika Qaruni alikuwa katika watu wa Musa, akawafanyia ujeuri”***

Hadi kauli yake: ﴿ كَسَفْنَا بِمِمْ وَبِدَارِهِ الْأَرْضَ

***“Tukamdidimiza yeye na nyumba yake ardhini.” (28:76-81)***

Ibnul-Jawzi amesema: Kuhusu ujeuri wa Qaruni kuna kauli nyingi:

Ya Kwanza: Kuwa yeye alimpa zawadi kahaba ili amsingizie Musa na akatekeleza; Musa akamuapisha yule kahaba kwa aliyoyasema, akamuambia kisa chake pamoja na Qaruni na huu ukawa ndio ujeuri wake. Hilo amelisema Ibn Abbaas رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا.

Ya Pili: Kuwa yeye alifanya ujeuri kwa kumkufuru Allah, hilo amelisema Adh-Dhahaak.

Ya Tatu: Kwa ukafiri, amelisema hilo Qatadah.

Ya Nne: Kuwa yeye alirefusha nguo yake kiasi cha shubiri moja. Hilo amelisema ‘Atwa al-Kharasani.

---

<sup>605</sup> Sahihi: Bukhari katika Adabul Mufradi 67; Abu Dawud 4902; Tirmidhi 2511 Angalia As Silsilah As Swahiihah 917

## Al - Kabair

---

Tano: Kuwa yeye alikuwa anamtumikia Firauni kwa hiyo akawafanyia ujeuri wana wa Israeli kwa hiyo akawadhulumu, Amelisimulia hilo Al-Mawardi.<sup>606</sup>

Kauli Yake:

كُفَسْنَا بِهِ وَبَدَارِهِ الْأَرْضَ

***“Tukamdidimiza yeye na nyumba yake ardhini”.***

Pindi Qaarun alipoamrisha kusingiziwa Musa, Musa alikasirika akamuapiza Qaarun, Allah akampa wahyi kuwa ningeamrisha ardhi ikutii, iamrishe akasema: ‘Ewe ardhi mchukue’ Ardhi ikamchukua hadi kitanda chake kikapotea. Qaarun alipoona hivyo akamlilia Musa, Musa akasema: ‘Ewe Ardhi mchukue, ikamchukua, Ewe ardhi mchukue, ikamchukua hadi nyayo zake zikapotea.’ Alipoona hivyo akaendelea, ‘Ewe ardhi mchukue, ikamchukua hadi akapotea’. Allah akampa wahyi akamwambia: “Ewe Musa ni ugumu ulioje ulionao? Naapa kwa Utukufu Wangu na Utisho Wangu lau angenililia Mimi Ningemuokoa!<sup>607</sup>”.

Ibn Abbaas: amesema: “Alimdidimiza hadi ardhi ya chini kabisa”. Samurah bin Jundub amesema: “Kila siku alimdidimiza kimo kimoja, kwa kimo hicho atafika nacho ardhi ya chini kabisa Siku ya Kiama<sup>608</sup>”.

Muqaatil amesema: ‘Qaarun alipoangamia Bani Israil walisema: ‘Musa amemuangamiza Qaarun ili achukue mali yake na nyumba yake. Basi Allah akadidimiza nyumba yake na mali yake baada ya siku tatu.

***“Kwa hiyo hakuwa na kundi linalomnusu bila Allah”.***

Yaani: Wenye kujizuia kutokana na Allah:

---

<sup>606</sup> Zaadul Masiiri 6/263

<sup>607</sup> Twabari ameipokea mfano wake 20/117 katika isinadi yake kuna mtu hajulikani

<sup>608</sup> Suyuuti amesema katika Ad durar 5/138: Ameipokea ibn Abi Haatim kutokana na njia Qatadah kutoka kwa Samurah.



فَمَا كَانَ لَهُ مِنْ فِئَةٍ يَنْصُرُونَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ

**“...wala hakuwa miongoni mwa wanao jitetea.” (28:86)**

Yaani wenye kujizuia kwa yalioteremka. Allah Ndie Mwenye kujua zaidi.<sup>609</sup>

Ewe Mola Ondoa dhuluma za dhambi zetu kwa Nuru ya Maarifa Yako na Uongofu wako, na tufanye miongoni mwa wenye kuyaelekea na kuwaepuka wasiokuwa Wewe. Tughufirie sisi na wazazi wetu na Waislamu wote. Aamiin.

\*\*\*

---

<sup>609</sup> Zaadul Masiiri 6/245.

DHAMBIB KUBWA YA HAMSINI NA MOJA

USTAHAMILIVU JUU YA MNYONGE,  
KIJAKAZI NA MNYAMA

Allah Mtukuka Aameamrisha kuwafanyia hisani hao, kwa Kauli Yake:

• وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۗ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ  
وَالْمَسْكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا  
مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿٤٦﴾

***“Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wanao jifakhiri”. (4:36)***

Al-Waahidi katika kauli ya Allah amesema:

• وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۗ

***“Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote”***

Ahmad bin Muhammad bin Ibrahim Al-Mahrajani kwa sanadi yake kutoka kwa Mu’adh bin Jabal amesema:

“Nilikuwa nyuma ya Mtume ﷺ juu ya punda, Mtume ﷺ akasema: “Ewe Muaadh”

Nikajibu: ‘Labaika Was’adayka Ya Rasulallah.’ Mtume ﷺ Akasema:

## Al-Kabair

---

« هل تدري ما حق الله على العباد وما حق العباد على الله ؟ » قلت : الله ورسوله أعلم ؟ قال : « فإن حق الله على العباد أن يعبدوه ولا يشركوا به شيئاً ، وحق العباد على الله أن لا يعذب من لا يشرك به شيئاً »

*“Je, unajua ni nini haki ya Allah juu ya waja?” Nikasema: “Allah na Mjumbe wake wanajua zaidi.” Akasema: “Haki ya Allah juu ya waja ni kumuabudu wala wasimshirikishe na chochote, na haki ya waja juu ya Allah ni kutokumuadhibu asiyemshirikisha na chochote.”<sup>610</sup>*

Ibn Mas’uud رضي الله عنهم amesema: Bedui wa Jangwani alikwenda kwa Mtume ﷺ na akamwambia: “Ewe Mtume wa Allah nipe nasaha Mtume ﷺ akamwambia:

« لا تشرك بالله شيئاً وإن قطعت وحرقت، ولا تدع الصلاة لوقتها فإنها ذمة الله، ولا تشرب الخمر فإنها مفتاح كل شر » .

*“Usimshirikishe Allah na chochote hata ukikatwakatwa na ukichomwa (moto), wala usiache Swala kwa wakati wake, kwani hiyo ni dhima ya Allah, wala usinywe pombe kwani huo ni ufunguo wa kila shari.”<sup>611</sup>*

Kauli Yake:

وَيَا أَوْلِيَّيْنَ إِحْسَنًا

**“Na kwa wazazi wawili kuwafanyia hisani”,**

Allah Anataka wema, upole na ulaini kwa wazazi wetu kwa kuzungumza nao kwa wema na kuyaenda mahitaji yao ya kila siku, na wasijibiwe kwa ukali, wala kuwatazama kwa jicho kali, wala kunyanyua sauti wakati wa kuzungumza nao, bali wawe mbele yao kama vile mtumwa mbele ya bwana wake, katika kunyenyekea kwao. Kauli Yake:

---

<sup>610</sup> Sahihi: Ahmad 5/228; Bukhari 2856, 5967; Muslim 30, 49

<sup>611</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/238, At-Tabarani 20/82/156 na kusahihishwa na Shaykh katika Al-Irwaa 2026 kutoka katika Hadithi ya Abu Dardaa na Mu’adh lakini sikuwepa riwaya ya Ibn Mas’ud.

وَيَذَى الْقُرْبَى وَالْيَتَمَى

**“Na kwa jamaa wa karibu”.**

Anawaunga na akawa na huruma nao,

وَالْيَتَمَى

**‘...na yatima...’**

Anawafanyia upole na kusogeza vichwa vyao kwake.

وَالْمَسْكِينِ

**‘...na masikini...’**

Kwa kuwasaidia

وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَى

**“...na jirani wa karibu...”.**

Anakusudia ambaye baina yako na yeye kuna ujamaa, yeye ana haki ya ujamaa, haki ya ujirani na haki ya Uislamu.

وَالْجَارِ الْجُنُبِ

**“...na jirani wa mbali”.**

Yeye ni ambaye hakuna baina yenu ujamaa, na anaitwa hivyo ikiwa ni mgeni na hana udugu wa karibu. Aisha anatoa taarifa kuwa Mtume ﷺ amesema:

«ما زال جبريل يوصيني بالجار حتى ظننت أنه سيورثه»

*“Jibril hakuacha kuniusia kuhusu jirani mpaka nilifikiri kuwa atamrithisha.”<sup>612</sup>*

---

<sup>612</sup> Sahihi: Ahmad 6/238; Bukhari 6014; Muslim 2624

Anas amesema: Mtume ﷺ amesema:

« إن الجار ليتعلق بالجار يوم القيامة يقول : يا رب أوسعت علي أخي هذا  
وقترت علي ، أمسى طاوياً ويمسي هذا شعبان ، سله لم أغلق بابه وحرمني ما  
قد وسعت به عليه »

*'Hakika jirani atamng'ang'ania jirani yake siku ya kياما atasema:  
Ewe mola wangu umemkunjulia jirani yangu na umenipunja mimi  
nalala na njaa na huyu analala ameshiba, muulize kwa nini  
alinifungia mlango wake na ameninyima uliyo mkunjulia'*<sup>613</sup>.

وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ

**'...na rafiki wa ubavuni...'**

Ibn Abbaas na Mujaahid wamesema: huyo ni rafiki katika safari, ana haki ya ujirani na haki ya ushuba.

وَأَبْنِ السَّبِيلِ

**'...na mpita njia..'**

Ni mgeni anaepasa kumkirimu hadi afike anapotaka. Ibn Abbaas amesema: "Ni mpita njia umpokee, umlishe hadi arudi kwake".

وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ<sup>4</sup>

**"...na walio milikiwa na mikono yenu...",**

Anakusudia mtumwa kumfanyia wema, anampa riziki nzuri na anamsamehe katika anayokosea. Kauli Yake:

---

<sup>613</sup> Sahihi: Bukhari katika Adabul Mufradi 111 kwa tamshi ni mara ngapi jirani atamngania jirani yake siku ya kياما anasema: "Ewe mola wangu huyu amefunga mlango wake dhidi yangu ameninyima mema yake" Swahili Al-Adabil Mufrad 81

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا

**'Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wanao jifakhiri.'**

Ibn Abbaas amesema: Yani, mwenye majivuno nafsini mwake hasimamii haki za Allah, na mwenye kujifakharisha na anajifakhiri juu ya waja wa Allah, kwa ukarimu na neema Aliyompa. Na Kutoka kwa Abu Hurayra kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*"Wakati mmoja kijana barobaro akiwa anatembea katika pambo kwa majivuno na kujifakhiri ghafla ardhi ikammeza basi yeye anadidimia ndani yake hadi kisimame kiama"<sup>614</sup>.*

Usamah amesema: Abdullah bin 'Umar رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ akisema:

*"Mwenye kuburuza nguo yake kwa maringo Allah hatomwangukia Siku ya kiyama."<sup>615</sup>.*

Hili limetajwa na Al-Wahidi.

Mjumbe wa Allah ﷺ alipofariki dunia, katika maradhi yake aliusia Swala na kuwafanyia wema watumwa anasema:

*"Allah katika Swala na waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia"<sup>616</sup>.*

Na katika hadithi nyingine:

---

<sup>614</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>615</sup> Sahihi: Ahmad 2/44,46, 81. Bukhari 5783. Muslim 2085

<sup>616</sup> Sahihi: Ahmad 3/117 Ibn Maajah 2697 kwa tamshi: ala ala na waliomilikiwa na mikono ya kuume kwenu

## Al- Kabair

---

*"Uzuri wa kumiliki ni wema, na uovu wa kumiliki ni ukorofi"*<sup>617</sup>.

Mtume ﷺ akasema:

*"Haingii peponi mmiliki muovu wa tabia"*<sup>618</sup>

Ibn Mas'uud amesema: "Nilikuwa nikimpiga mtumwa wangu kwa mjeledi nikasikia sauti nyuma yangu:

*"Jua ewe Abu Mas'uud Allah ni Muweza zaidi juu yako kuliko uwezo wako juu ya kijana huyu".*

Nikamwambia: "Ewe mjumbe wa Allah baada ya leo sitompiga tena mtumwa wangu". Mjeledi wangu ulinitoka mkononi na kuanguka chini kutokana na utisho wa Mjumbe wa Allah ﷺ. Na kwa maelezo mengine Ibn Masuud alisema: "Wewe uko huru kwa kutaka radhi ya Allah". Mtume ﷺ amesema:

*"Hakika lau usingefanya hivyo moto ungekufukuta siku ya kياما."*  
Muslim<sup>619</sup>

'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*"Mwenye kumpiga mtumwa wake bila kosa au akampiga kofi, basi kafara yake ni kumwacha uhuru".*<sup>620</sup>

---

<sup>617</sup> Dhaifu: Abdur Razzaaq 20118; Ahmad 3/502; Twabarani 4451 Sheikh akaidhoofisha katika As Silsilah Dhaiifah 796

<sup>618</sup> Dhaifu: Tirmidhi 1946; Ibn Maajah 3691; Twabarani katika Al Awswat 9312 sheikh amaidhoofisha katika dhaiifil Jaamii 6250

<sup>619</sup> Sahihi: Muslim 1649; Abu Dawud 5159; Tirmidhi 1948

<sup>620</sup> Sahihi: Ahmad 2/61; Muslim 1657

## Al - Kabair

---

Katika hadithi ya Hakim bin Hizam رَضِيَ اللهُ عَنْهُ anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*“Hakika Allah atawaadhibu wanaoadhibu watu duniani.”<sup>621</sup>*

Katika hadithi nyingine:

*“Mwenye kupiga mjeledi kwa dhuluma Allah Atamlipizia siku ya kياما”<sup>622</sup>.*

Mtume ﷺ aliulizwa: “Ni mara ngapi tunamsamehe mtumishi?”.

Akasema: *“Katika siku mara sabini”<sup>623</sup>.*

Siku moja mkononi mwa Mtume ﷺ kulikuwa na mswaki akamuita mtumishi wake akachelewa akasema:

« لولا القصاص لضربتك بهذا السواك »

*“Lau si kisasi ningekupiga kwa mswaki huu”<sup>624</sup>.*

Abu Hurairah alikuwa na mjakazi mweusi siku moja akainua mjeledi akasema: “Lau sio kisasi ningekuchapa lakini nitakuuza kwa ambaye atanilipa thamani yako, nenda uko huru kwa ajili ya radhi ya Allah”.

Alikuja mwanamke kwa Mtume ﷺ akasema: “Ewe Mtume wa Allah nilimwambia mjakazi wangu: ‘Ewe mzinifu’ Mtume akamuuliza: *“Je uliona hilo kwake?”*

---

<sup>621</sup> Sahihi: Ahmad 3/404; Muslim 2613; Abu Dawud 3045

<sup>622</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>623</sup> Sahihi: Abu Dawud 5164, At-Tirmidhi 1949 na kusahihishwa na Shaykh katika silsila As-Swahiha 488.

<sup>624</sup> Sahihi: Bukhari katika Adabul Mufradi 84 Abu Yaalaa 6901 Al Baani ameisahihisha katika Adabul Mufradi 34



## Al-Kabair

---

Akasema: 'Hapana.' Akasema: "Ama "Wewe bila shaka utalipiziwa siku ya kiama".

Kwa hiyo akarejea kwa mjakazi wake akampa mjeledi akamwambia: "Nichape", Mjakazi akakataa, basi akarudi kwa Mtume ﷺ akamwambia kuwa amemuacha huru, Mtume ﷺ akasema: "Pengine".

Yaani Pengine kumuacha kwako huru kukakufutia kumsingizia kwake<sup>625</sup>. Katika Sahihi mbili kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*"Mwenye kumsingizia mtumwa wake naye yuko mbali nalo, ataadhibiwa adhabu siku ya kiama la sivyo awe kama alivyosema"*<sup>626</sup>.

Katika hadithi nyingine:

« للمملوك طعامه وكسوته ولا يكلف ما لا يطيق »

*"Mtumwa ana chakula chake, mavazi yake, wala asilazimishwe asiloliweza."*<sup>627</sup>

Mtume ﷺ akiwausia wao kuhusu mwisho wa maisha yake duniani kwa kuwaambia:

« الله الله في الصلاة وما ملكت أيمانكم أطمعهم مما تأكلون واكسوهم مما تكسون ، ولا تكلفوهم من العمل ما لا يطيقون فإن كلفتموهم فأعينوهم ولا تعذبوا خلق الله فإنه ملككم إياهم ولو شاء لملكهم إياكم »

*"Allah Allah katika Swala na waliomilikiwa na mikono yenu"*<sup>628</sup>, *walisheni mnavyakula na wavisheni mnachovaa, wala msiwakalifishe*

---

<sup>625</sup> Dhaifu mno: Haakim 4/370 na kufuatiliwa na maneno ya Adh-Dhahabi kwa kauli yake bali 'Abdul Malik-yaani Ibn Harun bin 'Antara ambaye ni *Matruk*.

<sup>626</sup> Sahihi: Bukhari 6858; Muslim 1660

<sup>627</sup> Sahihi: Ahmad 2/248; Bukhari 2545; Muslim 1662

<sup>628</sup> Maelezo yake yametangulia

## Al - Kabair

---

*katika kazi wasizoweza, na mkiwalazimisha basi wasaidieni wala msiadhibu viumbe wa Allah kwani Yeye Amekumilikisheni hao, Angetaka Angewamilikisha hao nyinyi.*<sup>629</sup>

Baadhi ya watu walikuja kumzuru Salmaan Al-Faris akiwa Mtawala (wa Al-Madain) walimkuta akikanda ngano ya familia yake, wakamuuliza, 'kwanini hakumuachia mfanyakazi wako akafanya kazi hiyo?' Akajibu: 'Nilimtuma kazi nyingine kwa hiyo sipendi kumkusanyia kazi nyingine'.

Baadhi ya Salafi wamesema: usimpige mtumwa kwa kila kosa, lakini mhifadhie hilo. Kwa hivyo akimuasi Allah basi mpige juu ya maasi yake, na mtajie kosa lililo baina yako na yeye.

### FASILI

Miongoni mwa uovu mkubwa kwa mtumwa na kijakazi ni kufarikisha baina yake na mtoto wake, au baina yake na ndugu yake, kwa hadithi iliyokuja kutoka kwa Mtume ﷺ:

« من فرق بين والدها وولدها فرق الله بينه وبين أحبته يوم القيامة »

*"Mwenye kufarakisha baina ya mzazi na mtoto wake Allah Atafarikisha baina yake na baina ya wapendwa wake siku ya kiama."*<sup>630</sup>

Ali رضي الله عنه ﷺ amesema: Mtume ﷺ alinizawadia wavulana wawili ndugu nikamnunua mmoja wao, Mjumbe wa Allah ﷻ akasema:

« رده رده »

*"Mrudishe mrudishe."*<sup>631</sup>

---

<sup>629</sup> Sahihi: Bukhari 2545; Muslim 1661

<sup>630</sup> Sahihi: Ahmad 5/413; Tirmidhi 1566 Swahihil jaami'i 6412

<sup>631</sup> Dhaifu kwa tamshi hili: Tirmidhi 1284; Ibn Maajah 2249 Al-Baani ameidhoofisha katia Dhailiil Ibn Maajah 492; Al Mishkaat 3362; Al Baani ameisahihisha kwa tamshi jingine katika Sahihi Abi Dawud 1412 Jaami'i

## Al - Kabair

---

Miongoni mwa hayo ni kumuweka na njaa mtumwa na mnyama, Mtume ﷺ amesema:

« كفى بالمرء إثماً أن يحبس عمن يملك قوته »

*“Inamtosha mtu kuwa na dhambi kumfunga anayemiliki chakula chake”<sup>632</sup>.*

Katika hayo pia ni kumpiga mnyama pigo baya au kumfunga bila kusimamia mahitaji yake ya kumtosha, au kumbebesha juu ya uwezo wake. Imepokewa katika tafsiri ya Kauli Yake Taalaa:

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَيْرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمٌّ أَمْثَالِكُمْ

***“Na hapana mnyama katika ardhi, wala ndege anaye ruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi...” (6:38)***

Imesemwa: Wataletwa na watu wamesimama siku ya kيامa na atahukumu baina yao, mpaka atachukuliwa mbuzi asiye na pembe alipiziwe kwa mbuzi mwenye pembe, mpaka ilipizwe kwa *dharrah kutokana na dharra*, kisha wataambiwa kuweni udongo, hapo kafiri atasema:

يَلِيَّتِي كُنْتُ تُرَابًا

***“Laiti ningekuwa udongo”.***

Hii ni dalili ya kuhukumiwa baina ya wanyama, baina yao na wanadamu, Endapo mtu alimpiga mnyama bila kosa au alimweka mnyama na njaa au kiu au alimlazimisha kazi au mzigo ukamuelemea zaidi ya uwezo wake. Basi mtu huyo ataadhibiwa kwa kadiri ya alivyomdhulumu. Dalili ya hilo ni yaliyo thibiti katika sahihi mbili kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« عذبت امرأة في هرة ربطتها حتى ماتت جوعاً لا هي أطعمتها وسقته إذ حبستها، ولا تركتها تأكل من خشاش الأرض »

*"Mwanamke mmoja aliadhibiwa kwa ajili ya paka, alimfunga hadi akafa kwa njaa. Hakumlisha na kumnyweshwa, kwa kuwa alimfunga, wala hakumuacha anakula katika wadudu wa ardhi."*<sup>633</sup>

Katika Sahihi mbili: Mjumbe wa Allah ﷻ aliona mwanamke ananing'inizwa ndani ya moto na paka anamparura usoni na kifua ni na yeye (paka) anamuadhibu kama alivyomuadhibu kwa kumfunga na njaa<sup>634</sup>.

Hili linawaenea wanyama wote. Kadhalika akimbebesha juu ya uwezo wake atalipiziwa siku ya kيامa kwa kadiri ya alichomo mbebesha. Hadithi iliyothibitika katika Sahihi mbili, Abu Huraira anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*"Mtu mmoja alikuwa akiendesha ng'ombe akampanda kisha akampiga, Akasema (ng'ombe): Sisi hatukuumbwa kwa ajili ya hili, (sisi tumeumbwa kwa ajili ya kulima)."*<sup>635</sup>

Huyu ni ng'ombe, Allah amemtamkisha katika dunia ajitete ili asiudhiwe wala asitumiwe katika mengineyo. Kwa hiyo mwenye kumlazimisha bila uwezo wake au akampiga siku ya kيامa atalipiziwa kwa kadiri ya kumpiga kwake na kumuadhibu kwake.

Abu Sulaiman Daaraani amesema: Wakati mmoja nilikuwa nikimuendesha punda nikampiga mara mbili au tatu, punda akaniangalia akasema: "Ewe Abu Sulaiman: Hicho ni kisasi siku ya kيامa kwa hiyo ukitaka punguza na ukitaka zidisha". Abu Sulaiman alisema: "Baada ya hapo sikumpiga tena mnyama yeyote."

---

<sup>632</sup> Sahihi: Ahmad 5/160 Muslim 996

<sup>633</sup> Sahihi: Bukhari 2365, 2318; Muslim 2242

<sup>634</sup> Sahihi: Bukhari 745, 2364

<sup>635</sup> Sahihi: Bukhari 3471 Muslim 2388

## Al- Kabair

---

Abdullah bin 'Umar alipita karibu na vijana wa kikureish waliokuwa wamemfunga ndege na wanampiga mishale, na mishale unaomkosa unakuwa mali ya mwenye ndege huyo. Walipomuona Ibn 'Umar wakakimbia, Ibn 'Umar akauliza: 'Nani amefanya hivi? Allah amemlaani anayefanya hivi.' Mjumbe wa Allah ﷻ amemlani mtu anaye mfanya mnyama ni lengo<sup>636</sup> (kulengea shabaha) na Mtume ﷺ amekataza kumsubirisha mnyama, yaani: Kumfunga kwa ajili ya kuchinjwa,<sup>637</sup> na ikiwa ni miongoni mwa walioruhusiwa na sheria, na ikiwa ni miongoni mwa alivyoruhusu kuuawa kwake kama vile nyoka, nge, na panya na mbwa koko, kuuliwa kwake iwe kwa pigo la mwanzo tu wala si kumuadhibu. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

*"Mnapoua ueni vizuri, na mnapochinja chinjeni vizuri, na mmoja wenu anoe kisu chake na astareheshe kichinjo chake"*<sup>638</sup>.

Hali kadhalika inakatazwa kuchoma moto kiumbe chochote kwa hadithi sahihi iliyothibitika kutoka kwa Mtume ﷺ:

*"Nilikuwa nimekuamrisheni kumchoma fulani na fulani kwa moto, na moto haadhibu nao yeyote isipokuwa Allah, mkiwapata hao wawili basi waueni."*<sup>639</sup>

Ibn Masuud amesema: "Tulikuwa katika msafara pamoja na Mjumbe wa Allah ﷻ akaenda kwa ajili ya haja yake, tukaona kiota cha ndege ndani yake kuna vifaranga viwili tukavichukua vitoto vyake, yule ndege akawa anaruka ruka. Mtume ﷺ akasema:

*"Ni nani aliyemuumiza huyu kwa mtoto wake?, Mrudisheni mtoto wake".*

Akaona tumechoma moto kichuguu cha wadudu chungu akauliza:

---

<sup>636</sup> Sahihi: Bukhari 3471; Muslim 1958

<sup>637</sup> Sahihi: Al-Bukhari 5513 na Muslim 1956

<sup>638</sup> Sahihi: Muslim 5513; Abu Dawud 2815; Tirmidhi 1409

<sup>639</sup> Sahihi: Bukhari 3016

« من حرف هذه ؟ »

*“Ni nani aliyechoma hiki”*

Tukajibu: “Sisi” akasema: *“Haifai kwa yeyote kuadhibu kwa moto isipokuwa Mola wake”*<sup>640</sup>.

### FASILI

Ni karaha kuuu mnyama bure bure kwa hadithi iliyopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

*“Mwenye kuuu ndege burebure, siku ya kiama (ndege) kitapiga kelele: Ewe mola wangu! Muulize huyu kwa nini aliniua burebure na hakuniua kwa manufaa?”*<sup>641</sup>.

Inachukizwa kuwinda ndege mwenye vifaranga kama ilivyopokewa katika athari. Huchukizwa kumchinja mnyama mbele ya mama yake kwa yaliyopokewa kutoka kwa Ibrahim bin Adham رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, amesema: ‘Mtu alichinja ndama mbele ya mama yake na Mwenyezi mungu akaupooza mkono wake.’

### FASILI

Katika fadhila ya kuacha huru Mtumwa. Abu Hurairah رَضِيَ اللهُ عَنْهُ anasema: Mtume wa Allah ﷺ amesema:

*“Mwenye kuacha huru mtumwa muumini Allah ataacha huru kila kiungo chake mtu kwa kiungo chake motoni, mpaka aache huru tupu yake kwa tupu yake”.* (Bukhari)<sup>642</sup>

---

<sup>640</sup> Sahihi: Bukhari katika Adabul Mufradi 382; Abu Dawud 2675; Ameisahisha Al-Baani katika Silsilah Sahiihah

<sup>641</sup> Dhaifu: Ahmad 5/389; Nasaai 7/239; Shaykh ameidhoofisha katika Dhahifil Jaami'i 5763

<sup>642</sup> Sahihi: Bukhari 2517; Muslim 1509

## Al- Kabair

---

Abu Umaamah رضى الله عنه anatoa taarifa kuwa Mtume ﷺ amesema:

*“Muislam yeyote aliyemwacha huru mtumwa Muislam, basi jambo hilo ni mkombozi wake na moto, atasamehe kila kiungo chake kwa kiungo chake, na mwanamke yeyote Muislam amewacha huru mwanamke Muislamu atakuwa mkombozi wake na moto, atasamehe kila kiungo chake kwa kiungo chake”. (Tirmidhi) ameitaja kuwa ni Hasan Sahihi<sup>643</sup>*

Ewe Mola tujalie katika kundi lako la wenye kufaulu, na waja wako wema.

\*\*\*

---

<sup>643</sup> Sahihi: Tirmidhi 1584 Al Baani ameisahihisha Sahiihil Jaami'i, 2700





Katika riwaya nyingine:

وقال النبي ﷺ: «مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلَا يُوْذِي جَارَهُ»  
وفي لفظ لمسلم: «مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَلْيُحْسِنِ إِلَى جَارِهِ»<sup>(٣)</sup>.

*“Mwenye kuwa anamuamini Allah na siku ya mwisho na asimuudhi jirani yake.”<sup>647</sup>*

*“Majirani ni watatu: Jirani Muislam wa karibu, ana haki ya ujirani, na ya Uislam na haki ya ujamaa, na jirani muislam ana haki ya Uislam na haki ya ujirani, na kafiri ana haki ya ujirani.”<sup>648</sup>*

Ibn Umar alikuwa na jirani myahudi na alipochinja mbuzi akisema: “Mpelekeeni jirani yetu myahudi”<sup>649</sup>.

Imepokewa kuwa mjakazi maskini atamng’ang’ania jirani tajiri siku ya kiama, na atasema: “Ewe mola wangu muulize huyu kwa nini ameninyima mema yake na amenifungia mlango wake?”<sup>650</sup>.

Inatakiwa kwa jirani kuvumilia maudhi ya jirani yake na hayo ni katika jumla ya wema wake. Mtu mmoja alikwenda kwa Mtume ﷺ akasema: “Ewe mjumbe wa Allah nionyeshe amali nikisimama nayo nitaingia peponi.” Akasema: “Kuwa mwema.”

Akasema: ‘Ewe Mtume wa Allah nitajuaje kuwa mimi ni mwema?’  
Akasema:

---

<sup>647</sup> Sahihi: Bukhari 6118; 6146 Muslim: 47

<sup>648</sup> Dhaifu: Bazaar 1896; Abu Nuaim 5/207; Baihaqi katika Shi’ib 9560 ;Al- Baani ameidhoofisha katika Dhaiifil Jaami’i 2673

<sup>649</sup> Sahihi: Tirmidhi 1934, 584; Baihaqi 9562,9563 Al-Baani ameisahihisha katika Al Irwaa 26891

<sup>650</sup> Dhaifu: Al-Bukhari katika Al-Adab al-Mufrad 111 na Shaykh ameipa daraja la Hassan katika Swahih Al-Adab al-Mufrad 87.

## Al - Kabair

---

*“Waulize majirani zako wakisema wewe ni mwema basi wewe ni mwema, na wakisema wewe ni mbaya basi wewe kweli mbaya.”* (Baihaqi ameitaja katika riwaya ya Abu Hurairah<sup>651</sup>).

Imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

*“Mwenye kufunga mlango wake kwa jirani yake kwa kuogopa mali yake na familia yake huyo si muumini, na si muumini ambaye jirani yake hasalimiki na shari zake”<sup>652</sup>.*

Kukasemwa:

*“Kuzini mtu na wanawake kumi ni kwepesi kuliko kuzini na mke wa jirani yake, na mtu kuiba kwenye nyumba kumi ni kwepesi kuliko kuiba kwenye nyumba ya jirani nyake”<sup>653</sup>.*

Abu Hurairah رضي الله عنه amesema: “Mtu mmoja alikwenda kwa Mtume ﷺ akimlalamikia kuhusu jirani yake, Mtume ﷺ akamwambia: “Nenda na usubiri”.

Akamjia mara mbili au mara tatu (kwa malalamiko yale yale) Mtume ﷺ akamwambia: “Nenda katupe vyombo vyako njiani”.

Akafanya hivyo watu wakawa wanapita wanamuuliza, anawaambia habari ya jirani yake, wakamlaani jirani yake wakisema: ‘Allah amlaani fulani anafanya hivi?’ Jirani aliposikia hivyo akamjia kumtaka radhi na kusema: “Tafadhali ndugu yangu rudi nyumbani kwako, kwa hakika wewe hutasikia tena unayoyachukia milele.”<sup>654</sup>.

---

<sup>651</sup> Sahih: Haakim 1/378; Baihaqi katika Shi’bi 9567; Hakim amesema ni sahihi juu ya masharti yao na Dhahabi akaafikiana nae.

<sup>652</sup> Dhaifu: Ibn Adiy 5/171; Baihaqi 9560 na isinadi yake ni dhaifu

<sup>653</sup> Sahihi: Bukhari katika Adabul Mufradi 103; Ahmad 6/8 Shaykh ameisahihisha katika As-Silsilas Swahihah 65

<sup>654</sup> Sahihi: Abu Dawud 5153 Bukhari katika Al Adabul Mufradi 124 Shaykh ameisahihisha katika sahihil Adabul Mufradi 92

## KISA

### Kuvumilia Udhia wa jirani Hata kama ni Dhimmi

Sahl bin Abdullah Tastari alikuwa na jirani asiye Muislam, maji yakawa yanachuruzika kutoka choo cha jirani hupitia katika nyumba ya Sahl. Alikuwa akiyakusanya maji haya machafu ndani ya chombo na usiku mkubwa huyakuchukua bila ya mtu yoyote kumuona na kuyamwaga mbali. Sahl aliendelea na tabia hii kwa muda mrefu hadi alipokuwa karibu na *Sakaratul Mauti* akamwita jirani yake huyo asiye Muislam na akamuomba aje nyumbani kwake, ili apate kuona kinachotokea. Akauliza: 'Ni nini hiki ninachokiona?' jirani akaona yale maji machafu yanayomwagika ndani ya nyumba yake Sahl akamwambia: "Kwa kipindi kirefu nilikuwa nikikusanya uchafu huu mchana na kuumwaga nyakati za usiku, sasa karibu nitakufa na nina khofu ya kutoa siri ya kosa lako kwa mtu yeyote atakayehamia ndani ya nyumba yangu baada ya kifo changu, na hiyo ndiyo sababu ya mimi kukupa taarifa hiyo.

Yule jirani akamwambia: "Ewe Sheikh umekuwa mstahamilivu kwangu wakati huo wote nami bado nimebakia si muumini Tafadhali nyoosha mkono wako, ninashuhudia kuwa hakuna Mungu isipokuwa Allah na kuwa Muhammad ni Mjumbe Wake, baada ya muda mchache Sahl alitoa pumzi zake za mwisho. Allah Amrehemu.

Tunamuomba Allah kutuongoza sisi na nyinyi kwenye tabia njema, matendo na maneno, na kufanya mwisho wetu kuwa mwema kwa hakika Yeye ni Mpaji, Mkarimu, Mpole, Mwingi wa rehemu.

\*\*\*

**DHAMBI KUBWA YA HAMSINI NA TATU**  
**KUWAUDHI WAISLAMU NA KUWATUKANA**

Allah Mtukuka Amesema:

وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ بَغَيْرِ مَا كَتَبْنَا لَهُمْ فَحَدِّثْهُمْ بِمَا كَتَبْنَا وَتَمَّ

مُيِّنًا ﴿٥٨﴾

***“Na wale wanao waudhi Waumini wanaume na wanawake pasina wao kufanya kosa lolote, bila ya shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilio dhaahiri.” (33:58)***

Allah Amesema:

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَسْخَرُونَ مِنْ قَوْمٍ عَسَىٰ أَنْ يَكُونُوا خَيْرًا مِنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِنْ نِسَائِهِمْ  
عَسَىٰ أَنْ يَكُنَّ خَيْرًا مِنْهُنَّ وَلَا تَلْمِزُوا أَنْفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا بِاللِّغَابِ بِئْسَ الْإِلْمُ  
الْفُسُوقُ بَعْدَ الْإِيمَانِ ۚ وَمَنْ لَمْ يَتُبْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾

***“Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume, wala wanawake wasiwadharau wanawake. Huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu.” (49:11)***

وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَبِ بَعْضُكُم بَعْضًا

***“...Wala msipelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi.” (49:12)***

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

## Al - Kabair

---

« إن من شر الناس منزلة عند الله يوم القيامة من ودعه الناس أو تركه الناس  
اتقاء فحشه »

*“Hakika muovu wa watu kwa hadhi mbele ya Allah Mtukuka siku  
ya kiama, ni ambaye watu wamemwacha kwa kuogopa na kujilinda  
na machafu yake”<sup>655</sup>.*

Amesema:

« عباد الله إن الله وضع الحرج إلا من المقترض بعرض أخيه فذلك الذي  
حرج أو هلك »

*“Enyi waja wa Allah! Hakika Allah ameondoa makosa isipokuwa  
kwa mwenye kuvunja heshima ya ndugu yake basi huyo ni mkosaji  
au ameangamia”<sup>656</sup>.*

Katika hadithi nyingine:

« كل المسلم على المسلم حرام دمه وماله وعرضه »

*“Kila muislamu juu ya muislamu ni haramu damu yake, mali yake  
na heshima yake”<sup>657</sup>.*

Na katika hadithi nyingine:

« المسلم أخو المسلم لا يظلمه ولا يخذله ولا يحقره ، بحسب امرئ من  
الشر أن يحقر أخاه المسلم »

*“Muislamu ni ndugu wa muislam hamdhulumu, wala hamtelekezi,  
wala hamdharau, inatosha kuwa ni katika shari kumdharau ndugu  
yake muislamu”<sup>658</sup>.*

---

<sup>655</sup> Sahihi: Al-Bukhari 6131, 6054; Muslim 2591

<sup>656</sup> Sahihi; Bukhari katika Adabul Mufradi 291; Abu Dawud 2015; At-tirmidhy 2038; Ibn  
Maajah 3436; Swahihah 433; Al Mishkaat 4532, 5079

<sup>657</sup> Sahihi: Muslim 2564 Ahmad 2/277,287, 288.

<sup>658</sup> Hadithi iliyotangulia.

## Al - Kabair

---

Kadhalika Hadithi:

«سباب المسلم فسوق وقتاله كفر»

*“Kumtukana muislamu ni ufasiki na kumpiga ni ukafiri”<sup>659</sup>*

Abu Hurairah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ aliambiwa: “Ewe Mtume wa Allah! Hakika fulani anaswali usiku na anafunga mchana lakini anamuudhi jirani yake kwa ulimi wake”. Mtume ﷺ akasema:

« لا خير فيها هي في النار »

*“Hakuna kheri ndani yake huyo ni mtu wa motoni”<sup>660</sup>* Ameisahihisha Haakim

Katika hadithi nyingine:

« اذكروا محاسن موتاكم وكنفوا عن مساوئهم »

*“Tajeni mema ya maiti wenu na jizuieni na maovu yao”<sup>661</sup>*

Mtume ﷺ akasema:

« من دعا رجلا بالكفر أو قال يا عدو الله وليس كذلك إلا حار عليه »

*“Mwenye kumuita mtu kwa ukafiri, au akasema: wewe adui wa Allah na yeye hayuko hivyo, isipokuwa sifa hizo zitamrudia yeye”<sup>662</sup>*

---

<sup>659</sup> Sahihi: Al-Bukhari 48 na Muslim 64.

<sup>660</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/440, na Al-Bukhari Al-Adab Al-Mufrad 119 na Shaykh ameiweka katika As-Swahiha 190.

<sup>661</sup> Dhaifu: Imepokewa na At-Tirmidhi 1019, Abu Dawud 4900 na kudhoofishwa na Shaykh katika Dhaifu Al-Jami’ 839, Al-Mishkaat 1678 na Ar-Rawdh An-Nadhiir 482.

<sup>662</sup> Sahihi: Muslim 61 kwa tamshi ‘Sio katika sisi mtu anayejita jina la asiye baba yake”.

Mtume ﷺ akasema:

«مررت ليلة أسري بي يقوم لهم أظفار من النحاس يخمشون وجوههم  
وصدورهم، فقلت : من هؤلاء يا جبريل ؟ فقال : هؤلاء الذين  
يأكلون لحوم الناس ويقعون في أعراضهم»

*“Nilipita usiku nilioplekwa (Miraji) kwa watu wana kucha za shaba  
wanararua nyuso zao na vifua vyao, nikauliza: ‘Ni nani hawa ewe  
Jibrili?’, Jibrili akasema: “Hao ni ambao wanakula nyama za watu  
na wanaangukia katika heshima zao.”<sup>663</sup>*

## FASILI

### KATIKA KUOGOPESHA DHIDI YA UHARIBIFU NA KUGOMBANISHA BAINA YA WAUMINI NA BAINA YA WANYAMA

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« إن الشيطان قد أيس أن يعبد المصلون في جزيرة العرب ولكن في  
التحريش بينهم»

*“Shetani amekata tamaa kuwa yeye hataabudiwa tena ndani ya rasi  
ya arabuni lakini (ataweza) katika kuwagombanisha baina yao”<sup>664</sup>*

Kwa hivyo yeyote atakaye chochea uadui baina ya watu wawili miongoni  
mwa wanadamu na kusababisha mmoja kati yao kumjeruhi mwenziwe,  
basi mtu huyu ni mfitini na muovu na yupo katika chama cha shetani.  
Kama alivyosema Mtume ﷺ:

---

<sup>663</sup> Sahihi: Abu Dawud 4878, Ahmad 3/18,329 na As-Silsila As-Swahiha 533.

<sup>664</sup> Sahihi: Muslim 2812 na At-Tirmidhi 1937.

« ألا أخبركم بشراركم ؟ »

“Je nikuambieni waovu wenu?”

Wakasema: ‘Ndio (tuambie)’ Akasema:

« شراركم المشاءون بالنميمة. المفسدون بين الأحياء ، الباغون للبرآء العنت »

“Waovu wenu ni wenye kutembea kwa kuchonganisha, na wenye kuharibu baina ya wapenzi, wenye kuwadhulumu waliosalimika na matatizo.”<sup>665</sup>

Mtume ﷺ amesema: « لا يدخل الجنة نمام »

“Hataingia peponi msambazaji fitna.”<sup>666</sup>

Msambazaji fitina ni anayehamisha mazungumzo baina ya watu, yanaudhi mmoja wao au yanasononesha moyo wake, au rafiki yake, anamwambia: “Fulani na fulani wamesema kadha wa kadha, na fulani na fulani walifanya hivi na hivi bila masilahi wala faida. Kama vile kumtahadharisha shari inayoweza kutokea.”

Ama kupiganisha wanyama ndege na wengine ni haramu kama vile kuchonganisha majogoo, kugonganisha kondoo na kuchonganisha mbwa, baadhi yao wao kwa wao na mfano wake.

Mtume ﷺ amekataza hili na mwenye kulifanya amemuasi Allah na Mjumbe wake. Katika hayo ni kuharibu moyo wa mke kwa mumewe, na mtumishi na bwana wake. Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>665</sup> Hassan: Bukhari katika Adabul Mufradi 323, Twabarani 24/167/423 Shaykh ameifanya Hasan katika Al Adab 246

<sup>666</sup> Maelezo yake yametangulia



« ملعون من خيب امرأة على زوجها أو عبدا على سيده »

*“Amelaaniwa mwenye chuki kati ya mwanamke na mumewe au mtumwa dhidi ya bwana wake”<sup>667</sup>*

## FASILI

### KULETA UPATANISHO BAINA YA WATU

Allah Amesema:

﴿ لَا خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّنْ نَّجْوَاهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ  
وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴾

***“Hakuna kheri katika mengi ya wanayo shauriana kwa siri, isipo kuwa kwa yule anaye amrisha kutoa sadaka, au kutenda mema, au kupatanisha baina ya watu. Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi Tutakuja mpa ujira mkubwa.” (4:114)***

Mujahid anasema: Aya hii inaenea kwa watu wote. Anakusudia kuwa hakuna kheri katika ambayo watu wananong'onezana na kuzama ndani yake miongoni mwa mazungumzo, isipokuwa yenye kuwa katika amali za kheri. Hiyo ni Kauli Yake:

﴿ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ ﴾

***“...isipo kuwa kwa yule anaye amrisha kutoa sadaka...”***,

Kisha akasema:

﴿ أَوْ مَعْرُوفٍ ﴾

***“...au kutenda mema.”***

---

<sup>667</sup> Maelezo yake yametangulia

## Al - Kabair

---

Ibn 'Abaass رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ<sup>668</sup> amesema: "Kwa kuunga udugu, na kwa kumtii Allah." Imesemwa: "Vitendo vyema vyote vinajulikana, na kila mwenye akili anavijua." Kauli Yake Taalaa:

أَوْصَلِحْ بَيْنَ النَّاسِ<sup>669</sup>

**"au kupatanisha baina ya watu".**

Hili ni katika alilohimiza Mtume ﷺ. Alipomwambia Abu Ayyuub Al-Ansaar:

« أَلَا أَدُلُّكَ عَلَى صَدَقَةٍ هِيَ خَيْرٌ لَكَ مِنْ حَمْرِ النَّعَمِ »

*"Je sikujulishi sadaka ambayo hiyo ni kheri kwako kuliko kushinda ngamia wekundu?"*

Akasema: "Nijulishe ewe mjumbe wa Allah?", Mtume ﷺ akasema:

« تَصْلِحْ بَيْنَ النَّاسِ إِذَا تَفَاسَدُوا وَتَقْرَبْ بَيْنَهُمْ إِذَا تَبَاعَدُوا »

*"Utasuluhisha baina ya watu wakati wakigombana na utakaribisha baina ya watu wanapokuwa mbalimbali."<sup>668</sup>*

Ummu Habiibah anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« كَلَامُ ابْنِ آدَمَ كُلُّهُ عَلَيْهِ لَا لَهُ إِلَّا مَا كَانَ مِنْ أَمْرٍ بِمَعْرُوفٍ أَوْ نَهْيٍ عَنْ مَنكَرٍ أَوْ ذَكَرَ اللَّهَ »

*"Maneno yote ya mwanadamu ni dhidi yake, sio faida yake, isipokuwa yalio katika kuamrisha mema au kukataza mabaya, au Dhikru Ilaahi"<sup>669</sup>.*

---

<sup>668</sup> Dhaifu: Ameipokea Baihaqi katika Shi'bi 11903 na Twabarani katika Al Kabiir 8/257

<sup>669</sup> Dhaifu: Ameipokea Tirmidhi 2412; Ibn Maajah 3974; Al Baani ameidhoofisha katika dhaiifi ibn Maajah 761 na At Ta'aliq ar Raghiib 4/10.

Mtu mmoja alimwambia Sufyan Ath-Thawri: “Hadithi hii ni kali mno?”  
Sufyaan akasema: “Kwani hujasikia Kauli ya Allah Taalaa?.”

❖ لَا خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّن نَّجْوَاهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ  
وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤١١﴾

**“Hakuna kheri katika mengi ya wanayo shauriana kwa siri, isipo kuwa kwa yule anaye amrisha kutoa sadaka, au kutenda mema, au kupatanisha baina ya watu”. (4:114).**

Hivyo inamaanisha hayo. Kisha Allah Akajulisha kuwa hilo linamnufaisha mwenye kutaka yalio kwa Allah. Allah Amesema:

وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤١١﴾

**“Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi Tutakuja mpa ujira mkubwa.”**

Yaani: Thawabu zisizo na kikomo. Na katika hadithi nyingine:

« ليس الكذاب الذي يصلح بين الناس فينمي خيرا أو يقول خيرا »

**“Si muongo msuluhishaji baina ya watu, kwa hiyo akachonganisha kheri au akasema kheri.” Ameipokea Bukhari<sup>670</sup>**

Ummu Kulthuum amesema: “Sikumsikia ﷺ anaruhusu kitu katika wanayosema watu isipokuwa katika mambo matatu: katika vita, kusuluhisha baina ya watu, na mazungumzo ya mtu kwa mkewe na mazungumzo ya mtu kwa mumewe.”<sup>671</sup>

---

<sup>670</sup> Sahihi: Ahmad 6/403,404, Bukhari 2692, Muslim 2605

<sup>671</sup> Ziada hii iko kwa Muslim 2065.

## Al - Kabair

---

Sahli bin Saad Saa'idy رضي الله عنه amesema: Ilimfikia Mtume ﷺ kuwa Banu Amr bin Awf kulikuwa na shari baina yao, kwa hivyo akatoka pamoja na sahaba zake ili kusuluhisha baina yao." <sup>672</sup>

Abu Hurairah رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« ما عمل شيء أفضل من مشي إلى الصلاة أو إصلاح ذات البين وحلف  
جائز بين المسلمين »

*"Hakijatendwa kitendo chochote bora zaidi kuliko kuendea Swala, au kusuluhisha waliotengana, na kuleta muungano wa haki (kisheria) kati ya waislam." <sup>673</sup>*

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« من أصلح بين اثنين أصلح الله أمره وأعطاه بكل كلمة تكلم بها عتق رقبة  
ورجع مغفوراً له ما تقدم من ذنبه »

*"Mwenye kusuluhisha baina ya watu wawili, Allah Atamtengenezea mambo yake, kila neno moja alilolizungumza atampa kuacha huru mtumwa, na atarejea akiwa amesamehewa dhambi zake" <sup>674</sup>*

Na kwa Allah ndiko kwenye Taufiqi

Ewe Allah Amiliana nasi kwa Huruma Yako na Tudiriki kwa Msamaha Wako, ewe Mrehemevu wa wenye kurehemu.

\*\*\*

---

<sup>672</sup> Sahihi: Bukhari 1234

<sup>673</sup> Sahihi: Bukhari 1234 katika At Taariikh Al Kabair 1/63 Mundhir amesema: 3/321 ni hadithi ngeni sana

<sup>674</sup> Dhaifu: Al-Asbahaani katika at-Targhiib 186 na Al-Mundhiri akasema 3/321 Hadithi Gharib mno.

## DHAMBI KUBWA YA HAMSINI NA NNE

### KUWAUDHI WAJA WA ALLAH NA KUWAFANYIA UJEURI

Allah Mtukuka Anasema,

وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ بَغَيْرِ مَا اكْتَسَبُوا فَقَدِ احْتَمَلُوا  
بُهْتَنَا وَإِنَّمَا مِثْلُنَا

**"Na wale wanao waudhi Waumini wanaume na wanawake pasina wao kufanya kosa lolote, bila ya shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilio dhaahiri." (33:58)**

Akasema Allah Taalaa:

وَأَصْبَرَ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ

**"Na watwae kwa upole wanao kufuata miongoni mwa Waumini." (26:215).**

Abu Hurairah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema:

« إن الله تعالى قال : من عادى لي وليا فقد آذنته بالحرب »

**"Hakika Allah Aliyetukuka Anasema: "Mwenye kumuudhi walii wangu, kwa hakika Nimekwisha mtangazia vita".**

Katika riwaya nyingine:

« فقد بارزني بالمحاربة »

**"Amenikabili kwa vita"<sup>675</sup>.**

---

<sup>675</sup> Sahihi: Al-Bukhari 6502 na Ibn Hibbaan 347

Yaani: Nimemtangazia kuwa Mimi ni mgomvi wake.

Na katika hadithi: Abu-Sufyani aliwaendea Salmaan, Suhaib na Bilali wakiwa kikundi wakasema: “Hujachukua mapanga ya Allah toka kwa adui wa Allah kwa haki”. Abu Bakr رضي الله عنه akasema: “Mnasema hivi kwa mzee na mkuu wa Kureishi?” Kwa hiyo akamuendea Mtume ﷺ akampa habari, Mtume ﷺ akasema:

«يا أبا بكر لعلك أغضبتهم؟ لئن كنت أغضبتهم ، لقد أغضبت الله»

*“Ewe Abu Bakr labda umewakasirisha? na endapo umefanya hivyo, basi umemkasirisha Allah”.*

Abu Bakr رضي الله عنه akawaendea akasema: “Enyi ndugu zangu nimekuudhini?” Wakamjibu: “Hapana, Allah akusamehe, ewe ndugu.”<sup>676</sup>

## FASILI

Allah Mtukuka Anasema:

وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ

**“Na isubirisha nafsi yako pamoja na wanao muomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka radhi Yake.” (18:28)** (Zaad al-Masiir 5/132, na Asbabu Nuzuli ya al-wahidi, na Sanadi yake ni Dhaifu sana)

Aya hii iliteremshwa katika kufadhilisha mafukara, na sababu ya kushuka kwake ni kuwa watu wa mwanzo kumuamini walikuwa ni mafukara. Kadhalika kwa kila Mtume aliyetumwa na Allah wa mwanzo kumuamini walikuwa mafukara. Mjumbe wa Allah ﷺ alikuwa anakaa na masahaba

---

<sup>676</sup> Sahihi: Muslim 2504

zake mfano wa Salmaan, Suhaib, Bilaal na 'Ammar bin Yaasir, washirikina wakataka kumfanyia hila katika kuwafukuza mafukara kwa vile walisikia alama ya Mitume ni kuwa wafuasi wake wa mwanzo ni mafukara, kwa hiyo wakaja baadhi ya wakuu wa makureishi, wakasema:

“Ewe Muhammad wafukuze hao mafukara, kwani nafsi zetu zinaona kinyaa kukaa nao, kwa hakika ukiwafukuza kwako watakuamini watukufu wa watu na wakuu wao. Basi Allah akashusha:

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ

**“Wala usiwatupe wale ambao wanaomuomba Mola wao asubuhi na jioni wanataka Radhi Yake”**

Washirikina walipokata tamaa Mtume ﷺ kuwatupa masahaba wake wakasema: Ewe Muhammad ikiwa hutawafukuza hao basi panga siku moja yao na siku moja yetu, Allah Mtukuka akasema:

وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُمْ وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ﴿٢٨﴾

**“Na isubirisha nafsi yako pamoja na wanao muomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka Radhi Yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia..”(18:28)**

Yaani: Usiwafanyie uadui wala usizidishe kuwatazama kwa kuwachukia kwa kutaka usuhuba na wana wa duniani.

وَقُلِ الْحَقُّ مِن رَّبِّكُمْ ۖ فَمَن شَاءَ فَلْيُؤْمِن وَمَن شَاءَ فَلْيُكْفُرْ ۗ

**“Na sema: Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae”.(18:29)**

Kisha akapiga mfano wa tajiri na fukara kwa Kauli Yake:

• وَأَضْرَبَ لَهُمْ مَثَلًا رَجُلَيْنِ

**“Na wapigie mfano wa watu wawili” (18:32)**

وَأَضْرَبَ لَهُمْ مَثَلَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

**“Na wapigie mfano wa maisha ya dunia” (18:45)**

Kwa hiyo Mtume ﷺ alikuwa akithamini maskini na kuwakirimu.

Mtume ﷺ alipohama Makka kwenda Madina walihama pamoja naye na wakawa katika *Sufah* ya msikiti, wakiishi na kuabudu. Kwa hiyo wakaitwa *As'haabu Sufah*, kwa hiyo wakajiunga nao mafukara wanaohamia Madinah hadi wakawa wengi.

Hao walishuhudia Allah Aliyowaahidi mawalii wake wema kutokana na hisani yake, na wakaishuhudia kwa nuru ya imani, kwa hiyo nyoyo zao hazikujua chochote cha ulimwengu isipokuwa walisema:

“Wewe tu tunakuabudu na kusujudu, na Kwako tunaongoka na kutaka uongofu, na Kwako Wewe tumetegemea, na kwa Utajo Wako tunaneemeka na kufurahi, na katika uwanja wa upendo wako tunapanda na tunalisha, kwa ajili yako tunatenda na kujitaabisha. Na abadan hatuachi kuwa kwenye mlango Wako.”

Basi wakati huo Akawajengea Njia Yake, na Akamsemesha Mtume Wake kuhusu wao, Akasema:

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ

**“Wala usiwafukuze wanao mwomba Mola Mlezi wao asubuhi” (6:52)**



## Al - Kabair

---

Yaani: Usiwafukuze watu ambao wamekuwa wakielekea kwenye Utajo wa Mola wao, na kwenye Mlango wa Mola wao wanaelekea, usiwafukuze watu, msikiti ndio makazi yao, na Allah ndio Hitaji lao, na Mlinzi wao.

Njaa ndio chakula chao na kukesha watu wanapolala ndio kitoweo chao, na ufukara na ulofa ndio alama yao. Umasikini na haya ndio shuka yao, wamefunga farasi wa azima yao kwenye mlango wa Mola wao, wamekunjua nyuso zao kwenye mihirabu za minong'ono yao.

Ufukara upo wa aina mbili wa jumla na mahususi, wa jumla ni kumhitajia Allah Taalaa, na huu ni wasifu wa kila kiumbe muumini na kafiri, na hii ni maana ya Kauli Yake Taalaa:

﴿ يَا أَيُّهَا النَّاسُ أَنْتُمُ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّهِ <sup>ط</sup> ﴾

***"Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu."***  
...(35:15)

Ulio mahususi ni wasifu wa mawalii wa Allah na vipenzi Vyake wameondoa mikono yao kwenye dunia, na wameondoa nyoyo zao kwenye kufungamana nayo.

Ewe Allah tuonjeshe utamu wa kuzungumza Nawe, na kutupitisha njia ya Radhi Zako, na tukatie sisi kila chenye kutuweka mbali na Hadhara Yako, na tufanyiye wepesi uliowafanyia wepesi watu wa Upendo Wako, na tusamehe sisi na wazee wetu na waislam wote.

\*\*\*

**DHAMBIB KUBWA YA HAMSINI NA TANO**

**KUBURUZA KIKOI, MAVAZI NA SURUALI KWA  
KUJITUKUZA , KUJIONA, KUJIFAKHIRI NA MARINGO**

Allah Mtukuka Anasema:

وَلَا تَمْشِي فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٣١﴾

**"Wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu Hampendi kila anaye jivuna mwenye kujifakhirisha." (31:18)**

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« ما أسفل الكعبين من الإزار فهو في النار »

*"Kilicho (vuka) chini ya vifundo viwili kutokana na kikoi ni cha motoni."<sup>677</sup>*

Mtume ﷺ akasema:

« لا ينظر الله إلى من جر إزاره بطراً »

*"Allah hatamuangalia mwenye kuburuza kikoi chake kwa kiburi"<sup>678</sup>*

Mtume ﷺ akasema,

« ثلاثة لا يكلمهم الله يوم القيامة ولا ينظر إليهم ولا يزكّيهم ولهم »

*"(Watu) watatu Allah hatawaangalia Siku ya kiyama wala hatawatakasa, na wao wana adhabu kali; anayeburuza nguo yake, anayesimbulia, na anayeenza bidhaa zake huku akiapa yamini ya uongo."<sup>679</sup>*

---

<sup>677</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>678</sup> Sahihi: Bukhari 5788; Muslim 2087

<sup>679</sup> Maelezo yake yametangulia

Katika hadithi nyingine.

« بينما رجل يمشي في حلة تعجبه نفسه مرجل رأسه يخال في مشيه  
إذ خسف الله به الأرض فهو يتجلجل فيها إلى يوم القيامة »

*“Wakati mtu mmoja alikuwa akitembea katika mapambo na nafsi yake ikimvutia anaranga katika mwendo wake. Allah akamzamisha ardhini, na yeye anadidimia humo hadi siku ya kiyama.”<sup>680</sup>.*

Akasema ﷺ:

« من جر ثوبه خيلاء لم ينظر الله إليه يوم القيامة »

*“Mwenye kuburuza nguo yake kwa majivuno Allah hatamuangalia siku ya kiama”<sup>681</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

« الإسبال في الإزار والعمامة من جر شيئاً منها خيلاء لم ينظر الله إليه يوم  
القيامة »

*“Kuburuza ni katika kikoi na kilemba, na mwenye kuburuza chochote katika hivyo Allah Hatamuangalia siku ya kiama”<sup>682</sup>.*

Mtume ﷺ amesema:

« إزره المؤمن إلى نصف ساقه ولا حرج عليه فيما بينه وبين الكعبين وما كان  
أسفل من الكعبين فهو في النار »

*“Kikoi cha muumini ni nusu ya miguu yake, wala hapana makosa kilicho baina yake na fundo mbili, na kilicho chini ya fundo mbili ni katika moto”<sup>683</sup>.*

---

<sup>680</sup> Sahihi: Bukhari 5789, Muslim 2088

<sup>681</sup> Sahihi: Bukhari 5791, Muslim 2085

<sup>682</sup> Sahihi: Abu Dawud 4094, Ibn Maajah 3576, Swahihil Jaami i770

<sup>683</sup> Sahihi: Ahmad 3/136, Al-Bukhari 3665, 5784 na Muslim 2085

## Al - Kabair

---

Hili linaenea katika suruali, joho, juba, na mavazi mengine, Tunamuomba Allah uzima.

Abu Hurairah رضي الله عنه amesema: “Wakati mtu mmoja akiswali huku anaburuza kikoi chake, Mtume ﷺ alimwambia;

« اذهب فتوضاً »

“Nenda katawadhe”.

Mtu mmoja akamwambia Mtume ﷺ: “Ewe Mtume wa Allah ana nini umemwambia atawadhe!” Kisha akamnyamazia, akasema:

« إنه كان يصلي وهو مسبل إزاره ، ولا يقبل الله صلاة رجل مسبلاً إزاره »

“Hakika alikuwa anaswali na huku anaburuza kikoi chake, wala Allah Hakubali Swala ya mwenye kuburuza kikoi”<sup>684</sup>.

Mtume ﷺ aliposema:

« من جر ثوبه خيلاء لم ينظر الله إليه يوم القيامة »

“Mwenye kuburuza nguo yake kwa majivuno Allah hatamuangalia siku ya kiama”

Abu Bakr alisema: “Ewe Mjumbe wa Allah kikoi changu kinashuka hadi nikilinde”. Mtume ﷺ akamwambia:

« إنك لست ممن يفعل خيلاء »

“Wewe si miongoni mwa wanaoburuza kwa kiburi.”<sup>685</sup>

Ewe Allah Amiliana nasi kwa Upole Wako Mwema Ulio Mzuri, kwa Rehema Yako Ewe Mrehemevu zaidi kushinda wote.

---

<sup>684</sup> Dhaifu: Abu Dawud 638, 4086; Ameidhoofisha sheikh katika Dhaiifil Jaami'i 124

<sup>685</sup> Sahihi: Imepokewana Ahmad 2/136; Bukhari 3665, 5784; Muslim 2085

## DHAMBI KUBWA YA HAMSINI NA SITA

### KUVAH HARIRI NA DHAHABU SI KWA WANAUME

Katika Sahihi mbili Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

وقال النبي ﷺ: «مَنْ لَبَسَ الْحَرِيرَ فِي الدُّنْيَا لَمْ يَلْبَسْهُ فِي الْآخِرَةِ

*“Mwenye kuvaa hariri katika dunia hataivaa akhera”<sup>686</sup>.*

Hili linawaenea watu wote. Kwa kauli yake ﷺ:

وقال ﷺ: «حُرِّمَ لِبَاسُ الذَّهَبِ وَالْحَرِيرِ عَلَى ذَكَورِ أُمَّتِي، وَأُجِلَّ لِإِنَائِهِمْ»<sup>(٥)</sup> صححه الترمذي.

*“Imeharamishwa kuvaa hariri na dhahabu juu ya wanaume wa uma wangu”<sup>687</sup>*

Hudhaifa bin Yamaan amesema: Mjumbe wa Allah ﷺ ametukataza kunywa na kula katika vyombo vya dhahabu na fedha, na kuvaa hariri na dibaji, na kukaa juu yake au nguo yoyote iliyotarazwa kwa hariri.” Bukhari<sup>688</sup>

Kwa hiyo mwenye kuhalalisha kuvaa hariri kwa wanaume huyo ni kafiri. Mtume ﷺ ameruhusu tu kwa mwenye kuwashwa au upele na mengineyo<sup>689</sup>, na wapiganaji wakati wa kukutana na adui. Ama kuvaa hariri kwa mapambo hiyo inakuwa haramu kwa ijimai ya waislamu. Ni sawasawa ikiwa shati, kashida, joho au nguo yoyote nyingine ikiwa hariri ni nyingi inakuwa haramu. Pia kuvaa dhahabu ni haramu kwa wanaume,

---

<sup>686</sup> Sahihi: Bukhari 5832 Muslim 2073

<sup>687</sup> Sahihi: Ahmad 4/396 Tirmidhi 1720 Ibn Maajah 3595 An-Nasaai 16/8 Shaykh ameisahihisha katika Al Irwaa 277 Ghaayatul Maraam 77

<sup>688</sup> Sahihi: Bukhari 5837 Muslim 2067

<sup>689</sup> Sahihi: Ahmad 3/255, 272, Bukhari 2921, 2922 na Muslim 2076

## Al - Kabair

---

ni sawasawa iwe pete au kidani, au mkwiji wa upanga, ni haramu kuvaa na kuitumia. 'Mjumbe wa Allah ﷻ aliona katika kidole cha mtu mmoja pete ya dhahabu akaivua na akasema:

*"Hivi mmoja wenu anakusudia kaa la moto na kuliweka katika kidole chake!"<sup>690</sup>*

Hali kadhalika uvaaji wa nguo zilizodariziwa na nyuzi za dhahabu au zimenakishiwa na hariri imekatazwa kwa wanaume. Wanazuoni wametofautiana kuhusu ruhusa au katazo la uvaaji wa dhahabu au hariri kwa watoto wadogo. Baadhi yao walisema wanaruhusiwa wengine wanakataa kwa ujumla wa kauli yake Mtume ﷺ kuhusu hariri na dhahabu:

*"Hivi viwili ni haramu juu ya wanaume wa umati wangu na ni halali kwa wanawake wake".<sup>691</sup>*

Kwa hiyo akaingia na mtoto mdogo katika katazo hili. Haya ni madhehebu ya Imam Ahmad bin Hanbal رضى الله عنه na wengine. Tunamuomba Allah Taufiqi kwa yale Anayopenda na Kuyaridhia, hakika Yeye ni Mpaji na Mkarimu.

\*\*\*

---

<sup>690</sup> Sahihi: Muslim 2090

<sup>691</sup> Maelezo yake yametangulia

DHAMBI KUBWA YA HAMSINI NA SABA

UTORO WA MTUMWA

Muslim amepokea kutoka katika sahihi yake kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

قال النبي ﷺ: «إذا أبقَ العبدُ لم تُقبلْ له صلاةٌ»

*“Mtumwa akimtoroka (bwana wake) Swala yake haikubaliki.”<sup>692</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

وقال: «أَيُّمَا عَبْدٍ أَبَقَ فَقَدْ بَرَّتْ مِنْهُ الذُّمَّةُ»

*“Mtumwa yoyote akitoroka dhimma inajitenga nae.” (Muslim: 69)*

Jabir bin ‘Abdullah amesema kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

وروى ابن خزيمة في «صحيحه»، من حديث جابر [رضي الله عنه] قال: قال رسول الله ﷺ: «ثَلَاثَةٌ لَا يَقْبَلُ اللَّهُ لَهُمْ صَلَاةً، وَلَا تَصْعَدُ لَهُمْ حَسَنَةٌ: الْعَبْدُ الْأَبْقُ حَتَّى يَرْجِعَ إِلَى مَوَالِيهِ<sup>(1)</sup>، وَالْمَرْأَةُ السَّاخِطُ عَلَيْهَا زَوْجُهَا حَتَّى يَرْضَى، وَالسُّكْرَانُ حَتَّى يَصْحَوْ»

*“Watu wa aina tatu. ambao Swala zao hazikubaliki na matendo yao mema hayatopanda mbinguni: mtumwa aliyekimbia hadi arudi kwa bwana wake, mke aliyekasirikiwa na mumewe hadi amridhie, na mlevi hadi azinduke, (Ulevi uishe).”<sup>693</sup>*

Fudhalah ibn ‘Ubaid رضي الله عنه anasema, Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

---

<sup>692</sup> Sahihi: Muslim 70; Abu Dawud 360

<sup>693</sup> Maelezo yake yametangulia

وفي «المستدرک» علی شرط الشيخین<sup>(٥)</sup> من حدیث فضالة بن عبيد  
مرفوعاً: «ثلاثة لا تُسأل عنهم<sup>(٦)</sup>: رجلٌ فارق..  
الجماعة<sup>(١)</sup> وعصى إمامه ومات عاصياً، وعبد أيسق [فمات]<sup>(٢)</sup>، وامرأة غاب عنها  
زوجها<sup>(٣)</sup> [وقد]<sup>(٤)</sup> كفأها المؤمنة<sup>(٤)</sup> فتبرجت<sup>(٥)</sup>».

*“Watu watatu (Allah) Hatawaulizia: mtu anayejitenga na jamaa,  
na akamuasi kiongozi wake, mtumwa aliyetoroka na akafa hali ya  
kuasi, na mwanamke ambaye mume wake yuko mbali nae akatoka  
hovyo baada yake.”<sup>694</sup>*

Yaani amedhihirisha uzuri wake kama wale wanawake waliokuwa wakifanya wakati wa jahilia, na muda huo ulikuwa ni wakati wa baina ya Nabii Issa na Mtume ﷺ. Hili amelitaja Waahidi رضي الله عنه.

\*\*\*

---

<sup>694</sup> Sahihi: Ahmad 6/19; Bukhari katika Al Adabul Mufradi 590; Al Baani ameisahihisha katika *Silsilah as Swahiihah* 542



**DHAMBI KUBWA YA HAMSINI NA NANE**

**KUCHINJA KWA AJILI YA ASIYEKUWA  
ALLAH 'AZZA WA JALLA**

Mfano wa anayesema: *Bismi shaytwaan*, kwa jina la shetani, au kwa jina la sanamu, au kwa jina la Shaykh fulani. Allah Amesema:

وَلَا تَأْكُلُوا مِمَّا لَمْ يُذْكَرِ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ

**“Wala msile katika visivyotajwa jina la Allah juu yake.”  
(6:121)**

Ibn Abbaas amesema anamaanisha nyamafu na aliye kufa kwa kusongwa koo, hadi Kauli Yake Taalaa:

وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصَبِ

**“...aliye chinjiwa masanamu...”.**

Al Kalbi amesema: Ambacho hakijatajiwa Jina la Allah juu yake, 'Atwaa amesema: Anakataza vichinjwa walivyokuwa wakichinja makureishi na waarabu juu ya masanamu. Na Kauli Yake,

وَأِنَّهُ لَفِسْقٌ

**“Hayo yote ni upotovu”.**

Yaani: ikiwa ambacho hakikutajwa jina la Allah miongoni mwa maiti ni upotofu au kutoka katika haki na dini.

وَإِنَّ الشَّيْطَانَ لِيُوحِيَ إِلَىٰ آوَالِيهِمْ لِيُجْنِدُوا لَكُمْ

**“Na kwa yakini mashet’ani wanawafunza marafiki zao  
kubishana nanyi.” (6:121).**

Yaani: Shetani anawatia wasiwasi rafiki zake kwa hiyo anatia katika moyo wake mjadala wa batili. Na hapa ni kuwa washirikina wamejadiliana na waumini kuhusu nyamafu. Ibn Abbaas amesema: "Shetani anawafunulia rafiki zake katika wanadamu; vipi nyie hamli alichokiua Allah na hali ya kuwa mnakula mlichokiua wenyewe? Allah Akateremsha aya hii:

وَإِنْ أَطَعْتُمُوهُمْ

**"Na mkiwafuata"**

Yaani: katika kuhalalisha nyamafu,

إِنَّكُمْ لَشُرْكُونَ

**"..hakika nyinyi mtakuwa washirikina".**

Az-Zajjaaj anasema: "Katika hili kuna ushahidi kuwa mwenye kuhalalisha kilicho haramishwa na Allah, na kuharamisha Alichohalalisha Allah basi huyo ni mshirikina".

Kama ikisemwa: Vipi mnahalalisha kichinjwa cha Muislamu anapoacha *bismillaahi* na katika aya ni kama andiko la kuharamisha?. Nimesema: "Kwa hakika wafasiri wamefasiri:

مِمَّا لَمْ يَذْكُرْ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ

**"katika wale wasio somewa Jina la Mwenyezi Mungu",**

Katika aya hii kuwa ni maiti na hapana yeyote aliyechukulia kuwa ni kilichochinjwa na Muislam ambaye ameacha *Bismillaahi*. Na katika aya hii kuna mambo yanayoonyesha kuwa ni kuharamisha nyamafu, kama vile:

وَإِنَّهُمْ لَفِئْسَةٌ

**"Hayo yote ni upotovu".**

## Al - Kabair

---

Hapotoki mtu kwa kula nyama ya Muislamu aliyechinjwa bila kumtaja Allah. Na Kauli Yake:

وَإِنَّ الشَّيْطَانَ لَيُوحِيَنَّ إِلَىٰ أَوْلِيَآئِهِمْ لِيُجَدِّدُوا لَكُمْ

**“Na kwa yakini mashet’ani wanawafunza marafiki zao kubishana nanyi”.**

Na mjadala hapa ulikuwa juu ya maiti kwa makubaliano ya wafasiri wote, si kuhusu kuchinja kwa Muislamu aliyeacha kutaja Jina la Allah.

Na Kauli Yake Ta’alaa:

وَإِنْ أَطَعْتُمُوهُمْ إِنَّكُمْ لَمُشْرِكُونَ

**“Na mkiwafuata basi hapana shaka nyinyi mtakuwa washirikina”.**

Na ushirikina ni katika kuhalalisha nyamafu si katika kuhalalisha kilichochinjwa bila kutajwa Jina la Allah juu yake.

Abu Mansuur amepokea kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kuwa mtu alimuuliza Mjumbe wa Allah ﷺ: “Unaonaje mtu katika sisi anachinja na anasahau kutaja Jina la Allah Aliyetukuka, akasema:

«اسم الله على فم كل مسلم»

*“Jina la Allah lipo katika mdomo wa kila Muislam”<sup>695</sup>.*

Abu Mansuur amepokea kutoka kwa Ibn Abbaas kuwa Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>695</sup> Maudhuu: Ibn Adiy 6/395; Daaraqutni 4/275/94; Twabarani katika Al-Awsat 4769. Al Baani amesema; Ni hadithi maudhuu yaani iliyozushwa na ameiweka katika Dhaiifil Jaami’i 955

« يكفيه اسمه وإن نسي يسمي حين يذبح فليسم ويذكر الله ثم ليأكل »

*“Inamtosha mtu akisahau bismillaahi wakati anapochinja basi na apige bismillaahi na amtaje Allah anapokula kisha ale”.*<sup>696</sup>

Amru bin Abu Amr amepokea kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kuwa kuna watu walimuambia Mtume ﷺ: “Ewe Mjumbe wa Allah watu wanatuletea nyama na hatujui kama limetajwa Jina la Allah juu yake au la?” Mtume ﷺ akasema:

« سموا عليه وكلوا »

*“Tajeni Jina la Allah juu yake kisha kuleni”*<sup>697</sup>

Huu ndio mwisho wa kauli ya Al-Waahidi رضي الله عنه na imekwisha tangulia kauli yake Mtume ﷺ:

« لعن الله من ذبح لغير الله »

*“Allah Amemlani mwenye kuchinja kwa asiye kuwa Allah”*<sup>698</sup>.

\*\*\*

---

<sup>696</sup> Sahihi Mawqaf: Daaraqutni 4/296, 96, 98 na Bayhaqi 9/239.

<sup>697</sup> Sahihi: Malik 2/488/1; Bukhari 5507

<sup>698</sup> Maelezo yake yametangulia

**DHAMBI KUBWA YA HAMSINI NA TISA**

**MWENYE KUJIITA JINA LISILO LA BABA YAKE  
ILHALI ANAJUA**

Sa'ad bin Abi Waqqas anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« من ادعى إلى غير أبيه وهو يعلم أنه غير أبيه فالجنة عليه حرام »

*"Ikiwa mtu kwa makusudi akajipachika jina lisilo la baba yake naye anajua si baba yake basi ni haramu kwake pepo." (Bukhari)<sup>699</sup>*

Abu Huraira رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema

« لا ترغبوا عن آبائكم فمن رغب عن أبيه فهو كافر »

*"Msiwachukie baba zenu mwenye kumchukia baba yake basi huyo ni kafiri". (Bukhari)<sup>700</sup>*

Vile vile kuna,

« من ادعى إلى غير أبيه فعليه لعنة الله »

*"Anayejiiita jina lisilo la baba yake ana laana ya Allah."<sup>701</sup>*

Zaid bin Sharik amesema: Nilimuona Ali رضي الله عنه akihutubu katika minbari nikamsikia akisema: Wallah hatuna katika kitabu tunachosoma isipokuwa ni kitabu cha Allah na kilichomo katika sahifa hii akakunjua, ndani yake kuna meno ya ngamia na kitu katika jeraha. Vile vile ndani yake Mtume amesema:

---

<sup>699</sup> Sahihi: Bukhari 6767; Muslim 63

<sup>700</sup> Sahihi: Bukhari 6767 Muslim 62

<sup>701</sup> Sahihi: Muslim 1370

« المدينة حرام ما بين عير إلى ثور ، فمن أحدث فيها حدثاً ، أو أوى محدثاً فعليه لعنة الله والملائكة والناس أجمعين. لا يقبل الله يوم القيامة منه صرفاً ولا عدلاً. ومن تولى غير مواليه فعليه مثل ذلك ، وذمة المسلمين واحدة »

*“Madina ni haramu baina ya ngamia na ng’ombe, atakayezua ndani yake basi amezua, na atakayemhifadhi aliyezua basi juu yake laana ya Allah na Malaika na watu wote, Allah hakubali siku ya kiama chochote katika Swala zake za faradhi wala za Sunna, na atakayetawalia asiye kuwa Mawali wake basi juu yake mfano wa hayo, na dhima ya Waislamu ni moja.” Imepokewa na Al-Bukhari.<sup>702</sup>*

Abu Dharr anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« ليس منا رجل ادعى إلى غير أبيه وهو يعلمه إلا كفر ، ومن ادعى ما ليس له فليس منا وليتبوأ مقعده من النار ، ومن دعا رجلاً بالكفر أو قال يا عدو الله وليس كذلك إلا حار عليه »

*“Mtu yeyote kwa makusudi akajinasibu kwa jina si la baba yake atakuwa amekufuru, na mtu anayedai kitu chochote ambacho si chake basi anachukua nafasi ya motoni, na ikiwa mtu yeyote akimtuhumu au akimshitaki na kusema ewe adui wa Allah na wakati huyo anayetuhumiwa hayuko hivyo itamrudia yeye (anayemshitaki).”<sup>703</sup>*

\*\*\*

---

<sup>702</sup> Sahihi: Imepokewa na Al-Bukhari 1870, 6755 na Muslim 1370.

<sup>703</sup> Sahihi: Bukhari 6045; Muslim 61

## DHAMBI KUBWA YA SITINI

### KUBISHANA NA KUSHINDANA KWA HASIRA

Allah Mtukuka Anasema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُعْجِبُكَ قَوْلُهُ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيُشْهَدُ اللَّهُ عَلَىٰ مَا فِي قَلْبِهِ وَهُوَ أَلَدُّ

الْخِصَامِ ﴿٢٠٤﴾

***"Na katika watu yupo yule ambaye maneno yake kwa maisha ya kidunia hukufurahisha; naye humshuhudisha Mwenyezi Mungu kwa yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye ndiye mkubwa wa ukhasimu." (2:204)***

Miongoni mwa maneno yanayo shutumiwa ni ya mizozo, mabishano, mijadala, na magomvi.

Imamu Hujjatul Islamu Al-Ghazali amesema: Ubishani ni kumkosa mwenzako kwa ajili ya kuonyesha makosa yake bila lengo lolote isipokuwa kumdhalilisha msemaji wake na kuonyesha hadhi yako juu yake. Ama mjadala ni jambo linalohusiana na kudhihirisha madhehebu na kuyathibitisha.' Akasema: 'Uteshi ni majivuno katika mazungumzo ili kufikia makusudio katika mali au jambo jingine.' Haya ni maneno ya Ghazali.<sup>704</sup>

Imam Nawawi anasema, 'Ubishani unaweza kuwa wa haki na unaweza kuwa wa batili.' Allah Anasema:

﴿ وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ﴾

***"Wala msijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa." (29:46)***

---

<sup>704</sup> Al Ihyaa: 3/261

## Al - Kabair

---

Akasema:

وَجَدِلْتَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ هِيَ أَحْسَنُ

**"...Na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora..." (16:125)**

Allah Akasema tena:

مَا تُجَادِلُ فِي آيَاتِ اللَّهِ إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا

**"Hawazibishi Ishara za Mwenyezi Mungu ila walio kufuru." (40:4)**

Amesema: ikiwa mabishano yanayofanyika yatakuwa juu ya kusimamia haki, maelezo yake basi yanastahili kusifiwa. Lakini yakiwa dhidi ya ukweli au ikiwa ubishi usio na elimu basi unastahiki lawama.

Kwa ufafanuzi huu yameshuka maandiko katika kuhalilisha kwake. Mmoja wao amesema: "Sijaona kitu chenye kuondoa dini wala chenye kupunguza murua wala chenye kushughulisha moyo kuliko utesi."

Ikiwa utasema: Mtu hana budi kugombana ili kulinda haki yake. (Jawabu) Ni alilojibu Imam al Ghazali: "Jua kuwa lawama inayosisitizwa ni ya anayegombana kwa batili na bila elimu. Kama vile wakili wa kadhi kwani anawakilisha katika utesi kabla ya kujua haki iko katika upande gani, kwa hiyo anahasimiana bila elimu.

Anaingia lawamani pia anayetafuta haki yake kwani hapunguzi kadiri ya haja, bali anadhihirisha ubishi, uongo, maudhi na usaliti kwa mgomvi wake. Kadhalika mwenye kuchanganya ugomvi na maneno ya maudhi yasiyo na haja katika kupata haki yake. Kadhalika mwenye kupeleka ujeuri ili kumteza nguvu hasimu na kumvunja. Huyu ni mwenye kulaumiwa. Ama mdhulumiwa anayetetea hoja yake kwa njia ya kisheria bila ugomvi wala israfu wala kuzidisha ubishi bila ya haja pasina kukusudia inda wala maudhi, kufanya hivyo si haramu. Lakini bora kuacha hilo inapopatikana namna, kwa kuwa kuzuia ulimi katika ugomvi



## Al- Kabair

---

juu ya adhabu kumeruhusiwa. Ugomvi husonga kifua na kuamsha hasira. Ikiamka hasira hupatikana husuda ndani yake mpaka kila mmoja wao hufurahia kufikwa mabaya kwa mwingine na anahuzunika kwa furaha yake na ulimi wake unaingilia hadhi yake. Mwenye kugombana, basi ameyaingia maovu haya.

Machache yaliyomo humo ni kushughulisha moyo hata akiwa ndani ya Swala yake. Akili yake imefungamana na hoja na uhasama na hali yake hainyooki. Uhasama ndio chanzo cha shari, kadhalika ubishi na kushindana. Mwanadamu anatakikana asijifungulie mlango wa ugomvi isipokuwa kwa dharura isiyona budi. Tumesimuliwa katika kitabu cha Tirmidhi kutoka kwa Ibn 'Abass kuwa, Mtume ﷺ amesema:

« كفى بك إثماً أن لا تزال مخاصماً »

*"Inatosha kwako kuwa ni dhambi kwa kutoacha kugombana"*<sup>705</sup>.

Imekuja kutoka kwa Ali رضي الله عنه amesema: "Hakika utesi ni maangamivu".

## FASILI

Abu Hurairah رضي الله عنه amesema:

*"Mwenye kujadiliana katika ugomvi bila elimu haachi kuwa katika hasira za Allah hadi ajitoe."*<sup>706</sup>

Na kutoka kwa Abu Umaamah kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

*"Watu hawatapotea baada ya uongofu waliokuwa juu yake, isipokuwa watapewa kubishana."*

---

<sup>705</sup> Dhaifu: Tirmidhi 1994 Twabarani 11032 Baihaqi katika Ash Shi'ib 8432,

<sup>706</sup> Dhaifu: Ameipokea Ibn Abi Duniya katika Sahihi yake 153, katika Al Ghaibah 14 na hiyo ni dhaifu. Dhaiful Jaami'i 5551

## Al - Kabair

---

Kisha akasoma:

مَا ضَرَبْتُمْ لَكُمْ إِلَّا جَدَلًا

*“Hawakukupigia wewe isipokuwa ni mjadala”.*<sup>707</sup>

Akasema:

*“Hofu kubwa ninayoihofia kwenu ni makosa ya mwanachuoni na ubishi wa mnafiki katika Qur`aan na dunia inakata shingo zenu basi ituhumuni katika nafsi zenu”.* Imepokewa na Ibn ‘Umar<sup>708</sup>

Na Mtume ﷺ amesema:

المراء في القرآن كفر

*“Ubishani kuhusu Qur`an ni ukafiri”*<sup>709</sup>

## FASILI

Ni karaha kubadilisha maneno kwa mbwembwe, na kulazimisha kupanga maneno kwa mizani ili kuonesha ufasaha, kwenye utangulizi (Dibaji) waliouzozea umbuji wa kujilazimisha ni katika takilifu zilizo katazwa. Bali inatakiwa akusudie katika kusema kwake tamshi atakalofahamu wazi wazi wala hataliona zito. Tunasimuliwa katika kitabu cha Tirmidhi kuwa ‘Abdullah bin ‘Amri binil Aas رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« إن الله يبغض البليغ من الرجال الذي يتخلل بلسانه كما تتخلل البقرة »

---

<sup>707</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 5/552, At-Tirmidhi 3253, Ibn Majah 48 na Al-Bani amesema in sahihi na ameiweka katika sahihi Al-Jami' 5633.

<sup>708</sup> Dhaifu: Imepokewa na Al-Baihaqi katika Ash-Shi'ab 10311, 10313 na isnadi yake ni dhaifu.

<sup>79</sup> Sahihi: Imepokewa na Ahmad 2/286, 300, Abu Dawud 4603 sahihi Al-Jami' 6687.

## Al - Kabair

---

*“Allah anamchukia mwenye umbuji miongoni mwa watu ambaye anazungusha ulimi kama anavyozungusha ng`ombe”<sup>710</sup>.*

Jaabir رضي الله عنه anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

« إن من أحبكم إلي وأقربكم مني مجلسا يوم القيامة أحاسنكم أخلاقا ،  
وإن أبغضكم إلي وأبعدكم مني مجلسا يوم القيامة الثرثارون والمتشدقون  
والمتفبهتون. »

*“Hakika mpendwa wenu zaidi kwangu na mkaribu wenu zaidi kwangu wa kikao siku ya kiama ni mzuri wenu zaidi wa tabia, na hakika mchukivu wenu zaidi kwangu, na mbali wenu zaidi kwangu kwa kikao siku ya kiama ni domo kaya, na wenye kiburi.”*

Watu wakamuuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah sisi tunafahamu maana ya wanaozungumza sana na wenye midomo mirefu, lakini nini maana ya kubwabwaja?”

Mtume ﷺ alijibu: « المتكبرون »

“Wenye kiburi”.

Tirmidhi: Amesema: Hadithi Hasan<sup>711</sup>

Tambua kuwa haingii katika katazo hili kutengeneza vizuri matamshi ya khutuba, na mawaidha, kukiwa hakutakuwa na kupitiliza mpaka ugeni wa maneno, isipokuwa ikiwa makusudio ni kuhamasisha nyoyo katika kumtii Allah Taalaa. Na uzuri wa maneno kuna athari ya wazi katika hili. *Waallaahu A`alam.*

\*\*\*

---

<sup>710</sup> Sahihi: Ahmad 2/165,187; Abu Dawud 5005; Tirmidhi 853; Sahihah 878.

<sup>711</sup> Hasan: Tirmidhi 2018; Shaykh ameifanya hasan katika sahihil Jaami`i 2201; Sahihah 791

## DHAMBI KUBWA YA SITINI NA MOJA

### KUZUIA MAJI YA ZIADA

Allah Mtukuka Anasema:

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَصْبَحَ مَاؤُكُمْ غَوْرًا فَمَنْ يَأْتِيكُمْ بِمَاءٍ مَّعِينٍ ﴿٦٧﴾

**"Sema: Mwaonaje, yakiwa maji yenu yamedidimia chini, nani atakuleteni maji yanayo miminika?" (67:30)**

Mjumbe wa Allah ﷻ anasema:

« لا تمنعوا فضل الماء لتمنعوا به الكلاً »

*"Msizuie ziada ya maji ili mzuie nayo majani"<sup>712</sup>.*

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« من منع فضل مائه وفضل كلئه منعه الله فضله يوم القيامة »

*"Mwenye kuzuia ziada ya maji yake au majani yake, Allah Atazuia ziada yake siku ya kiama"<sup>713</sup>.*

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« ثلاثة لا يكلمهم الله ولا ينظر إليهم يوم القيامة ولا يزكّيهم ولهم عذاب أليم : رجل على فضل ماء بفلاة يمنعه ابن السبيل ، ورجل بايع إماماً لا يبايعه إلا للدنيا فإن أعطاه منها وفي له وإن لم يعطه منها لم يف له ، ورجل بايع رجلاً بسبعة بعد العصر فحلف له بالله لأخذتها بكذا وكذا فصدقه وهو على غير ذلك »

---

<sup>712</sup> Sahihi: Bukhari 2353; Muslim 1566

<sup>713</sup> Sahihi: Ahmad 2/179,221 ameisahihisha Al Baani katika Silsilah Swahiihah 1422

*“Watatu Allah Hatawasemesha wala Hatawaangalia siku ya kiama wala Hatawatakasa na wao wana adhabu kali, mtu ana maji ya ziada jangwani na anamnyima mpita njia, na mtu amembai kiongozi, hakumbai isipokuwa kwa ajili ya dunia, pindi akimpa kitu basi anamtekelezea (utii), asipompa hamtekelezei, na mtu amemuuzia mtu biashara baada ya alasiri akamuapia kwa Allah: ‘Nitaichukua kwa kadha kadha, kwa hiyo yeye akamswadikisha naye yu ghairi ya hivyo.’”*

Wameipokea katika sahihi mbili, na katika Bukhari amezidisha:

« ورجل منع فضل مائه فيقول الله اليوم أمنعك فضلي كما منعت فضل ما لم تعمل يداك »

*“Na mtu aliyezuia ziada ya maji yake, na Allah atasema: Nitakuzuia ziada yangu kama wewe ulivyozuia ziada isiyefanywa na mikono yako”<sup>714</sup>.*

\*\*\*

---

<sup>714</sup> Sahihi: Bukhari 2358 Muslim 108

**DHAMBI KUBWA YA SITINI NA MBILI**

**KUPUNGUZA KILO, MAZAO NA MFANO WAKE**

Allah Mtukuka Anasema:

وَبَلِّغْ لِلْمُطَفِّينَ ﴿١١﴾

**“Ole wao hao wapunjao” (83:1)**

Yaani: Ambao wanapunguzia watu na wanawapunja haki zao katika vipimo na mizani. Kauli Yake Taalaa:

الَّذِينَ إِذَا أَكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ ﴿١٢﴾

**“Ambao wanapojipimia kwa watu hudai watimiziwe.” (83:12)**

Yaani: ‘Wanajitimizia haki zao kwao.’ Az-Zajjaaj amesema: ‘Maana ya wanapojipimia kwa watu wanatimiza.’

وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿١٣﴾

**“Na wao wanapo wapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza.”** Yaani wanapunguza kilo na uzani.

Suddi anasema, “Mjumbe wa Allah ﷺ Alipokwenda Madina palikuweco mtu mmoja anaitwa Abu Juhaynah alikuwa na vipimo viwili (vya nafaka) anapimia watu kwa kingine na anajipimia kwa kingine.” Allah Akashusha Aya hii.<sup>715</sup>

وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿١٣﴾

**“Na wao wanapo wapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza”.** Yaani: Wanapunguza katika kilo na mizani.

---

<sup>715</sup> Asbaabun Nuzuul cha Al-Waahidi 909; Zaadul Maasiir 9/52

## Al - Kabair

---

Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« خمس بخمس »

“Tano kwa tano”.

Wakasema: “Ni nini tano kwa tano ewe Mtume wa Allah ﷻ”.  
Mtume ﷺ akasema:

« ما نقض قوم العهد إلا سلط الله عليهم عدوهم ، وما حكموا  
بغير ما أنزل الله إلا فشا فيهم الفقر ، وما ظهرت الفاحشة إلا أنزل  
الله بهم الطاعون ( يعني كثرة الموت ) ، ولا طففوا الكيل إلا  
منعوا نبات وأخذوا بالسنين ولا منعوا الزكاة إلا حبس الله عنهم  
المطر »

*“Watu hawapunguzi ahadi isipokuwa Allah Atawasalitishia adui wao, na hawahukumu kwa asichokiteremsha Allah isipokuwa kutaenea kwao ufukara, na hakukudhihirika uchafu isipokuwa Allah Atawateremsha Tauni, (yaani: wingi wa mauti) na hawakupunguza kipimo isipokuwa watanyimwa mazao, na wataletewa ukame, na hawakuzuia Zaka isipokuwa Allah Atawafungia mvua.”<sup>716</sup>*

أَلَا يَظُنُّ أُولَئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ ﴿٤٠٧﴾

**“Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa”**

Az-Zajjaaj anasema: “Maana yake ni kuwa lau wangedhania kuwa wao watafufuliwa wasingepunguza katika vipimo na mizani.”,

لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٤٠٨﴾

**“Katika Siku iliyo kuu”, Yaani: Siku ya kiama:**

---

<sup>716</sup> Tushaizungumzia hapo 715

يَوْمَ يَقُومُ النَّاسُ

**“Siku watakayo simama watu,**

Kutoka kwenye makaburi yao,

لِرَبِّ الْعَالَمِينَ

**“Kwa ajili ya Mola wa walimwengu”.**

Yaani: Kwa Amri Yake malipo na hesabu, na wao watasimama mbele yake kwa upambanuzi wa hukumu.

Malik bin Dinar رَضِيَ اللهُ عَنْهُ anasema: niliingia kwa jirani yangu aliyeshukiwa na mauti huku anasema: “Milima miwili ya moto! milima miwili ya moto!”. Nikauliza: “Unasema nini?” Akasema: “Ewe Abu Yahya (Yaani: Malik) Nilikuwa nina vipimo viwili napimia watu kwa kingine na najipimia kwa kingine”. Malik bin Dinar رَضِيَ اللهُ عَنْهُ akasema: “Nilisimamana nikavichukuwa vikombe hivyo na kupiga kimoja kwenye kingine ili vivunjike.” Akasema: “Ewe Abu Yahya, kila ukivigonga basi maumivu yanazidi kuwa makalii”, kwa hiyo alifariki kwa ugonjwa wake.

Na **‘mwenye kupunguza’**: huyo ni ambaye anapunguza kipimo na mizani, na ameitwa mwenye kupunguza kwa sababu anaiba kilichopunguzwa, na hiyo ni aina ya wizi, khiana na kula haramu. Allah Amemwahidi adhabu anayefanya hivyo.

Na imesemwa: ‘Ni bonde katika Jahannamu lau jabali la dunia likitiwa humo litayeyuka kwa ukali wa joto lake.’”

Baadhi ya Salafi wanasema: “Namshuhudia moto kila mpimaji kwa kilo au kwa mizani, kwani hakaribii kuokoka isipokuwa aliyehifadhiwa na Allah.”

Mmoja wao amesema: “Niliingia kwa mgonjwa anayekaribia kufa nikawa namtamkia shahada lakini kila akijaribu ulimi wake haukuweza kutamka



## Al- Kabair

---

alipata afueni kidogo nikamuuliza: “Ewe ndugu yangu kitu gani kilichozuia ulimi wako kutamka shahada nilipokulakinia?”. Akasema: “Ewe ndugu yangu! ulimi wa mizani umo juu ya ulimi wangu unanizulia kuitamka”. Nikasema: “Kwa Jina la Allah, kwani ulikuwa unawapimia watu kwa upungufu”. Akasema: “Wallah hapana, lakini nilikuwa kwa muda sijasimamia usahihi wa mizani yangu.’ Kwa hiyo hii ni hali ya ambaye hakagui usahihi wa mizani yake, sasa itakuwaje hali ya mwenye kupima kwa upungufu?!

Nafi (Mtumishi wa ‘Abdullah bin ‘Umar) anasema: Ibn ‘Umar alikuwa akipita kwa muuzaji akamwambia: “Muogope Allah na timiza kipimo kwani wanaodanganya watasimamishwa siku ya kiama hadi jasho litawameza masikioni mwao, kadhalika muuzaji atakapokaza mkono wake wakati wa kununua na atakapolegeza mkono wake katika (kupima kwa) dhiraa wakati wa kuuza.”

Baadhi ya Salafi wamesema: “Ole wake mwenye kuuza punje moja anayoitoa kwa upungufu, (Kwasababu hataiona pepo) pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, na ole wake mwenye kununua maangamivu kwa punje moja anayoichukua ziada”.

Tunamuomba Allah msamaha na atupe afya kutokana na kila balaa na majaribu, hakika Yeye ni Mpaji mkarimu.

\*\*\*

**DHAMBBI KUBWA YA SITINI NA TATU**

**KUJIAMINISHA NA VITIMBI VYA ALLAH**

Allah Mtukuka Anasema:

حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا أَخَذْنَاهُمْ بَغْتَةً ﴿٤٤﴾

**"...Mpaka walipo furahia yale waliyo pewa Tuliwashika kwa ghafla..." (6:44)**

Yaani: Adhabu Yetu iliwakamata kwa namna wasiyoitambua.

Al-Hasan amesema: 'Ambaye Allah Amemkunjulia na asione kuwa anafanyiwa vitimbi, basi huyo hana rai, na mwenye kupewa muda na asione kuwa yeye anaangaliwa hana rai, kisha akasoma aya hii:

حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا أَخَذْنَاهُمْ بَغْتَةً فَإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ ﴿٤٤﴾

**"...Mpaka walipo furahia yale waliyo pewa Tuliwashika kwa ghafla, na mara wakawa wenye kukata tama." (6:44)**

Amesema: Watu wamefanya vitimbi, na Mola wa Ka'aba Amewapa haja yao kisha Akaichukua, 'Uqbah bin 'Amir رضي الله عنه amesema:

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« إذا رأيت الله يعطي العبد ما يحب وهو مقيم على معصيته فإنما ذلك منه استدراج ثم قرأ: »

**"Mkiona Allah Amempa mja akipendacho na yeye amedumu juu ya maasi basi huko ndio kuvutwa kidogo kidogo, Kisha akasoma:**

فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ فَتَحْنَا عَلَيْهِمَ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ حَتَّى إِذَا فَرِحُوا  
بِمَا أُوتُوا أَخَذْنَاهُمْ بَغْتَةً فَإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ ﴿٤٤﴾

***“Basi walipo sahu waliyokumbushwa Tuliwafungulia milango ya kila kitu. Mpaka walipo furahia yale waliyo pewa Tuliwashika kwa ghafla, na mara wakawa wenye kukata tama.” (6:44)<sup>717</sup>.***

Ya kunusurika yanapofika maangamivu, Ibn ‘Abass رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ amesema: “Wamekata tamaa ya kheri zote.” Az-Zajaj amesema: “Mwenye kukata tamaa ni mwenye majuto sana na ni mwenye huzuni.”

Imepokewa katika athari: Ibilisi alipofanya vitimbi, wakati alikuwa miongoni mwa malaika, Jibrili na Mikail wakaanza kulia, Allah Akawauliza: “Mnalia nini?” Wakasema: “Ewe Mola wetu hatujiaminishi na Vitimbi Vyako”. Akasema:

« هَكَذَا كَوْنَا لَا تَأْمَنَّا مَكْرِي »

*“Kueni hivi hivi! msijiaminishe na Vitimbi Vyangu”<sup>718</sup>*

Mtume ﷺ mara nyingi alikuwa anasema:

« يَا مَقْلَبَ الْقُلُوبِ ثَبَّتْ قُلُوبَنَا عَلَى دِينِكَ »

*“Ewe Mpindujaji nyoyo thubutisha nyoyo zetu juu ya Dini Yako”.*

Kukasemwa: “Ewe Mjumbe wa Allah unahofia juu yetu?”. Akasema:

---

<sup>717</sup> Sahihi Ahmad 4/154; Twabarani 17/913; Al Awsat 9272; Shaykh ameisahihisha katika Silsilah Swahiihah 414

<sup>718</sup> Sijaiona

« إن القلوب بين إصبعين من أصابع الرحمن يقلبها كيف يشاء »

*“Hakika nyoyo ziko baina ya vidole viwili vya Ar Rahmaan Anazigeuza Atakavyo”.*<sup>719</sup>

Katika hadithi sahihi:

« إن الرجل ليعمل بعمل أهل الجنة حتى ما يكون بينه وبينها إلا ذراع فيسبق عليه الكتاب فيعمل بعمل أهل النار فيدخلها »

*“Hakika mtu atafanya amali ya watu na peponi hadi kusiwe baina yake na pepo isipokuwa dhira moja, kwa hiyo kitabu kitamtangulia atafanya matendo ya watu wa motoni na atauingia moto.”*<sup>720</sup>

Katika sahihi Bukhari kutoka kwa Sahl bin Sad as Sa’idi anatoa taarifa kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« إن الرجل ليعمل بعمل أهل النار وإنه من أهل الجنة ، ويعمل الرجل بعمل أهل الجنة وإنه من أهل النار ، وإنما الأعمال بالخواتيم »

*“Mtu atatenda matendo ya watu wa motoni lakini yeye ni mtu wa peponi, na mtu atatenda matendo ya watu wa peponi lakini yeye ni mtu wa motoni. Si vingine amali ni kwa mujibu wa matendo yake ya mwisho.”*<sup>721</sup>

## KISA

Allah Ameelezea kisa katika Kitabu Chake kitukufu kisa cha Bal ‘Aam na kuwa yeye alinyang’anywa imani baada ya elimu na maarifa<sup>722</sup>. Vilevile Birswiiswa - Mshika Ibada aliyekufa katika ukafiri.

---

<sup>719</sup> Sahihi: Tirmidhi 2140; Ibn Maajah 3834; Shaykh ameisahihisha katika Dhilaalul Jannah 225, na Takhrijul Iimaan; Ibn Abi Shaybah 7/55-58

<sup>720</sup> Sahihi: Bukhari 7454 Muslim 2643

<sup>721</sup> Sahihi: Bukhari 6607 Muslim 112

<sup>722</sup> Kisa hiki wamekieleza wafasiri wengi, kama vile Ibn Kathiiri na wengine rejea huko kama unataka.

## Al - Kabair

---

Imepokewa kuwa palikuwepo kijana mmoja wa Misri ambaye alikuwa akishikamana na msikiti kwa kuadhini na kuongoza Swala uso wake ulikuwa uking'ara na nuru ya imani na matendo mema. Siku mmoja kama kawaida yake akapanda mnara wa Msikiti ili aadhini, jirani ya Msikiti palikuwa na nyumba ya wakiristo akachungulia humo akamuona binti wa mwenye nyumba na alikuwa mzuri – akavutiwa naye basi akaacha adhana akamuendea. Yule binti akasema: “Una nini na unataka nini?” akasema: “Ninakutaka wewe”, Binti akamjibu: “Sitakujibu kwa mashaka”, Akasema: “Nitakuoa”, akamuambia: “Wewe ni Muislam na baba yangu hatoniozesha kwako.” Akasema “Nitakuwa mkristo”. Akasema: “Ukifanya nitafanya”. Akawa mkristo ili amuo, akaishi katika nyumba hiyo, basi ilipokuwa katikati ya siku hiyo alipanda dari la nyumba hiyo, akaanguka akafa, basi yeye hakufaulu kwa dini yake wala hakustarehe kwa kumuoa yule binti.<sup>724</sup>

Tunajilinda kwa Allah kutokana na Vitimbi Vyake, mwisho mbaya na kuhitimishwa vibaya.

Salim amesema kutoka kwa Abdillaah amesema: “Mara nyingi Mtume ﷺ alikuwa anaapa:

« لا ومقلب القلوب »

*“Hapana! Na ninaapa kwa mwenye kuzigeuza nyoyo.” Sahihi:  
Bukhari 7391; Abu Dawud 3262; Tirmidhi 1540*

Na maana yake ni kuwa anazisarifu haraka zaidi kuliko mapito ya upepo. Juu ya tofauti katika kukubali na kukataa, kukataa na kuchukia na sifa nyinginezo. Katika Uteremsho:

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ

***“...Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake...”(8:24)***

---

<sup>724</sup> Dhammil Hawaa cha Ibn Al Jawzi 348

Mujahidi anasema: "Inamaanisha kuwa anaingia baina ya mtu na akili yake, mpaka asijue vidole vyake vinachofanya,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى لِمَنْ كَانَ لَهُ

**"Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo."**  
...(50:37).

Yaani: Akili.

Tabari amechagua kuwa hiyo ni habari kutoka kwa Allah. Kuwa Yeye Anamiliki nyoyo za waja, na kuwa Anaingia kati baina yao na akili zao Anapotaka, mpaka hadiriki chochote isipokuwa kwa Matakwa Yake.

Aisha رضي الله عنها anatoa taarifa kuwa Mtume ﷺ mara nyingi alikuwa akisema:

« يا مقلب القلوب ثبت قلبي على طاعتك »

*"Ewe mgeuza nyoyo uthubutishe moyo wangu juu ya utiifu wako."*

Nikauliza: "Ewe Mjumbe wa Allah kwanini unazidisha kuomba hivyo? Je unaogopa?" Akasema:

« وما يؤمنني يا عائشة وقلوب العباد بين أصبعين من أصابع الرحمن يقلبها  
كيف أن يقلب قلب عبد قلبه »

*"Kipi kitakachoni aminisha na hali ya kuwa nyoyo za waja zipo baina ya vidole viwili vya Rahmaan Huzibadili Anavyotaka; Anapotaka kugeuza moyo wa mja Anaugeuza."*<sup>725</sup>

---

<sup>725</sup> Sahihi: Ahmad 6/91; Ibn Abi Aswim 224; Shaykh ameisahihisha katika Dhilaalil Jannah na Muslim akatoa mfano wake 2654

## Al- Kabair

---

Kwa hiyo ikiwa uongofu unajulikana na istiqama iko juu ya Matakwa Yake, na uzima uko mbali, na Kutaka - *Irada* Yake - haishindwi. Kwa hiyo usijivune kwa imani yako, amali yako, Swala yako, Saumu yako, na vikurubisho vyako vyote, ikiwa ni katika chumo lako kwa kuwa Mola Wako Muumba Amemfadhilisha juu yako katika nyumba hii. Vyovyote utakavyojifakhiri unakuwa unajifakhiri kwa vyombo vya ghairi yako, na huenda Akavinyang'anya kwako, na moyo wako utarudi mtupu bila kheri, kuliko tumbo la ngamia."

Bustani ngapi zilizopitiwa na usiku hali maua yake laini na yamenawiri, zimepitiwa na mchana huku maua makavu yasiyo na afya na upepo mkavu unavuma juu yake, kadhalika mja hulala ilhali moyo wake mtiifu kwa Allah, unaangaza na umesalimika, anaamka akiwa mwenye kumwasi Allah, huku pia dhalimu na mgonjwa. Hiyo ni kudura ya mtukufu mkuu.

Ewe mwanadamu siku ngapi zinapita juu yako, na wewe uko katika ghafla hujui, Ewe mwanadamu acha nyimbo na udi na makazi na miji, na kushindana katika nyumba hii, ili uone nini kudura zimefanya katika jambo lako.

\*\*\*

**DHAMBI KUBWA YA SITINI NA NNE**

**KUKATIA TAMAA REHEMA YA ALLAH**

Allah Mtukuka Anasema:

إِنَّهُ لَا يَأْتِسُّ مِنْ رُوحِ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْكَافِرُونَ ﴿١٢٨﴾

**“Hakika hawakati tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu isipo kuwa watu makafiri.” (12:87)**

Allah Mtukuka Akasema:

وَهُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ الْغَيْثَ مِنْ بَعْدِ مَا قَنَطُوا

**“Naye Ndiye Anaye iteremsha mvua baada ya wao kwisha kata tamaa” (42:28).**

Allah Mtukuka Akasema:

﴿ قُلْ يَعْبادِي الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ ﴾

**“Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. ” (39:53)**

Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

« لا يموتن أحدكم إلا وهو يحسن الظن بالله »

**“Asife yeyote isipokuwa anamdhania Allah vizuri”<sup>726</sup>.**

Ewe mola wetu lau si kupenda kwako msamaha usingempa muda mwenye kukabiliana kwa maasi, na lau si msamaha wako na ukarimu wako usingewaweka (waja) peponi'. “Ee Mola hakika Wewe ni Msamehevu unapenda Msamaha basi tusamehe.

---

<sup>726</sup> Sahihi: Muslim 2877



## DHAMBI KUBWA YA SITINI NA TANO

### MWENYE KUACHA SWALA YA JAMAA ANASWALI PEKE YAKE BILA UDHURU

Kutoka kwa Abdullaahi bin Mas'uud amesema: Mjumbe wa Allah ﷺ aliwaambia watu wanaohalifu jamaa:

عن ابن مسعود [رضي الله عنه-] <sup>(1)</sup>، أن النبي ﷺ قال لقوم يتخلفون عن الجمعة: «لقد هممتُ أن أمرَ رجلاً يُصَلِّي بالناس، ثم أحرقُ على رجال يتخلفون عن الجمعة بيوتهم» <sup>(2)</sup> أخرجه مسلم.

*“Nilitamani kumuamuru mtu kuswalisha watu kisha nichome moto nyumba za watu wanaohalifu kwenda jamaa!” (Muslim)<sup>727</sup>.*

Mtume ﷺ amesema:

وقال ﷺ: «لَيْتَهُنَّ أَقْوَامٌ عَنْ وَدْعِهِمُ الْجُمُعَاتِ، أَوْ لِيَخْتِمَنَّ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ، ثُمَّ لِيَكُونَنَّ مِنَ الْخَافِلِينَ» <sup>(3)</sup> أخرجه مسلم.

*“Watu watakoma kuacha kwao jamaa au Allah Atapiga mhuri juu ya nyoyo zao, kisha watakuwa katika walioghafilika”. (Muslim)<sup>728</sup>*

Mtume ﷺ amesema:

وعن أبي الجعد الضمري، أن رسولَ الله ﷺ قال: «مَنْ تَرَكَ ثَلَاثَ جُمُعٍ تَهَاوَنًا؛ طَبَعَ اللَّهُ عَلَى قَلْبِهِ»

*“Mwenye kuacha Ijumaa tatu kwa kuzizembea Allah Atapiga mhuri juu ya moyo wake”. (Abu Dawud na Nasaai)<sup>729</sup>*

---

<sup>727</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>728</sup> Sahihi: Muslim 865; Nasaai 3/88; Ibn Maajah 794

<sup>729</sup> Sahihi: Ahmad 3/434; Abu Dawud 1052; Tirmidhi 500; Swahihil Jaami'i 6140

## Al - Kabair

---

Mtume ﷺ amesema:

وعن حفصة [-رضي الله عنها-]<sup>(٢)</sup>، عن النبي ﷺ قال: «رَوَّاحُ  
الجمعة واجبٌ على كلِّ مُحتلمٍ»<sup>(٣)</sup> [رواه النسائي]<sup>(٢)</sup>.

*“Mwenye kuacha Ijumaa bila udhuru wala kuogopea madhara,  
anaandikwa kuwa mnafiki katika rejesta halifutwi wala  
halibadilishwi”<sup>730</sup>.*

Hafswah رضي الله عنها amesema: Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*“Kuwahi Ijumaa ni wajibu juu ya kila aliye baleghe.”<sup>731</sup>*

Tunaomba Tawfiki ya Allah kwa Anachopenda na kuridhia, hakika Yeye  
ni Mkarimu Mkwasi.

\*\*\*

---

<sup>730</sup> Sahihi: Ibn Habbaan 258; Ibn Khuzaimah 1857; Shaykh ameisahihisha katika At Taaliqi 'alaas Swahiih ibn Khuzaimah

<sup>731</sup> Sahihi: Abu Dawud 342; Nasaai katika Al Jumu'ah 9; Al Bayhaqi 3/187; Al Baani ameisahihisha katika Sahiihil Jaami'i 3521

**DHAMBI KUBWA YA SITINI NA SITA**

**KUDUMU KUACHA SWALA YA IJUMAA NA  
JAMAA BILA UDHURU**

Allah Mtukuka Anasema:

يَوْمَ يُكْشَفُ عَن سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٦٨﴾ خَشِيعَةً أَبْصَرُهُمْ  
تَزَهَّقُهُمْ ذِلَّةً ۖ وَقَدْ كَانُوا يُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ وَهُمْ سَلِيمُونَ ﴿٦٩﴾

***“Siku utakapo wekwa wazi muundi, na wataitwa kusujudu, lakini hawataweza. Macho yao yatainama chini, fedheha itawafunika. Na hakika walikuwa wakiitwa wasujudu walipo kuwa wazima.” (68:42-43)***

Ka’abul Ahbaar amesema: “Aya hii iliteremshwa kuhusu watu wanaohalifu jamaa”. Said Ibnul Mussayyib alisema: “Walikuwa wanasikia: “Njooi kwenye Swala hawajibu na wao ni wazima wamesalimika”

Katika sahihi mbili: Mjumbe wa Allah ﷻ amesema:

*“Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake, nilitamani kuamrisha kukusanya kuni zikakusanywa, kisha naamrisha mtu kuongoza watu Swala, kisha nawafuata watu ambao hawajahudhuria Swala katika jamaa na nizichome moto nyumba zao.”<sup>732</sup>*

Pia katika riwaya ya Muslim kutokana na hadithi ya Abu Hurairah, Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>732</sup> Maelezo yake yametangulia

عن ابن مسعود [-رضي الله عنه-]<sup>(1)</sup>، أن النبي ﷺ قال لقوم يتخلفون عن الجمعة: «لقد هممت أن أمر رجلاً يُصَلِّي بالناس، ثم أُحرقُ على رجال يتخلفون عن الجمعة بيوْتهم»<sup>(2)</sup> أخرجہ مسلم.

*“Kwa hakika nilitamani kuamuru vijana wangu wanikusanyie mafungu ya kuni, kisha niwaendee watu wanaoswali katika nyumba zao na hawana tatizo lolote ili nizichome nyumba zao.”<sup>733</sup>*

Katika hadithi hii na aya ilio kabla yake kuna kamio kali kwa mwenye kuacha Swala ya Jamaa bila udhuru.

Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُ Amesema: Mjumbe wa Allah ﷺ amesema:

*“Mwenye kumsikia muadhini na udhuru haukumzuia kuijia”*

Pakasemwa: “Udhuru nini ewe Mtume wa Allah?. Akasema: “Ni khofu au maradhi, hakubaliwi Swala alioiswali”<sup>734</sup>. Yaani: Nyumbani kwake

Ibn Abbaas رَضِيَ اللهُ عَنْهُ aliulizwa kuhusu mtu anayeswali, anayefunga mchana na anaswali usiku wala haswali katika jamaa wala hakisanyi? Akasema: “Huyu akifa basi huyo ni motoni”<sup>735</sup>

Kipofu alikwenda kwa Mtume ﷺ akamwambia: “Ewe Mjumbe wa Allah sina mtu wa kuniongoza msikitini, je nina ruhusa kuswali nyumbani?” Mtume ﷺ akamruhusu”. Alipogeuka akamwambia:

« هل تسمع النداء بالصلاة ؟ »

*“Je unamsikia mnadi Swala?”*

---

<sup>733</sup> Muslim 651

<sup>734</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>735</sup> Maelezo yake yametangulia

## Al- Kabair

---

Akasema: "Ndiyo", Mtume ﷺ akasema: "Basi jibu"<sup>736</sup>.

Ibn Ummi Maktuum alikwenda kwa Mtume ﷺ akamwambia: "Ewe Mjumbe wa Allah Madina kuna wadudu na wanyama na mimi ni kipofu, Je nina ruhusa kuswali nyumbani?" Akamwambia: "Je, unasikia, Njoooni kwenye Swala njooni kwenye kufaulu".

Akasema: "Ndio naisikia" Mtume ﷺ akamwambia:

« فَأَجِبْ ، فَحَيِّ هَلَا »

"Basi ijibu, hiyo njooni..."<sup>737</sup>

Katika riwaya nyingine kuwa alisema: 'Ewe Mtume wa Allah mimi ni kipofu mwenye nyumba kubwa na nina kiongozi asiyenifaa je nina ruhusa (nisiende msikitini).'

Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: Mtume ﷺ amesema:

« وَمَنْ سَمِعَ النِّدَاءَ فَلَمْ يَمْنَعْهُ مِنْ اتِّبَاعِهِ عَذْرٌ فَلَا صَلَاةَ لَهُ »

"Mwenye kumsikia muadhini na udhuru haukumzuia kuifuata hana Swala".

Wakasema: "Udhuru nini ewe Mtume wa Allah?. Mtume ﷺ Akasema:

« خَوْفٌ أَوْ مَرَضٌ »

"Hofu au maradhi"<sup>738</sup>.

Mtume ﷺ amesema:

---

<sup>736</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>737</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>738</sup> Maelezo yake yametangulia

## Al - Kabair

---

« لعن الله ثلاثة : من تقدم قوما وهم له كارهون ، وامرأة باتت وزوجها عليها ساخط ورجلا سمع حي على الصلاة حي على الفلاح ثم لم يجب »

*“Allah Amewalaani watu wa aina tatu; mwenye kuwaongoza watu na huku wao wanamchukia, na mwanamke amelala na mumewe amemkasirikia, na mtu amesikia “Njooi kwenye Swala, njooi kwenye kufaulu, kisha hakujibu”.*<sup>739</sup>

Abu Hurairah رضي الله عنه<sup>739</sup> amesema:

« لئن تمتلئ أذن ابن آدم رصاصاً مذاباً خيراً من أن يسمع حي على الصلاة حي على الفلاح ثم لا يجيب »

*“Sikio la mwanadamu kujaa risasi iliyoyeyushwa ni bora kwake kuliko kusikia “Njooi kwenye Swala njoo kwenye kufaulu kisha hajibu”.*<sup>740</sup>

Ali ibn Abu Talib رضي الله عنه<sup>741</sup> amesema: “Hakuna Swala kwa jirani ya msikiti isipokuwa msikitini.” Pakasemwa: “Ni nani jirani wa msikiti?” akasema: “Mwenye kusikia adhana”. Vile vile akasema: “Mwenye kusikia adhana na asiiendee basi Swala yake haitavuka kichwa chake isipokuwa udhuru”<sup>741</sup>.

Ibn Mas’uud amesema: Mwenye kufurahishwa kukutana na Allah kesho akiwa Muislamu, basi na ahifadhi juu ya hizi Swala tano pale zinapo adhiniwa. Kwa hakika Allah Taalaa ameweka sheria kwa Mtume wenu na suna za uongofu, na hakika hizo ni katika suna za uongofu, lau nyinyi mtaswali katika nyumba zenu kama anavyoswali huyu mhalifu katika nyumba yake, na lau mkiacha suna ya Mtume wenu mngepotea. Tulikuwa tunaona kuwa hahalifu katika nyumba yake isipokuwa mnafiki, na mwenye kujulikana unafiki wake, na mtu alikuwa analetwa

---

<sup>739</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>740</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>741</sup> Maelezo yake yametangulia

anabebwa baina ya watu wawili, hadi asimamishwe kwenye safu. Yaani; anawaegemea kwa udhaifu wake kwa pupa ya fadhila yake na hofu ya dhambi ya kuiacha<sup>742</sup>.

### FASILI

Fadhila ya Swala ya jamaa ni kubwa kama katika tafsiri ya Kauli Yake Taalaa:

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزُّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ﴿١٠٥﴾

***“Kwa hakika Tumeandika katika Zaburi baada ya dhikri kuwa ardhi watairithi waja wangu wema” (21:105).***

Hakika hao ni wenye kuswali swala tano katika jamaa. Na katika Kauli Yake Taalaa:

وَتَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا وَآثَرَهُمْ ؕ

***“Na Tunaandika walioyatanguliza na athari zao” (36:12).***

Yaani: Hatua zao

Na katika Sahihi kuwa Mtume ﷺ amesema:

« من تطهر في بيته ثم مشى إلى بيت من بيوت الله ليقضي فريضة من فرائض الله كانت خطواته إحداها تحط خطيئة والأخرى ترفع درجة »

***“Mwenye kujitoharisha nyumbani mwake kisha akatembea kuelekea nyumba miongoni mwa nyumba za Allah ili atekeleze faradhi miongoni mwa faradhi za Allah, itakuwa hatua zake moja wapo inapomoshha makosa yake, na nyingine inainua daraja”<sup>743</sup>.***

---

<sup>742</sup> Maelezo yake yametangulia

<sup>743</sup> Sahihi: Ameipokea Muslim (666)

« فإذا صلى لم تزل الملائكة تصلي عليه ما دام في مصلاه الذي صلى فيه  
يقولون : اللهم اغفر له ، اللهم ارحمه ما لم يؤذ فيه أو يحدث فيه »

*“ Kwa hiyo akisha swali malaika hawataacha kumswalia madamu  
yu katika mswala wake alioswali ndani yake, wanasema: Ewe Mola  
mghufirie ewe Mola msamehe, madam hajaudhi ndani yake au  
hajapata hadathi”<sup>744</sup>.*

Akasema: Wakasema: “Kwanini ewe Mtume wa Allah?”, Akasema:

« إسباغ الوضوء على المكاره ، وكثرة الخطا إلى المساجد ، وانتظار الصلاة  
بعد الصلاة ، فذلكم الرباط فذلكم الرباط »

*‘Kueneza udhu juu ya machukivu na wingi wa hatua kuelekea  
msikitini, na kungojea Swala baada ya Swala, Basi kwenu nyinyi  
hiyo ndio ribati, basi kwenu nyinyi hiyo ndio ribati’<sup>745</sup>*

\*\*\*

---

<sup>744</sup> Ameipokea Bukhari 477, 647; kwa tamshi: (Swala ya mtu katika Jamaa)

<sup>745</sup> Ameipokea Malik 1/176, Muslim (251); Nasaai 1/89, Tirmidhi 51,52.



**DHAMBIB KUBWA YA SITINI NA SABA**

**KUDHURU KATIKA WASIA**

Allah Amesema:

مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصَى بِهَا أَوْ دِينَ غَيْرِ مَضَارٍ

**"...Baada ya wasia ulio usiwa au kulipa deni, pasipo kuleta dhara..." (4:12)**

Yaani bila kuingiza madhara kwa warithi, nayo ni kuusia deni asilodaiwa, anakusudia kwalo kuwadhuru warithi. Kwa hiyo Allah Akazuia hilo, Akasema Allah:

وَصِيَّةٍ مِّنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَلِيمٌ

**"...Huu ndio wasia ulio toka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mpole". (4:12)**

Ibn Abbaas amesema: Anataka aliyo yahalalisha Allah katika mafungu yake katika mirathi.

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

**"Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anaye mt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake",**

Katika jambo la warithi.

يُدْخِلُهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

**"Atamtia katika Pepo zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na huko ndiko kufuzu kukubwa. ..." (4:14)**

Mujaahid amesema: katika aliyoyafaradhisha Allah. Ikrimah amepokea kutoka kwa Ibn Abbas: Ambae haridhii mgao wa Allah na akayafanyia jeuri Aliyoyasema Allah,

يُدْخِلُهُ نَارًا

**“Atamtia Motoni”.**

Kalbi amesema: Yaani anakataa mgao wa Allah wa mirathi na anafanya jeuri kwa mipaka yake kwa kuhalalisha,

يُدْخِلُهُ نَارًا خَلِيدًا فِيهَا وَلَهُ عَذَابٌ مُّهِينٌ

**“Atamtia Motoni adumu humo, na atapata adhabu ya kudhalilisha”.**

Abu Hurairah amesema, Mtume ﷺ amesema:

« إن الرجل أو المرأة ليعمل بطاعة الله ستين سنة ثم يحضرهما الموت فيضاران في الوصية فتجب لهما النار »

*“Hakika mwanamume au mwanamke atafanya utii kwa Allah miaka sitini kisha wanafikwa na mauti, kwa hiyo wanafanya madhara katika wasia, basi itapasa kwao moto”*

Kisha Abu Hurairah akasoma ayah hii.

مَنْ بَعْدَ وَصِيَّةٍ يُوصَىٰ بِهَا أَوْ دَيْنٍ غَيْرَ مُضَارٍّ

**“Baada ya wasia ulio usiwa au kulipa deni, pasio kuleta dhara”.** Ameipokea Abu Dawud<sup>746</sup>.

---

<sup>746</sup> Dhaifu: Abu Dawud 2867; At-Tirmidhi 2215; Shaykh ameidhoofisha katika Al Jaami'ii 1457

## Al - Kabair

---

Na imekuja kutoka kwake kuwa amesema:

*“Mwenye kukimbiza mirathi ya mrithi Allah Atakata mirathi yake peponi.”<sup>747</sup>*

Na akasema:

« إن الله قد أعطى كل ذي حق حقه فلا وصية لوارث »

*“Hakika Allah Amempa kila mwenye haki haki yake kwa hiyo hakuna wasia kwa mrithi”<sup>748</sup>. Tirmidhi ameisahihisha.*

\*\*\*

---

<sup>747</sup> Sahihi: Ibn Maajah 2703; Shaykh ameidhoofisha katika Dhaiifi Ibn Maajah 590

<sup>748</sup>Abdur Razaak 16308; Ahmad 5/267; Abu Dawud 2853; Tirmidhi 665, 2253 na Shaykh ameizingatia kuwa ni sahihi na ameiweka katika sahihi Al-Jami' 1788, 1789.

DHAMBI KUBWA YA SITINI NA NANE

VITIMBI NA HADAA

Allah Amesema:

وَلَا يَحِقُّ الْمَكْرُ السَّيِّئُ إِلَّا بِأَهْلِهِ ۗ

**“Na vitimbi viovu havimsibu ila mwenyewe”. (35:43)**

Mtume ﷺ amesema:

« المكر والخديعة في النار »

*“Vitimbi na hadaa ni katika moto.”<sup>749</sup>*

Na akasema:

« لا يدخل الجنة خب ولا بخيل ولا منان »

*“Haingii peponi, adui, wala bakhili, wala msimbulizi”<sup>750</sup>*

Allah Amesema kuhusu wanafiki,

مُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِّعُهُمْ

**“Wana mhadaa Allah na Yeye ni mwenye kuwahadaa wao” (4:142)**

Al-Wahidi amesema: Wanafanya matendo ya mhadaaji juu ya hadaa zao, na hilo ni wao kupewa nuru kama wanayo pewa waumini, wanapopita kwenye Swirati nuru yao inazimika na kubaki gizani.

---

<sup>749</sup> Al Hakim 4/607; Ibn Adiy 2/236; Al Baani ameisahihisha katika Sahihil Jaami'i 6725

<sup>750</sup> Maelezo yake yametangulia

## Al - Kabair

---

Na amesema Mtume ﷺ katika hadithi:

« وأهل النار خمسة »

*“Na watu wa motoni ni watano”*

Akataja miongoni mwao:

« رجلا لا يصبح ولا يمسي إلا وهو يخادعك عن أهلك ومالك »

*“Mtu hapambazuki wala hachwi isipokuwa anakuhadaa kwa mke wako na mali yako.”<sup>751</sup>*

\*\*\*

---

<sup>751</sup> Muslim 2865

**DHAMBBI KUBWA SITINI NA TISA**

**MWENYE KUPELELEZA WAISLAMU NA  
AKAONYESHA AIBU ZAO**

Kuna hadithi ya Hatib bin Abi Balta'a kuwa 'Umar alitaka kumuua kwa alilofanya, Mtume ﷺ akamzuia kumuua kwa kuwa yeye ameshuhudia Badri.<sup>752</sup> Itakapo ambatana katika kutekeleza kwake kudhoofisha Uislamu na watu wake na kuuu, au kupokonya au kuteka au chochote katika hivyo. Hili ni sawa na kwenda katika ardhi kwa ufisadi na kuangamiza mazao na roho na kusaidia kuuwa hivyo inakuwa ni haki kwake kupata adhabu. Tunamuomba Allah msamaha na uzima.

Na kwa dharura anajua kila mwenye ujasusi kuwa fitina ni katika maharamisho makubwa, basi fitina ya ujasusi ni kubwa mno.

Tunajilinda kwa Allah kutokana na hayo, na tunamuomba msamaha na uzima kwani Yeye ni Mpole Mtambuzi.

\*\*\*

---

<sup>752</sup> Kisa hiki amekipokea Bukhari 3007; Muslim 2494

## DHAMBI KUBWA YA SABINI

### KUMTUKANA SAHABA YOYOTE

Imethibiti katika Sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

« يقول الله تعالى : من عادى لي وليا فقد آذنته بالحرب »

*“Allah Taalaa anasema: “Mwenye kumfanyia uadui walii Wangu Nimekwisha mtangazia vita”<sup>753</sup>.*

Na Mtume ﷺ akasema:

« لا تسبوا أصحابي فوالذي نفسي بيده لو أنفق أحدكم مثل أحد ذهباً ما بلغ مد أحدهم ولا نصيفه »

*“Msitukane masahaba zangu, naapa kwa ambae nafsi yangu imo Mkononi Mwake lau mmoja wenu atatoa kibaba cha dhahabu hatafikia kibaba cha mmoja wao wala nusu yake.”<sup>754</sup> (Bukhari na Muslim).*

Mtume ﷺ akasema:

« الله الله في أصحابي لا تتخذوهم غرضا بعدي ، فمن أحبهم فبحبي أحبهم ،  
ومن أبغضهم فببغضي أبغضهم ، ومن آذاهم فقد آذاني ، ومن آذاني فقد آذى  
الله ومن آذى الله أوشك أن يأخذه »

*“Allah Allah katika sahaba zangu msiwafanye ni lengo baada yangu,  
kwani mwenye kuwapenda wao kwa upendo wangu nitawapenda,  
na mwenye kuwachukia kwa chuki yangu nitawachukia wao, na  
mwenye kuwaudhi wao ameniudhi mimi, na mwenye kuniudhi mimi*

---

<sup>753</sup> Mapokezi yake yametangulia

<sup>754</sup> Bukhari 3673 Muslim 2541

## Al - Kabair

---

*amemuudhi Allah, na mwenye kumuudhi Allah anakaribia kumchukua*". Tirmidhi<sup>755</sup>.

Katika hadithi hii na mifano yake ni ubainifu hali ya mwenye kuwafanya wao ni lengo baada ya Mtume ﷺ na akawatukana akawazushia, akawaabisha, akawakufurisha na akawafanyia ujeuri. Na kauli yake:

« الله الله »

*"Allah Allah"*

Ni neno la kutahadharisha na kuonya, kama asemavyo mwenye kuonya: *"An-Naar an-naar"* yaani 'Tahadharini na moto.' Na kauli yake:

« لا تتخذوهم غرضاً بعدي »

*"Msiwafanye lengo baada yangu."*

Yaani: 'Msiwachukue kwa ajili ya kuwatukana na kuwakosoa, ni kama inavyosemwa: 'Fulani amemfanya fulani kuwa lengo kwa matusi yake'; Na kauli yake:

« فمن أحبهم فبحبي أحبهم ، ومن أبغضهم فببغضي أبغضهم »

*"kwani mwenye kuwapenda wao kwa upendo wangu nitawapenda, na mwenye kuwachukia kwa chuki yangu nitawachukia wao."*

Hii ni kwa ajili ya fadhila na wasifu kwa kuwa kuwapenda masahaba ni kwa kuwa wao wamesuhubiana na Mtume ﷺ na wamemnusuru wakamuamini na wakamliwaza kwa nafsi zao na mali zao, kwa hiyo mwenye kuwapenda amempenda Mtume ﷺ.

---

<sup>755</sup> Sahihi: Imepokewa na Muslim 3022.



## Al - Kabair

---

Kwa hiyo kuwapenda masahaba wa Mtume ﷺ ni anuani ya upendo wake na kuwachukia ni anuani ya kumchukia, kama ilivyokuja katika hadithi,

« حب الأنصار من الإيمان وبغضهم من النفاق »

*“Kuwapenda ansari ni katika imani na kuwachukia ni katika unafiki.”<sup>756</sup>*

Na hilo ni kwa sababu ya kutangulia kwao na kupigana kwao na adui wa Allah mbele ya Mtume ﷺ; Na vilevile kumpenda Ali رضي الله عنه ni katika imani na kumchukia ni katika unafiki. Kwa hakika anajua fadhila za sahaba رضي الله عنهم ambaye amezingatia hali zao na nyendo zao na athari katika maisha ya Mtume ﷺ na baada ya mauti yake. Yote haya ni kutokana na kushindana kwenye imani na kupigana na makafiri, kueneza dini, na kudhihirisha alama ya Uislamu, na kuinua neno la Allah na Mtume wake, na kujifundisha faradhi zake na Sunnah zake. Lau sio wao tusingefikiwa na dini wala msingi wowote wa dini wala tawi lake, wala tusingejua faradhi na Sunnah wala tusingejua chochote kutokana na hadithi wala habari.

Kwa hiyo mwenye kuwatukana wao huyo ametoka katika dini na mila ya Uislamu, kwani kutukana hakuwi isipokuwa kwa kuitakidi maovu yao na kudhamiria shari juu yao, na kukanusha Aliyoyataja Allah Taalaa katika Kitabu Chake katika kuwasifu wao. Na ambayo Mtume ﷺ amewasifia wao, na fadhila zao, na daraja zao, na mapenzi yao, na kuwa wao ni nyenzo (wasila) inayoridhiwa zaidi. Kutokana na mapokezi na kiunganishi cha mapokezi, na kutukana kiunganishi ni kutukana asili, na kudharau mapokezi ni kudharau upokezi. Hili liko wazi kwa aliyelizingatia na akasalimika kutokana na unafiki na uzandiki, na ilihadi katika itikadi yake. Na yakutoshe yaliyokuja kwenye habari na athari miongoni mwa hizo ni kauli ya Mtume ﷺ,

---

<sup>756</sup> Bukhari (3784) Muslim (74)

« إن الله اختارني واختار لي أصحاباً . فجعل لي منهم وزراء وأنصاراً وأصحاباً  
فمن سبهم فعليه لعنة الله والملائكة والناس أجمعين ، لا يقبل الله منه يوم القيامة  
صرفاً ولا عدلاً »

*“Hakika Allah amenichagua mimi na akanichagulia masahaba na  
akanifanyia kwao mawaziri na ansari na wakwe, basi mwenye  
kuwatukana wao ni juu yake laana ya Allah na malaika na watu  
wote. Allah Hatakubali Siku ya Kiama Sunnah wala Faradhi zao.”<sup>757</sup>*

Anas bin Malik anasema: “Watu miongoni mwa masahaba wa  
Mtume ﷺ walisema: “Sisi tunatukanwa” Mtume ﷺ akasema:

« من سب أصحابي فعليه لعنة الله والملائكة والناس أجمعين »

*“Mwenye kuwatukana masahaba zangu basi juu yake laana ya Allah,  
Malaika na watu wote.”<sup>758</sup>*

Na Mtume ﷺ akasema:

« إن الله اختارني واختار لي أصحابي وجعل لي منهم أصحاباً وإخواناً  
وأصحاباً ، وسيجيء قوم بعدهم يعيرونهم وينقصونهم فلا تواكلوهم ولا

*“Hakika Allah amenichagua mimi na amenichagulia masahaba, na  
ndugu, na wakwe, watakuja watu baada yao wanawaaibisha na  
kuwakosoa, basi msile nao wala msinywe nao wala msioleane nao  
wala msiwaswalie wala msiswali pamoja nao.”<sup>759</sup>*

Ibn Masuud رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ akasema:

---

<sup>757</sup> Dhaifu, Ibn Abu Asim 1000 Abu Nuaim 2/11; Al Haakim 3/632; Al Baani  
ameidhoofisha katika Dhaiifil Jaami' 1536

<sup>758</sup> Hasan, Ibn Adiy 5/212, na Al Khatib katika tarehke yake, 14/241 Twabari 12709,  
Al-Baani ameifanya Hasan katika Sahihil Jaami'i 6285

<sup>759</sup> Dhaifu, Aqiili 1/126; Al Baani ameidhoofisha katika Dhaiifil Jaami'i 1538

« إذا ذكر أصحابي فأمسكوا، وإذا ذكر النجوم فأمسكوا ، وإذا ذكر القدر فأمسكوا »

*“Wanapotajwa masahaba wangu jizuieni, na inapotajwa kudra jizuieni.”<sup>760</sup>*

Wanazuoni wamesema: ‘Maana yake katika kuchunguza siri ya kudura katika kuumba, nayo, yaani kujizuia ni alama ya imani na kujisalimisha kwa amri ya Allah. Vile vile nyota, mwenye kuamini kuwa hizo zinafanya au zina athari bila matakwa ya Allah huyo ni mshirikina. Vile vile mwenye kutukana masahaba wa Mtume ﷺ kwa chochote na akafuatilia makosa yao na akayaunganisha kwao anakuwa mnafiki.

Basi wajibu juu ya Muislamu ni kumpenda Allah na kumpenda Mtume wake na kupenda aliyokuja nayo na kumpenda mwenye kusimamia amri yao, na kumpenda mwenye kuchukua uongofu wake na kutekeleza Sunna zake.

Na kupenda ali zake na sahaba zake, na wake zake na watoto wake na watumishi wake. Na kumpenda mwenye kuwapenda wao na kuwachukia wenye kuwachukia wao, kwa vile uzi madhubuti wa Imani ni kupenda katika Allah na kuchukua katika Allah.”

Ayuub As-Sikhstani رضي الله عنه amesema: ‘Mwenye kumpenda Abu Bakri amesimamisha minara ya Dini, mwenye kumpenda ‘Umar ameonyesha njia, mwenye kumpenda ‘Uthman amenawirika kwa nuru ya Allah, mwenye kumpenda ‘Ali ameshikamana na uzi madhubuti, mwenye kusema kheri kwa sahaba wa Mtume ﷺ amepukana na unafiki.’

---

<sup>760</sup> Sahiih, Twabarani katika Al-Kabiir 2/78/2; Abu Nuaim katika Al-Hilya 4/108; Al-Baani ameisahihisha katika Sahiihah 34.

## FASILI

Ama manaqibu ya masahaba na fadhila zao ni nyingi zisizotajika, wanazuoni wamekubaliana kuwa bora wa sahaba ni kumi walioshuhudiwa, nao ni Abu Bakri, kisha 'Umar binil Khattwab, kisha 'Uthmaan bin Affaan, kisha 'Ali رضي الله عنه wala hatii shaka katika hilo isipokuwa mzushi mnaiki khabithi.' Mtume ﷺ amesema katika hadithi ya 'Irbaadhi bin Saariya:

« عليكم بستي وستة الخلفاء الراشدين المهديين من بعدي ، عضوا عليها  
بالتواجد ، وإياكم ومحدثات الأمور »

*"Ni juu yenu Sunnah yangu na Sunnah ya makhalifa waongofu  
wenye kuongoza baada yangu yakamateni kwa magego, na  
tahadharini na vizushi vya mambo."*<sup>761</sup>

*Khulafaa Rashiduun; Abu Bakri, 'Umar, 'Ali, na 'Uthmaan رضي الله عنه kwao  
wote. Allah Ameteremsha katika fadhila za Abu Bakr رضي الله عنه Ayah za  
Qur'an, Allah Anasema:*

وَلَا يَأْتَلُ أُولُوا الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولَى الْقُرْبَىٰ وَالْمَسْكِينِ

***"Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wasaa wasiape  
kutowapa jamaa zao na masikini."*** (24:22)

Hakuna upinzani kuwa hilo liko kwake (Abu Bakri), kwa hiyo Allah Akamsifia kwa ubora رضي الله عنه. Allah Akasema:

وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِ أُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿٢٤﴾

---

<sup>761</sup> Sahihi: Ahmad 4/127, Abu Dawud 4607, At-Tirmidhi 4776, Ibn Majah 42, Sahiihil Jaami'i 2549.

**“Na aliyeleta Kweli na akaithibitisha hao ndio wachamngu”.**  
**(39:33)**

Hakuna upinzani kuwa hiyo ni kwa Abu Bakr رضي الله عنه Allah Ameshuhudia ushuba wake na Akambashiria utulivu na Akampamba kwa *thaaniyaythnain* kama alivyosema ‘Umar رضي الله عنه: ‘Ni nani atakuwa bora kuliko wa pili wa wawili Allah ni watatu wao?’

وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِ أُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿٣٣﴾

**“Na aliye ileta Kweli na akaithibitisha - hao ndio wachamngu.” (39:33).**

Ja-afar Swadiq amesema: “Hakuna upinzani kuwa aliyeleta ukweli ni Mtume ﷺ na ambae ameuswadikisha ni Abu Bakr, na ni sifa gani bora zaidi kuliko hilo katika wao? Allah Awawie radhi wote”.

\*\*\*